**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

National Economic Survey | The Economic Survey

2010

# Hali ya Uchumi wa Taifa Katika Mwaka,2010

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/775

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2010

Kimetolewa na :
Wizara ya Fedha
DAR ES SALAAM - TANZANIA
Juni, 2011

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA

# KATIKA MWAKA 2010

# YALIYOMO


ORODHA YA MAJEDWALI ..... X

KIREFU/TAFSIRI YA MANENO ..... XV

MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI MWAKA 2010 ..... XX

SURA YA I ..... 1

HALI YA UCHUMI WA TAIFA ..... 1

- Ukuaji wa Uchumi ..... 1
- Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa 2010 ..... 6
- Mwenendo wa Bei ..... 9
- Ukuzaji Rasilimali ..... 11

SURA YA 2 ..... 42

HALI YA UCHUMI DUNIANI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ..... 42

- Ukuaji wa Uchumi Duniani ..... 42
- Mwenendo wa Biashara Duniani ..... 43
- Hali ya Uchumi wa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ..... 44
- Jumuiya ya Afrika Mashariki ..... 47
- Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika ..... 48
- Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano (JPC) ..... 48
- Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za kusini mwa Afrika (SADC) ..... 49
- Mpango wa Kujitathimini na Kujipima Afrika Kuhusu Utawala Bora (APRM) ..... 50
- Mdahalo wa Uchumi Duniani (WEF) ..... 50

SURA YA 3 ..... 52

SEKTA YA NJE ..... 52

UTANGULIZI ..... 52

- BIDHAA ZILIZOUZWA NJE ..... 52
  - Kahawa ..... 53
  - Pamba ..... 53
  - Chai ..... 53
  - Tumbaku ..... 54
  - Korosho ..... 54
  - Karafuu ..... 54
  - Madini ..... 55
  - Bidhaa za Viwandani ..... 55
  - Samaki na Mazao ya Samaki ..... 55
  - Mazao ya Mboga na Maua ..... 56

Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje ..... 56
Mapato ya Huduma ..... 58
BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE ..... 58
Bidhaa za Kukuza Mitaji ..... 58
Bidhaa za Kati ..... 59
Bidhaa za Matumizi ya Kawaida ..... 59
MALIPO YA HUDUMA ..... 60
MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI MBALIMBALI ..... 60
MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE ..... 65
Urari wa Biashara ya Bidhaa ..... 65
Urari wa Biashara ya Huduma ..... 65
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi ..... 65
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida ..... 65
Urari wa Malipo ya Kawaida ..... 66
Urari wa Uhamisho wa Mitaji ..... 66
Urari wa Malipo ya Fedha katika Uwekezaji ..... 66
Urari wa Malipo Yote ..... 66
Akiba ya Fedha za Kigeni ..... 67
THAMANI YA FEDHA YA TANZANIA ..... 67

SURA YA 4 ..... 81

FEDHA ZA SERIKALI ..... 81

MAPATO YA NDANI ..... 81
MATUMIZI ..... 83
MGAWANYO WA BAJETI KWENYE HUDUMA ZA SERIKALI ..... 84
DENI LA TAIFA ..... 85
DENI LA NJE ..... 86
DENI LA NJE KWA WAKOPESHAJI ..... 87
DENI LA NDANI ..... 88
ULIPAJI WA DENI LA SERIKALI ..... 89

SURA YA 5 ..... 94

FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA ..... 94

UJAZI WA FEDHA NA KARADHA ..... 94
MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ..... 94
AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA ..... 95
MWENENDO WA VIWANGO VYA RIBA ..... 95
MFUKO WA PENSHENI WA MASHIRIKA YA UMMA (PPF) ..... 96
MFUKO WA PENSHENI KWA WATUMISHI WA UMMA (PSPF) ..... 97
MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF) ..... 97

Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali (GEPF) .......... 98
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) .......... 100
Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF) .......... 101
Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA) .......... 102
Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE) .......... 104
Benki ya Posta .......... 105

**SURA YA 6 .......... 112**

**RASILIMALI WATU .......... 112**

Idadi ya Watu na Maendeleo .......... 112
Nguvukazi na Ajira .......... 114

**SURA YA 7 .......... 118**

**UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI .......... 118**

Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini .......... 118
Mchanganuo wa Miradi Kimkoa .......... 119
Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa sekta binafsi .......... 120

**UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI .......... 121**

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi .......... 121
Utoaji na Upatikanaji wa Mikopo .......... 122

**SURA YA 8 .......... 125**

**MASUALA MTAMBUKA .......... 125**

UKIMWI .......... 125
Mazingira .......... 125
Utawala Bora .......... 127
Jinsia .......... 128
Usalama wa Raia .......... 129

**SURA YA 9 .......... 131**

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI TANZANIA (MKUKUTA) .......... 131**

Utangulizi .......... 131
Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato .......... 131
Utawala Bora na Uwajibikaji .......... 134

SURA YA 10 .......... 138

USHIRIKISHWAJI KATIKA HUDUMA ZA FEDHA KWA WATU WA KIPATO CHA CHINI .......... 138

Utangulizi .......... 138
Sekta ya Fedha Tanzania .......... 141
Malipo ya Pesa kwa Kutumia Simu za Mkononi .......... 144
Maendeleo Katika Taasisi Ndogo Ndogo za Fedha .......... 146
Changamoto .......... 147
Hitimisho .......... 150

SURA YA 11 .......... 153

KILIMO NA USHIRIKA .......... 153

Kiwango cha Ukuaji .......... 153
Mazao ya Chakula .......... 153
Uzalishaji wa Mazao ya Biashara .......... 154
Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta .......... 155
Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo .......... 156
Kilimo cha Umwagiliaji .......... 156
Huduma za Ugani na Mafunzo .......... 157
Shughuli za Utafiti .......... 158
Mfuko wa Pembejeo .......... 159
Utoaji wa Ruzuku za Pembejeo .......... 159

MIFUGO .......... 160

Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake .......... 160
Biashara ya Mifugo na Mazao yake .......... 162

USHIRIKA NA MASOKO .......... 165

Maendeleo ya Ushirika .......... 165
Mwenendo wa Bei za Mazao ya Biashara .......... 166

SURA YA 12 .......... 176

MALIASILI NA UTALII .......... 176

Kiwango cha ukuaji .......... 176
Misitu na Nyuki .......... 176
Wanyamapori .......... 179
Uvuvi .......... 181
Utalii .......... 185
Malikale .......... 187

SURA YA 13 ........ 200

MADINI ........ 200

Kiwango cha Ukuaji ........ 200
Utafutaji Madini ........ 200
Uchimbaji na Uuzaji Madini ........ 200
Almasi ........ 200
Dhahabu ........ 201
Vito vya thamani ........ 201
Makaa ya Mawe ........ 201
Thamani ya Mauzo ya Madini ........ 202

SURA YA 14 ........ 205

VIWANDA NA BIASHARA ........ 205

Kiwango cha Ukuaji ........ 205
Viwanda Vidogo ........ 205
Gharama za Uzaushaji ........ 205
Uzalishaji katika baadhi ya Viwanda Nchini ........ 205
Biashara ya Ndani ........ 206
Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ........ 207

SURA YA 15 ........ 215

UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI ........ 215

UJENZI ........ 215

Kiwango cha Ukuaji ........ 215
Mtandao wa Barabara ........ 215
Matengenezo ya Barabara na Madaraja ........ 216
Bodi ya Mfuko wa Barabara ........ 216
Bodi ya Usajili wa Makandarasi ........ 217
Bodi ya Usajili ya Wahandisi ........ 218
Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ........ 219
Baraza la Taifa la Ujenzi ........ 220
Wakala wa Majengo Tanzania ........ 220

MAENDELEO YA ARDHI ........ 220

MAENDELEO YA MAKAZI NA VIJIJI ........ 226
MAENDELEO YA NYUMBA ........ 228

SURA YA 16 .......... 229

MAWASILIANO NA UCHUKUZI .......... 229

Utangulizi .......... 229

UCHUKUZI .......... 229

Usafiri Wa Barabara .......... 229
Usafiri wa Abiria mijini .......... 230
Shirika la Usafiri Dar Es Salaam (UDA) .......... 232

USAFIRI KWA NJIA YA RELI .......... 232

Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) .......... 232
Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) .......... 233

USAFIRI WA ANGA .......... 233

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) .......... 233

HUDUMA ZA HALI YA HEWA .......... 234

USAFIRI WA MAJINI .......... 235

Uchukuzi Baharini .......... 235
Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) .......... 238
Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP) .......... 238

HUDUMA ZA MAWASILIANO .......... 238

Shirika la Posta Tanzania .......... 238
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) .......... 241

TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO .......... 243

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano .......... 243
Vituo vya Mawasiliano (Telecenters) .......... 243
Uanzishaji wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta .......... 244

SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU .......... 244

Uendelezaji wa utafiti wa kisayansi nchini .......... 244
Masijala ya Utafiti Tanzania .......... 244
Uendelezaji wa Rasilimali Watu .......... 245
Udhibiti wa Mionzi .......... 245

SURA YA 17 .......... 253

NISHATI .......... 253

Kiwangocha Ukuaji ........ 253
Umeme ........ 253
Utafutaji Mafuta na Gesi ........ 257
Bei za Mafuta ........ 257

**NISHATI MBADALA ........ 257**

Maporomoko Madogo ya Maji ........ 257
Umeme wa Jua ........ 258
Jotoardhi na Biofueli ........ 258

**SURA YA 18 ........ 259**

**MAJI ........ 259**

Utangulizi ........ 259
Huduma ya Maji Vijijini ........ 259
Huduma za Maji Mijini ........ 260

**SURA YA 19 ........ 263**

**ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI ........ 263**

Elimu ya Awali ........ 263
Elimu ya Msingi ........ 263
Elimu ya Sekondari ........ 264
Elimu ya Ualimu ........ 265
Elimu ya Watu Wazima ........ 267
Ukaguzi wa Shule na vyuo ........ 267
Elimu ya Ufundi na Mafunzo ........ 268
Elimu ya Ufundi Stadi ........ 269
Elimu ya Juu ........ 269

**SURA YA 20 ........ 282**

**AFYA ........ 282**

Utangulizi ........ 282
Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya ........ 282
Ukaguzi wa vituo vya Afya ........ 283
Elimu ya Afya kwa Wananchi ........ 284
Afya ya Uzazi na Mtoto ........ 284
Muda wa Kuishi ........ 284
Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria ........ 285
Chakula na Lishe ........ 285

Huduma za Ustawi wa Jamii ..... 286

SURA YA 21 ..... 291

**MAENDELEO YA JAMII ..... 291**

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ..... 291
Jinsia na Mendeleo ya Wanawake ..... 291
Maendeleo ya Watoto ..... 292
Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) ..... 293

Ukurasa

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali A: Takwimu Muhimu Katika Uchumi – Tanzania Bara ................xxi

Jedwali B: Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2002 – 2010..............xxii

Jedwali 1: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) .................................................. 14

Jedwali 1A Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko – Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za miaka inayohusika) .................................................. 15

Jedwali 2: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Bei za Soko (bei za miaka inayohusika) .................................16

Jedwali 2A: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko- Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za miaka inayohusika) .................................................. 17

Jedwali 2B: Pato la Taifa (PLT) na Matumizi yake, kwa bei za soko (bei za miaka inayohusika) .................................................. 18

Jedwali 3: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001) ..........................................19

Jedwali 3A: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) .................................................................20

Jedwali 4: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001) ....................................21

Jedwali 4A: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) .................................................................. 22

Jedwali 4B: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001) ...................................24

Jedwali 4C: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) ...................................................................27

Jedwali 4D: Pato la Taifa (PLT) na matumizi yake, kwa bei za soko (bei za mwaka 2001) .................................................................28

Jedwali 5: Ukuzaji Rasilimali (bei za miaka inayohusika) ..........................29

Jedwali 6: Ukuzaji Rasilimali (bei za mwaka 2001) .......... 30

Jedwali 7: Ukuzaji Rasilimali (sekta za umma na binafsi) .......... 31

Jedwali 8: Fahirisi ya bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (2001=100) .......... 32

Jedwali 9: Fahirisi ya bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (2001=100) .......... 33

Jedwali 10: Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (2001=100) .......... 34

Jedwali 11: Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na Wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (2001=100) .......... 35

Jedwali 12: Fahirisi ya gharama ya maisha ya wenye kipato cha juu Dar es Salaam (2001=100) .......... 36

Jedwali 13: Fahirisi ya gharama ya maisha wenye kipato cha juu Dar es Salaam (2001=100) .......... 37

Jedwali 14: Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2001=100) .......... 38

Jedwali 15: Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2001=100) .......... 39

Jedwali 16: Fahirisi mbali mbali za bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini – Tanzania Bara (2001=100) .......... 41

Jedwali 17: Thamani ya Bidhaa za biashara baina ya Tanzania na nchi za nje .......... 67

Jedwali 18: Kiasi na thamani ya bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje .......... 68

Jedwali 19: Kiasi na thamani ya bidhaa za asilia na zisizo asilia zilizouzwa nchi za nje .......... 69

Jedwali 20: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh.) .......... 74

Jedwali 21: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (US $) .......... 75

Jedwali 23: Aina na thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za nje .......... 77

Jedwali 24: Mizania ya malipo na nchi za nje .......... 78

Jedwali 25: Mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali .................... 89

Jedwali 26: Matumizi ya Serikali kwa huduma mbalimbali .................... 91

Jedwali 27: Mwenendo wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania bara....... 107

Jedwali 28: Viwango vya ukuaji wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania bara .................... 108

Jedwali 29: Mwenendo wa Viwango vya ubadilishaji kati ya Shilingi na Dola ya Marekani .................... 109

Jedwali 30: Mikopo ya benki za biashara kwa sekta mbalimbali .............. 110

Jedwali 31: Mwenendo wa amana katika benki za biashara .................... 111

Jedwali 32: Viwango vya wastani vya riba .................... 111

Jedwali 33: Idadi ya watu nchini Tanzania kimkoa .................... 116

Jedwali 34: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC): Miradi iliyopitishwa...... 124

Jedwali 35: Uzalishaji wa miwa na sukari .................... 170

Jedwali 36: Pamba iliyonunuliwa na mauzo nchini .................... 171

Jedwali 37: Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana .................... 172

Jedwali 38: Kahawa iliyonunuliwa na mauzo nchini .................... 173

Jedwali 39: Eneo lililopandwa mkonge na katani iliyopatikana .................... 174

Jedwali 40: Tumbaku iliyonunuliwa na mauzo nchini .................... 175

Jedwali 41: Maua ya pareto yaliyonunuliwa na mauzo ya bidhaa za pareto .................... 176

Jedwali 42: Korosho zilizonunuliwa na mauzo nchini .................... 177

Jedwali 43: Muhtasari wa mazao muhimu ya biashara yaliyonunuliwa .................... 178

Jedwali 45: Upandaji wa miti (Miche iliyooteshwa) .................... 189

Jedwali 47: Mauzo ya bidhaa za misitu nchi za nje .................... 190

Jedwali 48: Mwenendo wa biashara ya ndege, wanyamapori na vipusa nchi za nje .................... 191

Jedwali 48A: Mwenendo wa biashara ya wanyama hai na uwindaji wa kitalii .................... 192

| | | |
|---|---|---|
| Jedwali 48B: | Idadi ya Wawindaji wa Kitalii | 192 |
| Jedwali 50: | Uzalishaji katika sekta ya uvuvi | 193 |
| Jedwali 51: | Mauzo ya mazao ya uvuvi nchi za nje | 194 |
| Jedwali 51A: | Muhtasari wa Mauzo ya Mazao ya Uvuvi Nchi za Nje | 195 |
| Jedwali 51B: | Mwelekeo wa Mauzo ya Sangara Nchi za Nje | 195 |
| Jedwali 52: | Idadi ya Watalii, siku zao hotelini, na makadirio ya fedha za kigeni zilizopatikana | 196 |
| Jedwali 53: | Idadi ya Watalii walioingia nchini na kiasi cha fedha zilizopatikana | 197 |
| Jedwali 55: | Mwenendo wa Biashara ya Utalii | 198 |
| Jedwali 55A: | Idadi ya Wageni Waliotembelea Vituo vya Utalii | 199 |
| Jedwali 56: | Uchimbaji wa madini: Kiasi kilichopatikana | 203 |
| Jedwali 57: | Madini yaliyouzwa nchi za nje | 204 |
| Jedwali 58: | Matumizi ya saruji nchini | 208 |
| Jedwali 59: | Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwanda | 209 |
| Jedwali 60: | Viwanda - Idadi ya Watu walioajiriwa | 210 |
| Jedwali 61: | Viwanda - Gharama za kazi | 211 |
| Jedwali 62: | Viwanda - Muhtasari wa matokeo | 212 |
| Jedwali 63: | Viwanda - Muhtasari wa matokeo kimkoa | 213 |
| Jedwali 65: | Vigezo vya Ufanisi katika Sekta ya Viwanda | 214 |
| Jedwali 67: | Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) | 246 |
| Jedwali 68: | Reli ya Uhuru (TAZARA) | 247 |
| Jedwali 69: | Usafirishaji kwa Meli | 248 |
| Jedwali 70: | Huduma za Posta | 251 |
| Jedwali 73: | Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) | 252 |
| Jedwali 74: | Uwezo wa mitambo ya umeme | 254 |
| Jedwali 75: | Mauzo ya umeme kwa watumiaji mbali mbali | 255 |

Jedwali 76: Mauzo ya umeme kwa mikoa ........................................ 256

Jedwali 78: Jumla ya visima vilivyochimbwa nchini mwaka 2010 ............. 261

Jedwali 79: Usambazaji wa maji Katika Miji Mikuu ya Mikoa .................. 262

Jedwali 80: Shule za sekondari za Serikali - Idadi ya wanafunzi kwa kidato ........................................ 271

Jedwali 81: Shule za sekondari za binafsi - Idadi ya wanafunzi kwa kidato ........................................ 281

Jedwali 84: Vyombo vya afya nchini ........................................ 288

Jedwali 85: Huduma za Afya: Waliofaulu mafunzo kwa mwaka 2010 ...... 289

Jedwali 87: Idadi ya wataalamu wa afya ........................................ 290

Jedwali 87A: Idadi ya Vitanda katika Hospitali zote Nchini mwaka 2010 ..... 290

## KIREFU/TAFSIRI YA MAINENO

| | | |
|---|---|---|
| APRM | - | African Peer Review Mechanism (Mpango wa Kujitathmini na Kujipima kuhusu Utawala Bora Barani Afrika) |
| ASDP | - | Agricultural Sector Development Programme (Program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo) |
| ARVs | - | Anti-rctroviral ( Dawa za Kupunguza Makali ya UKIMWI) |
| TAA | - | Tanzania Aiipots Authority (Mamlaka ya Viwanja vya Ndege) |
| AU | - | African Union (Umoja wa Afrika) |
| ATMS | - | Automatic Teller Machine (Mashine za Kutolea Pesa) |
| BEST | - | Business Environment Strengthening for Tanzania (Mpango wa Maboresho ya Mazingira ya Biashara Tanzania) |
| BRELA | - | Business Registration and Licensing Authotity |
| BoT | - | Bank of Tanzania (Benki Kuu ya Tanzania) |
| Cif | - | Cost insurance and freight (Thamani ya bidhaa ikijumuisha gharama za usafiri na Bima) |
| COSTECH | - | Tanzania Commission for Science and Technology |
| CARMATEC | - | Centre for Agricultural Mechanisation and Rural Technology |
| CPI | - | Consumer Price Index (Fahirisi ya Bei za Walaji) |
| CRDB | - | Benki ya CRDB |
| COICOP | - | Classification of Individual Consumption by Purpose |
| COMESA | - | Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja la Nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika) |
| DAWASCO | - | Dar es Salaam Water and Sewerage Corporation (Shirika la Maji Safi na Taka Dar es Salaaam) |
| D by D | - | Decentralization by Devolution ( Kugatua Madaraka kwa Wananchi ) |
| DSM | - | Dar es Salaam |
| DSE | - | Dar es salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar Es Salaam) |
| DADPs | - | District Agricultural Development Plan (Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya) |
| DITF | - | Dar es Salaam International Trade Fair (Maonesho ya Kimataifa ya Biashara) |
| DIT | - | Dar es Salaam Institute of Technology |

| | | |
|---|---|---|
| ECA | - | Economic Commission for Africa (Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika) |
| EAC | - | East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| EPZ | - | Economic Processing Zone (Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje) |
| EWURA | - | Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati) |
| f.o.b | - | free on board (Thamani ya Bidhaa bila Kujumuisha Gharama za Usafiri na Bima |
| FDI | - | Foreign Direct Investment (Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni) |
| GEPF | - | Government Employees Provident Fund (Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali) |
| GBS | - | General Budget Support (Misaada na Mikopo ya Bajeti) |
| GDP | - | Gross Domestic Product (Pato la Taifa) |
| HBS | - | Household Budget Survey (Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya) |
| ISO | - | International Organization for Standardization (Shirika la Viwango la Kimataifa) |
| JPC | - | Joint Program Commissions (Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano) |
| IFMS | - | Integrated Financial Management System (Mfumo Tungamanishi wa Usimamizi wa Fedha) |
| LUKU | - | Lipa Umeme Kadri Unavyotumia |
| LSRP | - | Legal Sector Reform Programme (Programu ya Maboresho katika Serikali za Mitaa) |
| LAPF | - | Local Authorities Pensions Fund (Mfuko wa Pension wa Serikali za Mitaa) |
| LGRP | - | Local Government Reform Program (Programu ya Maboresho katika Sekta ya Sheria) |
| $M_2$ | - | Broad Money Supply (Uzaji wa Fedha kwa Tafsiri Pana) |
| $M_3$ | - | Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi) |
| IMF | - | International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa) |
| MDGs | - | Millenium Development Goals (Malengo ya Maendeleo ya Milenia) |
| MKUKUTA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania |
| MPAMITA | - | Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania |
| MKURABITA | - | Mpango wa Kurasimisha Biashara na Mali za Wanyonge Tanzania |
| MMEM | - | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi |
| MACEP | - | Marine and Coastal Environmental Management Project (Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari ya Pwani) |

| | | |
|---|---|---|
| MMES | - | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari |
| MAIR | - | MKUKUTA Annual Implementation Report (Taarifa ya Utekelezaji wa MKUKUTA) |
| MMS | - | MKUKUTA Monitoring System (Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA) |
| MSCL | - | Marine Service Company Ltd (Kampuni ya Huduma za Meli) |
| MRCC | - | Maritime Rescue Coordination Centre (Kituo cha Uokoaji na Utafutaji Majini) |
| MSMEs | - | Medium, Small and Micro Enterprises (Viwanda vya Kati, Vidogo na Vidogo sana) |
| MUKEJA | - | Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii |
| MEMKWA | - | Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Waliyoikosa |
| MMAM | - | Mpango Maalum wa Afya ya Msingi |
| MW | - | Mega Watts |
| NAIC | - | The National Artificial Insemination Centre (Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji) |
| NSSF | - | National Social Security Funds (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) |
| NASCAP | - | Anti-Coruption Strategy and Action Plan (Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa) |
| NEMC | - | National Environmental Management Council (Baraza la Taifa la Mazingira) |
| NEPAD | - | New Partnership for Africa's Development (Mpango wa Ushirikiano Mpya wa Kuleta Maendeleo Afrika) |
| NGO's | - | NonGovernmental Organisations (Asasi Zisizo ya Kiserikali) |
| NHIF | - | National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya) |
| NIC | - | National Insurance Corporation (Shirika la Bima la Taifa) |
| NMB | - | National Microfinance Bank (Benki ya Taifa ya Mikopo Midogo) |
| PSRP | - | Public Service Reform Program (Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma) |
| PSPF | - | Public Service Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma) |
| PPF | - | Parastatal Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma) |
| PFMRP | - | Public Financial Management Reform Program (Program ya Maboresho ya Fedha za Umma) |
| RAHCO | - | Railway Holding Company (Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli) |
| RITES | - | Kampuni ya RITES ya India |

| | | |
|---|---|---|
| RITA | - | Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) |
| SACCOS | - | Savings and Credit Cooperative Societies (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo) |
| SADC | - | Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika) |
| SCULT | - | Savings and Co-operatives Union League of Tanzania |
| SMEs | - | Small and Medium Enterprises (Viwanda Vidogo na vya Kati) |
| SUMATRA | - | Surface and Marine Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini) |
| TAKUKURU | - | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TaESA | - | Tanzania Employment Service Agency (Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania) |
| TANESCO | - | Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Umeme Tanzania) |
| TANROADS | - | Tanzania Roads Agency (Mamlaka ya Barabara Tanzania) |
| TAZARA | - | Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia) |
| TEUS | - | Twenty Equivalent Units |
| TDHS | - | Tanzania Demographic and Health Survey (Utafiti wa Afya na Demografia Tanzania) |
| TIRA | - | Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania) |
| TCAA | - | Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania) |
| TMA | - | Tanzania Meteorology Agency (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania) |
| TCRA | - | Tanzania Communications Regulatory Authority (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania). |
| TEKNOHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TICTS | - | Tanzania International Container Terminal Services (Kampuni ya Kupakua Makontena katika Bandari ya Dar es Salaam) |
| TIKA | - | Tiba kwa Kadi. |
| TRA | - | Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania) |

| | |
|---|---|
| TRC | - Tanzania Railways Corporation (Shirika la Reli Tanzania) |
| TRL | - Tanzania Railways Company Limited (Kampuni ya Reli Tanzania) |
| TTCL | - Tanzania Telecomunications Company Limited (Kampuni ya Simu Tanzania) |
| Tshs | - Shilingi ya Tanzania |
| UAE | - United Arab Emirate (Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu) |
| UFI | - Global Association of the Exhibition Industry – Fomerly known, Union Des Foires Internationales (Shirika la Maonesho ya Dunia) |
| UDA | - Shirika la Usafiri Dar es Salaam |
| UKIMWI | - Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| VAT | - Value Added Tax (Kodi ya Ongezeko la Thamani) |
| VVU | - Virusi Vya Ukimwi |
| WEF | - World Economic Forum (Mdahalo wa Uchumi Duniani) |
| WDL | - Williamson Diamonds Limited |
| WMO | - World Meteorological Organization (Shirika la Hali ya Hewa Ulimwenguni) |

## MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI MWAKA 2010

| TAREHE | MWEZI | MATUKIO |
|---|---|---|
| 5-7 | Mei | Mdahalo wa Uchumi Duniani (World Economic Forum – WEF) ulifanyika mjini Dar es salaam. |
| | Mei | Kuzinduliwa kwa Mpango wa Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT) |
| 08 | Julai | Tanzania ilisaini Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (Comprehensive Africa Agriculture Development Program - CAADP Compact) |
| 1-7 | Julai | Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara yalifanyika Dar es Salaam. |
| | Agosti | Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Binafsi. (Public – Private Partnership - PPP) Na. 19 ya mwaka 2010 ilipitishwa |
| | Septemba | Tanzania ilizawadiwa cheti cha kufanya vizuri kwenye uandikishwaji wa wanafunzi katika elimu ya msingi, ambapo imeonekana maendeleo ni mazuri na uwezekano wa kufikia malengo ya MDGs 2015 ni mkubwa, katika Mkutano wa Viongozi wa Nchi kuhusu Maendeleo ya Malengo ya Milenia (MDGs Summit), Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa |
| 31 | Oktoba | Uchaguzi Mkuu wa Taifa (Tanzania National Election) ulifanyika |
| 17 | Desemba | Taarifa toka Benki Kuu ya Tanzania kuhusu toleo la noti mpya ambazo ziliingizwa katika mzunguko tarehe 01 Januari 2011 |

Jedwali Na. A

TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA

| | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2009-10 Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watu (milioni) | 35.3 | 35.2 | 37.5 | 38.2 | 39.5 | 40.7 | 41.9 | 2.9 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka inayohusika (Sh. milioni) | 13971592 | 15965294 | 17941256 | 20948403 | 24754457.13 | 28212645 | 32293479 | 14.5 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2001 (Sh. milioni) | 11239735 | 12058090 | 12881163 | 13801927 | 14628344.91 | 15721301 | 16828563 | 7.0 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za mwaka inayohusika (Sh.) | 395798 | 441030 | 478434 | 547051 | 627097 | 693470 | 770464 | 11.1 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2001 (Sh.)** | 318408 | 333373 | 343498 | 360445 | 375642 | 386431 | 401499 | 3.9 |
| Kasi ya Upandaji Bei (asilimia) | 4.2 | 4.3 | 7.3 | 7.0 | 10.3 | 12.3 | 5.5 | |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni) | -1009.7 | -1321.8 | -1946.5 | -2634.0 | -3433.5 | -2539.5 | -2828.3 | 11.4 |
| Urari wa Bidhaa Huduma na Uhamisho wa Mali (US$ milioni) | -363.2 | 567.6 | -1143.2 | -1580.1 | -2295.4 | -1768.3 | -1863.5 | 4.8 |
| Saruji iliyozalishwa (Tani '000) | 1280.9 | 1375.2 | 1421.5 | 1629.9 | 1755.8 | 1940.8 | 2312.0 | 19.1 |
| Umeme Uliozalishwa (KWH milioni) | 3686.0 | 3623.0 | 2484.0 | 3057.0 | 3369.0 | 4802.1 | 5130.0 | 7.0 |
| Utalii (Mapato US$ milioni) | 746.0 | 823.0 | 862.0 | 1198.0 | 1354.0 | 1159.8 | 1254.5 | 8.2 |
| Reli: Usafirishaji Mizigo (Tani '000) | 1300 | 1467 | 1073 | 1012 | 727 | 535 | 583 | 5.2 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000)* | 482760 | 720035.0 | 785938 | 831693 | 843724 | 844135 | 841930 | -0.3 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000)* | 432.6 | 524.3 | 675.7 | 1020.5 | 1222.4 | 1460.4 | 1638.7 | 11.7 |
| Elimu: Wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu* | - | - | - | - | - | - | - | |
| Hospitali: Idadi ya Vitanda | 49074 | 37048 | 37226 | 37220 | 37228 | 40113 | 45241 | 12.8 |
| Madaktari | - | - | 862 | 1180 | 1364 | 1159.8 | 570 | |
| **Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (mil. US$)** | | | | | | | | |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | |
| Kahawa | 49.80 | 74.30 | 61.40 | 88.10 | 103.32 | 111.65 | 117.31 | 6.1 |
| Pamba | 74.60 | 111.50 | 56.80 | 66.40 | 80.87 | 111.15 | 97.79 | -12.0 |
| Katani | 7.20 | 7.30 | 8.10 | 8.40 | 0.00 | 0.00 | 6.31 | |
| Chai | 30.10 | 25.60 | 31.00 | 28.70 | 41.96 | 34.50 | 47.32 | 37.2 |
| Tumbaku | 57.60 | 80.80 | 65.20 | 72.90 | 175.92 | 127.29 | 129.19 | 1.5 |
| Korosho | 68.10 | 46.60 | 39.40 | 13.20 | 69.37 | 71.51 | 125.34 | 75.3 |
| Karafuu | 10.30 | 8.50 | 8.20 | 4.20 | 13.52 | 14.73 | 8.14 | -44.7 |
| **Bidhaa zisizo Asilia** | | | | | | | | |
| Madini | 650.20 | 711.30 | 836.80 | 888.50 | 42.52 | 1114.80 | 1560.10 | 39.9 |
| Bidhaa za Viwanda | 110.10 | 156.10 | 153.90 | 309.20 | 94.19 | 987.0 | 934.0 | -5.4 |
| Bidhaa nyinginezo | 385.10 | 454.40 | 436.30 | 920.70 | 2163.64 | 2163.17 | 2072.40 | -4.2 |

| | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11p | 09/10-10/11 Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Ujazi wa Fedha** | | | | | | | | |
| Ujazi wa Fedha-M3 (Sh. bilioni)² | 2803.0 | 3266.5 | 5317.2 | 6527.8 | 7634.1 | 9061.8 | | |
| Karadha (Sh. bilioni) | 1123.6 | 1504.2 | 2169.5 | 2477.7 | 4771.7 | 6124.1 | | |
| **Fedha za serikali** | | | | | | | | |
| Mapato ya Kawaida ya Serikali (Sh. bilioni) | 1716.3 | 2068.8 | 2739.0 | 3502.6 | 4293.1 | 4651.5 | 6003.6 | 28.8 |
| Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. bilioni) | 2017.5 | 2649.9 | 3137.5 | 3796.9 | 4681.5 | 5562.4 | 6950.6 | 25.0 |
| Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. bilioni) | 1091.6 | 1385.2 | 1337.2 | 2201.1 | 2130.4 | 2611.2 | 3819.1 | 46.3 |

Chanzo: Wizara ya Fedha

* Kwa shule za serikali na binafsi

** Kuanzia 1905 ni kwa bei za mwaka 2001

¹ Kwa mwaka wa masomo unaoishia mwaka unaohusika

² Kwa tafsiri Pana (M3)

\- Takwimu hazikupatikana

## Jedwali Na.B: Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2002 – 2010

| | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PATO LA TAIFA** | | | | | | | | | |
| Ukuaji halisi wa Pato la Taifa | 7.2% | 6.9% | 7.8% | 7.4% | 6.7% | 7.1% | 7.4% | 6.0% | 7.0% |
| Kilimo, Uwindaji na Misitu | 4.9% | 3.1% | 5.9% | 4.3% | 3.8% | 4.0% | 4.6% | 3.2% | 4.2% |
| Uvuvi | 6.8% | 6.0% | 6.7% | 6.0% | 5.0% | 4.5% | 5.0% | 2.7% | 1.5% |
| Viwanda na Ujenzi | 9.4% | 10.9% | 10.9% | 10.4% | 8.5% | 9.5% | 8.6% | 7.0% | 8.2% |
| Viwanda | 7.5% | 9.0% | 9.4% | 9.6% | 8.5% | 8.7% | 9.9% | 8.0% | 7.9% |
| Ujenzi | 11.9% | 13.8% | 13.0% | 10.1% | 9.5% | 9.7% | 10.5% | 7.5% | 10.2% |
| Huduma | 7.7% | 7.8% | 7.8% | 8.0% | 7.8% | 8.1% | 8.5% | 7.2% | 8.2% |
| Biashara na Matengenezo | 8.3% | 9.7% | 5.8% | 6.7% | 9.5% | 9.8% | 10.6% | 7.5% | 8.2% |
| Mawasiliano | 10.4% | 15.6% | 17.4% | 18.8% | 19.2% | 20.1% | 20.5% | 21.9% | 22.1% |
| Fedha | 10.1% | 10.7% | 8.3% | 10.8% | 11.4% | 10.2% | 11.9% | 9.0% | 10.1% |
| Ukuaji wa Pato la taifa kwa bei za mwaka husika | 14.8% | 15.9% | 15.4% | 14.3% | 12.4% | 16.8% | 18.3% | 13.8% | 14.5% |
| **MWENENDO WA BEI** | | | | | | | | | |
| Kasi ya Upandaji Bei ( Wastani wa Mwaka) | 4.5% | 5.3% | 4.7% | 5.0% | 7.3% | 7.0% | 10.3% | 12.1% | 5.5% |
| GDP deflator inflation (market price) | 7.1% | 8.4% | 7.0% | 6.4% | 5.3% | 9.0% | 10.1% | 7.4% | 4.9% |
| Riba za Mikopo ya muda mfupi | 15.9% | 15.6% | 14.2% | 15.7% | 15.7% | 15.0% | 13.6% | 14.0% | 14.4% |
| Riba za Mikopo ya muda mrefu | 13.2% | 12.5% | 12.6% | 14.1% | 14.9% | 16.7% | 16.5% | 14.5% | 14.6% |
| Riba za Amana (miezi 12) | 5.7% | 5.0% | 5.8% | 7.7% | 8.8% | 10.1% | 8.3% | 9.0% | 7.1% |
| Riba za Akiba | 2.7% | 2.5% | 2.6% | 2.6% | 2.6% | 2.7% | 2.7% | 2.8% | 2.4% |
| **FEDHA** | | | | | | | | | |
| Kiwango cha ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 25.6% | 18.0% | 13.5% | 34.8% | 21.5% | 20.5% | 19.8% | 17.7% | 25.4% |
| Kiwango cha ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 21.6% | 17.8% | 14.8% | 33.9% | 16.7% | 27.2% | 24.4% | 20.8% | 21.8% |
| Kiwango cha ukuaji wa Mikopo kwa sekta binafsi | 41.5% | 42.8% | 32.8% | 29.5% | 40.1% | 43.1% | 44.6% | 9.6% | 20.0% |
| **UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | | | |
| Bidhaa zilizouzwa nje | 9.1% | 10.5% | 11.5% | 11.9% | 12.2% | 12.0% | 15.0% | 15.7% | 18.4% |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 17.6% | 18.6% | 20.5% | 20.9% | 22.9% | 23.1% | 24.7% | 24.4% | 27.6% |
| Bidhaa zilizonunuliwa toka nje | 14.0% | 16.6% | 19.3% | 21.2% | 27.1% | 28.8% | 33.8% | 27.3% | 30.4% |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa toka nje | 19.8% | 22.8% | 26.9% | 29.8% | 35.8% | 37.1% | 41.8% | 35.3% | 38.2% |
| Akiba (miezi ya ununuzi toka nje) | 8.8 | 9.3 | 7.7 | 6.0 | 5.0 | 4.8 | 4.3 | 5.6 | 6.3 |
| **UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | | | |
| | 2001/2 | 2002/03 | 2003/04 | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 |
| Mapato | 10.7% | 10.8% | 11.2% | 11.9% | 12.4% | 14.1% | 15.9% | 16.2% | 15.2% |
| Matumizi | 21.9% | 21.8% | 26.6% | 29.4% | 31.9% | 31.7% | 22.8% | 25.7% | 26.9% |
| Matumizi ya kawaida | 18.4% | 18.9% | 20.9% | 22.2% | 24.2% | 24.8% | 14.9% | 17.7% | 18.3% |
| Matumizi ya Maendeleo | 3.5% | 2.9% | 5.7% | 7.2% | 7.7% | 6.9% | 7.9% | 8.0% | 8.6% |
| Nakisi (kabla ya Misaada) | -4.3% | -5.3% | -8.3% | -9.7% | -11.4% | -9.9% | -8.6% | -9.3% | -11.0% |
| Nakisi (baada ya Misaada) | -0.4% | -1.0% | -2.9% | -4.9% | -5.5% | -4.9% | -1.7% | -4.5% | -6.4% |
| Mikopo ya Nje | 1.2% | 1.4% | 3.3% | 3.9% | 3.3% | 3.7% | 3.2% | 3.6% | 4.5% |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu

# SEHEMU YA KWANZA

# MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA

# SURA YA 1

## HALI YA UCHUMI WA TAIFA

### Ukuaji wa Uchumi

1. Katika mwaka 2010, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2009. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa viwango vya ukuaji katika shughuli za kiuchumi zenye mchango mkubwa katika pato la Taifa ikijumuisha kilimo; biashara na matengenezo; na ujenzi. Ukuaji wa viwango vya juu ulijionesha katika shughuli ndogo za kiuchumi za: mawasiliano (asilimia 22.1); ujenzi (asilimia 10.2); umeme na gesi (asilimia 10.2); fedha (asilimia 10.1); na uzalishaji viwandani (asilimia 7.9). Hata hivyo, mwaka 2010 shughuli ndogo za uzalishaji viwandani na uvuvi ndizo pekee zilizokuwa na viwango vidogo vya ukuaji ikilinganishwa na viwango vya ukuaji vya mwaka 2009. Mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma; na viwanda na ujenzi umeendelea kuongezeka katika mwaka 2010 wakati ambapo mchango wa shughuli za kiuchumi za kilimo umeendelea kushuka ikiashiria kuongezeka zaidi kwa shughuli za kiuchumi katika maeneo mengine.

2. Mwaka 2010, Pato la Taifa lilikuwa shilingi 32,293,479 milioni kwa bei za mwaka husika au shilingi 16,828,563 milioni kwa bei za mwaka 2001. Hali kadhalika, kwa mujibu wa kiwango cha ukuaji wa watu cha asilimia 2.9, idadi ya watu Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa watu 41,914,311. Hivyo, pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 770,464.3 mwaka 2010, ikilinganishwa na shilingi 693,185 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 11.1.

3. Kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo kiliongezeka hadi asilimia 4.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2009. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kufuatia kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2009/10; kuimarika kwa miundombinu ya umwagiliaji; jitihada za Serikali za kuongeza ruzuku ya pembejeo za kilimo; na utekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo (ASDP). Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za uzalishaji mazao

kiliongezeka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2009 hadi asilimia 4.4 mwaka 2010. Ongezeko hii lilitokana na kuimarika kwa uzalishaji wa mazao nchini hususan mahindi, uwele, mtama, na mihogo. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za mifugo kiliongezeka kutoka asilimia 2.3 mwaka 2009 hadi asilimia 3.4 mwaka 2010. Sababu zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na upatikanaji wa malisho ya kutosha na kuongezeka kwa huduma za ugani katika shughuli za uendelezaji mifugo. Shughuli ndogo za kiuchumi katika misitu na uwindaji zilikua kwa kiwango cha asilimia 4.1 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2009. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao yatokanayo na misitu na wawindaji wa kitalii.

4. Kiwango cha ukuaji wa Pato lililotokana na shughuli za kilimo, uwindaji na misitu, sehemu ya kuuza, kilikuwa asilimia 5.3 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2009. Kwa upande wa sehemu isiyo ya kuuza, kiwango cha ukuaji kilipungua hadi asilimia 2.0 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2009. Hii inaashiria kuongezeka kwa shughuli za kilimo zinazolenga biashara zaidi kinyume na kilimo cha kijungujiko. Shughuli za kilimo, uwindaji na misitu zilichangia asilimia 24.1 ya Pato la Taifa mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 24.6 mwaka 2009.

5. Shughuli za kiuchumi katika uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 1.5 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2009. Kiwango kidogo cha ukuaji kilitokana na kupungua kwa mahitaji ya samaki na mazao ya samaki nje ya nchi; kupungua kwa uzalishaji wa samaki hasa wa maji baridi uliotokana na uharibifu wa mazingira katika mazalia ya samaki; uvuvi wa kupindukia; vitendo vya uvuvi haramu; na matumizi ya zana duni za uvuvi. Mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa uliendelea kubakia asilimia 1.4 mwaka 2010, sawa na ilivyokuwa mwaka 2009.

6. Shughuli za kiuchumi katika viwanda na ujenzi zilikua kwa asilimia 8.2 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2009. Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na kuimarika kwa sekta ndogo za ujenzi, usambazaji maji, na umeme na gesi. Hata hivyo, kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za kiuchumi za uzalishaji bidhaa viwandani kilipungua kidogo.

Mchango wa shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka kidogo kufikia asilimia 22.4 mwaka 2010, kutoka asilimia 22.0 mwaka 2009.

7. Kiwango cha ukuaji wa uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 7.9 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2009. Kupungua kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji. Hata hivyo, mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 9.0 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 8.6 mwaka 2009.

8. Ukuaji katika shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe uliongezeka kutoka asilimia 1.2 mwaka 2009 hadi asilimia 2.7 mwaka 2010. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uzalishaji wa dhahabu kufuatia kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia, baada ya kuyumba katika kipindi cha mdororo wa uchumi. Mchango wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 3.3 mwaka 2010 kama ilivyokuwa mwaka 2009.

9. Shughuli za kiuchumi katika ujenzi zilikua kwa asilimia 10.2 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2009. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; viwanja vya ndege; na miundombinu ya maji. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.0 mwaka 2010, ukilinganisha na asilimia 7.9 mwaka 2009.

10. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi kilikuwa asilimia 10.2 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2009. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme unaotokana na nguvu za maji; na juhudi za Serikali za kuweka mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi. Shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilichangia asilimia 1.8 katika Pato la Taifa mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2009.

11. Shughuli za kiuchumi za usambazaji maji zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.3 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2009. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali za kuendelea kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji mijini na vijijini na kuongezeka kwa watu waliounganishiwa maji. Mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa uliendelea kubakia asilimia 0.4 tangu mwaka 2003.

12. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikuwa asilimia 8.2 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2009. Viwango vya ukuaji katika shughuli zote ndogo za huduma viliongezeka mwaka 2010 kutokana na kuanza kuimarika kwa shughuli zilizoathiriwa na hali ya mdororo wa uchumi duniani kama vile shughuli ndogo za fedha, hoteli na migahawa, biashara na matengenezo na uchukuzi. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 43.9 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 43.6 mwaka 2009.

13. Shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 8.2 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2009. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji kufuatia kuanza kuimarika kwa uchumi wa Dunia. Shughuli ndogo za biashara na matengenezo zilichangia asilimia 12.1 ya Pato la Taifa mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 11.8 mwaka 2009.

14. Shughuli ndogo za mahoteli na migahawa (ikijumuisha utalii) zilikua kwa asilimia 6.1 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2009. Ukuaji huo ulitokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia na mikakati ya kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Mchango wa shughuli za huduma za mahoteli na migahawa katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.3 mwaka 2010, kama ilivyokuwa mwaka 2009.

15. Shughuli za kiuchumi katika huduma za uchukuzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 6.0 mwaka 2009. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara na maji; na kuongezeka kwa abiria katika safari za anga za ndani na

nje ya nchi. Mchango wa huduma za uchukuzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 5.1 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2009.

16. Huduma za mawasiliano katika mwaka 2010 zilikua kwa kiwango kikubwa zaidi ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji cha shughuli hizi kilikuwa asilimia 22.1 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 21.9 mwaka 2009. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa wateja wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 2.1 mwaka 2010, kama ilivyokuwa mwaka 2009.

17. Huduma za fedha zilikua kwa asilimia 10.1 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2009. Ukuaji huu ulitokana hasa na utekelezaji wa awamu ya pili ya maboresho ya sekta ya fedha; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; kuongezeka kwa mahitaji ya kifedha kwa ajili ya uwekezaji; huduma za bima; na huduma za kibiashara. Mchango wa shughuli za huduma za fedha katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.8 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2009.

18. Ukuaji wa huduma za upangishaji majengo na huduma za biashara ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2009. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za upangishaji wa majengo na huduma za kibiashara sehemu isiyo ya kuuza kilipungua hadi kufikia asilimia 6.1 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2009. Hata hivyo, ukuaji sehemu ya kuuza uliongezeka na kufikia asilimia 7.5 mwaka 2010, kutoka asilimia 5.7 mwaka 2009. Hii ilitokana hasa na utekelezaji wa MKURABITA na kuongezeka kwa shughuli za upangishaji wa majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi. Mchango wa shughuli za huduma za upangishaji majengo na huduma za biashara katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.8 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2009.

19. Katika mwaka 2010, shughuli za utawala zilikua kwa asilimia 6.5, ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2009. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Umma; na kuongezeka kwa ajira mpya katika vyombo vya ulinzi na usalama; na katika mahakama. Mchango wa shughuli za utawala katika Pato la Taifa mwaka 2010

ulipungua kidogo na kuwa asilimia 8.0, ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2009.

20. Viwango vya ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu na afya vilikuwa asilimia 7.3 na 6.9 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 7.1 na 6.7 mwaka 2009, kwa mtiririko huo. Ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu ulitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II);Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II); na kuongezeka kwa ajira mpya za walimu. Kwa upande wa shughuli za huduma za afya, ukuaji ulichangiwa na utekelezaji wa programu za chanjo, malaria, kifua kikuu na VVU/UKIMWI. Michango ya shughuli za huduma za elimu na afya katika Pato la Taifa iliendelea kuwa asilimia 1.4 na 1.6 mwaka 2010 kama ilivyokuwa mwaka 2009, kwa mtiririko huo.

## Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa 2010

### *Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei*

21. Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya marejeo ya fahirisi za bei za taifa kutoka mwaka 2001 hadi 2007 kwa kutumia matokeo ya utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi yaliyofanyiwa uchambuzi yakinifu. Mizania mpya za fahirisi za bei za taifa imetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania mpya zinajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini wakati mizania iliyokuwa inatumika zamani ilijumuisha kaya binafsi za maeneo ya mijini tu. Kizio cha bei za fahirisi za bei za taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### *Makundi ya bidhaa na huduma za jamii*

22. Marejeo ya fahirisi za bei za taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Mfumo huu wa Kimataifa utabadilisha muonekano wa toleo la kawaida la fahirisi za bei za taifa. Makundi 12 ya mfumo mpya yanajumuisha bidhaa na huduma mbalimbali ambazo ni tofauti na ilivyokuwa kwenye mfumo wa zamani. Kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini, makundi hayo pia yamechambuliwa

zaidi na kuunda makundi makuu manne ambayo ni: 1) Vyakula na vinywaji baridi - vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi na huduma zote za jamii isipokuwa nishati na mafuta.

**Jedwali Na. 1.1: Uhusiano wa Fahirisi za bei Mpya na ya Zamani**

| | FAHIRISI MPYA | | FAHIRISI ZA ZAMANI | |
|---|---|---|---|---|
| SNO. | KUNDI (MAIN GROUP) | MIZANIA (WEIGHT) | KUNDI (MAIN GROUP) | MIZANIA (WEIGHT) |
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | Chakula | 55.9 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | Vinywaji na sigara | 6.9 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | Nguo na viatu | 6.4 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | Kodi ya nyumba | 1.4 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | Umeme, mafuta ya taa na Maji | 8.5 |
| 6 | Gharama za afya | 0.9 | Huduma za afya | 2.1 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | Usafiri | 9.7 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | Fenicha na vyombo vya nyumbani | 2.1 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | Michezo na starehe | 0.8 |
| 10 | Elimu | 1.7 | Elimu | 2.6 |
| 11 | Hoteli na migahawa | 6.4 | Huduma mahitaji ya nyumbani | 2.1 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyingine | 4.5 | Bidhaa na huduma nyingine | 1.5 |
| | JUMLA - FAHIRISI BIDHAA ZOTE | 100 | JUMLA - FAHIRISI BIDHAA ZOTE | 100 |
| | | | | |
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | | | 51.0 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | | | 5.7 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | | | 49.0 |
49. Tume za Ushirikiano kati ya Tanzania na nchi marafiki ziliendeleza mahusiano mazuri mwaka 2010. Kutokana na mahusiano hayo mazuri, mkutano wa nne wa Tume ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Algeria ulifanyika Dar es Salaam mwezi wa Juni 2010. Mkutano huo ulikuwa wa manufaa makubwa kwa Tanzania kwani ulipelekea utiwaji wa saini kwa mkataba wa kufuta deni la dola za kimarekani milioni 144.14, deni ambalo Tanzania ilikuwa inadaiwa na Algeria tangu miaka ya 1970 na 1980. Aidha,

mazungumzo juu ya makubaliano ya kutotoza kodi mara mbili (*Avoidance of Double Taxation Agreement*) baina ya nchi hizi mbili bado yanaendelea.

50. Mkutano wa wataalam kati ya Tanzania na Brazil ulifanyika pia mwezi June 2010, ambapo masuala mbalimbali yalizungumziwa ikiwa ni pamoja na kuwapo masharti nafuu ya kulipa deni la Tanzania inalodaiwa na Brazil kiasi cha dola za kimarekani milioni 237.0.

51. Vile vile, ushirikiano mzuri kati ya Tanzania na Msumbiji umefanikisha ujenzi wa daraja la Umoja kati ya nchi mbili hizi, ambapo uzinduzi wake ulifanyika mwezi Mei 2010. Daraji hili la Umoja liko kilomita 300 toka Mtwara mjini. Inatarajiwa daraja hili litaimarisha umoja na ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji, pia litakuwa msaada mkubwa katika kupambana na umaskini kwa kukuza uwekezaji, biashara, utalii, mawasiliano na shughuli nyingine za kiuchumi kwenye maeneo ya mpakani.

**Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)**

52. Mwaka 2010, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ilishiriki kwenye Mkutano wa pamoja wa Uwekezaji kwenye Miundombinu kwa Jumuiya Tatu za Afrika Mashariki (EAC), Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Soko la Pamoja la Nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) mjini Nairobi. Mkutano huu wa pamoja kwa Jumuiya tatu ulikuwa nafasi ya pekee kwa SADC kuonesha maeneo ya uwekezaji ya miundombinu Mashariki na Kusini mwa Afrika kwa Wafadhili, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za fedha za kimataifa na Wawekezaji binafsi kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Kikao hiki kilienda sambamba na Programu ya Uhamasishaji wa Uwekezaji ndani ya SADC ya mwaka 2010 ambapo vipaumbele vilionekana katika miradi ya ukanda wa usafirishaji, usambazaji wa maji na usafi, nishati na mawasiliano.

53. SADC inaendelea kutekeleza programu zake kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na kuharakisha maendeleo. Baadhi ya programu hizo zinahusu kurahisisha taratibu za uhamiaji ili kuruhusu raia wa nchi moja kuingia nchi nyingine. Programu nyingine zinahusu: madawa ya binadamu na udhibiti wa

magonjwa ya kuambukiza; uanzishwaji wa Mfuko wa kupambana na UKIMWI; na uanzisbwaji wa Mfuko wa Maendeleo. Aidha, SADC inatekeleza programu za ushirikiano katika kupambana na fedha haramu, usafiri wa barabara na bandari, uendelezaji utalii, kilimo na usalama wa chakula na maendeleo na jinsia.

**Mpango wa Kujitathimini na Kujipima Afrika Kuhusu Utawala Bora (APRM)**

54. Mwaka 2010, mpango wa tathimini na kujipima hapa nchini uliendelea kutekeleza shughuli zake hasa katika maeneo ya utawala bora, utawala wa sheria, kujenga demokrasia shirikishi na kulinda haki za binadamu hususan makundi yaliyoko pembezoni. Ripoti ya utawala bora iliyoandaliwa mwaka 2009 kuhusu maeneo yaliyotajwa hapo juu iliendelea kuhuishwa ili iendane na mabadiliko na muktadha wa sasa kisiasa, kiuchumi na kijamii, kazi ambayo itakamilika katika mwaka wa fedha 2010/11.

55. Aidha, semina za uhamasishaji juu ya mchakato ziliendelea kufanyika kwa kuwashirikisha wananchi wengi. Takribani semina zaidi ya 320 za ana kwa ana zilifanyika mwaka 2010. Vile vile, vipeperushi vipatavyo 6,600 vilisambazwa na njia nyingine mbalimbali za mawasiliano zilitumika zikihusisha radio, TV na magazeti.

**Mdahalo wa Uchumi Duniani (WEF)**

56. Mwaka 2010, Mdahalo wa Uchumi Duniani ulifanyika mjini Dar es Salaam kwa ajili ya kujadili changamoto zinazolikabili bara la Afrika kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 5 Mei 2010. Mkutano huo ulihusisha wajumbe zaidi ya 1,000 kutoka nchi 85 duniani wakiwemo, Marais, Wakuu wa nchi, mawaziri, wanazuoni, wafanyabiashara, miongoni mwa wajumbe kadhaa. Katika mdahalo huo, mada kuu ilikuwa "Kufikiria Upya Mikakati ya Kukuza Uchumi wa Afrika na Changamoto Zake" baada ya kudhoofishwa na msukosuko wa uchumi duniani. Aidha, mdahalo ulitazama mabadiliko yanayotokea duniani na baadaye kutambulisha fursa zitakazosaidia kukwamua uwezo wa Afrika kukua na mipaka kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

57. Vile vile, mkutano ulijadili changamoto zilizopo kwenye Elimu ya Juu na umuhimu wake kwa maendeleo ya baadaye kiuchumi, ambapo vigezo kama vile kiwango cha chini cha kudahili na upungufu wa wahadhiri vilitazamwa.

# SURA YA 3

# SEKTA YA NJE

## UTANGULIZI

58. Mwaka 2010, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje uliendelea vizuri na ulikuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na mwaka 2009. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 24.1, ikilinganishwa na upungufu wa asilimia 7.7 mwaka 2009. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa bidhaa zisizo asilia hususan, madini ya dhahabu. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 19.0 kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa katika soko la dunia.

## BIDHAA ZILIZOUZWA NJE

59. Thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kutoka dola za Kimarekani 3,294.7 milioni mwaka 2009, hadi dola za Kimarekani 4,296.8 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 30.4. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia iliongezeka hadi Dola za Kimarekani 559.0 mwaka 2010, kutoka Dola za Kimarekani 479.6 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 16.5. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka hadi Dola za Kimarekani 3,177.3 kutoka Dola za Kimarekani 2,376.1 mwaka 2009, sawa ongezeko la asilimia 33.7. Mchango wa mauzo ya bidhaa asilia kwa ya mauzo yote ya bidhaa nje ulikuwa asilimia 13.1, bidhaa zisizo asilia ulikuwa asilimia 73.9 na bidhaa zisizorekodiwa zilikuwa asilimia 13.0. Dhahabu iliendelea kutoa mchango mkubwa katika mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia.

### Bidhaa Asilia

60. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia iliongezeka hadi dola za Kimarekani 559.0 milioni, kutoka dola 479.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 16.6. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa kiasi na bei ya tumbaku na korosho kilichouzwa nje. Mazao hayo yalichangia asilimia 41.6 na asilimia 17.3 ya mauzo ya bidhaa asilia kwa mtiririko huo. Vile

vile, mwaka 2010 wastani wa bei ya kahawa, pamba, chai, tumbaku, korosho na karafuu uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2009. Hata hivyo, thamani ya mauzo ya kahawa, pamba, chai na karafuu ilipungua.

**Kahawa**

61. Thamani ya mauzo ya kahawa nje ilipungua kutoka dola za Kimarekani 111.2 mwaka 2009 hadi dola za Kimarekani 101.7 milioni mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 8.6. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa kiasi cha mauzo ya kahawa nje. Kiasi cha kahawa kilichouzwa nje kilikuwa tani 35,600 ikilinganishwa na tani 56,000 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 36.4. Hata hivyo, wastani wa bei ya kahawa katika soko la dunia mwaka 2010 uliongezeka hadi dola za Kimarekani 2,852.4 kwa tani kutoka dola za Kimarekani 1,984.6 kwa tani mwaka 2009.

**Pamba**

62. Thamani ya mauzo ya pamba nje ilipungua hadi dola za Kimarekani 84.0 milioni mwaka 2010, kutoka dola 111.0 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 24.3. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa kiasi cha pamba kilichouzwa nje kulikotokana na kupungua kwa uzalishaji wa pamba nchini. Hata hivyo, wastani wa bei ya pamba katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 11.2 kutoka dola 1,116.7 kwa tani mwaka 2009, hadi wastani wa dola 1,241.8 kwa tani mwaka 2010.

**Chai**

63. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya chai nje ilipungua hadi dola za Kimarekani 36.4 milioni ikilinganishwa na dola 47.2 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 22.8. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa kiasi cha chai kilichouzwa nje kulikotokana na kupungua kwa uzalishaji wa chai nchini. Kiasi cha mauzo ya chai nje kilipungua hadi tani 18,700, kutoka tani 30,600 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 39.0. Aidha, wastani wa bei ya chai katika soko la dunia uliongezeka kutoka dola 1,538.7 kwa tani mwaka 2009, hadi dola 1, 948.9 kwa tani mwaka 2010.

### Tumbaku

64. Mwaka 2010, tumbaku iliyouzwa nje ilikuwa na thamani ya dola za Kimarekani 232.4 milioni, ikilinganishwa na dola 127.4 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 82.4. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa kiasi cha tumbaku kilichouzwa nje kutoka tani 33,800 mwaka 2009 hadi tani 53,500 mwaka 2010. Aidha, wastani wa bei ya tumbaku katika soko la dunia ulikuwa dola 4,339.3 kwa tani mwaka 2010 ikilinganishwa na dola 3,764.0 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 15.3.

### Korosho

65. Thamani ya mauzo ya korosho nje iliongezeka hadi dola za Kimarekani 96.9 milioni mwaka 2010, kutoka dola 68.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 41.3. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya korosho kutoka tani 95,500 mwaka 2009, hadi tani 125,000 mwaka 2010. Aidha, wastani wa bei ya korosho katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 7.9, kutoka dola 718.2 kwa tani mwaka 2009 hadi dola 775.3 kwa tani mwaka 2010.

### Karafuu

66. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya karafuu ilipungua hadi dola za Kimarekani 7.6 milioni kutoka dola 14.4 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 47.0. Upungufu huu ulichangiwa na kupungua kwa kiasi cha mauzo nje kutoka tani 4,800 mwaka 2009, hadi tani 2,200 mwaka 2010. Hata hivyo, wastani wa bei ya karafuu katika soko la dunia uliongezeka kutoka dola 2,977.9 milioni kwa tani mwaka 2009, hadi dola 3,449.6 milioni kwa tani mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 15.8.

### Bidhaa Zisizo Asilia

67. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka hadi dola za Kimarekani 3,177.8 milioni mwaka 2010, kutoka dola 2,376.2 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 33.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za madini hasa dhahabu. Mauzo ya bidhaa zisizo asilia yalichangia asilimia 73.9 ya mauzo yote ya bidhaa nje ikilinganishwa na asilimia 72.1 mwaka 2009. Kuongezeka kwa thamani ya

mauzo ya bidhaa zisizo asilia kulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani (asilimia 90.3), bidhaa za madini (asilimia 22.7) na bidhaa nyinginezo (asilimia 20.5).

## Madini

68. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya madini iliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,560.2 milioni kutoka dola 1,271.4 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 22.7. Dhahabu peke yake ilichangia asilimia 97.2 ya mauzo yote ya madini nje. Thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kutoka dola za Kimarekani 1,229.5 milioni mwaka 2009, hadi dola 1,516.6 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 23.4. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya dhahabu nje na bei ya dhahabu katika soko la dunia. Hata hivyo, mauzo ya almasi yalipungua hadi dola 10.1 milioni mwaka 2010 ikilinganishwa na dola 15.5 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 34.8. Aidha, dhahabu ilichangia asilimia 47.7 ya bidhaa zisizo asilia.

## Bidhaa za Viwandani

69. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka hadi dola za Kimarekani 963.9 milioni, kutoka dola 506.5 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 90.3. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani kulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zitokanazo na pamba na tumbaku. Hata hivyo, mauzo ya bidhaa zitokanazo na mkonge yalipungua kutokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa hiyo duniani. Mauzo ya bidhaa za viwandani yalichangia asilimia 30.3 ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia kwa mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 21.3 mwaka 2009.

## Samaki na Mazao ya Samaki

70. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya samaki na mazao ya samaki ilipungua hadi dola za Kimarekani 141.0 milioni, kutoka dola 155.0 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 9.0. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa mahitaji ya samaki na mazao ya samaki katika soko la nje.

### Mazao ya Mboga na Maua

71. Thamani ya mauzo ya mazao ya mboga na maua ilipungua kwa asilimia 6.6, kutoka dola za Kimarekani 33.3 milioni mwaka 2009, hadi dola 31.1 milioni mwaka 2010.

### Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje

72. Thamani ya mauzo ya bidhaa nyinginezo iliongezeka hadi dola za Kimarekani 349.1 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na dola 289.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa zilizouzwa tena ilikuwa dola 132.5 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na dola 120.4 milioni mwaka 2009. Vilevile, mauzo ya bidhaa ambazo hazikurekodiwa yalikuwa na thamani ya dola 560.4 milioni mwaka 2010.

Jedwali Na.3.1: THAMANI, KIASI NA BEI YA BIDHAA ZILIZOUZWA NJE (2006-2010)

| Bidhaa | 2006 | 2007 | 2008 | 2009r | 2010p | 2009-2010 (Badiliko) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | |
| Kahawa | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 61.4 | 98.1 | 99.1 | 111.2 | 101.7 | -8.6 |
| Kiasi ('000 tani) | 31.5 | 45.0 | 44.2 | 56.1 | 35.6 | -36.4 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,953.1 | 2,177.6 | 2,203.4 | 1,984.6 | 2,852.4 | 43.7 |
| Pamba | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 55.8 | 66.4 | 115.0 | 111.0 | 84.0 | -24.3 |
| Kiasi ('000 tani) | 55.0 | 59.1 | 91.4 | 99.4 | 67.6 | -32.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,014.2 | 1,123.8 | 1,257.8 | 1,116.7 | 1,241.8 | 11.2 |
| Katani | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 6.1 | 8.8 | 3.3 | - | - | - |
| Kiasi ('000 tani) | 8.0 | 9.5 | 2.7 | - | - | - |
| Bei (US$ kwa tani) | 766.7 | 928.4 | 1,251.4 | - | - | - |
| Chai | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 31.0 | 28.7 | 40.8 | 47.2 | 36.4 | -22.8 |
| Kiasi ('000 tani) | 22.4 | 21.5 | 28.1 | 30.6 | 18.7 | -389.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,384.9 | 1,334.8 | 1,511.2 | 1,538.7 | 1,948.9 | 26.7 |
| Tumbaku | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 65.2 | 87.8 | 176.4 | 127.4 | 232.4 | 82.4 |
| Kiasi ('000 tani) | 25.0 | 37.9 | 35.6 | 33.8 | 53.5 | 58.2 |
| Bei (US$ kwa tani) | 2,611.4 | 2,291.5 | 3,041.2 | 3,764.0 | 4,339.3 | 15.3 |
| Korosho | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 39.4 | 25.6 | 40.2 | 68.6 | 96.9 | 41.3 |
| Kiasi ('000 tani) | 66.3 | 41.3 | 55.0 | 95.5 | 125.0 | 30.9 |
| Bei (US$ kwa tani) | 594.4 | 621.1 | 730.1 | 718.2 | 775.3 | 7.9 |
| Karafuu | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 8.2 | 4.2 | 13.5 | 14.4 | 7.6 | -47.0 |
| Kiasi ('000 tani) | 2.4 | 1.4 | 3.8 | 4.8 | 2.2 | -54.3 |
| Bei (US$ kwa tani) | 3,346.2 | 2,968.3 | 3577.5 | 2,977.9 | 3,449.6 | 15.8 |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **267.1** | **319.7** | **507.3** | **479.8** | **559.0** | **16.5** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia** | | | | | | |
| **Madini** | **836.8** | **848.7** | **1,186.7** | **1,271.4** | **1,560.2** | **22.7** |
| Dhahabu | 786.4 | 788.2 | 1108.3 | 1,229.5 | 1,516.6 | 23.4 |
| Almasi | 22.2 | 26.0 | 20.3 | 15.5 | 10.1 | -34.8 |
| Madini mengine | 28.3 | 34.4 | 58.1 | 26.4 | 33.5 | 26.9 |
| **Bidhaa za Viwandani** | **195.8** | **309.8** | **741.8** | **506.5** | **963.9** | **90.3** |
| **Samaki na Mazao ya Samaki** | **145.9** | **163.6** | **184.7** | **155.0** | **141.0** | **-9.0** |
| **Mazao ya mbogo na Maua** | **15.4** | **19.1** | **45.7** | **33.3** | **31.1** | **-6.6** |
| **Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)** | **128.3** | **149.7** | **160.3** | **120.4** | **132.5** | **10.0** |
| **Bidhaa nyinginezo** | **154.0** | **213.7** | **285.5** | **289.6** | **349.1** | **20.5** |
| **Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)** | **1,476.2** | **1704.5** | **2604.7** | **2,376.1** | **3,177.3** | **33.7** |
| **Bidhaa zisizorekodiwa** | **174.3** | **202.4** | **347.8** | **438.9** | **560.4** | **27.7** |
| **JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)** | **1917.6** | **2226.6** | **3459.8** | **3,294.9** | **4,297.1** | **30.4** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha

\- Takwimu Hazikupatikana

### Mapato ya Huduma

73. Mwaka 2010, mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka hadi dola za Kimarekani 2,091.5 milioni kutoka dola 1,854.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 12.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na usafirishaji na utalii. Mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji yaliongezeka kwa asilimia 33.2 kutoka dola 334.4 milioni mwaka 2009, hadi dola 445.5 milioni mwaka 2010. Vilevile, mapato yatokanayo na huduma za utalii yaliongezeka kwa asilimia 8.2 kutoka dola 1,159.8 milioni mwaka 2009, hadi dola 1,254.5 milioni mwaka 2010. Aidha, mapato yatokanayo na huduma nyingine zinazojumuisha huduma za kisheria, uhasibu, ushauri wa kitaalam na tafiti yaliongezeka kwa asilimia 8.6, kutoka dola 360.4 milioni mwaka 2009, hadi dola 391.5 mwaka 2010. Hata hivyo, mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano yalipungua kwa asilimia 19.6 mwaka 2010.

## BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE

74. Mwaka 2010, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje (f.o.b) iliongezeka hadi dola za Kimarekani 7,125.1 milioni kutoka dola 5,834.1 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 22.1, ikilinganishwa na upungufu wa asilimia 16.8 mwaka 2009. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za bidhaa za kati hususan, mafuta na malighafi za viwandani.

### Bidhaa za Kukuza Mitaji

75. Mwaka 2010, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoagizwa nje iliongezeka hadi dola za Kimarekani 2,715.2 milioni kutoka dola 2,539.2 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa vifaa vya usafirishaji na ujenzi. Uagizaji wa vifaa vya usafirishaji uliongezeka kwa asilimia 20.4, kutoka dola 748.5 milioni mwaka 2009, hadi kufikia dola 901.1 mwaka 2010. Uagizaji wa vifaa vya ujenzi uliongezeka kwa asilimia 9.4, kutoka dola 558.2 milioni mwaka 2009 hadi dola 610.6 milioni mwaka 2010. Hata hivyo, thamani ya uagizaji wa mitambo ilipungua hadi dola za Kimarekani 1,203.4 milioni mwaka

2010 kutoka dola 1,232.5 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 2.4.

**Bidhaa za Kati**

76. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati iliongezeka kutoka dola za Kimarekani 1,890.3 milioni mwaka 2009, hadi dola 2,700.8 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 42.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa thamani ya uagizaji wa mafuta na malighafi za viwandani. Thamani ya uagizaji wa mafuta ilikuwa dola za Kimarekani 1,983.8 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na dola 1,323.0 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 49.9. Ongezeko la uagizaji wa mafuta lilitokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na kuongezeka kwa kiasi cha mafuta yaliyoagizwa. Aidha, thamani ya uagizaji wa malighafi za viwanda iliongezeka hadi dola za Kimarekani 602.0 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na dola 472.1 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 27.5. Vilevile, uagizaji wa mbolea uliongezeka kwa asilimia 20.8, ikilinganishwa na upungufu wa asilimia 36.7 mwaka 2009.

**Bidhaa za Matumizi ya Kawaida**

77. Mwaka 2010, uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida uliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,709.2 milioni kutoka dola 1,404.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 21.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za chakula na bidhaa nyinginezo za matumizi ya kawaida. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za chakula ilifikia dola za Kimarekani 461.6 milioni mwaka 2010, kutoka dola 343.3 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 34.5. Kuongezeka kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa za chakula kulitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa nafaka hasa ngano. Vile vile, uagizaji wa bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida zikiwemo dawa, bidhaa za plastiki, na bidhaa za makaratasi, uliongezeka kwa asilimia 17.5 kutoka dola 1,061.3 milioni mwaka 2009, hadi dola 1,247.5 milioni mwaka 2010.

## MALIPO YA HUDUMA

78. Mwaka 2010, malipo ya huduma yaliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,849.6 milioni, kutoka dola 1,709.1 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Hii ilitokana na kupanda kwa gharama za malipo ya huduma za usafirishaji. Thamani ya gharama za usafirishaji iliongezeka kutoka dola 604.9 milioni mwaka 2009 hadi dola 716.1 milioni 2010, sawa na ongezeko la asilimia 18.4.

## MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI MBALIMBALI

79. Tanzania iliendelea kuwa na mahusiano mazuri ya kibiashara na nchi mbalimbali duniani zikiwemo nchi za Bara la Ulaya, Amerika, Asia na Afrika. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Bara la Ulaya iliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,151.1 milioni, kutoka dola 909.0 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 26.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo kwa nchi ya Uswisi na nchi za Jumuiya ya Ulaya. Thamani ya mauzo kwa nchi ya Uswisi iliongezeka kwa asilimia 46.7 kufikia dola 685.9 milioni mwaka 2010 na mauzo kwa nchi za Jumuiya ya Ulaya yaliongezeka kwa asilimia 5.5, kufikia dola 464.0 milioni mwaka 2010. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Bara hilo iliongezeka kutoka dola 1,222.1 milioni mwaka 2009, hadi dola 1,669.8 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 36.6. Aidha, urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za Bara la Ulaya ulikuwa na nakisi ya dola 518.7 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na nakisi ya dola 313.1 milioni mwaka 2009.

80. Thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliongezeka kwa asilimia 70.6 kutoka dola za Kimarekani 263.8 milioni mwaka 2009, hadi dola 450.0 milioni mwaka 2010. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo zaidi kwenda nchi ya Kenya. Thamani ya mauzo kwa nchi ya Kenya iliongezeka kwa asilimia 67.6 kufikia dola 297.3 milioni mwaka 2010. Aidha, mauzo ya bidhaa kwa nchi ya Kenya yalichangia asilimia 66.1, Rwanda asilimia 12.2, Burundi asilimia 11.3 na Uganda ilichangia asilimia 10.4, ya mauzo yote kwa Jumuiya. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi

za Afrika ya Mashariki ilipungua hadi dola za Kimarekani 285.2 milioni mwaka 2010 kutoka dola 310.5 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 8.2. Urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ulikuwa na ziada ya dola 164.8 milioni mwaka 2010 ikilinganishwa na nakisi ya dola 46.7 milioni mwaka 2009.

81. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) iliongezeka kwa asilimia 67.0 hadi dola za Kimarekani 625.1 milioni kutoka dola 374.2 milioni mwaka 2009. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi ya Afrika ya Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kati ya mauzo hayo, asilimia 66.7 yalikwenda nchi ya Afrika ya Kusini na asilimia 21.9 yalikwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za SADC iliongezeka kwa asilimia 12.9, hadi dola 827.7 milioni mwaka 2010, kutoka dola 733.2 milioni mwaka 2009. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Afrika ya Kusini, Swaziland, Zambia na Msumbiji. Urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za SADC ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 202.6 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na nakisi ya dola 417.8 milioni mwaka 2009.

82. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi zote za Afrika iliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,080.9 milioni, kutoka dola 638.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 69.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi za Afrika ya Kusini, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka Afrika iliongezeka kwa asilimia 6.6, kutoka dola za Kimarekani 1,044.0 milioni mwaka 2009, hadi dola 1,112.9 milioni mwaka 2010. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Afrika ya Kusini na Kenya. Urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi zote za Afrika ulikuwa na nakisi ya dola 32.0 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na nakisi ya dola 464.2 milioni mwaka 2009.

83. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia zikiwemo China, Japan, India, Hong Kong na Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 29.0, hadi dola za Kimarekani 1,200.2 milioni kutoka dola 930.3 milioni mwaka 2009. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi za China, India na Japan. Vilevile, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Bara hilo iliongezeka hadi dola 4,158.1 milioni mwaka 2010, kutoka dola 3,282.5 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 26.7. Urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za Bara la Asia ulikuwa na nakisi ya dola 2,957.9 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na nakisi ya dola 2,352.2 milioni mwaka 2009.

84. Mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda Bara la Amerika iliongezeka hadi dola za Kimarekani 51.0 milioni, kutoka dola 45.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 12.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa kwenda Marekani. Thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka Bara hilo ilipungua kwa asilimia 1.4, hadi dola za Kimarekani 259.0 milioni mwaka 2010, kutoka dola 262.7 milioni mwaka 2009. Aidha, urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za Bara la Amerika ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 208.0 milioni mwaka 2010, ikilinganishwa na nakisi ya dola 217.1 milioni mwaka 2009.

**Jedwali Na. 3.2: Urari wa Biashara ya Bidhaa Kati ya Tanzania na Jumuiya Mbalimbali za Ushirikiano Kikanda (Dola milioni)**

| Jumuiya/ Mwaka | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009r | 2010p |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bara la Ulaya | (210.5) | 176.7 | 3.9 | (77.8) | (515.2) | (567.0) | (313.1) | (518.7) |
| Jumuiya ya nchi za SADC | (233.7) | 213.4 | (103.2) | (284.8) | (355.4) | (510.2) | (417.8) | (202.6) |
| Jumuiya ya Afrika Mashariki | (35.6) | (42.3) | (64.0) | (56.7) | 66.5 | 110.7 | (46.7) | 164.8 |
| Bara la Asia | - | - | - | - | (1,582.0) | (2,212.8) | (2,352.2) | (2,957.9) |
| Bara la Amerika | - | - | - | (174) | (291.5) | (313.7) | (217.1) | (208.0) |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha, r = iliyorekebishwa
p = ya muda

Jedwali Na. 3.3: Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje (Dola Milioni)

| JUMUIYA/NCHI | 2005 | 2006 | 2007 | 2008r | 2009r | 2010p | 2009/10 (Badiliko) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA | 359.7 | 334.1 | 340.7 | 461.9 | 440 | 464 | 5.5% |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 259.9 | 421.6 | 454.2 | 533.3 | 469 | 687.1 | 46.5% |
| JUMLA - BARA LA ULAYA | 619.6 | 755.7 | 800.9 | 995.2 | 909 | 1151.1 | 26.6% |
| JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC) | | | | | | | |
| Afrika ya kusini | 275.4 | 268.9 | 176.1 | 232.5 | 170.9 | 416.8 | 143.9% |
| Zambia | 8.7 | 18.5 | 22.4 | 36.6 | 44.3 | 53.5 | 20.8% |
| Swaziland | 0.6 | 1.9 | 0.2 | 0.6 | 20.8 | 0 | |
| Zimbabwe | 1.6 | 1.2 | 0.7 | 1.2 | 5.7 | 0 | |
| Msumbiji | 6.5 | 10.6 | 19.1 | 31.4 | 20.3 | 17.7 | -12.8% |
| Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo | 12.6 | 18.3 | 58.9 | 124 | 79.9 | 137.1 | 71.6% |
| Nchi nyingine za SADC | 16.9 | 21.7 | 23.7 | 17.8 | 32.3 | 0 | |
| JUMLA-SADC | 322.3 | 341.1 | 301.1 | 443.4 | 374.2 | 625.1 | 67.0% |
| JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC) | | | | | | | |
| Burundi | 0 | 0 | 41.5 | 19.5 | 23.6 | 51 | 116.1% |
| Kenya | 76.3 | 97.2 | 101.1 | 235 | 177.4 | 297.3 | 67.6% |
| Rwanda | 0 | 0 | 11.2 | 20.6 | 15.1 | 55 | 264.2 % |
| Uganda | 20.1 | 20.5 | 19.3 | 40.5 | 47.7 | 46.8 | -1.9% |
| JUMLA – EAC | 96.4 | 117.7 | 173.1 | 315.5 | 263.8 | 450 | 70.6% |
| Nchi nyingine za Afrika | 34.7 | 29.9 | 72.8 | 96.1 | 0.6 | 5.8 | 866.7% |
| JUMLA –AFRIKA | 453.4 | 488.7 | 547.0 | 855.0 | 638.6 | 1080.9 | 69.3% |
| BARA LA AMERIKA | | | | | | | |
| Marekani | 16.5 | 20.7 | 34.2 | 55.1 | 39.5 | 46.5 | 17.7% |
| Canada | 39.2 | 6 | 2.3 | 3.8 | 6.1 | 4.6 | -24.6% |
| Nchi nyingine za Bara la Amerika | 3.7 | 1.1 | 6 | 5.4 | 0 | 0 | |
| JUMLA-BARA LA AMERIKA | 59.4 | 27.8 | 42.5 | 64.3 | 45.6 | 51.1 | 12.1% |
| ASIA | | | | | | | |
| China | 0 | 0 | 141.3 | 223.5 | 363.9 | 634.2 | 74.3% |
| India | 63.2 | 63.8 | 77.3 | 171.8 | 183.8 | 218.5 | 18.9% |
| Japan | 68.7 | 82 | 57.1 | 136.9 | 164.7 | 209.7 | 27.3% |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 33.7 | 47.3 | 88.4 | 65.4 | 66.8 | 55.3 | -17.2% |
| Hong Kong | 9.6 | 7.6 | 14.1 | 13.4 | 85.6 | 12.6 | -85.3% |
| Singapore | 18.7 | 4.4 | 4.0 | 11.0 | 6.4 | 13.5 | 110.9% |
| Nchi nyingine za Asia | 133.8 | 123.1 | 65.1 | 52.4 | 59.1 | 56.4 | -4.6% |
| JUMLA- ASIA | 327.7 | 328.2 | 447.3 | 674.4 | 930.3 | 1200.2 | 29.0% |
| NCHI NYINGINEZO | 242.4 | 317.2 | 388.9 | 989.9 | 771.1 | 813.4 | 5.5% |
| JUMLA KUU | 1,702.50 | 1,917.60 | 2,226.60 | 3,578.80 | 3,294.60 | 4,296.70 | 30.4% |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha

r = iliyorekebishwaa

p = ya muda

Jedwali Na. 3.4: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa Nje (USD Milioni)

| JUMUIYA/NCHI | 2006 | 2007 | 2008r | 2009r | 2010p | 2009/10 (Badiliko) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 744.4 | 1,061.60 | 1,280.80 | 1,076.60 | 1,111.40 | 3.2% |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 74.7 | 181.7 | 153.8 | 145.5 | 558.4 | 283.8% |
| JUMLA - BARA LA ULAYA | 819.1 | 1,243.3 | 1,434.6 | 1,222.1 | 1,669.8 | 36.6% |
| AFRIKA | | | | | | |
| JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC) | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 569.6 | 585.8 | 791 | 672.8 | 745.3 | 10.8% |
| Zimbabwe | 1.3 | 1.8 | 27.6 | 0.6 | 1.1 | 83.3% |
| Zambia | 11.6 | 18.5 | 27.0 | 23.3 | 29.8 | 27.9% |
| Msumbiji | 17.2 | 16.9 | 18.2 | 9 | 18.5 | 105.6% |
| Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo | 0.2 | 0.6 | 19.6 | 1.2 | 1.1 | -8.3% |
| Swaziland | 16.8 | 20.1 | 76.5 | 26.3 | 31.7 | 20.5% |
| Nchi nyingine za SADC | 9.2 | 12.4 | 19.2 | 0 | 0 | |
| JUMLA -SADC | 625.9 | 656.1 | 979.7 | 733.2 | 827.7 | 12.9% |
| JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC) | | | | | | |
| Burundi | 0 | 0.02 | 0.4 | 0.3 | 0.6 | 100.0% |
| Kenya | 169.1 | 100.1 | 197.9 | 298.3 | 265.9 | -10.9% |
| Rwanda | 0 | 0.01 | 0.1 | 0.02 | 1.4 | 6900.0% |
| Uganda | 5.3 | 6.4 | 6.4 | 11.9 | 17.3 | 45.4% |
| JUMLA -EAC | 174.4 | 106.5 | 204.8 | 310.5 | 285.2 | -8.2% |
| Nchi nyingine za Afrika | 62.9 | 60.2 | 71.9 | 0.3 | 0.03 | -90.0% |
| JUMLA NCHI ZOTE ZA AFRIKA | 863.2 | 822.8 | 1,256.4 | 1,044.0 | 1,112.9 | 6.6% |
| BARA LA AMERIKA | | | | | | |
| Marekani | 123.3 | 187.1 | 200.4 | 136 | 150.6 | 10.7% |
| Canada | 37.3 | 35.6 | 57.1 | 35.2 | 36.4 | 3.4% |
| Nchi nyingine za Bara la Amerika | 41.2 | 111.2 | 120.3 | 91.4 | 72 | -21.2% |
| JUMLA - BARA LA AMERIKA | 201.8 | 333.9 | 377.8 | 262.6 | 259.0 | -1.4% |
| ASIA | | | | | | |
| Japan | 257.5 | 261.8 | 711.8 | 413.6 | 548.8 | 32.7% |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 500.6 | 773.6 | 839.7 | 618.8 | 649.3 | 4.9% |
| China | 309.4 | 406 | 711.8 | 678.1 | 846.8 | 24.9% |
| India | 241.3 | 507 | 891.2 | 757.3 | 864.6 | 14.2% |
| Hong Kong | 0 | 11.8 | 18.1 | 30.7 | 23.3 | -24.1% |
| Singapore | 13.2 | 25.3 | 433 | 188.2 | 429.3 | 128.1% |
| Nchi nyingine za Asia | 653.3 | 475.1 | 398.4 | 595.8 | 721.3 | 21.1% |
| JUMLA - ASIA | 1,975.3 | 2,480.6 | 4,024.0 | 3,282.5 | 4,083.4 | 24.4% |
| NCHI NYINGINEZO | 4.7 | 0 | 80.5 | 22.9 | 0 | |
| JUMLA KUU | 3,864.1 | 4,860.6 | 7,012.3 | 5,834.1 | 7,125.3 | 22.1% |

**Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania**

p = ya muda

r = iliyorekebishwa

## MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

### Urari wa Biashara ya Bidhaa

85. Urari wa biashara ya bidhaa kwa mwaka 2010 ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 2,828.3 milioni ikilinganishwa na nakisi ya dola 2,539.3 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 13.4. Kuongezeka kwa nakisi kulitokana na kuongezeka kwa kasi ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje dhidi ya kasi ya uongezekaji wa mauzo ya bidhaa nje.

### Urari wa Biashara ya Huduma

86. Mwaka 2010, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani 242.0 milioni ikilinganishwa na ziada ya dola 145.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 66.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na biashara ya usafirishaji na utalii kufuatia kuimarika kwa uchumi wa dunia.

### Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi

87. Mwaka 2010, urari wa mapato ya vitega uchumi yanayojumuisha fidia kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba uliongezeka kwa asilimia 27.6 hadi nakisi ya dola za Kimarekani 90.9 milioni kutoka nakisi ya dola za Marekani 71.2 milioni mwaka 2009. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya fidia kwa wafanyakazi wasio wakazi wa Tanzania.

### Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida

88. Urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani 823.9 milioni mwaka 2010 ikilinganishwa na ziada ya dola 696.9 mwaka 2009. Ongezeko hili lilisababishwa na kuongezeka kwa misaada ya nchi wahisani kwa Serikali toka dola za Kimarekani 658.4 milioni mwaka 2009 mpaka dola 798.1 milioni.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

89. Mwaka 2010, urari wa malipo ya kawaida, unaojumuisha urari wa biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi, na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 2,677.2 milioni kutoka nakisi ya dola 2,465.2 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 8.6. Kuongezeka kwa nakisi kulitokana na kuongezeka kwa kasi ya uagizaji wa bidhaa nje.

**Urari wa Uhamisho wa Mitaji**

90. Mwaka 2010, urari wa uhamisho wa mitaji, unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani, uliongezeka kwa asilimia 25.1 na kufikia ziada ya dola za Kimarekani 616.5 milioni ikilinganishwa na ziada ya dola 492.8 mwaka 2009. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa misaada ya vitega uchumi kwa Serikali.

**Urari wa Malipo ya Fedha katika Uwekezaji**

91. Urari wa malipo ya fedha unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani 1,587.8 milioni mwaka 2010 ikilinganishwa na ziada ya dola 1,328.2 milioni mwaka 2009. Ongezeko hili lilitokana na kupungua kwa rasilimali za kigeni zinazomilikiwa na benki za biashara nchini kutoka rasilimali zenye thamani ya dola za Kimarekani 333.8 milioni mwaka 2009 hadi rasilimali zenye thamani ya dola 75.2 milioni mwaka 2010.

**Urari wa Malipo Yote**

92. Mwaka 2010, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola 369.8 milioni ikilinganishwa na ziada ya dola 366.2 milioni mwaka 2009.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

93. Mwaka 2010, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka hadi kufikia dola za Kimarekani 3,948.0 milioni, kutoka dola 3,552.5 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Hata hivyo, kiasi hiki kilikuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi 5.3 tu ikilinganishwa na miezi 5.7 iliyofikiwa mwaka 2009.

**Thamani ya Fedha ya Tanzania**

94. Mwaka 2010, thamani ya Shilingi ya Tanzania ilikuwa na wastani wa shilingi 1,432.3 kwa dola moja ya Kimarekani ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,320.0 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 8.5. Hata hivyo, upungufu huu ni mdogo ukilinganisha na mwaka 2009 ambapo thamani ya shilingi ilishuka kwa asilimia 10.4. Kushuka kwa thamani ya shilingi kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya dola nchini pamoja na kuimarika kwa dola ya Kimarekani dhidi ya sarafu za mataifa mengine. Aidha, bei ya dola moja ya Kimarekani ilikuwa na thamani ya shilingi 1,453.5 mwishoni mwa Desemba 2010 ikilinganishwa na shilingi 1,313.3 mwishoni mwa Desemba 2009.

## THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na.17 — Sh. Milioni

| Aina ya Bidhaa | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje | 926,892 | 1,267,322 | 1,582,111 | 1,874,265 | 2,156,732 | 2,628,866 | 3,194,929 | 3,671,935 | 5604496 |
| Bidhaa Halisi | 853,158 | 1,178,027 | 1,437,423 | 1,726,241 | 1,967,358 | 2,413,809 | 2,992,530 | 3,568,071 | 3921648 |
| Zilizouzwa Tena | 73,734 | 89,295 | 144,688 | 148,024 | 189,374 | 215,057 | 202,399 | 103,864 | 128913 |
| Zilizoagizwa | 1,615,037 | 2,277,176 | 2,758,953 | 3,659,962 | 5,534,418 | 7,296,763 | 8,839,274 | 8,446,721 | 11086891 |
| Jumla | 2,541,929 | 3,544,498 | 4,341,064 | 5,534,227 | 7,691,150 | 9,925,629 | 12,034,203 | 12,118,656 | 16691387 |
| Urari | -688,145 | -1,009,854 | -1,176,842 | -1,785,697 | -3,377,686 | -4,667,897 | -5,644,345 | (4,774,785) | -5482395 |
| Thamani ya Fedha (Shs/US$) | 966.7 | 1038.4 | 1,089.4 | 1,122.7 | 1,251.9 | 1,232.8 | 1,196.3 | 1,320 | 1409.3 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

## KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 18

| Bidhaa | Kiasi (Tani) 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 38,822 | 53,685 | 46,229 | 56,079 | 35,359 | -37% |
| Pamba | 46,467 | 40,743 | 54,089 | 100,361 | 74,859 | -25% |
| Katani | 9,964 | 7,101 | 13,786 | 8,198 | 9,041 | 10% |
| Chai | 24,803 | 30,506 | 26,654 | 19,191 | 44,254 | 131% |
| Tumbaku | 37,325 | 40,743 | 45,284 | 33,839 | 69,095 | 104% |
| Korosho | 99,160 | 14,841 | 60,468 | 99,313 | 132,675 | 34% |
| Karafuu | 3,033 | 3,200 | 3,605 | 4,853 | 2,566 | -47% |
| Almasi (Carat) | 201,782 | 149,592 | 132,477 | 158,838 | 367,649 | 132% |
| Dhahabu (gms) | 44,449,460 | 67,334,000 | 32,319,880 | 34,600,000 | 33,560,000 | -3% |

| Bidhaa | Thamani (Sh. Milioni) 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 92794 | 143255 | 122162 | 147427 | 162310 | 10% |
| Pamba | 56780 | 49807 | 98613 | 146752 | 133087 | 9% |
| Katani | 9296 | 7438 | 13046 | 28190 | 11774 | -58% |
| Chai | 41682 | 48258 | 49615 | 45552 | 65479 | 44% |
| Tumbaku | 129108 | 118893 | 208004 | 168057 | 178748 | 6% |
| Korosho | 62663 | 33816 | 82025 | 94413 | 173572 | 84% |
| Karafuu | 9964 | 10628 | 15891 | 19453 | 11266 | -42% |
| Almasi (Carat) | 28023 | 23381 | 20891 | 24988 | 12410 | -50% |
| Dhahabu (gms) | 968026 | 672111 | 1115163 | 1420756 | 1335700 | 6% |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mapato Tanzania

## KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 19

| Bidhaa | Kiasi (Tani) | | | | | | | | Thamani (Mil.US$) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko(%) 2009/10 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko(%) 2009/10 |
| Bidhaa Asilia: | | | | | | | | | | | | | | |
| Kahawa | 38528 | 46100 | 38,832 | 53685 | 44,246 | 56,079 | 35,359 | (37) | 61.4 | 98.1 | 99.1 | 111.2 | 101.7 | -8.5 |
| Pamba | 47334 | 112900 | 46467 | 43743 | 86995 | 100,361 | 74,853 | (25) | 56.8 | 66.4 | 115.8 | 111.0 | 84.0 | 24.3 |
| Katani | 11933 | 9300 | 9.984 | 7.101 | 2,659 | 8,198 | 9,041 | 10 | 6.1 | 8.8 | 15.7 | - | - | - |
| Chai | 21716 | 21800 | 24803 | 30,506 | 25,898 | 19,191 | 44,254 | 131 | 31.0 | 28.7 | 42.5 | 47.2 | 36.4 | 22.9 |
| Tumbaku | 29198 | 31109 | 37,525 | 40,743 | 35,567 | 33,839 | 69,095 | 104 | 65.2 | 87.8 | 176.4 | 127.4 | 232.4 | 82.4 |
| Korosho | 83192 | 62000 | 59,180 | 14,841 | 55,011 | 99,313 | 132,675 | 34 | 39.4 | 25.6 | 44.3 | 68.6 | 96.9 | 41.3 |
| Karafuu | 4353 | 3000 | 3,033 | 3,200 | 3774 | 4,863 | 2566 | (47) | 8.2 | 4.2 | 13.5 | 14.4 | 7.6 | -47.2 |
| Jumla | | | | | | | | | 267.1 | 319.6 | 507.3 | 479.8 | 559.0 | 16.5 |
| Bidhaa zisizo asilia: | | | | | | | | | | | | | | |
| Bidhaa za Petroli | | | | | | | | | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | |
| Madini | | | | | | | | | 886.8 | 848.7 | 1108.7 | 1271.4 | 1560.2 | 22.7 |
| Bidhaa za Viwandani | | | | | | | | | 195.8 | 309.8 | 741.8 | 506.5 | 963.9 | 90.3 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | | | | | | | | | 145.9 | 163.6 | 184.7 | 155.0 | 141.0 | 9.0 |
| Mazao ya Mboga na Maua | | | | | | | | | 15.4 | 19.1 | 45.7 | 33.3 | 31.1 | -6.6 |
| Bidhaa zilizouzwa tena | | | | | | | | | 128.3 | 149.7 | 160.3 | 120.4 | 132.5 | 10.0 |
| Bidhaa nyinginezo | | | | | | | | | 154.0 | 213.7 | 285.5 | 289.6 | 349.1 | 20.5 |
| Jumla | | | | | | | | | 1476.2 | 1704.6 | 2604.7 | 2376.2 | 3177.8 | 33.7 |
| Bidhaa Zisizorekodiwa | | | | | | | | | 174.3 | 202.4 | 347.8 | 438.9 | 560.4 | 27.7 |
| JUMLA KUBWA | | | | | | | | | 1917.6 | 2226.6 | 3459.8 | 3294.9 | 4297.2 | 30.4 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Ofisi ya Taifa ya Takwimu

- Takwimu Hazikupatikana

I: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE
(US$ Milioni)



## II: PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE
(Kiasi kwa Tani '000)




IIIB: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2010
Kahawa 2.8%
Pamba 2.3%
Katani 0.2%
Chai 1.1%
Tumbaku 3.0%
Karafuu 0.2%
Korosho 2.9%
Bidhaa nyinginezo 48.7%
Madini 36.6%
Bidha za Viwanda 2.2%


IIIB: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE 2009
Bidhaa nyinginezo 77.7%
Kahawa
Pamba
Katani
Chai
Tumbaku
Bidha za Viwanda 3.4%
Korosho
Madini
Karafuu

## WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 20

Sh/Tani*

| Bidhaa | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko(%) 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 926,170.0 | 1,107,030.0 | 1380,191.0 | 1,812,959.0 | 2390,242.6 | 2,668,414.0 | 2,642,540.0 | 2,628.933.6 | 4,069,398.6 | 54.8% |
| Pamba | 811,982.0 | 1,051,900.0 | 1,147,061.0 | 1,126,467.0 | 1,221,942.5 | 1,222,475.0 | 1,767,694.2 | 1,462,235.9 | 1,775,007.6 | 21.4% |
| Katani | 491,650.0 | 533,190.0 | 624,068.0 | 879,366.0 | 931,089.7 | 1,047,444.0 | 946,323.4 | 3,475,212.6 | 1,302,328.7 | -62.5% |
| Chai | 1,166,030.0 | 1,233,010.0 | 1,495,671.0 | 1,322,780.0 | 1,680,522.5 | 1,581,921.0 | 1,861,434.9 | 2,373,682.9 | 2,501,896.8 | 5.4% |
| Tumbaku | 1,993,530.0 | 2,101,200.0 | 2,109,220.0 | 2,938,727.0 | 3,440,586.3 | 2,869,021.0 | 4,593,309.3 | 4,966,396.2 | 2,586,996.0 | -47.9% |
| Korosho | 596,730.0 | 618,290.0 | 890,338.0 | 874,903.0 | 1,058,854.3 | 2,278,459.0 | 1,356,503.9 | 950.656.4 | 1,284,307.6 | 35.1% |
| Karafuu | 3,117,980.0 | 1,901,360.0 | 2,524,410.0 | 3,210,533.0 | 3,285,196.2 | 3,321,160.0 | 4,202,786.1 | 4,008,131.5 | 4,390,289.5 | 9.5% |
| Almasi (kwa carat) | 114,719.0 | 29,421.0 | 128,582.0 | 129,576.0 | 138,878.0 | 156,300.0 | 157,692.0 | 15,731.9 | 33,737.8 | 114.5% |
| Dhahabu (kwa gramu) | 7,409.0 | 8,679.0 | 11,316.0 | 24,223.0 | 21,778.0 | 9,982.0 | 34,503.9 | 41,062.3 | 39,830.1 | 3.0% |

Chanzo: Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

## WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

**Jedwali Na. 21**

US$/Tani*

| Bidhaa | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010p | Badiliko(%) 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 970 | 1,080 | 1,285 | 1,612 | 1,932 | 2,165 | 2,203 | 1,991 | 3,318 | 66.6% |
| Pamba | 840 | 1,020 | 1,063 | 988 | 988 | 992 | 1,321 | 1,108 | 1,306 | 18.0% |
| Katani | 510 | 520 | 578 | 785 | 751 | 850 | 1,251 | 2,632 | 924 | -64.9% |
| Chai | 1,220 | 1,200 | 1,386 | 1,174 | 1,359 | 1,283 | 1,575 | 1,798 | 1,069 | -40.5% |
| Tumbaku | 2,090 | 2,050 | 2,079 | 2,598 | 2,779 | 2,327 | 3,041 | 3,762 | 1870 | -50.3% |
| Korosho | 620 | 600 | 831 | 752 | 855 | 1,848 | 730 | 720 | 945 | 31.2% |
| Karafuu | 3,260 | 1,850 | 2,338 | 2,833 | 2,638 | 2,694 | 3,578 | 3,036 | 3,173 | 4.5% |
| Almasi (kwa carat) | 120 | 29 | 119 | 115 | 111 | 127 | 133 | 1,192 | 2,747 | 130.5% |
| Dhahabu (kwa gramu) | 7.70 | 8.45 | 10.47 | 2.30 | 17.40 | 8.10 | 1.78 | 6.22 | 4.52 | -27.4% |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

p=Provisional



IIA: MWENENDO WA BEI YA PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE (US$/Tani)
3500
3000
2500
2000
1500
1000
500
0
US$
1997 1998 1999 2000 2001 2002 2003 2004 2005 2006 2007 2008 2009 2010
Kahawa
Pamba

Jedwali Na. 23 Sh. Milion

| Mwaka | Bidhaa za Matumizi ya Kawaida | Bidhaa za Kati | Bidhaa za Viwanda | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1986 | 8014 | 13058 | 18899 | 39971 |
| 1987 | 13180 | 23819 | 41948 | 78947 |
| 1988 | 29841 | 55284 | 43950 | 129075 |
| 1989 | 34779 | 60176 | 96804 | 191759 |
| 1990* | 18783 | 116277 | 96223 | 231283 |
| 1991 | 62000 | 69710 | 139668 | 271378 |
| 1992 | 101641 | 94233 | 196791 | 392665 |
| 1993 | 194604 | 107481 | 229657 | 531742 |
| 1994 | 247076 | 128544 | 290638 | 666258 |
| 1995 | 201347 | 294224 | 275207 | 770778 |
| 1996 | 182340 | 267600 | 252501 | 702441 |
| 1997 | 301018 | 203418 | 198670 | 703106 |
| 1998 | 441025 | 155225 | 311244 | 907495 |
| 1999 | 503868 | 197271 | 360225 | 1061363 |
| 2000 | 401612 | 222399 | 444427 | 1068438 |
| 2001 | 468173 | 386317 | 648361 | 1502851 |
| 2002 | 499346 | 408872 | 697209 | 1605426 |
| 2003 | 654630 | 705729 | 846251 | 2206610 |
| 2004 | 917953 | 1024705 | 1029389 | 2972046 |
| 2005 | 934526 | 1447183 | 1337876 | 3719585 |
| 2006 | 1068323 | 1977275 | 1799472 | 4845070 |
| 2007 | 1399488 | 2479491 | 2195837 | 6074816 |
| 2008 | 1689789 | 3191039 | 3508181 | 8389009 |
| 2009 | 1854493 | 2495763 | 3352506 | 7702762 |
| 2010 | 2408494 | 3806237 | 3826531 | 10041262 |

*Angalia: Kuanzia mwaka 1990, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ni f.o.b. badala ya c.i.f.

## MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 24

USS milioni

| | 2002 Halisi | 2003 Halisi | 2004 Halisi | 2005 Halisi | 2006 Halisi | 2007 Halisi | 2008 Halisi | 2009 Halisi | 2010 Matarajio |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Urari wa Biashara** | **-531.7** | **-717.4** | **-1009.7** | **-1321.8** | **-1946.5** | **-2634.0** | **-3433.5** | **-2539.5** | **-2828.3** |
| Zilizouzwa nje (fob) | 979.6 | 1216.1 | 1473.1 | 1675.8 | 1917.6 | 2226.6 | 3578.8 | 3294.6 | 4296.8 |
| Zilizonunuliwa toka nje (fob)* | 1511.3 | 1933.5 | 2482.8 | 2997.6 | 3864.1 | 4860.6 | 7012.3 | 5834.1 | 7125.1 |
| Urari wa Huduma | 287.6 | 222.1 | 158.9 | 61.8 | 278.8 | 462.0 | 349.9 | 145.5 | 241.9 |
| Mapato | 920.1 | 947.8 | 1133.6 | 1269.2 | 1528.1 | 1875.7 | 1998.8 | 1854.6 | 2091.5 |
| Malipo | 632.5 | 725.7 | 974.7 | 1207.3 | 1249.3 | 1413.7 | 1648.9 | 1709.1 | 1849.6 |
| Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi | -88.9 | -149.1 | -119.1 | -104.1 | -94.8 | -123.1 | -121.6 | -71.2 | -90.9 |
| Yaliyoingia | 67.9 | 87.1 | 81.8 | 80.9 | 80.3 | 107.3 | 122.7 | 161.1 | 164.6 |
| Yaliyotoka | 156.8 | 236.2 | 200.9 | 185.0 | 175.1 | 230.4 | 244.3 | 232.3 | 255.5 |
| Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida | 431.3 | 556.9 | 586.7 | 496.4 | 588.7 | 652.0 | 609.8 | 696.9 | 823.8 |
| Iliyoingia | 494.3 | 619.9 | 651.7 | 563.9 | 654.6 | 724.0 | 689.0 | 765.3 | 902.8 |
| Serikalini | 427.7 | 553.3 | 582.0 | 478.5 | 559.7 | 626.9 | 588.5 | 658.4 | 798.1 |
| Sekta nyingine | 66.6 | 66.6 | 69.7 | 85.4 | 94.9 | 97.1 | 100.5 | 106.9 | 104.7 |
| Iliyotoka | 63.0 | 63.0 | 65.0 | 67.5 | 65.9 | 71.9 | 79.1 | 68.4 | 79.0 |
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **98.3** | **-87.5** | **-383.2** | **-867.6** | **-1173.8** | **-1643.1** | **-2595.4** | **-1768.3** | **-1853.5** |
| Urari wa Uhamisho wa Mitaji | 785.7 | 692.8 | 460.0 | 393.2 | 5183.5 | 911.7 | 537.0 | 492.8 | 616.5 |
| Iliyoingia | 785.7 | 692.8 | 460 | 393.2 | 5183.5 | 911.7 | 537.0 | 492.8 | 616.5 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Urari katika uwekezaji | 255.4 | 61.2 | 275.6 | 807.6 | -4081.6 | 853.3 | 1621.0 | 1328.2 | 1587.8 |
| Uwekezaji katika miradi | 387.6 | 308.2 | 330.6 | 494.1 | 403.0 | 581.5 | 400.0 | 414.5 | 433.4 |
| Uwekezaji katika hisa | 2.2 | 2.7 | 2.4 | 2.5 | 2.6 | 2.8 | 2.9 | 3.0 | 3.2 |
| Uwekezaji aina nyingine | -134.4 | -249.7 | -57.4 | 311.0 | -4487.3 | 269.0 | 1218.1 | 910.7 | 1151.2 |
| Makosa na Masahihisho | -806.8 | -277.4 | -146.3 | -555.4 | 532.6 | 282.7 | 585.4 | 313.4 | 18.8 |
| **Urari wa Malipo yote** | **332.6** | **389.1** | **206.1** | **-222.2** | **460.8** | **404.6** | **148.0** | **366.1** | **369.7** |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia mwaka 2006 bidhaa zilizouzwa nje zinajumuisha pia zile zisizorekodiwa (Unrecorded trade)


MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE
US $ milioni
1000.0
500.0
0.0
-500.0
-1000.0
-1500.0
-2000.0
-2500.0
-3000.0
-3500.0
-4000.0
2002
2003
2004
2005
2006
2007
2008
2009
2010
Urari wa Biashara
Huduma na Uhamisho Mali
Urari wa Malipo yote

## SURA YA 4

## FEDHA ZA SERIKALI

95. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/11, ulizingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA); Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs); Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Madeni; Vipaumbele vya uwekezaji wa umma kama vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2010/11-2012/13; na Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA). Kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na shabaha za bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/11, Serikali ilikadiria kupata jumla ya shilingi milioni 11,609,557 ikijumuisha mapato ya ndani, mikopo na misaada kutoka nje, na kutumia kiasi hicho kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 6,003,590 zilikadiriwa kupatikana kutokana na mapato ya ndani; shilingi milioni 172,582 mapato kutoka Serikali za Mitaa; shilingi milioni 821,645 misaada na mikopo ya kibajeti; shilingi milioni 2,452,908 misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na ya kisekta; shilingi milioni 1,331,212 mikopo ya ndani na nje; shilingi milioni 797,620 mikopo ya kulipia dhamana na hatifungani; na shilingi milioni 30,000 mapato kutokana na ubinafsishaji.

**Mapato ya Ndani**

96. Katika kipindi cha Julai 2010 – Machi 2011, mapato ya ndani yakijumuisha ya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 4,256.3 au asilimia 92, ikilinganishwa na makisio ya shilingi bilioni 4,629.9. Kati ya makusanyo hayo, shilingi bilioni 3,910.6, au asilimia 91.9 ya mapato yote, zilitokana na kodi, shilingi bilioni 227.4 au asilimia 5.3 ya mapato yote zilitokana na mapato yasio ya kodi na shilingi bilioni 118.2 au asilimia 2.8 ni mapato ya Halmashauri. Vilevile, katika kipindi hicho makusanyo ya kodi yalifikia asilimia 93 ya makisio ya shilingi bilioni 4,216.1 na makusanyo yasiyo ya kodi yalikuwa asilimia 80, ikilinganishwa na makisio ya shilingi bilioni 284.3. Hii ilitokana na kupungua kwa nishati ya umeme ambayo inaathiri shughuli za kiuchumi, kupanda kwa

bei ya mafuta katika soko la dunia; tishio la maharamia wanaoteka meli kwenye bahari ya Hindi; kupungua kwa samaki katika maziwa na bahari na uvuvi haramu. Pamoja na kutokufikiwa kwa malengo, mapato ya ndani yaliongezeka kwa asilimia 21, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2009/10 na wastani wa makusanyo kwa mwezi uliongezeka kutoka shilingi 390 bilioni mwaka 2009/10, hadi shilingi 473 bilioni mwaka 2010/11.

**Maboresho Katika Mfumo wa Kodi**

97. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kupanua wigo wa kodi na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ili kuweza kugharamia sehemu kubwa ya bajeti. Aidha, Serikali iliendelea kurejea sheria na taratibu zinazosimamia misamaha ya kodi kwa nia ya kupunguza na kudhibiti usimamizi wake. Vilevile, Mamlaka ya Mapato Tanzania iliendelea kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maboresho wa miaka mitano (2008/09 – 2012/13) ambao ndio umekuwa msingi wa kukua kwa mapato ya ndani. Kwa upande wa mapato yasiyo ya kodi, Serikali iliimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato hayo ili yaweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa.

**Misaada na mikopo**

98. Katika kipindi cha Julai 2010 – Machi 2011, Serikali iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Pamoja wa Misaada, kudumisha uhusiano mzuri na Washirika wa Maendeleo na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa katika kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu ili kusaidia jitihada za Serikali katika kutekeleza MKUKUTA, sambamba na Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025. Jumla ya shilingi 845,748 milioni zilipatikana kama misaada na mikopo ya Bajeti (GBS) katika kipindi cha Julai 2010 – Machi, 2011, ikiwa ni asilimia 103 ya shilingi milioni 821,645 zilizokadiriwa kwenye bajeti. Hii ilitokana hasa na mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji wa fedha kati ya sarafu yetu na zile za nchi wafadhili ikilinganishwa na makadirio ya awali.

99. Misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha Mfuko wa Basketi, ilifikia shilingi 1,427,604 milioni, ambayo ni asilimia 77 ya makadirio katika kipindi hicho. Upungufu uliojitokeza unatokana hasa na

kutopatikana kwa wakati kwa taarifa za misaada inayopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa miradi (D-Fund), pamoja na baadhi ya fedha za wafadhili kutokutolewa kwa wakati.

100. Serikali pia ililenga kukopa kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2011 kiasi cha shilingi milioni 1,107,471 kilipatikana. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi milioni 607,621 zilizotumika kulipia dhamana na hati fungani zilizoiva na shilingi milioni 499,850 zilitumika kugharamia miradi mbalimbali ya miundombinu.

## Mikopo ya Kibiashara

101. Mwaka 2010/11, Serikali ilipanga kukopa dola za Kimarekani milioni 525 kwa masharti ya kibiashara. Hadi Machi 2011, Serikali ilikuwa imeshakamilisha majadiliano na Benki ya HSBC kwa ajili ya kupata mkopo wenye thamani ya Dola 192.7 milioni. Mkopo huo utagharamia ununuzi wa mitambo miwili ya kuzalisha umeme Dar es Salaam na Mwanza. Kati ya kiasi hicho, dola milioni 103 ni kwa ajili ya mradi wa umeme Ubungo – Dar es Salaam. Vilevile, Serikali ilifanya majadiliano na Benki ya Standard kwa ajili ya mkopo wa dola milioni 250 na maandalizi ya mkataba wa mkopo huo yanaendelea. Aidha, majadiliano na taasisi nyingine za fedha yanaendelea ili kupata kiasi cha dola milioni 84 kilichobakia kulingana na malengo ya kukopa dola milioni 525 kutoka chanzo hicho.

## Matumizi

102. Katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, Serikali iliendelea kuwianisha matumizi na mapato. Matumizi halisi katika kipindi hicho yalikuwa shilingi 7,169.3 milioni sawa na asilimia 90 ya makadirio ya shilingi 8,009,917 milioni. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,226,893 milioni zilikuwa za matumizi ya kawaida na shilingi 1,942,443 milioni ni matumizi ya maendeleo.

103. Malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Machi, 2011 yalikuwa shilingi 1,749,096 milioni, sawa na asilimia 79 ya lengo la mwaka 2010/11 la shilingi 2,205,430 milioni. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 569,962 zilitolewa kwa ajili ya Wizara na Idara zinazojitegemea, shilingi 52,928 milioni zilitolewa kwa ajili ya watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi 1,126,206 milioni kwa ajili ya mishahara ya Halmashauri. Aidha, shilingi 443,987 milioni zilitumika kulipia mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Serikali.

104. Katika kipindi cha Julai 2010 – Machi 2011, matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi 1,955,278 milioni ikiwa ni asilimia 89 ya makadirio kwa kipindi hicho. Aidha, matumizi katika miradi ya maendeleo yalifikia shilingi 1,942,443 milioni, ambapo fedha za ndani zilikuwa shilingi 514,839 milioni, sawa na asilimia 52 ya makadirio ya shilingi 1,000,537 milioni. Matumizi ya maendeleo yanayogharamiwa na fedha za nje yalifikia shilingi 1,427,604 milioni, sawa na asilimia 77, ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 1,839,681 milioni.

**Mgawanyo wa Bajeti Kwenye Huduma za Serikali**

105. Serikali iliendelea kutenga fedha katika bajeti za sekta mbalimbali kwa mwaka 2010/11. Katika Bajeti ya mwaka 2010/11 ilitenga asilimia 6.0 ya bajeti yote kwa ajili ya kugharamia matumizi katika sekta ya elimu, ikilinganishwa na asilimia 5.7 mwaka 2009/10. Bajeti ya elimu ya sekondari na elimu ya juu zimeendelea kuchangia ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa. Bajeti ya sekta ya afya iliongezeka hadi asilimia 5.5 ya bajeti mwaka 2010/11, kutoka asilimia 5.2 mwaka 2009/10. Hii inaonesha juhudi za Serikali kuendeleza kugharamia huduma za afya.

106. Sekta ya kilimo, misitu, uvuvi na uwindaji ilitengewa asilimia 3.0 ya bajeti yote ya mwaka 2010/11. Bajeti hiyo ya kilimo iliongezeka kwa asilimia 4 ikilinganishwa na ile ya mwaka 2009/10, ambapo sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilichangiwa na bajeti ya shughuli za kilimo. Vile vile, bajeti ya sekta ya madini, viwanda na ujenzi iliendelea kutengewa asilimia 0.4 ya bajeti kama ilivyokuwa mwaka 2009/10. Licha ya mwenendo huo, bajeti ya shughuli za

madini iliongezeka kwa asilimia 24 ikilinganishwa na ile ya mwaka 2009/10. Sekta ya usafiri na mawasiliano imeonesha ongezeko kubwa katika bajeti yake, ambapo asilimia 10.1ya bajeti ilitengwa kwa ajili hiyo ikilinganishwa na asilimia 8.9 iliyotolewa mwaka 2009/10. Sekta nyingine iliyoonesha ongezeko kubwa ni huduma zingine za kiuchumi ambayo ilitengewa asilimia 7.7 mwaka 2010/11 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2009/10.

**Deni la Taifa**

107. Hadi kufikia Desemba 2010, deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na sekta binafsi lilifikia Dola za Kimarekani 11,380.2 milioni, sawa na ongezeko la asilimia 6.1 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2009/10. Kati ya kiasi hicho, Dola za Kimarekani 9,516.8 milioni zilikuwa deni la Serikali na Dola za Kimarekani 1,863.4 milioni ni deni la sekta binafsi. Ongezeko hilo lilitokana na malimbikizo ya riba ya deni la nje hasa kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris ambazo hazijatoa misamaha ya madeni kulingana na makubaliano. Vilevile, mikopo mipya iliyotokana na kuongezeka kwa mahitaji ya Serikali kwa ajili ya kugharamia miradi ya uendelezaji wa miundombinu ilisababisha kuongezeka kwa deni la taifa. Aidha, kati ya Dola za Kimarekani 9,516.8 milioni ambazo ni deni la Serikali, Dola za Kimarekani 6,529.6 milioni ni deni la nje na Dola za Kimarekani 2,986.9 milioni ni deni la ndani.

108. Katika kutekeleza mkakati wa madeni wa Taifa, Serikali iliendelea kusimamia kwa umakini deni lake kwa kukopa zaidi kutoka vyanzo nafuu na kuchambua athari zinazotokana na mikopo mipya. Aidha, katika kipindi cha Julai – Desemba 2010, Serikali ilifanya tathmini ya uhimilifu wa deni (Debt Sustainability Analysis) ambayo ilionesha deni la taifa ni himilifu kulingana na viwango vya kimataifa vya viashiria vya madeni.

**Jedwali Na.4.1: Tathmini ya Viashiria vya Deni la Taifa**

| Viashiria % | 2010 | 2013 | 2015 | 2020 | 2030 | Msingi (Threshold) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni la Taifa (PV) kwa Pato la Taifa | 14.6 | 16.6 | 14.1 | 12.9 | 10.3 | 50 |
| Deni la Taifa (PV) kwa kwa Mauzonje | 56.3 | 55.8 | 45.6 | 38.1 | 25 | 200 |
| Deni la Taifa (PV) kwa Mapato ya ndani | 85.05 | 88.2 | 73.3 | 63.5 | 45.1 | 300 |
| Ulipaji wa deni la Taifa la nje kwa mapato ya ndani | 1.7 | 3.4 | 3.8 | 1.3 | 1.0 | 25 |
| Ulipaji wa deni la nje la Taifa kwa mauzo nje | 2.5 | 5.3 | 6.1 | 2.2 | 1.8 | 35 |

Chanzo: Wizara ya Fedha

**Deni la Nje**

109. Deni la nje lilikuwa Dola za Kimarekani 8,363 milioni Desemba 2010 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 7,641.9 milioni mwishoni wa mwezi Desemba 2009, hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9. Kati ya Dola za Kimarekani 8,363 milioni; Dola za Kimarekani 7,699.6 milioni ni bakaa halisi ya deni, na Dola za Kimarekani 693.7 milioni ni malimbikizo ya riba. Kuongezeka kwa deni kulitokana na mikopo mipya na malimbikizo ya riba hasa kutoka nchi za kundi lisilo la wanachama wa Paris ambazo hazijatoa misamaha ya madeni kulingana na makubaliano. Aidha, kati ya deni la nje Dola za Kimarekani 6,529.6 milioni ni deni la Serikali na Dola za Kimarekani 1863.4 milioni ni deni la sekta binafsi. Uchambuzi wa deni la nje kwa sarafu unaonesha kuwa, sehemu kubwa ya deni la taifa lilikuwa katika sarafu za Dola za Kimarekani, Euro na Yen ambazo ni asilimia 37, 28 na 11 kwa mtiririko huo.

Kielelezo Na. 4.1: Bakaa Halisi la Deni kwa Sarafu Desemba 2010




**Deni la nje kwa Wakopeshaji**

110. Mchanganuo wa deni kwa wakopeshaji ulionesha kwamba, wakopeshaji wakubwa ni mashirika ya fedha ya kimataifa ambayo yalichangia asilimia 72 ya deni la nje. Nchi wahisani zilichangia asilimia 25 na wengine walichangia asilimia 3. Serikali imekuwa ikikopa zaidi kutoka katika mashirika makubwa ya kifedha kwa sababu ya unafuu wa masharti katika mikopo hiyo.

Kielelezo Na. 4.2: Deni la Nje kwa Mkopeshaji, hadi Desemba 2010




**Deni la Ndani**

111. Hadi kufikia Desemba 2010, Deni la ndani la Serikali lililikia kiasi cha shilingi 4,385.4 bilioni, (au Dola za Kimarekani 2,986.9 milioni) ikilinganishwa na shilingi 3,837.7 bilioni mwezi Desemba, 2009, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya Serikali kugharamia miradi ya miundombinu na utumiaji wa dhamana za Serikali kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei katika uchumi. Kiasi kikubwa cha deni la ndani kilitokana na: Hati Fungani za Serikali ambazo ni sawa na asilimia 61.1; dhamana za Serikali za muda mfupi asilimia 38.7; na madeni mengine asilimia 0.2.

112. Uchambuzi wa deni la ndani la Serikali kwa makundi yanayohodhi ulibainisha kuwa benki za biashara zinahodhi sehemu kubwa ya deni hilo. Hadi kufikia Desemba 2010, benki za biashara zilikuwa zinahodhi asilimia 48.8 ya deni la ndani. Hii ilichangiwa na kukua kwa sekta ya benki nchini pamoja na hofu ndogo ya kuikopesha Serikali ikilinganishwa na sekta binafsi. Benki Kuu ya Tanzania ni ya pili ikihodhi asilimia 30.0, mifuko ya hifadhi ya jamii asilimia 20.7 na watu binafsi na mashirika madogo asilimia 0.5

**Ulipaji wa Deni la Serikali**

113. Katika kipindi cha Julai 2010 – Machi 2011, Serikali ilitumia Shilingi 801,443 milioni kulipia madeni. Kati ya kiasi hicho, shilingi 71,193 milioni zilitumika kulipia madeni ya nje na shilingi milioni 730,250 milioni zilitumika kulipia madeni ya ndani. Malipo ya mtaji wa deni la nje yaligharimu shilingi 26,610 milioni wakati malipo ya riba yalikuwa shilingi 44,583 milioni. Aidha, kati ya shilingi 730,250 milioni zilizotumika kulipia madeni la ndani, shilingi 556,695 milioni zililipia dhamana za Serikali zilizoiva kwa utaratibu wa utoaji wa hatifungani mpya kulipia zinazoiva tuu (rollover), na shilingi 173,555 milioni zilitumika kulipia ya riba.

MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Jedwali Na. 25

Sh. milioni

| | 2006/07 Halisi | 2007/08 Halisi | 2008/09 halisi | 2009/10 halisi | 2010/11 Bajeti | 2010/11 Matokeo hadi Machi | 2010/11 Matarajio hadi Juni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri) | 2739022 | 3634581 | 4293075 | 4661540 | 6176172 | 4256288 | 5726253 |
| MAPATO YA NDANI | 2739022 | 3634581 | 4293075 | 4661540 | 6003590 | 4138082 | 5553671 |
| 1. Mapatoyatokanayo na Kodi | 2529439 | 3359250 | 4043674 | 4427834 | 5638593 | 3910654 | 5266169 |
| Ushuru wa Forodha na Excise Duty | 765644 | 965498 | 1130860 | 1214626 | 1520194 | 1056823 | 1451404 |
| Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) | 861050 | 1110951 | 1333789 | 1488452 | 1991653 | 1275766 | 1737990 |
| Bidhaa toka nje | 431614 | 550289 | 641392 | 729040 | 999329 | 664609 | 899989 |
| Bidhaa za ndani | 429436 | 560661 | 692397 | 759412 | 992324 | 611158 | 838002 |
| Kodi ya Mapato | 790877 | 1028902 | 1257861 | 1388778 | 1702338 | 1255840 | 1634733 |
| Kodi nyingine | 218581 | 382792 | 462544 | 499497 | 620912 | 449725 | 615715 |
| Merejesho (Refunds Accounts) | -106713 | -128893 | -141380 | -163519 | -196504 | -127499 | -173673 |
| 2. Mapato yasiyotokana na Kodi | 209583 | 275331 | 249401 | 233707 | 364997 | 227427 | 287502 |
| 3. Mapato ya Halmashauri | | | | | 172582 | 118206 | 172582 |
| B. JUMLA YA MATUMIZI | 4474680 | 5208996 | 6811827 | 8173749 | 10769612 | 7169336 | 9557706 |
| 1. Matumizi ya Kawaida | 3137469 | 3398024 | 4681459 | 5562443 | 6950561 | 5226893 | 6316281 |
| 2. Matumizi ya Maendeleo | 1337211 | 1810972 | 2130368 | 2611306 | 3819051 | 1942443 | 3241425 |
| Fedha za ndani | 503291 | 567421 | 906023 | 1004530 | 1366143 | 514839 | 978425 |
| Fedha za nje | 833920 | 1243551 | 1224345 | 1606776 | 2452908 | 1427604 | 2263000 |
| C. NAKISI/SALIO (A-B) | -1735658 | -1574415 | -2518752 | -3512209 | -4593440 | -2913048 | -3831453 |
| D. KUZIBA NAKISI | 1735660 | 1574415 | 2518752 | 3512209 | 4593440 | 2913048 | 3831453 |
| 1. Fedha kutoka nje | 1689337 | 2302805 | 2201485 | 2784944 | 3963440 | 2246742 | 3484933 |
| Ruzuku | 971547 | 1573195 | 1257283 | 1405288 | 2020907 | 1287187 | 2050677 |
| Basket support | 47331 | 200628 | 151370 | 194071 | 256219 | 207684 | 246150 |
| Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL | 266946 | 365038 | 331315 | 558320 | 189837 | 173806 | 201806 |
| Mikopo ya miradi | 433203 | 209342 | 488795 | 695597 | 807590 | 604674 | 692300 |
| Mikopo ya masharti ya kibiashara | | | | | 731212 | 0 | 342000 |
| Kulipia madeni ya nje (Amortization Fore | -29690 | -45399 | -27278 | -68331 | -42326 | -26610 | -48000 |
| 2. Fedha za Ndani | 46323 | -728390 | 317267 | 727265 | 630000 | 666306 | 346520 |
| Mikopo isiyo ya mabenki | 212475 | -19795 | 1108 | 24754 | 0 | 0 | 0 |
| Mikopo ya mabenki | 25533 | -316755 | 212567 | 593023 | 600000 | 760972 | 346520 |
| Mikopo ya ndani (Rollover) | | | | 714315 | 797620 | 556695 | 797620 |
| Mapato ya Ubinafsishaji | 0 | 0 | 45000 | 9659 | 30000 | 0 | 0 |
| Marekebisho (Adjustment to Cash) | -60370 | -78308 | 275298 | 595034 | 0 | 385461 | 0 |
| Kulipia madeni ya ndani (amortization) | 0 | -14648 | 0 | -723776 | -797620 | -556695 | -797620 |
| Expenditure float | -131315 | -298884 | -216706 | -436236 | 0 | -480127 | 0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha



Sh. million
12000000
10000000
8000000
6000000
4000000
2000000
12000000
2000000
4000000
6000000
2007/08
2008/09
2009/10
2010/11
MAPATO YA NDANI
B. JUMLA YA MATUMIZI
C. NAKISI / SALIO (A-B)

## MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI

Jedwali Na. 26 — Sh milioni

| | 2008/2009 | | | 2009/2010 | | | 2010/2011* | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi Ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **1 HUDUMA ZA KAWAIDA** | 1985848 | 516184 | 2522191 | 2895011 | 717801 | 3612812 | 3413018 | 973032 | 4386[illegible] |
| 1.1 Utawala | 1,811,107 | 432,037 | 1926 4690 | 2,695,305 | 613,601 | 3308906 | 3,153 243 | 830,220 | 3583403 |
| 1.2 Misaada ya kiuchumi kutoka nje | 10,179 | 0 | 69145 | 6 826 | 0 | 6826 | 7 261 | 0 | 7261 |
| 1.3 Huduma za ubifu | 19 727 | [illegible]495 | 1310092 | 21,751 | 14,586 | 36337 | 22,934 | 42,731 | 65665 |
| 1.4 Huduma | 161 298 | 70,470 | 4425489 | 163,031 | 79586 | 242619 | 171 509 | 84,756 | 256265 |
| 1.5 Huduma za utawala zisizotajwa hapo juu | 3,446 | 7 782 | 130397 | 8,098 | 10,026 | 1812[illegible] | 56071 | 15 326 | 72395 |
| **2 ULINZI** | 331524 | 55079 | 3840174 | 393868 | 33650 | 427518 | 459669 | 145304 | 604970 |
| 2.1 Utawala | 287,445 | 8,959 | 3,743,225 | 372,082 | 33,850 | 406,732 | 330,900 | 31,104 | 362004 |
| 2.2 Misaada ya nje ya ulinzi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 2.3 Utafiti na maendeleo ya ulinzi | 242 | 46,920 | 47,162 | 360 | 0 | 386 | 213 | 114 200 | 114413 |
| 2.4 Huduma za ulinzi zisizotajwa hapo juu | 43637 | 0 | 49,787 | 21,426 | 0 | 21,426 | 128553 | 0 | 128553 |
| **3 USALAMA** | 226497 | 35341 | 2158661 | 268311 | 63957 | 332287 | 329624 | 55087 | 384611 |
| 3.1 Polisi na zimamoto | 160 619 | 14,876 | 1,346,685 | 162,938 | 25,371 | 187,908 | 210,770 | 17,718 | 221,486 |
| 3.2 Mahakama | 49 298 | 3,812 | 413,046 | 52,882 | 18,433 | 71 315 | 57,114 | 7 661 | 64,775 |
| 3.3 Magereza | 10 453 | 600 | 79,054 | 8,602 | 800 | 9,402 | [illegible] 782 | 800 | 7 652 |
| 3.4 Huduma za usalama zisizotajwa hapo juu | 25,927 | 11,350 | 320,055 | 44,289 | 19 363 | 63 642 | 34,988 | 28,809 | 83,796 |
| **4 ELIMU** | 510015 | 105614 | 5266541 | 406638 | 135302 | 511939 | 552274 | 148316 | 700590 |
| 4.1 Elimu ya msingi | 6,027 | 7,925 | 871,271 | 6,977 | 3,889 | 10,866 | 2,639 | 3,115 | 5,955 |
| 4.2 Elimu ya sekondari | 165,278 | 26,879 | 1,138,879 | 2,308 | 550 | 2,858 | 1,732 | 14,680 | 16,412 |
| 4.3 Elimu ya juu | 302,703 | 45,570 | 2,988,829 | 338,446 | 113,112 | 451,557 | 483,532 | 113,213 | 596,748 |
| 4.4 Elimu isiyo pambanuliwa | 0 | 17,213 | 66,616 | 546 | 4,300 | 5,246 | 3,315 | 6,798 | 10,110 |
| 4.5 Huduma za ziada kwa elimu | 0 | 0 | 0 | 184 | 0 | 184 | 125 | 0 | 125 |
| 4.6 Huduma za elimu zisizotajwa hapo juu | 40,908 | 6,027 | 511,245 | 57,779 | 13,450 | 71,230 | 60,731 | 10,512 | 71,244 |
| **5 AFYA** | 221093 | 187226 | 3728936 | 236600 | 255412 | 491912 | 248942 | 389403 | 636425 |
| 5.1 Huduma za hospitali | 34,573 | 146,037 | 1,291,595 | 318,466 | 190,201 | 236,667 | 31,005 | 304,103 | 335,108 |
| 5.2 Kliniki, maabara, huduma za meno n.k. | 179 284 | 40,939 | 2079,507 | 191,027 | 64,673 | 255,990 | 202,287 | 84,880 | 287,167 |
| 5.3 Huduma za afya | 0 | 250 | 150,519 | 0 | 338 | 338 | 0 | 500 | 50 |
| 5.4 Madawa na vifaa | 3,513 | 0 | 4(5978 | 6,390 | 0 | 5,398 | 6678 | 0 | 6,678 |
| 5.5 Utafiti wa afya | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | [illegible] |
| 5.6 Huduma za afya zisizotajwa hapo juu | 3,723 | 0 | 169,995 | 3,610 | 0 | 3,610 | 4,772 | 0 | 4,772 |
| **6 USALAMA, USTAWI NA HUDUMA ZA JAMII** | 70275 | 7928 | 843617 | 99366 | 13633 | 112,999 | 95068 | 9396 | 104464 |
| 6.1 Usalama wa jamii | 1,966 | 290 | 57,616 | 1 800 | 590 | 2,390 | 1,494 | 736 | 2 231 |
| 6.2 Ustawi na huduma za jamii | 64940 | 7,112 | 757,473 | 95,620 | 12,665 | 108,285 | 92,114 | 5,804 | 97,910 |
| 6.3 Huduma nyingine za jamii zisizotajwa hapo juu | 3,369 | 526 | 28 727 | 1,947 | 378 | 2,325 | 1 460 | 2,855 | 4,315 |
| **7 NYUMBA NA HUDUMA ZA JAMII** | 20337 | 148471 | 2315015 | 26179 | 215862 | 242040 | 32621 | 223760 | 256381 |
| 7.1 Nyumba na ustawi wa jamii | 5,620 | 556 | 254,945 | 8,143 | 607 | 8,750 | 7 615 | 477 | 8 092 |
| 7.2 Usambazaji wa Maji | 7,032 | 140,988 | 1,675,936 | 8 763 | 205,889 | 214,652 | 8 868 | 204,410 | 213 278 |
| 7.3 Usafi wa mazingira | 6367 | 2,656 | 181,600 | 7 345 | 9,365 | 16,711 | 4,446 | 18,072 | 23,318 |
| 7.4 Umeme wa barabarani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.5 Huduma za nyumba na za jamii zisizotajwa hapo juu | 1,316 | 0 | 3,234 | 1926 | 0 | 1 926 | 11693 | 0 | 11693 |
| **8 HUDUMA ZINGINE ZA JAMII** | 9715 | 7926 | 17 641 | 13 434 | 6939 | 22373 | 19996 | 9218 | 29214 |
| 8.1 Upumzikaji, burudani, dini na huduma zingine | 9,715 | 7926 | 17 641 | 13,434 | 8939 | 22373 | 19 996 | 9,218 | 29 214 |

500

Jedwali hili linaendelea ukurasa unaofuata....

Jedwali Na. 28 linaendelea

| | 2008/09 | | | 2009/10 | | | 2010/11* | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi Ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi Ya Kawaida | Matumizi Ya Maendeleo | Jumla |
| **9 MAFUTA NA UMEME** | 33127 | 116822 | 149946 | 32801 | 153517 | 186344 | 36735 | 166453 | 203188 |
| 9.1 Mafuta | 33,127 | 116,822 | 149,948 | 32,801 | 153,547 | 186,348 | 36,735 | 166,453 | 203,188 |
| 9.2 Umeme | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 9.3 Huduma zingine za mafuta na umeme | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **10 KILIMO, MISITU, UVUVI NA UWINDAJI** | 177264 | 80511 | 257775 | 178485 | 161972 | 340457 | 182951 | 160312 | 353263 |
| 10.1 Kilimo | 127,232 | 55,631 | 182,863 | 122,722 | 117,640 | 240,362 | 142,217 | 129,681 | 271,897 |
| 10.2 Misitu | 11,681 | 6,401 | 18,180 | 14,754 | 12,399 | 27,153 | 16,420 | 5,473 | 21,893 |
| 10.3 Uvuvi na uwindaji | 17,116 | 8,648 | 25,764 | 19,888 | 17,998 | 37,887 | 20,764 | 13,309 | 34,073 |
| 10.4 Utafiti wa kilimo | 14,700 | 9,751 | 24,450 | 14,621 | 13,133 | 27,754 | 12,926 | 11,351 | 24,277 |
| 10.5 Huduma zingine za kilimo, misitu, uvuvi na uwindaji | 6,535 | 0 | 6,535 | 6,501 | 800 | 7,301 | 626 | 496 | 1,122 |
| **11 MADINI, VIWANDA NA UJENZI** | 7450 | 3729 | 11179 | 18627 | 20295 | 38923 | 27208 | 19394 | 46602 |
| 11.1 Madini | 5,544 | 1,537 | 7,081 | 13,590 | 16,095 | 29,685 | 21,121 | 15,580 | 36,701 |
| 11.2 Viwanda | 192 | 392 | 584 | 497 | 1,200 | 1,697 | 431 | 816 | 1,247 |
| 11.3 Ujenzi | 1,715 | 1,800 | 3,514 | 4,540 | 3,000 | 7,540 | 5,653 | 3,000 | 8,653 |
| 11.4 Huduma zingine za madini, viwanda na ujenzi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12 USAFIRI NA MAWASILIANO** | 219957 | 219191 | 439148 | 280063 | 567736 | 847800 | 303075 | 870961 | 1174037 |
| 12.1 Usafiri wa Barabara | 166,065 | 210,883 | 376,948 | 552 | 0 | 552 | 3,021 | 0 | 3,021 |
| 12.2 Usafiri majini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12.3 Huduma za reli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12.4 Usafiri wa anga | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12.5 Usafirishaji kwa mabomba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12.6 Huduma ya usafirishaji | 40,914 | 3,850 | 44,764 | 257,226 | 539,668 | 796,894 | 280,240 | 854,967 | 1,135,206 |
| 12.7 Mawasiliano | 11,561 | 3,580 | 15,141 | 14,231 | 2,100 | 16,334 | 11,729 | 5,582 | 17,311 |
| 12.8 Huduma zingine za usafiri na mawasiliano | 1,417 | 878 | 2,295 | 8,051 | 25,968 | 34,019 | 8,086 | 10,413 | 18,499 |
| **13 HUDUMA ZINGINE ZA KI - UCHUMI** | 224295 | 219400 | 443695 | 244652 | 441795 | 686446 | 251750 | 638170 | 889921 |
| 13.1 Biashara - maghala, hoteli na migahawa | 6,211 | 3,077 | 9,288 | 9,520 | 4,867 | 14,387 | 9,795 | 7,470 | 17,264 |
| 13.2 Utalii | 6,074 | 1,753 | 7,827 | 6,127 | 4,444 | 10,571 | 11,521 | 62 | 11,583 |
| 13.3 Huduma za miradi | 194,163 | 145,816 | 339,978 | 204,160 | 235,445 | 439,605 | 204,755 | 332,744 | 537,499 |
| 13.4 Huduma za uchumi na biashara mbali na zilizochukuliwa | 9,338 | 13,337 | 22,675 | 10,837 | 2,275 | 13,112 | 12,052 | 2,389 | 14,440 |
| 13.5 Huduma za kazi | 3,048 | 2,934 | 5,981 | 4,693 | 5,010 | 9,704 | 4,986 | 778 | 5,765 |
| 13.6 Huduma nyinginezo za maendeleo | 5,461 | 52,484 | 57,945 | 9,314 | 189,753 | 199,067 | 8,642 | 294,728 | 303,370 |
| **14 MATUMIZI MENGINEYO** | 788840 | 4211 | 763051 | 1613418 | 12051 | 1625460 | 1829578 | 10265 | 1839843 |
| 14.1 Deni la Taifa | 693,748 | 0 | 693,748 | 1,528,094 | 0 | 1,528,094 | 1,757,093 | 0 | 1,757,093 |
| 14.2 Huduma za Fedha | 94,218 | 4,211 | 98,429 | 84,483 | 12,051 | 96,534 | 71,922 | 10,265 | 82,187 |
| 14.3 Malipo ya uzeeni | 875 | 0 | 875 | 842 | 0 | 842 | 562 | 0 | 562 |
| **JUMLA** | 4,817,137 | 1,704,934 | 45,508,092 | 6,707,354 | 2,801,950 | 9,509,304 | 7,790,507 | 3,819,051 | 11,609,558 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Makadirio

## SURA YA 5

## FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

**Ujazi wa Fedha na Karadha**

114. Katika mwaka 2009/10, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka na kufikia shilingi 4,134.7 bilioni, kutoka shilingi 3,149.1 bilioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 31.3. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka kwa asilimia 26.3, kutoka shilingi 5,772.5 bilioni mwaka 2008/09 hadi shilingi 7,288.1bilioni mwaka 2009/10. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka na kufikia shilingi 9,801.8 bilioni mwaka 2009/10, kutoka shilingi 7,834.1 bilioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 25.1. Ukuaji wa ujazi wa fedha ulitokana na kuongezeka kwa akiba halisi ya mali/rasilimali za kigeni kwenye mabenki na kuongezeka kwa mikopo ya Serikali katika kipindi hicho.

115. Hadi kufikia mwezi Desemba 2010, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 21.8, ikiwa ni juu kidogo ya lengo la asilimia 20.7 kwa kipindi hicho. Vivyo hivyo, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 25.3, ikilinganishwa na lengo la asilimia 23.5. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa amana za fedha za kigeni na kuimarika kwa thamani ya Dola ya Kimarekani dhidi ya shilingi ya Tanzania.

116. Karadha nchini iliongezeka kutoka shilingi 4,771.7 bilioni mwaka 2008/09 hadi kufikia shilingi 6,124.1 bilioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 28.3. Hadi kufikia Desemba 2010, karadha iliongezeka na kufikia shilingi 6,798.5 bilioni, sawa na ukuaji wa asilimia 32.8 ikilinganishwa na shilingi 5,120.2 bilioni Desemba 2009. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi.

**Mikopo ya Benki za Biashara kwa shughuli za Kiuchumi**

117. Hadi kufikia Desemba 2010, mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa shilingi 6,029.4 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 4,805.8 bilioni Desemba 2009, sawa na ongezeko la asilimia 25.5. Ongezeko hili ni juu ya lengo la asilimia 19.2

katika kipindi hicho ambalo lilitokana na kujengeka kwa imani kwa mabenki katika utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi kufuatia kuimarika kwa hali ya uchumi wa dunia. Mikopo ilielekezwa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kama ifuatavyo: shughuli binafsi (asilimia 23.1); shughuli za biashara (asilimia 17.6); uzalishaji viwandani (asilimia 13.6); kilimo (asilimia 12.3); na shughuli za uchukuzi na mawasiliano (asilimia 9.0).

118. Mwaka 2010, dhamana zilizouzwa na Serikali zilikuwa na thamani ya shilingi 3,124.3 bilioni ikilinganishwa na shilingi 2,746.5 bilioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 13.8. Aidha, hatifungani za Serikali zilizouzwa mwaka 2010 zilikuwa na thamani ya shilingi 714.0 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 392.1 bilioni zilizouzwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 82.1. Ongezeko kubwa katika hatifungani za Serikali zilizouzwa mwaka 2010 lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha serikalini kwa ajili ya kugharamia miradi ya miundombinu.

**Amana katika Benki za Biashara**

119. Mwaka 2010, amana katika benki za biashara ziliongezeka na kufikia shilingi 9,748.7 bilioni, kutoka shilingi 7,852.7 bilioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 24.1. Kati ya hizo, sekta binafsi ilichangia shilingi 9,049.5 bilioni, sawa na asilimia 92.8 kwenye amana zote katika benki za biashara na Serikali Kuu ilichangia asilimia iliyobakia. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshaji na uanzishwaji wa huduma mpya za kibenki. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote uliongezeka na kufikia asilimia 30.0, kutoka asilimia 27.5 mwaka 2009. Ongezeko hili lilitokana hasa na kuimarika kwa Dola ya Marekani dhidi ya sarafu za mataifa mengine.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

120. Wastani wa jumla wa viwango vya riba za mikopo katika benki za biashara ulipungua hadi asilimia 13.45 Desemba 2010, kutoka asilimia 14.38 Desemba 2009. Wastani wa riba za kukopa kwa muda mfupi (hadi mwaka mmoja) ulipungua kutoka asilimia 13.96 Desemba 2009, hadi asilimia 12.40 Desemba 2010. Aidha, wastani wa jumla wa amana za akiba za muda maalum ulipungua kutoka asilimia 6.36 Desemba 2009, hadi asilimia 5.11 Desemba

2010. Vilevile, wastani wa riba za amana za akiba za muda maalum (miezi 12) ulipungua na kufikia asilimia 7.09 Desemba 2010 kutoka asilimia 8.99 Desemba 2009. Kutokana na mwelekeo huo wa riba, tofauti baina ya viwango vya riba za amana na mikopo (mwaka mmoja) iliongezeka kutoka asilimia 4.97 Desemba 2009, hadi asilimia 5.31 Desemba 2010.

**Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)**

121. Mwaka 2010, idadi ya wanachama katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma iliongezeka na kufikia wanachama 160,068, kutoka wanachama 132,878 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Mfuko kuendelea kuandikisha wanachama wapya kutoka sekta binafsi. Ukusanyaji wa michango ya wanachama uliongezeka na kufikia shilingi 146,943.6 milioni mwaka 2010, kutoka shilingi 126,963.5 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Aidha, Mfuko ulilipa mafao ya shilingi 63,527.8 milioni kwa wanachama, ikilinganishwa na shilingi 47,191.25 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 34.6. Mafao kwa wanachama yaliongezeka kutokana na: kupanda kwa kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 21,000 hadi shilingi 50,000 kwa mwezi; nyongeza ya pensheni kwa wastaafu; na kuongezeka kwa wanachama waliostaafu kwa kutimiza umri na baadhi kuacha ajira zao.

122. Thamani ya Mfuko kwa mwaka 2010 iliongezeka kwa asilimia 17.1 na kufikia shilingi 731,421.7 milioni, kutoka shilingi 624,850 milioni mwaka 2009. Vilevile, uwekezaji wa Mfuko katika dhamana za Serikali uliongezeka kutoka shilingi 86,875.4 mwaka 2009, hadi shilingi 117,100.95 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 34.8. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yalipungua kwa asilimia 10.5, kutoka shilingi 67,079.3 milioni mwaka 2009, hadi shilingi 60,047.8 mwaka 2010. Hii ilitokana na athari za mtikisiko wa uchumi duniani ambao uliathiri viwango vya riba katika mabenki na dhamana za Serikali pamoja na vitega uchumi vipya.

**Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)**

123. Mwaka 2009/10, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma ilikuwa 298,046, ikilinganishwa na 285,329 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Makusanyo ya Mfuko kutokana na vitega uchumi vilivyokomaa yalipungua na kufikia shilingi 400,164.4 milioni mwaka 2009/10, kutoka shilingi 408,836.5 milioni mwaka 2008/09, sawa na upungufu wa asilimia 2.1. Aidha, katika kipindi hicho, faida kutokana na mapato ya uwekezaji katika vitega uchumi yalifikia shilingi 63.6 bilioni, kutoka shilingi 56.2 bilioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 13.2. Hadi Juni 2010, thamani ya Mfuko ilifikia shilingi 732,111 milioni, ikilinganishwa na shilingi 715,825.43 milioni Juni 2009, sawa na ongezeko la asilimia 2.3.

124. Katika mwaka 2009/10, malipo ya mafao kwa wastaafu yaliongezeka na kufikia shilingi 274.3 bilioni, kutoka shilingi 142.4 bilioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 92.6. Hii ilitokana na ongezeko la mishahara ya watumishi wa umma ambayo ilipelekea wastaafu kulipwa mafao makubwa na kuongezeka kwa idadi ya wastaafu.

125. Mwaka 2009/10, uwekezaji katika dhamana za Serikali ulishuka hadi shilingi 7,584 milioni, kutoka shilingi 141,516 milioni mwaka 2008/09, sawa na upungufu wa asilimia 94.6. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa faida itokanayo na riba katika dhamana za Serikali.

**Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

126. Katika mwaka 2009/10, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulisajili wanachama 506,218 ikilinganishwa na wanachama 475,993 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 6.35. Mfuko ulikusanya michango kutoka kwa wanachama yenye thamani ya shilingi 295,787.14 milioni mwaka 2009/10, ikilinganishwa na shilingi 253,343.47 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilima 16.8. Ongezeko hilo lilitokana na usajili wa wanachama wapya 89,255 na waajiri wapya 1,755 kuwasilisha michango kwa wakati.

127. Mwaka 2009/10, mafao yaliyotolewa kwa wanachama yalikuwa shilingi 111,651.15 milioni ikilinganishwa na shilingi 84,638.22 milioni mwaka

2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 31.9. Aidha, idadi ya wanachama waliopata mafao ilipungua hadi 138,999 mwaka 2009/10 kutoka 207,860 mwaka 2008/09.

128. Thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi iliongezeka kutoka shilingi 847,486.6 milioni mwaka 2008/09, hadi shilingi 1,029,206.2 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 21.4. Vilevile, thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka kutoka shilingi 158,838.5 milioni mwaka 2008/09, hadi shilingi 185,316.8 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Aidha, mapato kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi yalifikia shilingi 73,920.0 milioni mwaka 2009/10, kutoka shilingi 45,606.0 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 62.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji katika mitaji mbalimbali ikiwemo mali zisizohamishika, mikopo ya muda mrefu, amana za muda maalum na dhamana za Serikali.

129. Thamani halisi ya mali za Mfuko kwa ajili ya mafao ilikuwa shilingi 1,129,179.9 milioni mwaka 2009/10, ikilinganishwa na shilingi 921,192.8 milioni mwaka 2008/09. Mali za Mfuko zilikuwa na thamani ya shilingi 1,198,201.0 milioni mwaka 2009/10, ikilinganishwa na shilingi 969,835.0 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 23.6.

**Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali (GEPF)**

130. Mwaka 2009/10, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali iliongezeka na kufikia 35,279, kutoka wanachama 30,227 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Aidha, mafao yaliyotolewa kwa wanachama yaliongezeka kutoka shilingi 1,575.7 milioni mwaka 2008/09, hadi shilingi 3,323.7 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 110.9.

131. Thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi vya Mfuko iliongezeka kutoka shilingi 64,935.8 milioni mwaka 2008/09, hadi shilingi 81,673.5 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 25.8. Aidha, mapato yatokanayo

na vitega uchumi hivyo yaliongezeka hadi shilingi 7,693.6 milioni mwaka 2009/10, kutoka shilingi 5,475.1 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 40.0.

**Jedwali Na. 5.1: Thamani ya Uwekezaji katika Vitega Uchumi vya Mfuko (Shs.Milioni)**

| Aina ya Uwekezaji | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Hati fungani | 9,082.73 | 12,365.55 | 11,845.49 | 14,556.60 | 2,099.94 | -85.6% |
| Hawala za Serikali | 7,183.13 | 10,974.80 | 16,727.45 | 21,787.89 | 31,230.34 | 43.3% |
| Mali za Serikali | 78.35 | 78.35 | 4.40 | 4.40 | 4.41 | 0.2% |
| Amana za Muda Maalumu | 4,915.00 | 10,030.00 | 15,790.00 | 20,040.00 | 37,864.90 | 88.9% |
| Hisa | 941.14 | 2,077.63 | 2,314.96 | 3,320.94 | 3,320.94 | 0.0% |
| "Corporate Bond" | 1,000.00 | 1,000.00 | 800.00 | 1,600.00 | 1,400.00 | -12.5% |
| Mikopo | - | | 2,000.00 | 2,000.00 | 4,100.00 | 105.0% |
| UTT | 1,000.00 | 799.99 | 799.99 | 799.99 | 799.99 | 0.0% |
| Majengo | - | - | - | 826.00 | 853.00 | 3.3% |
| **Jumla** | **24,200.35** | 37,326.32 | 50,282.29 | 64,935.82 | 81,673.52 | 25.8% |

Chanzo: Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali

**Jedwali Na. 5.2: Mapato kutokana na Uwekezaji mwaka 2005/06 – 2009/10 (Shs.miln)**

| Aina | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Hawala za Hazina | 968.70 | 994.41 | 1,702.55 | 1,064.88 | 812.30 | -23.7% |
| Hawala za Serikali | 519.20 | 890.81 | 1,510.25 | 2,233.26 | 3,454.94 | 54.7% |
| Mali za Serikali | 13.70 | 13.70 | 15.42 | 1.28 | 1.28 | |
| Amana za Muda Maalumu | 437.50 | 717.49 | 1,337.17 | 1,591.56 | 2,525.21 | 58.7% |
| Gawio | 68.70 | 119.76 | 177.23 | 171.96 | 296.75 | 72.6% |
| "Corporate Bond" | 127.00 | 126.65 | 120.98 | 95.26 | 226.47 | 137.7% |
| UTT | - | 233.47 | - | - | - | |
| Riba | - | - | - | 311.50 | 376.67 | 20.9% |
| Kodi ya Pango | - | - | - | 5.40 | - | - |
| **Jumla** | 2,134.80 | 3,096.29 | 4,863.60 | 5,475.10 | 7,693.62 | 40.5% |

Chanzo: Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

132. Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya iliongezeka na kufikia 373,326 mwaka 2009/10, ikilinganishwa na wanachama 332,650 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa wafanyakazi wapya Serikalini na marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambayo yalijumuisha makundi mengine kama wanafunzi, vikundi vya dini na halmashauri. Vilevile, michango kutoka kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi 79,388.5 milioni mwaka 2008/09, hadi shilingi 96,618.8 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 21.7. Michango hii ilitokana na ongezeko la mishahara ya wafanyakazi wa Serikali na wanachama katika Mfuko.

133. Hadi kufikia Juni, 2010, Mfuko ulisajili vituo vya afya 5,576, ikilinganishwa na vituo vya afya 4,493 Juni 2009. Kati ya hivyo, vituo 4,652

sawa na asilimia 83.4 ni vya Serikali; vituo 658 sawa na asilimia 11.8 ni vya mashirika ya dini; na vituo 266 sawa na asilimia 4.8 ni vya watu binafsi.

134. Mwaka 2010, Mfuko uliendelea kutoa huduma mbalimbali za mafao kama vile, ada ya uandikishaji; huduma kwa wagonjwa wa nje; huduma kwa wagonjwa waliolazwa; huduma ya upasuaji na vipimo vya uchunguzi. Mfuko pia ulitoa huduma ya matibabu ya meno; na miwani ya kuonea na kusomea.

135. Mwaka 2009/10, Mfuko ulitoa mafao yenye thamani ya shilingi 25,154.1 milioni, kati ya maombi ya shilingi 27,825.3 milioni ikilinganishwa na mafao yenye thamani ya shilingi 16,359.0 milioni, kati ya maombi ya shilingi 17,781.6 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 53.8 ya mafao yaliyolipwa. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanachama wanaotumia kadi za bima ya afya.

136. Mwaka 2009/10, mapato yatokanayo na vitega uchumi yaliongezeka hadi shilingi 17,115.7 milioni kutoka shilingi 16,359.0 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Mapato kutoka vyanzo vinginevyo yalipungua kutoka shilingi 274.5 milioni mwaka 2008/09 hadi shilingi 205.6 milioni mwaka 2009/10, sawa na upungufu wa asilimia 25.1.

**Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)**

137. Katika mwaka 2009/10, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa iliongezeka na kufikia 73,833, kutoka wanachama 66,394 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 11.2. Aidha, Mfuko ulikusanya michango kutoka kwa wanachama wake kiasi cha shilingi 54,235.9 milioni katika mwaka 2009/10, ikilinganishwa na shilingi 47,048.5 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 16.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa usajili wa wanachama wapya. Vilevile, mafao yaliyolipwa kwa wanachama mwaka 2009/10 yalikuwa shilingi 22,507.9 milioni, ikilinganishwa na shilingi 14,892.4 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 51.1. Aidha, mwaka 2010, Mfuko uliongeza mafao mapya mawili ambayo ni: mafao ya

uzazi na mafao ya msaada wa mazishi, na hivyo kufanya jumla ya mafao yanayotolewa na Mfuko kufikia sita.

138. Thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi iliongezeka kutoka shilingi 209,698.4 milioni mwaka 2008/09, hadi shilingi 265,567.2 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 26.6. Thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka kutoka shilingi 104,767.6 milioni mwaka 2008/09, hadi shilingi 133,487.0 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la la asilimia 27.4 .

139. Mwaka 2009/10, mapato kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi yalifikia shilingi 26,648.9 milioni, kutoka shilingi 20,911.7 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 27.4. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji katika mitaji mbalimbali ikiwemo mali zisizohamishika, mikopo ya muda mrefu, amana za muda maalum na dhamana za Serikali. Aidha, thamani halisi ya mali za Mfuko ilikuwa ni shilingi 361,959.4 milioni mwaka 2009/10, ikilinganishwa na shilingi 271,478.8 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 33.3.

**Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA)**

140. Mwaka 2010, idadi ya makampuni yaliyoandikishwa kufanya biashara ya bima nchini yalikuwa 25, ikilinganishwa na makampuni 24 mwaka 2009. Kati ya hayo, makampuni 19 yaliandikishwa kufanya biashara ya bima za kawaida pekee, makampuni mawili yalifanya biashara ya bima za maisha pekee na makampuni manne yalifanya bima za kawaida na za maisha. Aidha, mauzo katika soko la Bima kwa mwaka 2010 yalikua kwa asilimia 18.4, kufikia shilingi 283.2 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 231.2 bilioni mwaka 2009. Bima za kawaida zilichangia asilimia 89.3 na bima za maisha zilichangia asilimia 10.7 ya jumla ya mauzo hayo.

**Jedwali Na 5.3: Mauzo ya Bima 2006 – 2010**

| | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|
| Bima za Kawaida (Sh.milioni) | 105,268 | 135,891 | 164,497 | 209,559 | 252,947 |
| Ukuaji % | 16% | 22.5% | 17.4% | 21.5% | 17.2% |
| Mchango kwa Jumla (%) | 91.3% | 88.2% | 86.2% | 90.6% | 89.3% |
| Bima za Maisha (Sh.milioni) | 10,014 | 18,149 | 26,338 | 21,678 | 30,273 |
| Ukuaji % | 9.0% | 44.8% | 31.1% | -21.5% | 28.4% |
| Mchango kwa Jumla (%) | 8.7% | 11.8% | 13.8% | 9.4% | 10.7% |
| Jumla ya Mauzo (Sh.milioni) | 115,282 | 154,040 | 190,835 | 231,237 | 283,220 |
| Ukuaji % | 15.1% | 25.2% | 19.3% | 17.5% | 18.4% |

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

141. Thamani ya mali za makampuni ya bima kwa mwaka 2010 zilifikia shilingi 369.2 bilioni kutoka shilingi 320.6 bilioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 13.2. Madeni ya makampuni ya bima yaliongezeka na kufikia shilingi 248.2 bilioni mwaka 2010, ikilinganishwa na shilingi 219.0 bilioni mwaka 2009.

**Jedwali 5.4: Thamani za Mali na Madeni ya Makampuni ya Bima 2006 - 2010**

| Mali na Madeni | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Mali (Sh. milioni) | 183,717 | 212,458 | 289,456 | 320,611 | 369,187 |
| Ukuaji (%) | 28.00 | 13.53 | 26.60 | 9.72 | 13.16 |
| Jumla ya Madeni (Sh. milioni) | 111,367 | 133,081 | 202,238 | 219,022 | 248,223 |
| Ukuaji (%) | 12.00 | 16.32 | 34.20 | 7.66 | 11.76 |
| Ziada ya Mali (Shs. milioni) | 72,350 | 79,377 | 87,218 | 101,589 | 120,960 |
| Ukuaji (%) | - | 8.85 | 8.99 | 14.15 | 16.02 |

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

**Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE)**

142. Mwaka 2010, thamani ya hisa zote zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es salaam ilishuka kufikia shilingi 4,895.5. bilioni kutoka shilingi 5,013.2 bilioni Mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 2.4. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa bei ya hisa za NMB, CRDB na Kenya Airways. Aidha, Vilevile, katika kipindi kilichoishia Desemba 2010, jumla ya hisa 190.4 milioni zenye thamani ya shilingi 35.99 bilioni ziliuzwa na kununuliwa katika Soko la hisa ikilinganishwa na hisa 121.1 milioni zenye thamani ya shilingi 48.7 bilioni Desemba 2009, sawa na upungufu wa asilimia 26.1 kwa upande wa thamani ya mauzo na asilimia 57.3 kwa upande wa idadi ya hisa. Aidha, Katika kipindi hicho, fahirisi katika Soko ilipungua kutoka 1,239.93 mwaka 2009, hadi 1,163.89 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 6.1.

143. Hatifungani za Serikali zenye thamani ya shilingi 1,615.79 bilioni ziliorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es salaam mwaka 2010, ikilinganishwa na shilingi 966.41 bilioni zilizoorodheshwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 67.2. Aidha, thamani ya hatifungani za Serikali zilizouzwa na kununuliwa katika soko la hisa ziliongezeka na kufikia shilingi 205.8 bilioni mwaka 2010, kutoka shilingi 139.4 bilioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 47.6. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka uhamasishaji na elimu inayotolewa kwa umma kuhusu masoko ya mitaji, dhamana na uwekezaji. Aidha, katika mwaka 2009/10, faida katika Soko la Hisa iliongezeka hadi shilingi 196.8 milioni, kutoka shilingi 133.4 milioni mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 47.5.

Jedwali Na. 5.5: Muhtasari wa Utendaji wa Soko la Hisa 2010

| Kigezo cha Soko | 2009 | 2010 | Badiliko, % |
|---|---|---|---|
| Jumla ya Hisa zote zilizotolewa sokoni | 6,981,012,160 | 6,981,012,160 | 0.0% |
| Thamani ya Hisa zote Zilizouzwa/Kununuliwa kwa Shilingi za Tanzania (Bilioni) | 48,698.98 | 35,986.31 | -26.1% |
| Thamani ya Hisa zote zilizoorodheshwa kwa Shilingi ya Tanzania (Bilioni) | 5,013.17 | 4,895.47 | -2.3% |
| Idadi ya hisa zilizouzwa na kununuliwa | 121,065,172 | 190,387,510 | 57.3% |
| Idadi ya Maafikiano | 21,149 | 11,336 | -46.4% |
| Fahirisi | 1,239.9256 | 1,163.891 | -6.1% |

Chanzo: Soko la Hisa la Dar es salaam

**Benki ya Posta**

144. Mwaka 2010, idadi ya wateja wapya waliojiunga na benki walikuwa 57,505, hivyo kufanya jumla ya wateja kufikia 582,774, ikilinganishwa na wateja 525,269 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Aidha, amana za wateja katika Benki ya Posta ziliongezeka hadi shilingi 107,797 milioni, kutoka shilingi 88,331 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 22.0. Ongezeko hilo lilitokana na mikakati ya kuongeza amana ikiwa ni pamoja na uhamasishaji na kampeni za ukuzaji wa masoko na vilevile mikakati ya kuboresha huduma kwa kutumia ATM.

145. Mwaka 2010, Benki iliendelea kuwekeza rasilimali zake katika mabenki mengine, dhamana za Serikali za muda mrefu na dhamana za makampuni binafsi. Hadi Desemba 2010, thamani ya vitega uchumi iliongezeka na kufikia shilingi 112,464 milioni, ikilinganishwa na shilingi 86,572 milioni Desemba 2009, sawa na ongezeko la asilimia 29.9. Uwekezaji katika hatifungani za Serikali uliongezeka hadi shilingi 25,229 milioni mwaka 2010, kutoka shilingi 21,229 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 19.8. Mikopo iliyotolewa ilikuwa na thamani ya shilingi 64,790 milioni mwaka 2010,

ikilinganishwa na shilingi 37,069 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 74.8. Aidha, idadi ya wakopaji iliongezeka kutoka 27,899 hadi wakopaji 30,564 katika kipindi hicho. Mchanganuo wa mikopo unaonesha kuwa sehemu kubwa ya mikopo ilitolewa kwa watumishi (asilimia 90.7) kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 5.6. Mchanganuo wa Mikopo katika**

**Benki ya Posta (Sh. Milioni)**

| Aina ya Mkopo | 2009 | 2010 | Mchango (%) |
|---|---|---|---|
| Mikopo ya biashara | 2,325.0 | 4,244.0 | 6.6 |
| Mikopo ya watumishi | 33,204.0 | 58,757.0 | 90.7 |
| Mikopo midogo midogo | 1,143.0 | 1,534.0 | 2.4 |
| Mikopo ya uwezeshaji | 397.0 | 255.0 | 0.4 |
| **Jumla** | **37,069.0** | **64,790.0** | 100.0 |

Chanzo: Benki ya Posta Tanzania

146. Mwaka 2010, mapato ya Benki kutokana na riba na mapato mengineyo yalikuwa shilingi 20,122 milioni, ikilinganishwa na shilingi 17,887 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Ongezeko hili lilitokana ukuaji wa mikopo iliyotolewa na Benki. Aidha, faida ya Benki kabla ya kodi iliongezeka na kufikia shilingi 955 milioni, kutoka shilingi 897 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 6.5.

Jedwali Na.27

## MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Sh. milioni

| | Kipindi kinachoishia mwezi Juni | | | | | | | | | Badiliko 2009-2010 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2006 | 2009 | 2010 | Kiasi | % |
| Ujazi wa fedha, maana finyu zaidi (M0)* | 429384 | 473704 | 590441 | 734912 | 853959 | 1047221 | 2079537 | 2678959 | 3369300 | 690341 | 25.8% |
| Ujazi wa fedha, maana finyu (M1) | 815576 | 981148 | 1186063 | 1528833 | 1810429 | 2170664 | 2829944 | 3149153 | 4134700 | 985547 | 31.3% |
| Amana za Akiba na za Muda Maalum | 517948 | 577636 | 670263 | 837675 | 1226999 | 1480065 | 2000773 | 2623306 | 3153400 | 530094 | 20.2% |
| Ujazi wa fedha, maana pana (M2) | 1333524 | 1558784 | 1856326 | 2366508 | 3037428 | 3650728 | 4830716 | 5772458 | 7288100 | 1515642 | 26.3% |
| Amana za fedha za kigeni | 464366 | 647109 | 746609 | 899976 | 1368687 | 1666476 | 1781555 | 2061636 | 2513800 | 452164 | 21.9% |
| Ujazi wa fedha, maana pana zaidi (M3) | 1797890 | 2205893 | 2602935 | 3266484 | 4406115 | 5317204 | 6612271 | 7834095 | 9801900 | 1967805 | 25.1% |
| Akiba halisi ya mali za kigeni (Foreign Assets) | 1293645 | 1871286 | 2134183 | 2279294 | 2914493 | 3383818 | 3628827 | 4196787 | 5265500 | 1068713 | 25.5% |
| Amana Halisi Nchini | 750102 | 334607 | 468752 | 987131 | 1491622 | 1936424 | 2983319 | 3669241 | 4536400 | 867159 | 23.6% |
| Karadha Nchini | 684920 | 858203 | 1123588 | 1504012 | 2439087 | 2785793 | 3384781 | 4771737 | 6124100 | 1352363 | 28.3% |
| Mikopo kwa Serikali | 202879 | 199679 | 157607 | 284638 | 729393 | 449793 | -151058 | 61509 | 721300 | 659791 | 1072.7% |
| Mikopo kwa sekta isiyo serikali | 482041 | 658524 | 965981 | 1219374 | 1709694 | 2336000 | 3535839 | 4710228 | 5402800 | 692572 | 14.7% |
| Amali halisi nyinginezo (net other items) | 65181 | -523596 | -654836 | -516881 | -947466 | -849365 | -401462 | -1102495 | -1587700 | -485205 | 44.0% |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania.

* Fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mabenki

## VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 28

| | Kipindi kinachoishia Juni | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
| **Ujazi wa fedha, maana finyu zaidi (M0)*** | 14.5% | 10.3% | 24.6% | 24.5% | 16.2% | 22.6% | 98.6% | 28.8% | 25.8% |
| **Ujazi wa fedha, maana finyu (M1)** | 18.0% | 20.3% | 20.9% | 28.9% | 18.4% | 19.9% | 67.7% | 21.0% | 31.3% |
| Amana za Akiba na za Muda maalum | 27.0% | 11.5% | 16.0% | 25.0% | 46.5% | 20.6% | 35.2% | 31.1% | 20.2% |
| **Ujazi wa fedha, maana pana (M2)** | 21.3% | 16.9% | 19.1% | 27.5% | 28.4% | 20.2% | 52.9% | 24.7% | 26.3% |
| Amana za fedha za kigeni | 24.2% | 39.4% | 15.4% | 20.5% | 52.1% | 21.8% | 6.9% | 17.5% | 21.9% |
| **Ujazi wa fedha, maana pana zaidi (M3)** | 22.1% | 22.7% | 18.0% | 25.5% | 34.9% | 20.7% | 38.5% | 22.9% | 25.1% |
| **Akiba halisi ya mali za kigeni (Foreign Assets)** | 29.2% | 44.7% | 14.0% | 6.8% | 27.9% | 16.1% | 7.2% | 15.7% | 25.5% |
| **Amana Halisi Nchini** | 59.1% | -55.4% | 40.1% | 110.6% | 51.1% | 29.8% | 54.1% | 23.0% | 23.6% |
| Karadha Nchini | 5.8% | 25.3% | 30.9% | 33.9% | 62.2% | 14.2% | 21.5% | 41.0% | 28.3% |
| Mikopo kwa serikali | -24.6% | -1.6% | -21.1% | 80.6% | 156.3% | -38.3% | -133.6% | -140.7% | 1072.7% |
| Mikopo kwa sekta isiyo serikali | 27.4% | 36.6% | 46.7% | 26.2% | 40.2% | 36.6% | 51.4% | 33.2% | 14.7% |
| Amali halisi nyinginezo (other items net) | -137.1% | 903.3% | 25.1% | -21.1% | 83.3% | -10.4% | -52.7% | 174.6% | 44.0% |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mabenki

## MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na. 29

| | 2000/01 | 2001/02 | 2002/03 | 2003/04 | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shs/dola mwishoni mwa mwaka | 888.0 | 946.9 | 1047.4 | 1107.3 | 1126.3 | 1258.5 | 1268.3 | 1180.9 | 1299.41 | 1379.4 |
| Shs/dola wastani wa mwaka | 830.5 | 931.2 | 1003.4 | 1089.4 | 1122.7 | 1182.9 | 1267.2 | 1183.8 | 1313.5 | 1331.5 |
| Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%) | 4.1% | 12.1% | 7.8% | 8.6% | 3.1% | 5.4% | 7.1% | [illegible]6% | 11.0% | 1.4% |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Jedwali Na. 30

| Aina ya Shughuli | Kiwango kilichokuwa mwezi Desemba (Sh. Milioni) | | | | Ukuaji (%) | Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | | |
| Sekta ya Umma | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | - | - |
| Uzalishaji katika kilimo | 298,419.8 | 515,936.0 | 467,097.1 | 741,288.7 | 58.7 | 53.2 |
| Uvuvi | 18,180.1 | 17,227.6 | 15,660.1 | 35,363.7 | 125.8 | 2.5 |
| Misitu | 6,800.2 | 7,183.3 | 18,058.5 | 19,219.9 | 6.4 | 1.4 |
| Uwindaji | 4,323.0 | 242.3 | 56.2 | 122.3 | 117.8 | 0.0 |
| Huduma za kifedha | 92,269.3 | 122,001.1 | 105,843.7 | 123,314.9 | 16.5 | 8.9 |
| Madini na Uchimbaji mawe | 41,480.8 | 37,727.8 | 18,926.3 | 44,545.4 | 135.4 | 3.2 |
| Bidhaa za Viwandani | 559,422.8 | 612,670.6 | 565,775.5 | 819,315.0 | 44.8 | 58.8 |
| Majengo na Ujenzi | 104,102.5 | 142,992.8 | 148,713.4 | 192,777.8 | 29.6 | 13.8 |
| Mali Isiyohamishika | 49,137.9 | 76,446.0 | 101,055.8 | 240,162.2 | 137.7 | 17.2 |
| Kukodisha | 890.5 | 11,906.3 | 3,438.7 | 13,031.4 | 279.0 | 0.9 |
| Uchukuzi na Mawasiliano | 208,556.8 | 320,600.6 | 457,407.2 | 543,724.5 | 18.9 | 39.0 |
| Biashara | 511,317.6 | 737,105.8 | 926,626.3 | 1060,807.5 | 14.5 | 76.1 |
| Utalii | 15,903.4 | 29,165.5 | 27,097.6 | 43,935.7 | 62.1 | 3.2 |
| Mahoteli na Migahawa | 112,782.0 | 150,978.4 | 187,204.6 | 297,162.0 | 58.7 | 21.3 |
| Ghala na Uhifadhi | 16,202.1 | 4,020.3 | 5,061.4 | 148.1 | -97.1 | 0.0 |
| Umeme | 117,059.9 | 183,487.0 | 193,609.6 | 153,626.0 | -20.7 | 11.0 |
| Gesi | 12,466.0 | 20,938.2 | 37,097.1 | 135,680.9 | 265.7 | 9.7 |
| Maji | 1,453.8 | 2,035.7 | 2,193.8 | 2,235.4 | 1.9 | 0.2 |
| Elimu | 33,309.1 | 42,927.7 | 70,921.5 | 70,849.7 | -0.1 | 5.1 |
| Afya | 10,310.2 | 21,713.3 | 20,847.6 | 12,692.6 | -39.1 | 0.9 |
| Huduma nyingine zo | 253,069.7 | 390,654.2 | 369,979.3 | 86,207.3 | -76.7 | 6.2 |
| Watu Binafsi | 508,818.3 | 928,510.5 | 1,063,142.9 | 1,393,170.7 | 31.0 | 100.0 |
| Jumla | 2,976,276.0 | 4,376,471.1 | 4,805,814.0 | 6,029,381.9 | 25.5 | 432.8 |
| Dhamana za Serikali | 1,211,837.0 | 1049,237.6 | 1,127,500.0 | 1,429,403.7 | 26.8 | |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali Na. 31

## MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA

Sh. milioni

| Aina ya amana | Kipindi kinachoishia mwezi Juni | | | | | | | Badiliko 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Kiasi | % |
| Amana za hundi | 793920 | 942660 | 1125533 | 1556902 | 1721150 | 2454300 | 733150 | 42.6 |
| Amana za muda maaium | 328711 | 455180 | 541020 | - | - | - | - | - |
| Amana za akiba/Transferable deposits* | 508964 | 691508 | 864118 | 2000252 | 2622901 | 3153400 | 530499 | 20.2 |
| Amana za fedha za kigeni | 899976 | 1353523 | 1666479 | 1780934 | 2037101 | 2513800 | 476699 | 23.4 |
| Jumla | 2531571.8 | 3442871.0 | 4197150.1 | 5338087.3 | 6381151.9 | 8121500.0 | 1740348 | 27.3 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia Juni 2009 Amana za muda maalum na zile za akiba zimejumuishwa pamoja

Jedwali Na. 32

## VIWANGO VYA WASTANI VYA RIBA

| Aina ya riba | Kipindi kinachoishia mwezi Juni | | | | | Kuishia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Dec. 2010 |
| Riba ya Benki Kuu (Discount rate) | 13.40 | 21.42 | 12.84 | 10.31 | 7.58 | 7.58 |
| Riba za Amana | | | | | | |
| Amana za akiba | 2.50 | 2.63 | 2.79 | 2.69 | 2.82 | 2.41 |
| Amana za muda maalum | 6.60 | 7.69 | 6.66 | 6.77 | 5.88 | 5.11 |
| Riba za mikopo | | | | | | |
| Mikopo ya muda mfupi | 15.80 | 13.95 | 13.93 | 14.57 | 13.92 | 12.40 |
| Mikopo ya muda wa kati na mrefu | 14.53 | 15.68 | 16.64 | 15.23 | 14.73 | 12.48 |
| Riba za Hawala za Hazina | | | | | | |
| Siku 91 | 7.80 | 12.62 | 5.76 | 5.56 | 2.89 | 5.24 |
| Siku 182 | 8.50 | 16.74 | 7.63 | 7.86 | 2.59 | 6.20 |
| Siku 364 | 9.60 | 18.39 | 10.00 | 9.11 | 6.08 | 7.67 |

Chanzo:Benki Kuu ya Tazania

# SURA YA 6

## RASILIMALI WATU

### Idadi ya Watu na Maendeleo

147. Idadi ya watu Tanzania kwa mwaka 2010 ilikadiriwa kuwa 43,187,823. Kati ya hao, wanawake walikuwa 21,935,400, sawa na asilimia 50.8 na wanaume walikuwa 21,252,423, sawa na asilimia 49.2. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na jumla ya watu 41,914,311, sawa na asilimia 97.1 ya watu wote ambapo Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 1,273,512, sawa na asilimia 2.9 ya watu wote. Mgawanyo wa watu unaonesha kuwa watu 31,809,808, sawa na asilimia 73.7 ya watu wote wanaishi vijijini, wakati watu 11,378,015, sawa na asilimia 26.3 wanaishi mijini. Makadirio haya yanatokana na kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu cha asilimia 2.9 cha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002.

148. Mchanganuo wa idadi ya watu Tanzania mwaka 2010 unaonesha kuwa asilimia 44.4 ya watu wote ni wenye umri chini ya miaka 15. Idadi ya watu wenye umri chini ya miaka mitano ni 7,798,254, sawa na asilimia 18.1 ya watu wote. Kati ya hao, wanaume walikadiriwa kuwa 3,932,089 na wanawake 3,866,165. Idadi ya watu wenye umri kati ya miaka 5-14 ilikuwa ni 11,366,854, sawa na asilimia 26.3 ya watu wote. Kati ya hao, wanaume walikuwa 5,700,541 na wanawake 5,666,403. Idadi ya watu waliokuwa na umri kati ya miaka 15 - 24 walikadiriwa kuwa 8,580,351, sawa na asilimia 19.9 ya watu wote. Kati ya hao, 4,279,696 walikuwa ni wanawake na wanaume 4,300,655. Idadi ya watu wenye umri kati ya miaka 25 - 64 ilikadiriwa kuwa 14,080,929, sawa na asilimia 32.6 ya watu wote. Idadi ya watu wenye miaka kati ya 15 - 64, ambao ndio nguvukazi, ilikuwa ni 22,661,280, sawa na asilimia 52.5 ya watu wote. Kati ya hao 11,684,533 walikuwa ni wanawake na wanaume 10,976,747. Watu wenye umri wa miaka 65 au zaidi walikuwa ni 1,361,435, sawa na asilimia 3.2 ya watu wote. Kati ya hao, wanawake walikuwa 718,299 na wanaume ni 643,136.

**Jedwali Na. 6.1: Mchanganuo wa Idadi ya Watu kwa Umri**

| Umri | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| < 5 | 3,932,089 | 3,866,165 | 7,798,254 | 18.1% |
| 5 hadi 14 | 5,700,451 | 5,666,403 | 11,366,854 | 26.3% |
| 15 hadi 24 | 4,300,655 | 4,279,696 | 8,580,351 | 19.9% |
| 25 hadi 64 | 6,676,092 | 7,404,837 | 14,080,929 | 32.6% |
| 65+ | 643,136 | 718,299 | 1,361,435 | 3.2% |
| **Jumla kuu** | 21,252,423 | 21,935,400 | 43,187,823 | |
| 15 hadi 64 | 10,976,747 | 11,684,533 | 22,661,280 | 52.5% |

**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

149. Kutokana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2010, msongamano wa watu ulikadiriwa kuwa watu 49 kwa kila kilometa moja ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Bara, msongamano wa watu ulikuwa ni watu 47 wakati upande wa Tanzania Zanzibar ulikuwa ni watu 518 kwa kila kilometa ya mraba. Mgawanyiko wa watu unaonesha kuwa mkoa wenye msongamano mkubwa zaidi wa watu ni Dar es Salaam, ambao una watu 2,238 kwa kila kilometa ya mraba, ikifuatiwa na Mwanza iliyokuwa na watu 181 kwa kila kilometa ya mraba, Kilimanjaro watu 123 kwa kila kilometa ya mraba na Mara watu 84 kwa kila kilometa ya mraba. Mkoa uliokuwa na kiwango kidogo zaidi cha msongamano wa watu ulikuwa ni Lindi, ambao ulikuwa na watu 14 kwa kila kilometa ya mraba ukifuatiwa na Ruvuma na Rukwa ambayo ilikuwa na watu 22 kwa kilometa ya mraba kila mmoja. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mikoa yote ina msongamano mkubwa wa watu, kuanzia watu 132 hadi 2,101 kwa kilometa ya mraba.

150. Mwaka 2010, mtawanyiko wa watu kimkoa unaonesha kuwa mkoa wa Shinyanga uliendelea kuwa na idadi kubwa zaidi ya watu. Mkoa huo ulikuwa na watu 3,841,788 mwaka 2010, sawa na asilimia 8.9 ya watu wote Tanzania; ukifuatiwa na Mwanza wenye jumla ya watu 3,566,263 (asilimia 8.3); na Dar es Salaam watu 3,118,132 (asilimia 7.2). Idadi kubwa ya watu mkoani Shinyanga

inatokana na kiwango kikubwa cha uzazi kilichofikia watoto 7.3 kwa mwanamke mmoja. Mwaka 2010, mkoa wa Lindi ulikuwa na watu 923,607 ambayo ni idadi ndogo zaidi ya watu ikilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa uliokuwa na watu wengi zaidi ulikuwa ni Mjini Magharibi (483,205) na mkoa uliokuwa na idadi ndogo ya watu ulikuwa ni Kusini Unguja (112,612). Idadi ndogo ya watu katika mikoa ya Lindi na Kusini Unguja ilitokana na idadi kubwa ya watu kuhamia mikoa mingine.

151. Mwaka 2010, idadi ya watu waliozaliwa walikadiriwa kuwa 1,678,325 na idadi ya vifo ilikadiriwa kuwa 573,213. Wastani wa idadi ya watoto waliozaliwa ilikuwa 38.1 kwa kila watu 1,000 *(Crude Birth Rate)* wakati kiwango cha vifo kilikuwa wastani wa watu 13.5 kwa kila watu 1,000. Kiwango cha uzazi *(Total Fertility Rate)* nchini kilikadiriwa kuwa watoto 5.4 kwa mwanamke mmoja. Kiwango cha vifo vya watoto wachanga kilikadiriwa kuwa vifo 51.0 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa, wakati kiwango cha vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano kilikadiriwa kuwa vifo 81.0 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa.

**Nguvukazi na Ajira**

152. Kulingana na matokeo ya Utafiti wa Nguvukazi na Ajira ya mwaka 2006, nguvukazi nchini ilikuwa watu milioni 18.8 ambapo milioni 9.0 walikuwa wanaume na milioni 9.7 walikuwa wanawake. Vilevile, matokeo hayo yanaonesha kuwa watu milioni 16.6 walikuwa wameajiriwa na milioni 2.2 walikuwa hawajaajiriwa, sawa na asilimia 11.7 ya nguvukazi yote nchini. Kati ya walioajiriwa, watu milioni 8.5 walikuwa wanawake na wanaume milioni 8.0. Kati ya wasiokuwa na ajira, wanaume walikuwa 967,847 na wanawake walikuwa 1,226,545. Hata hivyo, kulingana na matokeo ya Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, maoteo ya nguvukazi nchini (miaka 15 – 64) mwaka 2010 ilikadiriwa kuwa watu 22,661,280. Sekta ya kilimo iliendelea kuongoza, ambapo zaidi ya asilimia 70 ya waliojiriwa nchini wanajishughulisha na kilimo.

153. Mwaka 2010, Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) ilisaidia wananchi 6,645 kupata ajira. Kati ya hao wanaume walikuwa 4,398, sawa na asilimia

66.2 na wanawake 2,247, sawa na asilimia 33.8. Aidha, Wakala ulitoa huduma kwa wateja wanaotafuta ajira kwa kuboresha wasifu wao na kuwaelekeza mbinu za ujasiriamali. TaESA pia iliendesha mafunzo kwa wanaotafuta ajira juu ya mbinu mbalimbali za kutafuta ajira, kufaulu usaili, taarifa za soko la ajira na ushauri juu ya masuala yanayohusu huduma za ajira. Vilevile, katika kuhakikisha uwepo wa viwango na ubora katika utoaji wa huduma za ajira nchini, TaESA ilisajili wakala binafsi 14 za huduma za ajira nchini na kuzitambua kampuni nyingine 20 za huduma hiyo.

JUMLA YA IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2005-2009

Jedwali Na. 33

| Mkoa | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009* | 2010** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 1,786,073 | 1,896,786 | 1,951,071 | 2,004,544 | 2,058,630 | 2111764 |
| Arusha | 1,427,904 | 1,475,489 | 1,522,975 | 1,570,394 | 1,617,728 | 1664780 |
| Kilimanjaro | 1,435,847 | 1,503,014 | 1,535,975 | 1,569,212 | 1,602,530 | 1635870 |
| Tanga | 1,716,271 | 1,753,284 | 1,837,661 | 1,880,389 | 1,923,468 | 1966908 |
| Morogoro | 1,881,113 | 1,929,087 | 1,975,160 | 2,021,713 | 2,068,426 | 2115275 |
| Pwani | 944,145 | 968,637 | 991,586 | 1,014,968 | 1,038,654 | 1062574 |
| Dar es Salaam | 2,799,241 | 2,801,675 | 2,881,548 | 2,961,150 | 3,040,118 | 3118132 |
| Lindi | 816,815 | 851,764 | 869,522 | 887,434 | 905,480 | 923607 |
| Mtwara | 1,176,112 | 1,220,248 | 1,246,089 | 1,271,912 | 1,297,751 | 1323568 |
| Ruvuma | 1,192,680 | 1,235,161 | 1,268,738 | 1,303,330 | 1,338,800 | 1375017 |
| Iringa | 1,553,392 | 1,617,696 | 1,649,200 | 1,679,828 | 1,709,225 | 1737382 |
| Mbeya | 2,201,206 | 2,346,388 | 2,423,635 | 2,502,258 | 2,581,792 | 2662156 |
| Singida | 1,150,367 | 1,222,810 | 1,258,545 | 1,294,584 | 1,330,931 | 1367481 |
| Tabora | 1,887,507 | 2,004,115 | 2,086,048 | 2,170,926 | 2,258,664 | 2349374 |
| Rukwa | 1,251,697 | 1,302,278 | 1,349,579 | 1,398,866 | 1,450,118 | 1503184 |
| Kigoma | 1,910,592 | 1970,750 | 1,601,020 | 1,669,078 | 1,740,111 | 1814158 |
| Shinyanga | 3,060,176 | 3,277,784 | 3,411,023 | 3,549,342 | 3,692,941 | 3841787 |
| Kagera | 2,206,814 | 2,210,217 | 2,293,093 | 2,379,637 | 2,469,904 | 2563870 |
| Mwanza | 3,196,714 | 3,168,904 | 3,265,729 | 3,364,378 | 3,464,566 | 3566263 |
| Mara | 1,461,270 | 1,572,068 | 1,631,031 | 1,692,449 | 1,756,442 | 1822866 |
| Manyara | 1,141,376 | 1,198,051 | 1,241,994 | 1,288,280 | 1,337,015 | 1388295 |
| **Tanzania Bara** | **36,197,312** | **37,526,206** | **38,291,222** | **39,474,672** | **40,683,294** | **41,914,311** |
| | | | | | | |
| Kaskazini Unguja | 146,221 | 155,066 | 160.175 | 165,544 | 171,150 | 177095 |
| Kusini Unguja | 99,678 | 103,191 | 105,456 | 107,811 | 110,183 | 112612 |
| Mjini Magharibi | 441446 | 461,759 | 447,716 | 459,502 | 471,341 | 483205 |
| Kaskazini Pemba | 196,221 | 216,174 | 224,951 | 234,142 | 243,759 | 253999 |
| Kusini Pemba | 186,651 | 207,348 | 216,479 | 226,055 | 236,072 | 246601 |
| **Zanzibar** | **1,070,217** | **1,143,538** | **1,154,777** | **1,193,054** | **1,232,505** | **1,273,512** |
| | | | | | | |
| **Tanzania** | **37,267,529** | **38,669,744** | **39,445,999** | **40,667,726** | **41,915,799** | **43,187,823** |

Chanzo: Wizara ya Fedha

Kielelezo: Kwa miaka kati ya 1988 - 2002, jedwali limetayarishwa kutokana na takwimu za Sensa ya Watu ya mwak

* Takwimu za matokeo ya Sensa 2002

** Makadirio kulingana na takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2002

# SEHEMU YA PILI

## UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

## SURA YA 7

## UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

**Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini**

154. Mwaka 2010, miradi 509 yenye thamani ya sh. milioni 7,092,618.68 na fursa za ajira 43,640 ilisajiliwa, ikilinganishwa na miradi 572 yenye thamani ya sh. milioni 2,970,730.1 na fursa za ajira 56,615 iliyosajiliwa mwaka 2009. Kati ya miradi iliyosajiliwa, miradi 438 ilikuwa mipya, ambapo 71 ilikuwa ya upanuzi na ukarabati. Miradi inayomilikiwa na wawekezaji wa ndani ilikuwa 242, wawekezaji wa nje ni 160 na miradi ya ubia ilikuwa 139.

155. Mwaka 2010, shughuli zinazohusiana na uzalishaji viwandani zilivutia wawekezaji wengi zaidi, zikiwa na miradi 183 yenye thamani ya sh.705, 299.14 milioni na fursa za ajira 14,327. Mchanganuo wa uwekezaji katika sekta nyingine ni kama ifuatavyo: Utalii miradi 103 yenye thamani ya sh. 417,083.94 milioni na fursa za ajira 5,452; Majengo ya biashara miradi 92 yenye thamani ya sh. 1,925,186.06 milioni na fursa za ajira 5,078; usafirishaji miradi 62 yenye thamani ya sh. 436,513.14 milioni na fursa za ajira 7,197; kilimo miradi 23 yenye thamani ya sh. 663,710.60 milioni na fursa za ajira 5,169; rasilimali watu miradi 8 yenye thamani ya sh. 6,076.6 milioni na fursa za ajira 412; huduma kwa vitega uchumi miradi 19 yenye thamani ya sh. 213,127.60 milioni na fursa za ajira 4,717; taasisi za fedha miradi 4 yenye thamani ya sh. 2,294.6 milioni na fursa za ajira 86; miundombinu ya kiuchumi miradi 1 yenye thamani ya sh. 6,076.00 milioni na fursa za ajira 22; mawasiliano miradi 5 yenye thamani ya sh. 260,008.00 milioni na fursa za ajira 529; utangazaji miradi 4 yenye thamani ya sh. 158,886.00 milioni na fursa za ajira 463; kompyuta miradi 1 wenye thamani ya sh. 1,218.60 milioni na fursa za ajira 43 na maliasili mradi 1 wenye thamani ya sh. 4,494.00 na fursa za ajira 100.

Mchanganuo wa Miradi Kimkoa

156. Mwaka 2010, mikoa iliyoongoza kwa kupata miradi mingi zaidi ya uwekezaji ni Dar es Salaam iliyosajili miradi 321 ikifuatiwa na Arusha iliyosajili miradi 55. Uwekezaji katika mikoa mingine ulikuwa kama ifuatavyo: Pwani 28; Mwanza 20; Tanga 12; Morogoro 11; Iringa 9; Kilimanjaro, Mbeya, Dodoma miradi sita kila mmoja; Mara 5, Shinyanga, Mtwara, Ruvuma, Lindi miradi minne kila mmoja; Kigoma, Kagera na Manyara miradi mitatu kila mmoja; Tabora, Singida miradi miwili kila mmoja na Rukwa mradi mmoja.

157. Mwaka 2010, idadi ya maombi 11,098 yalishughulikiwa na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji, ikilinganishwa na maombi 12,703 mwaka 2009. Mchanganuo wa maombi unaoneshwa katika Jedwali Na. 7.1.

**Jedwali Na 7.1: Maombi Yaliyoshughulikiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania**

| Huduma | 2009 | 2010 |
|---|---|---|
| Uhamiaji: Daraja A | 327 | 276 |
| Daraja B | 2,578 | 2,386 |
| Kazi | 3,473 | 3,284 |
| Usajili wa Makampuni | 104 | 49 |
| Leseni za Biashara | 62 | 75 |
| Ardhi | 2,191 | 1,677 |
| Kodi | 3,968 | 3,351 |
| **JUMLA** | **12,703** | **11,098** |

Chanzo: Kituo cha Taifa cha Uwekezaji

158. Mwaka 2010, thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 573.3, ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 558.4 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 2.7.

Jedwali Na. 7.2 Uwekezaji Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja, 1995-2010

| Mwaka | Thamani ya Mitaji iliyowekezwa (Dola za Kimarekani Milioni) |
|---|---|
| 1995 | 150.9 |
| 1996 | 148.6 |
| 1997 | 157.8 |
| 1998 | 172.2 |
| 1999 | 516.7 |
| 2000 | 463.4 |
| 2001 | 467.2 |
| 2002 | 387.6 |
| 2003 | 308.2 |
| 2004 | 330.6 |
| 2005 | 447.6 |
| 2006 | 616.6 |
| 2007 | 653.4 |
| 2008 | 744.0 |
| 2009 | 558.4 |
| 2010 | 573.3* |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*Makisio

**Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa sekta binafsi**

159. Mwaka 2010, Serikali iliidhinisha Sera na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Madhumuni ya Sera na Sheria hii ni kuweka mfumo mzuri wa kisheria kwa ajili ya kuratibu ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa miradi na huduma za ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Sambamba na hilo, Serikali kupitia programu za maboresho katika sekta za Sheria (LSRP), Umma (PSRP), Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP), Serikali za Mitaa (LGRP) na Maboresho ya Mazingira ya Biashara (BEST), inaendeleza jitihada za kuondoa urasimu ili kupunguza muda na gharama za kuendesha shughuli za uchumi na biashara. Aidha, Tanzania ilishika nafasi ya 131 ya wepesi wa kufanya biashara (ease of doing business index) kati ya nchi 183, kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia, ikilinganishwa na nafasi ya 127 kwa mwaka 2009.

160. Mwaka 2010, Serikali iliidhinisha rasmi utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji na Biashara. Mpango huu umeainisha majukumu ya kutekelezwa katika viashiria kumi ambavyo ni: uanzishaji wa biashara; ufungaji wa biashara; upatikanaji wa vibali vya ujenzi; uandikishaji wa rasilimali; kuajiri wafanyakazi; ulipaji kodi; wepesi wa biashara ya nje; urahisi wa kupata mikopo; ulinzi wa mikataba ya biashara; na ulinzi wa wawekezaji. Mafanikio kadhaa yalipatikana katika utekelezaji wa Mpango huu ikiwa ni pamoja na: kurahisisha uhakiki wa jina la biashara kupitia tovuti ya BRELA (www.brela-tz.org), pasipo kulazimika kuandika barua kama ilivyokuwa hapo awali; Kuwekwa kwa '*Memorandum and Article of Association*' ya mfano kwenye tovuti ya BRELA kwa lengo la kupunguza gharama kwa wanaohitaji kusajili kampuni; na Kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa shughuli za biashara inayozingatia kikamilifu dhana ya *One Stop Centre*.

161. Vilevile, katika kuboresha mazingira ya biashara ya usafirishaji, mwaka 2010 Serikali ilisaini mkataba wa kutekeleza mradi wa kuboresha usafirishaji katika barabara kuu. Lengo la mradi huu ni kuainisha na kupunguza vikwazo vya kudumu vya barabarani. Tayari uchambuzi unaolenga kuondoa vizuizi vya kuhamahama na kubaki na vizuizi vya kudumu kwenye maeneo ya mizani umeanza kufanyika ambapo katika barabara ya Dar es Salaam-Rusumo, jumla ya vizuizi vya barabarani 15 vya kudumu vimebainishwa kuwa ndivyo vitabaki.

## UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

### Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi

162. Hadi kufikia Desemba 2010, Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi ilitoa mikopo yenye masharti nafuu ya thamani ya shilingi bilioni 4.6 kwa wajasiriamali, ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.4 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 35.3. Mikopo hiyo ilitolewa kwa vyama 30 vya akiba na mikopo (SACCOS) katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara, Singida na Rukwa. Aidha, mikopo hiyo iliwawezesha wajasiriamali kukuza uchumi wao kwa kusaidia ununuzi wa pembejeo za kilimo, kama matrekta ya mikono (power tillers) na hivyo kuwa na uwezo wa kuongeza

ukubwa wa mashamba na kipato. Hadi kufikia Desemba 2010, kiasi cha shilingi bilioni 4.34 zilirejeshwa, ikiwa ni sawa na asilimia 94 ya fedha zilizokopeshwa.

**Utoaji na Upatikanaji wa Mikopo**

163. Utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na kuongeza Ajira uliendelea mwaka 2010 kupitia Benki za CRDB na NMB na Asasi nyingine 12 zilizoidhinishwa. Mwaka 2010, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 47.14 ilitolewa kwa wajasiriamali 72,197. Kati ya wajisiriamali hao, wanaume walikuwa 45,858, sawa na asilimia 64 na wanawake walikuwa 26,339, sawa na asilimia 36. Hadi kufikia Desemba 2010, shilingi bilioni 36.1 ambazo ni sawa na asilimia 76.6 ya mikopo iliyotolewa zilikuwa zimerejeshwa.

164. Mwaka 2010, Serikali kupitia Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogo (SELF) ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 8.7. Pia, katika kipindi hicho, Mradi ulikusanya marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi bilioni 6.1, sawa na asilimia 70.1 ya mikopo iliyotolewa. Mikopo hiyo iliwafikia wananchi 8,631, wenye kipato cha chini waliopo mijini na vijijini, kati ya hao wanawake walikuwa 5,092, sawa na asilimia 58 na wanaume walikuwa 3,539 sawa na asilimia 41.

**Jedwali Na. 7.1: Mgawanyo wa Miradi Kisekta Katika Mikoa kwa Mwaka 2010**

| Na. | SEKTA | D'SALAAM | MWANZA | MOROGORO | ARUSHA | K/NJARO | TANGA | MBEYA | DODOMA | S'NYANGA | TABORA | KIGOMA | KAGERA | RUKWA | MTWARA | LINDI | RUVUMA | COAST | MARA | SINGIDA | MANYARA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilimo na Ufugaji | 1 | 0 | 4 | 2 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 6 | 1 | 0 | 1 | 23 |
| 2 | Maliasili | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 3 | Utalii | 55 | 3 | 2 | 22 | 3 | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 5 | 2 | 1 | 1 | 103 |
| 4 | Uzalishaji Viwandani | 104 | 15 | 5 | 16 | 2 | 4 | 2 | 2 | 3 | 0 | 1 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1 | 15 | 1 | 0 | 0 | 183 |
| 5 | Bidhaa za Petroli na Madini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6 | Majengo ya Biashara | 76 | 1 | 0 | 7 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 92 |
| 7 | Usafirishaji | 49 | 0 | 0 | 5 | 0 | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 62 |
| 8 | Huduma | 17 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 |
| 9 | Kompyuta | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 10 | Asasi za Fedha | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| 11 | Mawasiliano | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| 12 | Nishati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| 13 | Rasiliamali watu | 5 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 8 |
| 14 | Miundombinu ya Kiuchumi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 15 | Utangazaji | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| 16 | **JUMLA** | **321** | **20** | **11** | 55 | **6** | **12** | **6** | **6** | **4** | **2** | **3** | **3** | **1** | **4** | **4** | **4** | **28** | **5** | **2** | **3** | **509** |

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI ILIYOPITISHWA KWA MWAKA 2010

Jedwali Na. 34

| Sekta | Jumla ya miradi iliyopitishwa | Miradi Mipya | Miradi ya zamani (Upanuzi na Ukarabati) | Miradi ya Nchini | Miradi ya Nje | Miradi ya Ubia | Jumla ya Ajira | Jumla ya Thamani ya uwekezaji (Million Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo na Ufugaji | 23 | 21 | 2 | 12 | 6 | 5 | 5169 | 663,710.6 |
| Maliasili | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 100 | 4,494.0 |
| Utalii | 103 | 84 | 19 | 66 | 22 | 15 | 5452 | 417,083.9 |
| Uzalishaji Viwandani | 183 | 162 | 21 | 68 | 76 | 39 | 14327 | 705,299.1 |
| Bidhaa za Petroli na Madini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Majengo ya Biashara | 92 | 85 | 7 | 43 | 30 | 19 | 5078 | 1,925,186.1 |
| Usafirishaji | 62 | 44 | 18 | 37 | 13 | 12 | 7197 | 436,513.1 |
| Huduma | 19 | 19 | 0 | 4 | 10 | 5 | 4717 | 213,127.6 |
| Kompyuta | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 43 | 1,218.0 |
| Asasi za Fedha | 4 | 2 | 2 | 0 | 0 | 4 | 86 | 2,294.6 |
| Mawasiliano | 5 | 5 | 0 | 2 | 1 | 2 | 529 | 260,008.0 |
| Nishati | 3 | 3 | 0 | 1 | 1 | 1 | 45 | 2,277,800.0 |
| Rasiliamali watu | 8 | 6 | 2 | 5 | 0 | 3 | 412 | 20,921.6 |
| Miundombinu ya Kiuchumi | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 22 | 6,076.0 |
| Utangazaji | 4 | 4 | 0 | 3 | 0 | 1 | 463 | 158,886.0 |
| JUMLA | 509 | 438 | 71 | 242 | 160 | 107 | 43640 | 7,092,618.7 |

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

# SURA YA 8

## MASUALA MTAMBUKA

### UKIMWI

165. Katika kipindi cha mwaka 2010, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kutoa huduma za tiba na matunzo kwa wagonjwa wa UKIMWI, ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya UKIMWI. Pia Serikali iliendelea kuboresha huduma hizi kwa kuhakikisha kuwa dawa za kupunguza makali ya VVU zinapatikana katika vituo vya kutoa huduma. Aidha, katika kipindi hicho upanuzi wa huduma za wagonjwa ulifanyika ambapo huduma ziliongezeka kutoka halmashauri 110 mwaka 2009, hadi halmashauri 133. Idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na ambao wanapata dawa za kupunguza makali ya VVU iliongezeka kwa asilimia 10.3, kutoka watu 284,227 mwaka 2009 hadi 313,384 mwaka 2010. Katika idadi hiyo watoto chini ya miaka 15 walikuwa 28,309 na watu wazima zaidi ya miaka 15 walikuwa 285,075.

166. Mwaka 2010, vituo vinavyotoa huduma ya unasihi na upimaji viliongezeka kwa asilimia 24.5, kutoka vituo 1,743 mwaka 2009, hadi vituo 2,170. Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa washauri nasaha 300 zaidi na kufanya idadi ya watoa huduma kuwa 5,365 nchini kote. Mwaka 2010, upanuzi wa huduma za wagonjwa ulifanyika ambapo huduma ziliongezeka kutoka halmashauri 110 mwaka 2009, hadi halmashauri 133. Hadi mwezi Desemba 2010, watu wapatao 8,890,207 walikuwa wamepimwa na kupewa majibu yao.

### Mazingira

167. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kutekeleza sera, mikakati, sheria na kanuni ya usimamizi wa mazingira (Sura ya 191). Mwaka 2010, kanuni tatu kwa ajili ya kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ziliandaliwa, na hivyo kufanya sheria iwe na kanuni 15, ikilinganishwa na kanuni 12 mwaka 2009, kati ya kanuni 29 zinazohitajika. Aidha, miongozo mitatu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliandaliwa. Miongozo hiyo ni: Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira ya Wizara, Wakala wa Serikali

na Serikali za Mitaa; Mwongozo wa Ujenzi na Minara ya Mawasiliano; na Mwongozo wa Kushughulikia Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi.

168. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kuwabana wawekezaji mbalimbali hapa nchini kufanya Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM) kabla ya kuanza kutekeleza miradi yao. Aidha, kumekuwa na ongezeko la miradi iliyofanyiwa tathmini na kupatiwa hati kutoka miradi 160 mwaka 2008/09, hadi miradi 220 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 37.5. Hii inatokana na wawekezaji wengi kupata mwamko wa kufuata na kutimiza matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, ambayo pamoja na mambo mengine inawataka kutimiza masharti ya TAM kabla na baada ya uwekezaji. Hadi Desemba 2010, wataalamu 49 wa TAM na 22 wa ukaguzi wa Mazingira walikuwa wamesajiliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Vilevile, makampuni 12 yanayotoa utaalamu elekezi wa TAM na 10 ya ukaguzi wa mazingira yalisajiliwa.

169. Mwaka 2010, Serikali ilikamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka. Mkakati huu unabainisha usimamizi wa taka za aina nane ambazo zinatokana na shughuli mbalimbali mijini; madini; kilimo na mifugo; huduma za afya; plastiki; vifaa vya umeme na elektroniki; bidhaa za petroli ikiwa ni pamoja na mafuta machafu; na viwanda. Aidha, Serikali ilikamilisha makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuboresha usimamizi wa taka katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Upembuzi yakinifu kuhusu utekelezaji wa Mradi huo umeshafanyika. Serikali iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutenganisha taka ngumu ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Jumla ya vipindi 60 kuhusu wajibu wa wadau katika udhibiti wa taka vilirushwa kupitia vituo vya luninga vya TBC, ITV na STAR TV.

170. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali kwa ajili ya kuhifadhi baoanuwai. Programu hizi ni pamoja na: Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Tanganyika, katika Programu hii, Serikali ilielekeza uanzishwaji wa vikundi shirikishi (Beach Management Units) katika vijiji 10 kwa mikoa ya Kigoma na Rukwa kwa lengo la

kuhamasisha uvuvi endelevu pamoja na hifadhi endelevu ya Bonde la Ziwa Tanganyika; Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Bonde la Kihansi, ambapo Serikali iliendelea kutekeleza mpango wa mazalia ya vyura katika bustani za Bronx na Toledo zilizopo Marekani, ambapo hadi Mei 2010 kulikuwepo na vyura zaidi ya 5,500 katika bustani hizo; Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari ya Pwani (MACEMP), ambapo Serikali imewezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango kazi ya usimamizi kamilifu wa mazingira ya Pwani katika Halmashauri 14 za pwani; na Programu ya Kikanda ya Usimamizi Endelevu wa Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi (ReCoMap), ambapo jumla ya miradi 16 inayosimamiwa na Asasi za Kijamii na zisizo za Kiserikali imefadhiliwa .

171. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kyoto unaolenga kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa. Serikali pia iliidhinisha Miradi mitatu ya kupunguza gesijoto. Miradi hiyo ni: Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya maji ya mto Mwega (Mufindi); Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya mto Ruhudji (Njombe); na mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya mabaki ya miti na pumba za mpunga katika kiwanda cha saruji Mbeya. Miradi hii inalenga katika kuzalisha nishati jadidifu na kuunganisha katika Gridi ya Taifa.

## Utawala Bora

172. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kutekeleza azma yake ya utoaji haki kwa wote kwa kutafsiri Sheria kumi na nne kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili. Vilevile, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea na juhudi zake za kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora katika jamii.

173. Mwaka 2010, Tume iliendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi ambapo jumla ya malalamiko mapya na ya zamani 7,858 yalishughulikiwa. Kati ya hayo, malalamiko 1,003 yalihitimishwa na 6,855 yaliendelea kushughulikiwa, ikilinganishwa na malalamiko 1,746 yaliyopokelewa mwaka 2009, ambapo malalamiko 657 yalishughulikiwa na kuhitimishwa.

174. Kwa upande wa Mahakama ya Rufani, mwaka 2010, jumla ya mashauri 2,624 yalipokelewa, kati ya hayo, mashauri 627 yalikamilishwa na mashauri 1,997 yaliendelea kushughulikiwa ikilinganishwa na mashauri 18,805 katika mwaka 2009 ambapo mashauri 9,590 yalishughulikiwa. Aidha, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi na Wilaya kulikuwa na jumla ya mashauri 62,154. Kati ya hayo, mashauri 46,977 yalisikilizwa na mashauri 15,177 yaliendelea kufanyiwa kazi ikilinganishwa na mashauri 61,237 yaliyopokelewa mwaka 2009 ambapo mashauri 42,725 yalishughulikiwa na kukamilishwa. Vilevile, katika Mahakama za Mwanzo, jumla ya mashauri 218,767 yalitolewa taarifa ambapo mashauri 167,228 yalisikilizwa na 51,939 yaliendelea kushughulikiwa.

175. Mwaka 2010, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP II). Katika utekelezaji wa Mkakati huo, mwaka 2010 TAKUKURU ilipokea na kufanyia uchunguzi kesi za rushwa 870, kati ya kesi hizo, kesi 587 zilifikishwa mahakamani na kesi 64 zilitolewa hukumu ikilinganishwa na kesi 884 zilizofanyiwa uchunguzi mwaka 2009 ambapo kesi 463 zilifikishwa mahakamani na kesi 46 zilitolewa hukumu.

176. Mwaka 2010, Serikali iliendelea na utoaji wa mafunzo ya Utawala Bora ambapo kamati za maadili za wizara 21 na taasisi za umma 32 zilipatiwa mafunzo ya utawala bora na usimamiaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ikilinganishwa na kamati za maadili za wizara 15 na taasisi za umma 25 mwaka 2009.

**Jinsia**

177. Mwaka 2010, washiriki 40 kutoka sekta mbalimbali walipata mafunzo ya uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango, programu na bajeti. Washiriki hao walijumuisha wajumbe 11 kutoka Kamati ya jinsia ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na maafisa 29 kutoka wizara mbalimbali. Idadi hii ya washiriki katika mafunzo hayo ilipungua toka washiriki 175 mwaka 2009 hadi washiriki 40 mwaka 2010 kutokana na ufinyu wa bajeti.

178. Mwaka 2010, mafunzo kuhusu "Utokomezaji wa Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto na Albino" yalitolewa. Mafunzo haya yalijumuisha wakuu

wa vituo vya polisi 40 na viongozi wa vijiji 43, kutoka Mikoa ya Kigoma, Arusha, Dodoma, Tabora na Manyara. Aidha, mafunzo hayo pia yalitolewa kwa wasimamizi wa sheria 106 katika wilaya ya Rorya, Tarime, Bukombe na Kahama.

**Usalama wa Raia**

179. Mwaka 2010, hali ya usalama nchini ilikuwa tulivu kwa ujumla pamoja na kuwepo kwa matukio ya uhalifu na matukio ya makosa ya usalama barabarani ambayo yalijenga hisia kwa wananchi. Makosa ya jinai 62,133 yaliripotiwa katika vituo vyote vya Polisi mwaka 2010 ikilinganishwa na makosa 69,134 yaliyoripotiwa mwaka 2009. Idadi ya makosa ilipungua kwa makosa 7,001 sawa na punguzo la makosa kwa asilimia 10.1.

180. Mwaka 2010, matukio 24,926 ya ajali barabarani yaliripotiwa katika vituo vya Polisi, ikilinganishwa na ajali 22,019 mwaka 2009, sawa na ongezeko la ajali 2,907 au asilimia 13.2. Aidha, jumla ya watu 3,687 walikufa na wengine 22,064 kujeruhiwa katika ajali hizo ikilinganishwa na watu 3,851 waliokufa na 18,830 waliojeruhiwa mwaka 2009. Idadi ya vifo ilipungua kwa asilimia 4.3 ambapo idadi ya watu waliojeruhiwa iliongezeka kwa asilimia 17.2. Ongezeko kubwa la ajali za barabarani lilitokana na: uzembe wa madereva; mwendo kasi kwa baadhi ya madereva; miundombinu duni katika baadhi ya maeneo nchini; ubovu wa magari; baadhi ya watumiaji wa barabara (waenda kwa miguu, wapanda pikipiki na baiskeli) kutozingatia kanuni za usalama barabarani; na ulevi.

181. Hadi kufikia Desemba, 2010 idadi ya wakimbizi nchini ilifikia 109,286, ikilinganishwa na wakimbizi 273,782 mwaka 2009. Wakimbizi hawa walitoka Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Somalia na mataifa mengine ya Rwanda, Uganda, Sudan, Ethiopia na Zimbabwe. Mchanganuo wa idadi hii ni kama ifuatavyo: Burundi 47,350; Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo 60,186; Somalia 1,488; Mataifa mengine 262. Aidha, mwaka 2010 jumla ya wakimbizi 162,256 walipewa uraia wa Tanzania na jumla ya wakimbizi 1,092 walirejea nchini Burundi.

182. Mwaka 2010, jumla ya wageni 628,795 waliingia nchini kutoka mataifa mbalimbali, ikilinganishwa na wageni 756,363 walioingia nchini mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 16.9. Aidha, wageni 775,310 walitoka nchini mwaka 2010, ikilinganishwa na wageni 755,004 waliotoka nchini mwaka 2009 ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.7. Mwaka 2010, jumla ya hati za ukaazi 19,550 zilitolewa kwa wageni walioingia nchini kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali ikilinganishwa na hati za ukaazi 17,650 zilizotolewa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 10.8.

## SURA YA 9

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI TANZANIA (MKUKUTA)

### Utangulizi

183. Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) awamu ya kwanza ulikamilika mwaka 2010. Mkakati huu ulitekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2005/06 hadi 2009/10. Katika utekelezaji wake, wadau mbalimbali ikijumuisha taasisi za Serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi na washirika wa maendeleo walishiriki kikamilifu katika maeneo makuu matatu yaliyoainishwa ambayo ni: Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Uboreshaji wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na Uwajibikaji. Mafanikio yaliyopatikana, changamoto, na mambo tuliyojifunza katika kipindi chote hicho yamechambuliwa kwa kina katika Taarifa ya Utekelezaji wa MKUKUTA I kwa mwaka 2009/10 (MAIR). Aidha, kufuatia kufikia ukomo wa MKUKUTA I, Serikali iliandaa awamu ya pili ya MKUKUTA ambao ulipitishwa mwezi Oktoba 2010. Maandalizi ya MKUKUTA II yalizingatia changamoto na mambo tuliyojifunza wakati wa utekelezaji wa MKUKUTA I ili kuboresha utekelezaji. Mchakato wa maandalizi ya MKUKUTA II uliwahusisha wadau wengi na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2010/11 – 2014/15). Baadhi ya mambo yanayoendelea kutekelezwa katika awamu hii ya pili ya MKUKUTA ni pamoja na: Maandalizi ya Mwongozo wa Utekelezaji na kuainisha programu za vipaumbele za ki-sekta, Mfumo wa Ufuatiliaji MKUKUTA na Mkakati wa Mawasiliano.

184. Kwa vile mwaka 2010 ulikuwa wa mwisho katika utekelezaji wa MKUKUTA I, uchambuzi wa mwenendo wa viashiria mbalimbali vya MKUKUTA umeainishwa katika nguzo kuu tatu katika kipindi chote cha utekelezaji kama ifuatavyo:

### Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

185. Katika kipindi cha miaka minne (2006 2009), ya utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya kwanza uchumi, wa Tanzania umeendelea kuimarika licha ya kukumbwa na misukosuko ya kupanda kwa bei za mafuta ya petroli

katika soko la dunia, ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini katika kipindi cha mwaka 2005/06 na 2008/09 na ukosefu wa umeme wa uhakika. Wastani wa kiwango cha ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 6.9 kati ya mwaka 2005 na 2010 na hivyo kuwa ndani ya shabaha ya MKUKUTA ya asilimia 6 – 8 hadi mwaka 2010.

186. Matokeo ya utafiti wa nguvu kazi na ajira wa mwaka 2005/2006 yalionesha kwamba ajira imekuwa ikipanuka kwa kasi ya watu 40,000 kwa mwaka wakati ambapo watu 760,000 wanaingia katika soko la ajira kila mwaka. Lengo la MKUKUTA ni kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hadi kufikia asilimia 6.9 mwaka 2010, kutoka asilimia 12.9 uliokuwepo mwaka 2000/01. Utafiti uliofanyika mwaka 2006, ulionesha kuwa asilimia 11 ya Watanzania hawana ajira. Tatizo la ukosefu wa ajira ni kubwa zaidi jiji la Dar es Salaam ambalo takwimu zinaonesha kwamba asilimia 31.4 ya wakazi wake hawana ajira. Katika miji mingine, ukosefu wa ajira ni asilimia 16.3. Kadhalika takwimu zinaonesha kuwa idadi ya wanawake wasio na ajira ni kubwa kuzidi ile ya wanaume katika maeneo ya mijini.

187. Tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya kwa Tanzania Bara za mwaka 2000/01 na 2007 zinaonesha kuwa idadi ya watanzania walioko katika viwango vya chini vya mahitaji ya msingi vilipungua kutoka asilimia 35.6 mwaka 2000/01, hadi asilimia 33.4 mwaka 2007. Hali ya umaskini vijijini imepungua kutoka asilimia 38.7 mwaka 2000/01 hadi asilimia 37.4 mwaka 2007. Katika Jiji la Dar es Salaam umaskini ulipungua kutoka asilimia 17.6 mwaka 2000/01, hadi asilimia16.2 mwaka 2007 na maeneo mengine ya mijini umaskini ulipungua kutoka asilimia 25.8, hadi asilimia 24.1 katika kipindi hicho. Kwa ujumla, kiwango cha umaskini kimepungua kwa asilimia 2.2 katika kipindi cha mwaka 2000/01 hadi 2007.

188. Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2009 inaonesha kwamba, kuna uhusiano wa karibu kati ya umaskini, ukuaji wa uchumi na tofauti ya kipato. Matokeo ya uchambuzi katika ripoti hiyo yanaonesha pia kuwa kukua kwa uchumi tangu mwaka 2000/01 hakujaweza kupunguza umaskini wa kipato kwa kiwango kikubwa. Kuongezeka kwa tofauti ya kipato ingekuwa sababu mojawapo, lakini tofauti ya kipato miongoni mwa

watanzania haijabadilika. Matokeo ya uchambuzi wa utafiti wa matumizi ya kaya wa miaka ya 2000/01 na 2007 unaonyesha kuwa tofauti ya kipato (kwa kipimo cha Gini Coefficient) iliendelea kubakia asilimia 35. Katika Jiji la Dar es Salaam tofauti ya kipato ilipungua kutoka asilimia 36 hadi asilimia 34 katika kipindi hicho.

**Jedwali Na. 9.1: Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini**

| Viashiria | Mwaka wa Utafiti | Kitaifa | DSM | Miji Mingine | Vijijini |
|---|---|---|---|---|---|
| Umaskini | 2000/01 | 35.6 | 17.6 | 25.8 | 38.7 |
| Tofauti ya Kipato | | 0.35 | 0.36 | 0.36 | 0.33 |
| | | | | | |
| Umaskini | 2007 | 33.4 | 16.2 | 24.1 | 37.4 |
| Tofauti ya Kipato | | 0.35 | 0.34 | 0.35 | 0.33 |
| | | | | | |
| Badiliko (2001-2007) | | 2.2 | 1.4 | 1.7 | 1.3 |

Chanzo: PHDR 2009

189. Katika kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii viashiria vinavyoangaliwa zaidi ni vile vinavyohusu masuala ya elimu, afya na maji. Taarifa zinazotokana na mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya umaskini, zinaonesha kuwa kumekuwa na mafanikio makubwa kwa mwaka 2009/10 katika ngazi zote za elimu, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa uandikishaji katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vya ufundi na elimu ya juu. Mafanikio pia yamepatikana katika huduma ya afya ya mama na mtoto kwa kupungua kwa vifo vya akina mama wakati wa kujifungua , hii ni kulingana na Utafiti wa Afya na Idadi ya Watu wa mwaka 2009/10. Mpango na Mkakati wa kuzuia Malaria nao umekuwa na mafanikio kwani idadi ya kaya zinazomiliki angalau chandarua kimoja imeongezeka kutoka asilimia 56.3 mwaka 2007/08 na kufikia asilimia 74.7 mwaka 2009/10. Idadi ya wanawake wenye VVU wanaopata dawa za kurefusha maisha (ARV) na kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (MTCT) na idadi ya watu wenye maambukizi ya VVU katika kiwango cha juu wanaopata muunganiko wa dawa za kurefusha maisha, imeongezeka. Idadi ya watu wanaopata maji safi na salama mijini na vijijini

nayo imeongezeka. Mwenendo wa baadhi ya viashiria vya Ustawi wa Jamii ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 9.2: Mwenendo wa Viashiria vya Maisha na Ustawi wa Jamii**

| | 2005/06 | 2010 | 2010 |
|---|---|---|---|
| Kiashiria | Kianzio (Baseline) | Halisi | Lengo |
| Vifo vya watoto (<5) kati ya 1000 | 112 | 81 | 79 |
| Vifo vya watoto wachanga kati ya 1000 | 68 | 51 | 50 |
| Vifo vya mama wajawazito kati ya 1000 | 578 | 454 | |
| Maambukizi ya virusi vya UKIMWI | 7.4% | 5.7% | 5% |
| Kiwango halisi cha uandikishaji elimu ya msingi | 96.1% | 95.4% | 99% |
| Kiwango cha ukatishaji masomo kwa elimu ya msingi | | 2.6% | |
| Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu elimu ya msingi | 56:1 | 51:1 | 45:1 |
| Watoto (umri<5) wenye upungufu wa uzito | 21.9% | 21% | |
| Watoto (umri<5) waliodumaa | 21.9% | 35% | |

**Utawala Bora na Uwajibikaji**

190. Katika kipindi cha utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya kwanza, kumekuwepo na usimamizi mzuri wa mapato na matumizi ya Serikali. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine iliendelea kuimarisha uwajibikaji katika taasisi zake hususan serikali za mitaa. Sera ya kupeleka madaraka katika ngazi za chini, yaani`D by D` imeboresha upatikanaji wa fedha katika halmashauri na hivyo kuboresha uwajibikaji katika matumizi ya fedha. Hivi sasa, serikali za

mitaa hulazimika kubandika taarifa za bajeti, ikiwa ni mapato na matumizi kwenye mbao za matangazo ili zisomwe na watu wote.

191. Mwaka 2009/10 Serikali ilianza mchakato wa kuwa na mfumo wa vitambulisho vya taifa kwa kuanzisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Wakala hii imepewa mamlaka ya kuratibu mfumo ambao hatimaye utatoa vitambulisho vya taifa kwa raia wote. Kampeni za kutoa elimu kwa umma ili kuwaandaa wananchi juu ya umuhimu wa vitambulisho vya taifa zinaendelea nchini.

192. Katika kuleta usawa wa jinsia katika ngazi ya utawala na uongozi, wanawake katika nafasi za maamuzi wameongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2005 na kufikia asilimia 31 mwaka 2010. Idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi kati ya mwaka 2005 na 2010 imeongezeka kama ifuatavyo: Majaji 13 hadi 34; mawaziri 4 hadi 7; makatibu wakuu 7 hadi 9; Makatibu Tawala wa Mikoa 4 hadi 10; Wakuu wa Wilaya 20 hadi 25; Wakurugenzi wa Halmashauri 14 hadi 35; na Wakurugenzi katika wizara na wakala 19 hadi 133.

193. Katika mwaka 2009/10, Serikali iliendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya ardhi katika nyanja mbalimbali. Viwanja 21,160 vilipimwa chini ya Mpango wa Kurasimisha Biashara na Mali (MKURABITA). Viwanja 17,526 kati ya vilivyopimwa vilisajiliwa katika mfumo wa kompyuta ili kuandaa hati za ardhi na kati ya hivyo, hati 8,109 ziliandaliwa. Suala la kutoa hati ni la msingi katika kutatua migogoro, kupata rasilimali mbalimbali kama vile mikopo na pia kukuza makusanyo ya mapato ya Serikali.

194. Idadi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zenye ripoti nzuri za ukaguzi imeongezeka kutoka Mamlaka 53 mwaka 2005/06 na kufikia 77 mwaka 2008/09. Mafanikio haya yanatokana na kuongezeka kwa uwezo wa rasilimali watu, hususan kada ya wahasibu, pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya mfumo wa usimamizi wa fedha (IFMIS) na Mipango na Ripoti (Plan Rep).

195. Katika kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, kati ya mwaka 2005 na 2010, kesi mpya 755 za rushwa zilifunguliwa katika mahakama za kisheria. Kati ya hizo, Serikali ilishinda jumla ya kesi 155 na ikaokoa kiasi cha TZS 28,827,667,374. Aidha, Serikali imefungua jumla ya kesi kubwa za rushwa 19 tangu mwaka 2005. Ili kuongeza kasi ya usikilizwaji wa kesi mahakamani, juhudi mbalimbali zilichukuliwa na Serikali, zikiwa ni pamoja na: kuteua majaji wengi zaidi, mahakimu wakazi, mahakimu wa mahakama za mwanzo, mawakili wa Serikali na makatibu wa sheria. Kwa mfano, idadi ya majaji katika Mahakama ya Rufaa iliongezeka kutoka majaji 8 mwaka 2005 na kufika 21 mwaka 2010, na katika mahakama kuu, waliongezeka kutoka majaji 24 mwaka 2005 na kufika 68 mwaka 2010.

# SEHEMU YA TATU

# SUALA MAALUM KIMAENDELEO

# SURA YA 10

## USHIRIKISHWAJI KATIKA HUDUMA ZA FEDHA KWA WATU WA KIPATO CHA CHINI

### Utangulizi

196. Mpango wa upanuzi wa huduma za kifedha una lengo la kuhakikisha kuwa hudutna za kibenki zinawafikia watu wengi zaidi ambao walikuwa hawapati huduma hizi hususan wale wa vijijini, kwa wakati na kwa gharama nafuu. Mpango huu unajumuisha dhana kuu tnbili za kupanua huduma za kifedha kulingana na tafsiri ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2006. Kwanza, ushirikishwaji katika huduma za fedha kunamaanisha kuwa wananchi wanakuwa na uwezo wa kupata huduma mbalimbali za kifedha katika mfumo rasmi kuanzia zile za kawaida kama kuweka na kukopa fedha mpaka zile za juu kama bima na mafao ya uzeeni. Pili, ushirikishwaji katika huduma za fedha, kunamaanisha kuwa wateja wanapata huduma za kibenki kutoka kwa mtoa huduma zaidi ya mmoja, ili wananchi waweze kulinganisha aina ya huduma na kuchagua huduma iliyo bora na nafuu. Serikali inauchukulia Mpango huu kama jambo muhimu la kuzingatia kwani tafiti mbalimbali zimebainisha kuwa mfumo wa kibenki unaofanya kazi kwa ufanisi unaweza siyo tu kuharakisha ukuaji wa uchumi, bali pia ukuaji ulio na uwiano sawa.

### Chimbuko

197. Umasikini katika Afrika umejikita zaidi katika maenco ya vijijini, ingawa kasi ya ukuaji wa umasikini mijini inaongezeka kutokana na kuendelea kukua kwa miji kwa kasi ambayo haiendani na ongezeko la ajira. Shughuli za kilimo, sekta isiyo rasmi, na ujasiriamali mdogo na wa-kati kwa pamoja ndizo njia kuu za kipato kwa maisha ya watu wengi hususan maskini. Ukuaji wa sekta hizi kama inavyobainishwa katika taarifa mbalimbali unakwamishwa na upatikanaji wa mikopo na huduma nyingine za kifedha. Mfano, kulingana na utafiti uliofanywa na "Overseas Development Initiative – ODI" mwaka 2010, ulibainisha kuwa huduma za kifedha zinaziwezesha kaya kuwekeza kwenye shughuli ambazo zina uwezekano mkubwa wa kuchangia katika kuongeza

kipato na hivyo kupelekea kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi. Utafiti huo uliofanyika katika nchi za Kenya na Tanzania, ulionesha kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya kufikiwa na huduma za kibenki, na uwekezaji wa kaya katika elimu au biashara, ambao utachangia kwenye ukuaji wa uchumi. Watu waliohojiwa walieleza sababu kubwa za kukopa kuwa ni kuwekeza katika biashara kwa upande wa Tanzania na elimu kwa upande wa Kenya. Aidha, pamoja na kwamba huduma za kifedha kupitia mfumo usio rasmi zina umuhimu wake na ni rahisi kupatikana, kaya nyingi nchini Kenya zinapendelea kuwekeza kwa kutumia mfumo rasmi wa huduma za kifedha kuliko kaya za Kitanzania.

198. Taarifa ya "Alliance for Financial Inclusion" ya mwaka 2009 ilibainisha kuwa zaidi ya nusu ya watu wazima wote duniani, ambao ni kama watu milioni 2.5 hawapati huduma za kifedha kupitia mfumo rasmi. Takriban asilimia 90 ya jamii ambazo hazitumii mfumo rasmi wa kifedha zipo katika nchi zinazoendelea. Taarifa iliendelea kubainisha kuwa utaratibu wa ushirikishwaji katika huduma za fedha unaweza kuziweka jamii hizi kwenye mfumo wa kifedha na hivyo kuwa na fursa za kupata huduma za kibenki, zikiwemo kuweka fedha, kufanya malipo, kuhamisha fedha na huduma za bima. Mpango huu utaleta matokeo mazuri kwenye ukuaji wa uchumi, utulivu wa kifedha na utengemano wa kijamii.

199. Aidha, kulingana na utafiti wa Benki ya Dunia, inakadiriwa kuwa ni asilimia 20 tu ya kaya zote zilizoko Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo zimefungua akaunti katika taasisi za fedha, ikilinganishwa na asilimia 90 ya kaya katika nchi zilizoendelea. Hali kadhalika, ni asilimia 15 tu ya uwekezaji mpya unafanyika na kampuni ndogo kwa msaada wa mikopo ya benki, ikilinganishwa na asilimia 30 kwa kampuni kubwa, hali inayokwamisha uwezo wa kampuni kukua. Makampuni mengi katika Afrika yanalalamikia zaidi kuhusu ukosefu wa mikopo na huduma za bima kuliko makampuni katika sehemu zingine duniani. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, tawi moja la benki linahudumia watu zaidi ya 50,000 ukilinganisha na watu chini ya 4,000 katika nchi zilizoendelea.

200. Hata hivyo, wastani huu wa jumla kwa Afrika, unaficha hali halisi na utofauti mkubwa ulioko baina ya nchi na nchi. Utafiti uliofanywa na "FinScope Africa Brief" mwaka 2010 unaonesha kuwa uwiano wa watu ambao hawapati huduma za kibenki ni kubwa zaidi nchini Uganda (asilimia 62), Rwanda asilimia 56, Tanzania asilimia 52 na Kenya ni asilimia 32 tu. Idadi ya watu ambao hawapati kabisa huduma kutoka taasisi za fedha ziwe rasmi au zisizo rasmi ni zaidi ya asilimia 40 kwa nchi nyingi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Uwiano wa watu wanaopata huduma za kifedha kupitia mfumo usio rasmi katika nchi nyingi za ukanda huu, unazidi wale wanaopata huduma kupitia mfumo rasmi wa kibenki.

201. Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, muundo wa sekta ya fedha katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara umebadilika kwa kasi, ambapo kwa sasa mfumo wa benki unatoa huduma za aina mbalimbali kwa kiwango kikubwa na kusambaa katika eneo kubwa. Mambo kadhaa yamechangia katika maendeleo haya, matatu muhimu kati ya hayo ni pamoja na:

i) Maboresho katika sekta ya fedha ambayo yamepunguza kwa kisasi kikubwa urasimu na vikwazo vya uanzishwaji wa asasi za kifedha, kuimarisha uwezo wa taasisi za fedha kuhimiza uwekaji akiba na kuongeza ushindani katika utoaji huduma za kifedha;

ii) Uvumbuzi wa Tekinologia, ambayo imewezesha huduma za kibenki kuwa rahisi na za uhakika hasa kwa maeneo ya vijijini; na

iii) Ukuaji wa taasisi ndogo za kifedha zilizobobea, ambazo zimevumbua njia rahisi za kutoa mikopo kama kutoa mikopo kwa watu maskini waliojiunga pamoja katika vikundi.

202. Pamoja na kuwa mfumo wa fedha katika nchi zilizo Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara umeonesha kukua kwa kasi katika miongo ya hivi karibuni, bado kuna changamoto ambapo kundi kubwa la watu hasa wanaoishi mazingira hatarishi kama vile watu wa kipato cha chini, wanaendelea kutengwa hata

katika fursa za msingi na huduma zinazotolewa katika sekta ya fedha. Sababu zinaweza kutofautiana kati ya nchi moja hadi nyingine, hivyo mkakati wa kuondokana na hali hii unaweza pia kutofautiana. Hata hivyo, mpango wa kupanua huduma za kifedha kuwafikia watu wenye kipato cha chini, unaweza kuboresha hali zao za maisha na hatimaye kuweza kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

**Sekta ya Fedha Tanzania**

203. Sekta ya fedha nchini Tanzania imeendelea kufanyiwa maboresho makubwa tangu kuanza kwa mageuzi katika sekta ya fedha mwaka 1991. Sekta ya fedha zaidi inajumuisha mabenki, mifuko ya pensheni, makampuni ya bima na mawakala wa fedha. Hata hivyo, sekta ya fedha imetawaliwa na benki ambazo kwa pamoja zina asilimia 75 ya mali zote za taasisi za fedha, ikifuatiwa na mifuko ya pensheni ambayo mali zake ni asilimia 21 na mali za makampuni ya bima zikiwa na uwiano wa asilimia 2.0 za mali zote, wakati asilimia 2 iliyobaki ni mali za mawakala wa fedha. Kielelezo hapa chini kinaonesha mgawanyo huo.

**Mgawanyo katika Sekta ya Fedha – Juni 2010**




204. Mali za sekta ya fedha zimeongezeka kwa haraka katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, kutoka jumla ya shilingi bilioni 1,637 mwishoni mwa mwezi Desemba 2001, hadi kufikia shilingi bilioni 10,040 mwezi Desemba 2009. Ukuaji huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na amana za sekta binafsi katika mfumo wa benki.

205. Pamoja na ukuaji wa haraka wa mali za sekta ya fedha, bado mfumo wa fedha nchini haujawafikia watu wengi na upatikanaji wa huduma za fedha ni mdogo kwa sehemu zote za mijini na vijijini. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti uliofanywa na "Fin-Scope" mwaka 2009, ni asilimia 12.4 tu ya watu wazima wanatumia huduma za kibenki na za taasisi nyingine za kifedha zilizo katika mfumo rasmi sawa na watu wazima milioni mbili (wengi wakiwa wa mjini), kati ya makadirio ya watu wazima milioni ishirini. Jitihada za kuimarisha ufahamu wa mambo ya fedha ili kuongeza ushirikishwaji katika huduma za kifedha na kuwalinda wateja ni moja ya madhumuni ya Awamu ya Pili ya Maboresho ya Sekta ya Fedha. Programu ya kuongeza ufahamu katika masuala ya fedha inalenga kuwawezesha wananchi wengi katika kufanya maamuzi sahihi juu ya masuala ya fedha na kuongeza juhudi za kuwafikia walengwa wengi zaidi. Ni muhimu kutambua kuwa uwezo wa wateja kufanya maamuzi sahihi katika masuala ya kifedha kunachangia kuwepo kwa utulivu katika sekta ya fedha, kwa kuwezesha ufanisi katika kuwekeza na kuweka tahadhari katika matumizi ya huduma mbalimbali za kifedha. Kwa kuzingatia hayo, Benki Kuu ya Tanzania imeweka kipaumbele katika kupanua huduma za kifedha kama njia mojawapo ya kuimarisha ufanisi na utulivu katika mfumo wa fedha na ambao utawezesha ukuaji wa uchumi.

206. Mageuzi ya kitekinolojia yamekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa gharama nafuu hasa katika maeneo ya vijijini. Tekinolojia imeziwezesha taasisi za fedha kupunguza gharama za uendeshaji na kurahisisha huduma za kibenki kutolewa kwa haraka zaidi, kwa uhakika na kwa usalama zaidi katika eneo kubwa. Kwa mfano, uanzishwaji wa mashine za kutolea pesa (ATMs) katika miji ya Tanzania miaka ya hivi karibuni kumewezesha taasisi za fedha kutoa huduma masaa 24, na kwa siku 7 za juma. Vilevile, kuongezeka kwa kasi kwa watumiaji na watoa huduma za kifedha kupitia simu za mkononi kumesaidia kwa kiasi kikubwa kupeleka huduma sehemu kubwa ambayo hapo awali ilikuwa haipatikani, huduma hizi ni kama vile, kuhamisha fedha na huduma ya kufanya malipo.

**Malipo ya Pesa kwa Kutumia Simu za Mkononi**

207. Idadi ya watumiaji wa simu za mkononi nchini Tanzania inaongezeka kwa kasi kubwa. Kwa mujibu wa takwimu za awali, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010, idadi ya watumiaji wa simu za mkononi ilikuwa imefikia watu milioni 18.5, wakati waliojiandikisha kwa ajili ya kufanya malipo kwa kutumia simu za mkononi walikuwa wamefikia watu milioni 9.2 hadi kipindi kilichoishia Julai mwaka 2010. Kuongezeka kwa watumiaji wa simu za mkononi kwa ajili ya kufanya malipo kunatokana na uhaba wa huduma za kibenki katika maeneo mengi hasa ya vijijini. Kwa mantiki hiyo, huduma ya malipo kwa kutumia simu za mkononi imewezesha kuwaunganisha watu wenye akaunti benki na wale wanaoishi maeneo ambayo hayana huduma za kibenki. Aidha, huduma hii ya malipo kwa njia ya simu za mkononi imewezesha kufanya malipo ya ankara mbalimbali kama za maji na umeme bila usumbufu wowote. Vilevile, huduma ya malipo kwa njia ya simu za mkononi inatumiwa zaidi kuwezesha wateja kuongeza salio, kuhamisha muda wa maongezi kwa mtumiaji mwingine wa simu, kuhamisha malipo na kufanya malipo ya ankara kwa huduma zinazotolewa na makapuni mbalimbali.

208. Miaka michache iliyopita, watu walikuwa wanatembea na kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kufanya malipo mbalimbali. Watu wengine walikuwa wanatuma pesa kwa kutumia mabasi ambyo ni ya gharama kubwa na hatari kwa usalama wa fedha. Jamii ilikuwa inalazimika kufanya hivyo kwa sababu huduma rasmi za kibenki zilikuwa chache na za gharama kubwa. Katika siku za hivi karibuni, tekinolojia ya kutumia simu za mkononi imeleta mapinduzi katika sekta ya fedha na hivyo kuwezesha kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma hizi ikijumuisha wadau wengine kama watoa huduma za simu za mkononi na makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano kwa kutumia tekinologia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) kutoa huduma za fedha nje ya utaratibu wa kawaida wa kutumia mabenki, kwa kutumia huduma za simu za mkononi na tovuti (internet). Huduma za malipo kwa kutumia simu za mkononi inayojumuisha masuala yote ya huduma za fedha zimekuwa na ufanisi kwa kiasi kikubwa katika kufikisha huduma za kibenki maeneo mengi ya nchi ambayo yasingeweza kufikiwa na mabenki kwa urahisi.

209. Kuingia kwa watoa huduma hawa katika sekta ya fedha kumeongeza ufanisi katika huduma za fedha kwa maana ya kupata huduma kwa haraka, kwa njia rahisi, kwa gharama ndogo na kwa kuwezesha upatikanaji wake. Huduma zinazotolewa zinaweza kugawanyika katika sehemu kuu mbili: Huduma zinazohusisha mfumo wa kibenki na huduma zisizohusisha mfumo wa benki. Mfumo unaohusisha huduma za kibenki unatumika pale ambapo taasisi za fedha zinabuni na kutumia mfumo wao wenyewe wa kutoa huduma kwa njia ya mtandao na simu za mikononi. Kwa kutumia utaratibu huu wa simu za mkononi, wateja wenye akaunti benki wanapata fursa ya kuangalia mwenendo wa fedha zilizoingia na kutoka, kuulizia salio, na kufanya malipo kwa kiasi kinachoruhusiwa kupitia kwenye akaunti zao. Huduma za malipo zisizohusisha mfumo wa benki zinatumika pale ambapo mtoa huduma wa simu za mkononi hushirikiana na taasisi ya fedha kutoa huduma hiyo. Utaratibu huu unahusisha mtumizi ya fedha kupata huduma za kibenki kupitia simu ya mkononi na kwa kutumia mawakala wanaoweza kufanikisha huduma ya kutoa na kutuma fedha kwa kutumia njia za kielektroniki. Mawakala wanatumika kama kituo cha kutolea huduma wakati fedha halisi zinapotumwa au kupokelewa na kiwango cha fedha kinachozunguka sharti kiwe sawa na kile kilichowekwa kwenye akaunti maalumu iliyofunguliwa kwenye benki husika.

210. Tekinologia hii imeunganishwa na njia ambazo mteja aliyejiunga na huduma ya malipo kwa kutumia simu za mkononi anaweza kupata huduma za kifedha akiwa popote nchini. Huduma zinazotolewa ni pamoja na kuhamisha fedha kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine (P2P), kutoka kwa mteja kwenda kwenye biashara (C2B), kutoka kwenye biashara kwenda kwa mteja (B2C), na kulipa na kupokea pesa taslimu kwenye vituo vya makala vilivyowekwa. Huduma hii imerahisisha kutuma fedha kwa ndugu na jamaa waliopo vijijini, kufanya malipo ya huduma mbalimbali kama vile za umeme (LUKU), maji (DAWASCO), TV za kulipia (DSTV), bima pamoja na kutoa na kurudisha mikopo.

211. Kwa hapa Tanzania huduma hizi hutolewa na M-Pesa ambayo inaendeshwa na kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom ikishirikiana na benki ya NBC Ltd; ZAP inayoendeshwa na kampuni ya simu za mkononi ya

Airtel ikishirikiana na banki ya Citibank; na Z Pesa inayoendeshwa na kampuni ya simu za mkononi ya Zantel na E Fulusi wakishirikiana na benki ya FBME. Huduma hii ya malipo kwa kutumia simu za mkononi, ambayo nchini Tanzania ilizinduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2007, tayari imesha sajili watumiaji milioni 6 mpaka ilipofikia tarehe 31Mei 2010. Idadi ya wateja inatarajiwa kuongezeka kadiri makampuni haya yatakavyoendelea kuboresha na kupanua huduma.

212. Teknologia imedhihirisha kuwa inaweza kusaidia kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa huduma hii kama vile kulika maeneo ya mbali na ya vijijini na gharama za utoaji wa huduma hii. Kulingana na matokeo ya utafiti uliofanywa na "FinAcccss" mwaka 2006 na 2009, upatikanaji wa huduma rasmi za kifedha (benki na sizizo za benki) ziliongezeka kutoka asilimia 26.4 mwaka 2006 hadi asilimia 40.5 mwaka 2009.

**Maendeleo Katika Taasisi Ndogo Ndogo za Fedha**

213. Ukuaji wa haraka wa taasisi ndogo ndogo za fedha nao pia umechangia kufikisha huduma za fedha kwa watu masikini vijijini. Benki za kawaida hazitoi huduma hii kwa watu masikini kwa sababu watu masikini: wanachukuliwa kuwa na uwezekano mdogo wa kurejesha mikopo; wanakopa mikopo midogo ambayo ina gharama kubwa ya uendeshaji, na hawana mali zisizohamishika zinazoweza kutumika kama rehani/dhamana kwa mikopo wanayohitaji.

214. Taasisi ndogo ndogo za fedha zimeweza kuziba pengo hilo kwa kutoa huduma maalum za kifedha kwa kundi hili la watu wa kipato cha chini. Taasisi hizi zinatumia njia mbalimbali za kiubunifu, kama vile kutoa mikopo kwa kikundi cha watu waliojiunga pamoja na mbinu nyingine kama njia ya kukabiliana na vikwazo vilivyopo katika kuwafikishia huduma za kifedha watu wa kipato cha chini. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na ODI mwaka 2010 unaonesha kuwa mahitaji ya huduma za fedha ni makubwa miongoni mwa wananchi, lakini wanachi wamekuwa wakipata huduma hizi kupitia zaidi njia na mifumo isiyo rasmi kuliko njia zilizo rasmi. Huduma za fedha zilizo rasmi zinatumika zaidi nchini Kenya kuliko zinavyotumika nchini Tanzania. Katika

nchi zote mbili, kuna kiwango sawa cha kuweka akiba na kukopa fedha ambapo zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanaweka akiba na/au kukopa fedha, japokuwa kuna tofauti kubwa ya upatikanaji wa huduma za fedha. Uwiano wa watu wanaotumia huduma za fedha kupitia mifumo ambayo haijarasimishwa kikamilifu, kama vile Ushirika wa Kuweka na Kukopa; Vyama vya Kuweka na Kukopa kwa Mzunguko; na Vyama vya Kudunduliza Akiba na Kukopa, na maduka ya kutoa mikopo ni mkubwa nchini Kenya kuliko ilivyo Tanzania. Matokeo ya utafiti huo pia yanaonesha kuwa katika nchi hizi kuna matumizi makubwa ya huduma za fedha kupitia mfumo/utaratibu usio rasmi ikilinganishwa na matumizi ya huduma kwa mfumo rasmi. Kwa kuweza kugharamia shughuli za kuinua kipato miongoni mwa watu maskini, ni dhahiri kuwa taasisi ndogo ndogo za fedha zinatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuondoa umasikini.

215. Kwa kiasi kikubwa, ubunifu ulitajwa hapo juu umetokana na maamuzi ya kujitolea yaliyofanywa na kampuni binafsi kwa manufaa yao, hususan ya kupata faida. Hata hivyo, hakuna shaka kwamba gharama za awali za uanzishwaji wa mpango huu zilikuwa kubwa na itachukua miaka mingi ili kuweza kuanza kupata faida. Kwa mantiki hiyo, watunga sera wanatakiwa kuvutia ubunifu zaidi wa kitekinologia kwa kuweka sera ambazo zinalinda kikamilifu hati miliki za uvumbuzi/ ubunifu wao ili makampuni yaweze kuingia gharama hizi kubwa za awali yakiwa na uhakika kuwa wao ndio watakaofaidika na uvumbuzi huo na wala siyo kampuni nyingine ambazo hazikuhusika na uwekezaji. Vile vile, watunga sera wanayo nafasi kubwa ya kuwajengea imani wananchi ili waweze kubuni/kuvumbua teknologia mpya za bidhaa na huduma za fedha. Jambo hili ni muhimu kwa kuwa, tofauti na masoko mengine ya bidhaa na huduma, soko la fedha linategemea imani na uaminifu kiasi kwamba, jukumu la waratibu na wasimamizi wa sekta ya fedha katika kujenga imani kwa umma juu ya ubunifu mpya wa bidhaa na huduma za fedha ni la muhimu sana.

**Changamoto**

216. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, huduma za malipo ya fedha kupitia simu za mkononi zimeleta changamoto kadhaa, ikiwemo suala zima la

usimamizi, kwani huu ni utaratibu mpya, ambapo watoa huduma za fedha ambao kimsingi sio taasisi za fedha, nao sasa wanaweza kutoa huduma za kifedha. Changamoto hapa ni kuweka mfumo imara wa usimamizi utakaowawezesha mamlaka husika kufuatilia kikamilifu athari zinazoweza kujitokeza katika utoaji wa huduma hizi. Kwa hivi sasa, huduma ya malipo kwa kutumia simu za mkononi hapa nchini Tanzania inatolewa na benki mbili za biashara na makampuni manne ya mitandao ya simu za mkononi. Sheria na taratibu za kuendesha mfumo huu wa malipo kwa kutumia simu za mkononi, inawataka watoa huduma ambao ni makampuni ya simu za mkononi kushirikiana na mabenki ya biashara katika kutoa huduma hizo. Utaratibu huu wa sasa unaweka pengo katika mfumo wa usimamizi kwa sababu huduma hii ya malipo kwa kutumia simu za mkononi inasimamiwa na mamlaka mbili tofauti na kila moja ikiwa na mipaka ya eneo la usimamizi. Wakati ambapo Benki Kuu ya Tanzania inasimamia masuala ya fedha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inasimamia mitandao ya mawasiliano. Kwa kutambua umuhimu wa kuanzisha chombo imara cha usimamizi wa sekta ya huduma ya malipo kwa kutumia simu za mkononi ambayo inakuwa kwa haraka, Benki Kuu ya Tanzania ilisaini Kumbukumbu za Maelewano na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inayotoa utaratibu wa kuratibu na kusimamia huduma hii kwa pamoja. Benki Kuu ya Tanzania imeanza kuandaa mfumo rahisi wa utaratibu wa usimamizi. Madhumuni ya mfumo huu ni kuhamasisha uvumbuzi mpya utakaowezesha wateja kupata huduma ya fedha kwa urahisi na kupunguza matumizi ya fedha taslimu.

217. Changamoto nyingine ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za fedha kuwafikia watu wengi zaidi na kuimarisha umadhubuti wa taasisi ndogo ndogo za kifedha. Pamoja na umuhimu wa kuendelea kuimarisha mafanikio yaliyopatikana kutokana na mchango wa taasisi ndogo ndogo za fedha wa kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha, kuna changamoto kadhaa zinazohitaji kutafutiwa ufumbuzi. Mojawapo ya changamoto ni kuhakikisha kuwa taasisi hizi zinakuwa endelevu. Kutokana na maendeleo ya teknolojia, ubunifu na uboreshaji wa mazingira ya kibiashara, ufanisi wa taasisi ndogo ndogo za fedha katika nchi nyingi duniani umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, sehemu kubwa ya sekta ndogo ya fedha na hususan ile

inayohudumia watu wa kipato cha chini inategemea kwa kiasi kikubwa misaada na ruzuku kutoka kwa wafadhili wa nje. Wadau wakubwa wa misaada ambao ni wafadhili na serikali, wameonesha kuchoka kuendelea kutoa ruzuku kulipia gharama za uendeshaji wa taasisi hizi, na msimamo uliopo ni kuacha kutoa ufadhili ili taasisi hizo zijiendeshe kibiashara.

218. Changamoto nyingine inatokana na ukweli kwamba taasisi hizi zinalenga zaidi kutoa mikopo kwa kaya masikini na kampuni ndogo ndogo. Mbali ya mikopo, inafahamika kuwa watu wa kipato cha chini wanahitaji huduma zingine pia kama bima na huduma za kuazimana vifaa. Changamoto iliyopo hapa ni jinsi ya kuzisaidia taasisi hizi ndogo za fedha kujiingiza katika ubunifu wa utoaji wa aina tofauti za huduma na bidhaa hasa zikiwalenga watu wanaoishi vijijini na wa kipato cha chini. Kwa mfano, huduma ndogo ndogo za bima (mfano ya mazao shambani) zingeweza kutoa mchango mkubwa katika kupunguza makali ya athari zinazoweza kutokea kutokana na hali mbaya ya hewa.

219. Aidha, usimamizi wa sekta hizi ndogo za fedha ni changamoto nyingine inayoikabili sekta ya fedha kwa ujumla. Nchi nyingi ikiwemo Tanzania zina mamia ya taasisi za aina hii, hali inayowafanya Mamlaka husika kuwa na wakati mgumu katika kufuatilia kikamilifu utendaji wa taasisi hizi kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinasimamiwa ipasavyo.

220. Changamoto nyingi zilizotajwa hapo juu ni za upande wa ugavi, hata hivyo kwa upande wa mahitaji napo kuna mapungufu, kama vile ukosefu wa mali zitakazotumika kama rehani ili kuweza kupata mkopo. Katika nchi nyingi, mali za vijijini kama vile ardhi na nyumba ambazo zingeweza kutumika kama rehani bado hazijaandikishwa katika mfumo rasmi na hata pale ambapo zimeandikishwa, thamani yake ni ya chini sana. Hali hii inahitaji serikali kuingilia kati na kuchukua hatua ambazo zitawezesha taasisi za fedha kutoa huduma za kifedha kwa watu wenye kipato cha chini na wa vijijini bila kuhitaji kuweka rehani mali zisizohamishika. Kwa mantiki hiyo, kuanzishwa kwa taasisi itakayokuwa inasimamia na kuweka kumbukumbu za wakopaji ("Credit Reference Bureau") kutaenda sambamba na upanuzi wa mfumo wa utoaji wa

huduma za fedha. Taasisi hiyo itazisaidia taasisi za fedha kupata taarifa za mwenendo wa wakopaji na hivyo kuwezesha wakopaji ambao hawana mali za kuweka rehani kutumia kumbukumbu zao za marejesho ya mkopo kama ishara ya uaminifu katika kupata mkopo. Baadhi ya nchi zimechukua hatua zaidi ya hii na zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuondoa kikwazo cha rehani katika kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha.

221. Njia nyingine inayotumika ni ya utaratibu wa kutoa sehemu ya Dhamana (Partial Guarantee Schemes) kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha, hususan, kwa wajasiriamali wadogo na wa-kati pamoja na wakulima. Mpango huu utawasaidia wakopaji wadogo wadogo na watu wa kipato cha chini kupunguza gharama zinazotozwa na taasisi za fedha, wakati wa kuchukua mikopo, ambapo mara nyingi gharama hizi zinakwamisha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kutekeleza miradi yenye faida. Tofauti na utaratibu wa kutoa mikopo kwa maelekezo maalum, (Directed Lending Programmes), Mpango huu ni rahisi kutekeleza kwa sababu pamoja na kuwa Serikali inahusishwa kwa kiasi kikubwa katika kutoa fedha na usimamizi wa mpango huu, tathmini na ufuatiliaji wa mikopo hufanywa na sekta binafsi. Changamoto kubwa hapa ni kuepuka kujenga mazingira ambayo benki zitashawishika kutoa fedha kwa shughuli zile tu ambazo zimedhaminiwa na Serikali na kuziacha zile ambazo hazitadhaminiwa na serikali.

**Hitimisho**

222. Benki hazina budi kuweka mikakati maalum ya kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha kuwafikia watu wenye kipato cha chini na hii itumike kama fursa ya kibiashara na wakati huo huo kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii. Namna mojawapo ya kufanikisha hili na kwa gharama ndogo, ni kuangalia jinsi ya kuunganisha taasisi ndogo ndogo za fedha na jamii, ikiwemo kutumia njia mpya za kiteknoligia.

223. Hara hivyo, watunga sera hawana budi kutambua kuwa mpango wa kueneza huduma za kifedha katika maeneo mengi sio wa mwisho bali njia tu ya kuelekea kwenye mafanikio. Hatima ya mpango huu ni kuwasaidia wananchi, hususan maskini kupata maendeleo ya kijamii na kiuchumi, na hivyo

kuchangia katika kupunguza umasikini. Ili kufanikisha hili, mpango wa kueneza/kuongeza huduma za kifedha lazima utekelezwe kwa pamoja na mikakati mingine ya kupunguza umasikini, kuanzia ngazi ya juu kitaifa, mpaka ngazi ya chini. Kwa mfano, sera ambazo zinaweka vipaumbele katika kuimarisha miundombinu ya vijijini, kama vile barabara, umeme na umwagiliaji, zinaweza kuwa na manufaa zaidi katika jamii kuliko sera ambazo zinalenga kupunguza gharama za kukopa.

# SEHEMU YA NNE

## MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

# SURA YA 11

# KILIMO NA USHIRIKA

## Kiwango cha Ukuaji

224. Shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha: mazao; mifugo; na misitu na uwindaji zilikua kwa asilimia 4.2 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2009. Ukuaji katika shughuli ndogo za kiuchumi za mazao; mifugo; na misitu na uwindaji zilikuwa asilimia 4.4, 3.4 na 4.1 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 3.4, 2.3 na 3.5 mwaka 2009, kwa mtiririko huo. Shughuli za kilimo zilichangia asilimia 24.1 ya Pato la Taifa mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 24.6 mwaka 2009. Mchango wa shughuli ndogo za mazao na mifugo katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 18.4 na 4.0 mwaka 2009, hadi asilimia 17.8 na 3.8 mwaka 2010, kwa mtiririko huo. Hata hivyo mchango wa shughuli ndogo za misitu na uwindaji katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 2.4 mwaka 2010, kutoka asilimia 2.2 mwaka 2009.

## Mazao ya Chakula

225. Mwaka 2010, uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi, ulezi/mtama, ndizi na mihogo ulikuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na mwaka 2009 kutokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika msimu wa kilimo 2009/10. Uzalishaji wa zao la mahindi uliongezeka kutoka tani 3,324,000 mwaka 2009 hadi tani 3,326,000 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 0.1. Uzalishaji wa mazao ya ulezi na mtama uliongezeka hadi tani 929,000 kutoka tani 204,000, sawa na ongezeko la asilimia 355.4. Vilevile, uzalishaji wa zao la ngano uliongezeka kutoka tani 94,000 mwaka 2009, hadi tani 95,000 mwaka 2010 na uzalishaji wa zao la muhogo uliongezeka kutoka tani 1,759,000 mwaka 2009, hadi 1,972,000 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Hata hivyo, uzalishaji wa mchele ulipungua kutoka tani 886,000 mwaka 2009, hadi tani 868,000 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 2.0. Uzalishaji wa mazao ya chakula ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 11.1: Uzalishaji wa mazao ya chakula 2007 – 2010 (Tani 000)**

| Zao | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 3,302 | 3,555 | 3,324 | 3,326 | 0.1 |
| Mchele | 872 | 875 | 886 | 868 | -2.0 |
| Ngano | 83 | 92 | 94 | 95 | 1.1 |
| Mtama/Ulezi | 1,165 | 1,064 | 204 | 929 | 355.4 |
| Mihogo | 1,733 | 1,797 | 1,759 | 1,972 | 12.1 |
| Maharage/Mikunde | 1,156 | 1,125 | 1,184 | 1,116 | -5.7 |
| Ndizi | 1,027 | 982 | 991 | 1,073 | 8.3 |
| Viazi vitamu | 1,322 | 1,379 | 1,381 | 1,392 | 0.8 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

**Uzalishaji wa Mazao ya Biashara**

226. Mwaka 2010, uzalishaji wa mazao ya biashara hususan kahawa, pareto, mkonge, korosho, tumbaku, chai na sukari uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2009. Kuongezeka kwa uzalishaji kulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya miche bora, wakulima kutumia mbinu bora za kilimo, kuongezeka kwa upanuzi wa mashamba ya kilimo na ufufuaji wa mashamba yaliyotelekezwa. Zao la pamba ndilo lililopungua kiwango cha uzalishaji ikilinganishwa na mazao mengine kwa mwaka 2010. Uzalishaji huo ulipungua kwa asilimia 38.7 mwaka 2010 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 33.1 mwaka 2009. Kushuka kwa uzalishaji wa pamba kulitokana na hali mbaya ya hewa kwenye maeneo yanayolima zao hilo.

**Jedwali Na. 11.2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara 2007-2010 (Tani).**

| Zao | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 199,954 | 200,662 | 267,004 | 163,644 | 38.7 |
| Tumbaku | 50,784 | 55,356 | 60,900 | 130,000 | 113.5 |
| Sukari | 279,494 | 276,605 | 279,850 | 317,000 | 13.3 |
| Chai | 34,763 | 34,770 | 33,160 | 55,699.13 | 68.0 |
| Pareto | 1,000 | 1,500 | 3,320 | 5,000 | 50.6 |
| Kahawa | 33,708 | 58,052 | 40,000 | 60,575 | 51.4 |
| Mkonge | 33,039 | 33,000 | 26,363 | 35,000 | 32.8 |
| Korosho | 92,573 | 99,107 | 74,169 | 121,070 | 63.2 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Bodi za mazao husika

**Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta**

227. Mwaka 2010, uzalishaji wa mazao ya mafuta yakiwemo alizeti, karanga, ufuta na soya uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2009. Ongezeko hilo lilitokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo yanayozalisha kwa wingi mazao hayo na kuendelea kupanuka kwa wigo wa soko la ufuta. Mchanganuo wa uzalishaji wa mazao ya mafuta ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 11.3 Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta 2007 – 2010 (Tani)**

| Zao | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | 369,803 | 418,317 | 466,831 | 489,387 | 4.8 |
| Karanga | 408,058 | 396,769 | 385,480 | 395,420 | 2.6 |
| Ufuta | 155,794 | 46,767 | 115,295 | 125,369 | 8.7 |
| Soya | 3,000 | 3,450 | 3,900 | 4,300 | 10.3 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

#### Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo

228. Mwaka 2010, jumla ya matrekta makubwa mapya 1,586 yaliingizwa nchini, ikilinganishwa na matrekta 472 mwaka 2009. Vilevile, matrekta madogo (*Power Tillers*) 2,553 yaliingizwa nchini, ikilinganishwa na matrekta madogo 495 mwaka 2009. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya matrekta nchini kwa ajili ya kilimo pamoja na mikopo iliyotolewa kwa ajili ya ununuzi wa zana bora za kilimo.

#### Kilimo cha Umwagiliaji

229. Mwaka 2010, eneo la jumla ya hekta 90,000 za umwagiliaji lilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu na kufikia jumla ya hekta 365,744, kutoka hekta 275,744 za mwaka 2009. Jumla ya hekta 331,490 za umwagiliaji ziliendelezwa ikilinganishwa na hekta 310,745 zilizoendelezwa mwaka 2009 kwa kujengewa miundombinu ya umwagiliaji, sawa na ongezeko la asilimia 6.7. Aidha, katika mwaka 2010, jumla ya wakulima 510 na wataalam 30 katika ngazi mbalimbali walipatiwa mafunzo kuhusu kuendeleza teknolojia sahihi za umwagiliaji na matumizi bora ya maji kwa umwagiliaji, ikilinganishwa na wakulima 300 na wataalam 50 katika mwaka 2009.

230. Mwaka 2010, tija katika skimu za umwagiliaji ziliboreshwa katika mazao ya mpunga, vitunguu, nyanya na mahindi ikilinganishwa na mwaka 2009. Tija katika uzalishaji wa mpunga uliongezeka na kufikia wastani wa tani 7.5 kwa hekta kutoka tani 2; vitunguu tani 26 kwa hekta kutoka tani 13; nyanya tani 18 kwa hekta kutoka tani 5 na mahindi ni wastani wa tani 4 kwa hekta kutoka tani 1.5. Ufanisi wa matumizi ya maji katika kilimo cha umwagiliaji kwenye skimu ambazo miundombinu yake iliboreshwa uliongezeka kati ya asilimia 30 hadi asilimia 45, ikilinganishwa na ufanisi wa kati ya asilimia 10 hadi asilimia15 katika skimu ambazo miundombinu yake ni ya asili. Muhtasari wa mafanikio kwa ujumla ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 11.4: Huduma za Umwagiliaji**

| Mafanikio | 2009 | 2010 | Badiliko (%) 2009/10 |
|---|---|---|---|
| Hekta zilizofanyiwa upembuzi yakinifu. | 275,744 | 365,744 | 32.6 |
| Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji. | 4 | 6 | 50 |
| Hekta zilizoendelezwa. | 310,745 | 331,490 | 6.7 |
| Jumla ya idadi ya kaya zinazonufaika na miundombinu ya umwagiliaji katika skimu zilizoendelezwa. | 342,700 | 351,720 | 2.6 |
| Uundaji na usajili wa vikundi vya umwagiliaji. | 182 | 210 | 15.4 |
| Mafunzo kwa wakulima katika matumizi bora ya maji kwa umwagiliaji na teknolojia za umwagiliaji. | 300 | 510 | 70 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika.

**Huduma za Ugani na Mafunzo**

231. Mwaka 2010, jumla ya wanafunzi tarajali 5,442 wa ngazi ya Stashahada na Astashahada walidahiliwa na kufundishwa katika fani mbalimbali. Kati ya hao, wanafunzi 3,500 walikuwa wa mwaka wa kwanza na wa pili ambao wanaendelea na masomo na wanafunzi 1,942 wamemaliza masomo yao mwezi Novemba 2010. Kati ya waliomaliza, wanafunzi 1,911 wanasubiri kibali cha ajira.

232. Mwaka 2010, wataalam wapya 1,738 waliajiriwa katika Halmashauri za Wilaya nchini, nakufanya idadi ya wataalam wa ugani kufikia 6,175 ikilinganishwa na wataalam 4,437 waliokuwepo mwaka 2009.

233. Mwaka 2010, jumla ya wakulima 174,376 waliwezeshwa kupitia mbinu shirikishi ya Shamba Darasa ambapo walipatikana wakulima wawezeshaji 930 waliowez a kutoa huduma kwa wakulima wenzao 69,750 chini ya usimamizi wa wataalam wa ugani. Aidha, jumla ya wakulima 593,400 waliwezeshwa kupata mafunzo ya kilimo bora pamoja na taarifa za bei za mazao kupitia vituo vya

rasilimali za kilimo vya kata. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi 199 (NGOs, CBOs na Vikundi vya wakulima) ilitoa huduma za ugani kwa wakulima katika Halmashuri 38 za mikoa 12 ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Mara, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Kigoma, Tabora na Mwanza. Baadhi ya huduma hizo ni pamoja na mafunzo ya kanuni za kilimo bora kwa wakulima/wafugaji, huduma ya uhimilishaji na chanjo za mifugo, ujenzi wa malambo na utafutaji masoko.

234. Katika kuboresha huduma za ugani, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPs) ilinunua magari 100, pikipiki 1,612 na baiskeli 3,389 ili kurahisisha usafiri kwa waratibu wa ASDP na maafisa ugani. Hadi Desemba 2010, zaidi ya asilimia 80 ya wataalam katika ngazi ya kata walikuwa wamepata a pikipiki.

## Shughuli za Utafiti

235. Mwaka 2010, mbegu mpya 25 za mazao ya chakula na biashara zilizogunduliwa mwaka 2009 zilipitishwa ili ziweze kutumika kwa wakulima. Jumla ya kilo 30,465 za mbegu na vipando 422,000 katika ngazi ya mbegu mama na vipando 1,260,000 katika ngazi ya mbegu ya msingi vilizalishwa. Uzalishaji wa mbegu hizo unaainishwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 11.5 Uzalishaji wa Mbegu Mama**

| Na | Zao | Uzalishaji mbegu mama (tani) | |
|---|---|---|---|
| | | 2009 | 2010 |
| 1 | Jamii ya nafaka | 51.2 | 13.13 |
| 2 | Jamii ya mikunde | 43.5 | 11.53 |
| 3 | Jamii ya mafuta | 10.3 | 4.3 |
| 13 | Pamba | 6.0 | 1.48 |
| 14 | *Muhogo (Vipingili) | 27.6 milioni | 422,000 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.
*Jamii ya mizizi vipando

### Mfuko wa Pembejeo

236. Mwaka 2010, Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo ilitoa mikopo 30 ya matrekta madogo ya mikono (power tillers), ikilinganishwa na mikopo 57 iliyotolewa mwaka 2009. Aidha, mikopo 89 ya matrekta makubwa ilitolewa mwaka 2010, ikilinganishwa na mikopo 165 mwaka 2009. Mikopo 46 ilitolewa kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo, ikilinganishwa na mikopo 238 mwaka 2009 . Vilevile, mkopo mmoja tu ulitolewa kwa zana za umwagiliaji mwaka 2010. Kupungua kwa utoaji wa mikopo hiyo kulitokana na ufinyu wa bajeti.

**Jedwali Na. 11.6: Utoaji Mikopo kwa Mfuko wa Pembejeo (Idadi)**

| Na. | Aina ya mikopo | Mikopo iliyotolewa Mwaka 2009 | Mikopo iliyotolewa Mwaka 2010 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mikopo ya matrekta madogo ya mikono (Power tillers) | 57 | 30 | - 47.4 |
| 2 | Mikopo ya matrekta makubwa mapya. | 165 | 89 | 46.06 |
| 3 | Mikopo ya ukarabati wa matrekta | 1 | 3 | 200 |
| 4 | Mikopo ya Pembejeo za kilimo na mifugo mchanganyiko | 238 | 46 | -80.7 |
| 5 | Mikopo ya zana za umwagiliaji | 0 | 1 | 100 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika.

### Utoaji wa Ruzuku za Pembejeo

237. Mwaka 2008/2009, Serikali iliamua kubadilisha utaratibu wa zamani wa kulipa fedha za ruzuku moja kwa moja kwa makampuni na kuamua kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa kutumia utaratibu wa vocha. Katika utaratibu huo, Vocha zilizotolewa kwa mkulima ni za aina tatu: vocha moja ya mbegu bora; vocha moja kwa ajili ya mbolea ya kupandia na vocha moja kwa ajili ya mbolea ya kukuzia. Vocha hizi zilitolewa kwa mazao ya chakula, ambayo ni mahindi au mpunga. Vilevile, mwaka 2009/2010, Serikali iliamua kuongeza ruzuku kwa mkulima wa zao la pamba. Mkulima wa zao la pamba

alipata vocha za aina mbili: Vocha moja kwa ajili ya mbegu ya pamba na Vocha moja kwa ajili ya madawa ya pamba. Hadi kufikia mwaka 2010, mikoa 20 ilinufaika na ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa utaratibu wa vocha, ikilinganishwa na mikoa 11 iliyonufaika mwaka 2008/09. Kutokana na utaratibu huo, uzalishaji wa zao la mahindi uliongezeka kwa asilimia 45.0, hadi wastani wa tani 3.35 milioni mwaka 2010 kutoka tani 2.31 milioni mwaka 2007, wakati ambapo uzalishaji katika zao la mpunga uliongezeka kwa asilimia 10.3 hadi wastani wa tani 0.96 milioni mwaka 2010, kutoka tani 0.87 milioni mwaka 2007.

**MIFUGO**

**Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake**

238. Mwaka 2010, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku uliongezeka na kufikia tani 449,673 kutoka tani 422,230 zilizozalishwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na mazao yake na kupanuka kwa wigo wa masoko.

239. Mwaka 2010, uzalishaji wa maziwa nchini uliongezeka kwa asilimia 2.9, kutoka lita 1.60 bilioni mwaka 2009, hadi lita 1.65 bilioni. Kati ya hizo, lita milioni 653 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita milioni 997 zilitokana na ng'ombe wa asili. Hii ilitokana na ongezeko la ukusanyaji wa maziwa kutoka maeneo ya wafugaji na idadi ya ng'ombe wa maziwa. Uzalishaji wa mbegu bora za uhimilishaji kutoka Kituo cha uhimilishaji (National Artificial Insemination Centre – NAIC) uliongezeka kutoka dozi 74,200 mwaka 2009, hadi dozi 86,800 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 17.0. Aidha, idadi ya ng'ombe waliohimilishwa iliongezeka kutoka ng'ombe 68,900 mwaka 2009 hadi ng'ombe 73,900 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 7.3.

240. Uzalishaji wa mayai ya kuku uliongezeka kutoka mayai bilioni 2.81 mwaka 2009, hadi mayai bilioni 2.9 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 4.0. Idadi ya kuku wa asili iliongezeka kwa asilimia 2.9, kutoka kuku milioni 34 mwaka 2009 hadi kufikia kuku milioni 35 mwaka 2010. Ongezeko hilo lilitokana na wafugaji kuendelea kutumia chanjo stahimilifu ya joto ya kuzuia

ugonjwa wa mdondo wa kuku, ambayo ilisaidia kupunguza vifo vya kuku wa asili kutoka asilimia 90.0 hadi asilimia 4.0.

241. Mwaka 2010, tani 45.0 za mbegu bora za aina mbalimbali za malisho zilizalishwa katika mashamba ya Serikali, ikilinganishwa na tani 43.0 zilizozalishwa mwaka 2009. Aidha, jumla ya marobota 303,000 ya hei yalizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali, ikilinganishwa na marobota 420,000 yaliyozalishwa mwaka 2009. Pia, jumla ya marobota 418,831 ya hei yalizalishwa na sekta binafsi, ikilinganishwa na marobota 509,680 ya mwaka 2009. Mwaka 2010, tani 801,727 za aina mbalimbali ya vyakula vya mifugo zilizalishwa, ikilinganishwa na tani 717,231 zilizozalishwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 11.8.

**Jedwali Na. 11.7: Uzalishaji wa Mazao yatokanayo na Mifugo 2006 - 2010**

| Mazao | Uzalishaji/Kipimo | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | % Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Nyama:** | | | | | | | |
| Ng'ombe | Tani | 210,370 | 180,629 | 218,976 | 225,178 | 243,943 | 8.3% |
| Mbuzi/Kondoo | Tani | 78,579 | 80,936 | 81,173 | 82,884 | 86,634 | 4.5% |
| Nguruwe | Tani | 29,925 | 31,721 | 33,307 | 36,000 | 38,180 | 6.1% |
| Kuku | Tani | 69,420 | 77,280 | 77,250 | 78,168 | 80,916 | 3.5% |
| **Jumla** | | 388,294 | 370,566 | 410,706 | 422,230 | 449,673 | 6.5 |
| **Maziwa:** | | | | | | | |
| Ng'ombe asilia | Lita (000) | 941,815 | 945,524 | 980,000 | 1,012,436 | 997,261 | -1.5% |
| Ng'ombe wa kisasa | Lita (000) | 470,971 | 475,681 | 520,000 | 591,690 | 652,596 | 10.3% |
| **Jumla** | | 1,412,786 | 1,421,205 | 1,500,000 | 1,604,126 | 1,649,857 | 2.9 |
| Mayai | Idadi | 2,145,000 | 2230,900 | 2,690,000 | 2,806,350 | 2,917,875 | 4.0% |
| Uzalishaji Vyakula vya Mifugo | Tani | - | - | - | 801,827 | 720,711 | -10.1% |

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

242. Mwaka 2010, idadi ya mifugo nchini ilikadiriwa kufikia ng'ombe milioni 19.2, mbuzi milioni 13.7, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.9 na kuku milioni 58. Kati ya ng'ombe hao, 680,000 ni ng'ombe wa maziwa, vilevile kati ya kuku hao, milioni 35 ni kuku wa asili na milioni 23 ni kuku wa kisasa, ambapo milioni 7 kati yao ni kuku wa mayai na milioni 16 ni kuku wa nyama.

Wastani wa ulaji mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka ni kilo 12 za nyama, lita 43 za maziwa na mayai 75. Ulaji huu ni mdogo ikilinganishwa na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo Duniani vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

**Biashara ya Mifugo na Mazao yake**

243. Mwaka 2010, idadi ya mifugo iliyouzwa minadani iliongezeka hadi kufikia ng'ombe 857,208, mbuzi 682,992 na kondoo 122,035, ikilinganishwa na ng'ombe 781,230, mbuzi 623,732 na kondoo 114,564 mwaka 2009. Aidha, idadi hiyo ya mifugo iliyouzwa minadani ilikuwa na thamani ya shilingi 382.2 bilioni mwaka 2010, ikilinganishwa na shilingi 319.2 bilioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 19.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarishwa kwa huduma za minada na wafugaji kuongeza mauzo ya mifugo yao.

244. Mwaka 2010, jumla ya ng'ombe 2,970 na mbuzi 302 wenye thamani ya shilingi 2.8 bilioni waliuzwa katika nchi za Comoro, Burundi na Kenya ikilinganishwa na jumla ya ng'ombe 3,264 na mbuzi na kondoo 1,834 wenye thamani ya shilingi 2.1 bilioni waliouzwa nje mwaka 2009. Aidha, jumla ya tani 36.9 za nyama ya ng'ombe zenye thamani ya shilingi 183,852,732, tani 122 za nyama ya mbuzi zenye thamani ya shilingi 550,516,392 na tani 34.6 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi 186,687,992 ziliuzwa nje katika nchi za Oman, Kuwait, Umoja wa fahne za Kiarabu (UAE), Muscat, Malawi na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, ikilinganishwa na tani 139.8 za nyama ya ng'ombe zenye thamani ya shilingi 416.9 milioni, tani 35.4 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi 120.2 milioni na tani 46.7 za nyama ya mbuzi zenye thamani ya shilingi 117.3 milioni, zilizouzwa nje mwaka 2009.

245. Mwaka 2010, jumla ya vipande milioni 1.5 vya ngozi za ng'ombe, milioni 2.4 vya mbuzi na milioni 0.65 vya kondoo, vyenye thamani ya shilingi 8.5 bilioni vilikusanywa. Kati ya hivyo, vipande vya ngozi ya ng'ombe 739,315, mbuzi milioni 1.9 na kondoo 176,400 viliuzwa nje ya nchi, ikilinganishwa na vipande vya ngozi ya ng'ombe 982,668, mbuzi milioni 2.7 na kondoo 769,936 mwaka 2009. Mapato yatokanayo na mauzo ya ngozi yalishuka kwa asilimia 36.0, kutoka shilingi 12.8 bilioni mwaka 2009 hadi shilingi 8.19 bilioni mwaka 2010. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa bei ya ngozi katika soko la kimataifa.

246. Mwaka 2010, idadi ya vipande vya ngozi iliyosindikwa ilipungua hadi vipande milioni 1.96, kutoka vipande milioni 2.3 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 14.8. Aidha, thamani ya mauzo ya vipande vilivyosindikwa ilishuka hadi shilingi 6.57 bilioni, kutoka shilingi 7.3 bilioni mwaka 2009. Uwiano wa ngozi iliyosindikwa na kuuzwa nje ya nchi uliongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2009, hadi asilimia 69 mwaka 2010 ya ngozi zote zilizouzwa nje. Ongezeko la usindikaji lilitokana na kuhamasika kwa wafanyabiashara kuuza ngozi zilizosindikwa ili kupata bei nzuri kwenye masoko ya nje kuliko kuuza ngozi ghafi.

Jedwali Na. 11.8: Ukusanyaji, Uuzaji wa Ngozi Ndani na Nje ya Nchi na Madaraja ya Ngozi hizo – (2002 - 2010)

| A. UKUSANYAJI WA NGOZI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za Mbuzi | Ngozi za Kondoo | Thamani Tshs.'000 |
| 2002 | 1,400,000 | 700,000 | 350,000 | 4,500,000 |
| 2003 | 1,400,000 | 800,000 | 460,000 | 5,500,000 |
| 2004 | 1,600,000 | 1,200,000 | 650,000 | 6,500,000 |
| 2005 | 1,600,000 | 1,500,000 | 750,160 | 5,500,000 |
| 2006 | 1,660,000 | 1,400,000 | 950,000 | 6,800,000 |
| 2007 | 1,980,000 | 1,520,000 | 1,200,000 | 8,700,000 |
| 2008 | 2,500,000 | 1,900,000 | 1,500,000 | 13,500,000 |
| 2009 | 1,650,000 | 2,990,000 | 1,250,000 | 10,900,000 |
| 2010 | 1,500,000 | 2,400,000 | 650,000 | 8,500,000 |

| B. UUZAJI NGOZI NJE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za Mbuzi | Ngozi za Kondoo | Thamani Tshs.'000 |
| 2002 | 1,200,000 | 511,700 | 165,000 | 4,000,000 |
| 2003 | 1,300,000 | 600,000 | 300,000 | 4,600,000 |
| 2004 | 1,774,000 | 1,431,000 | 488,000 | 5,712,000 |
| 2005 | 1,400,000 | 1,200,000 | 597,155 | 4,025,400 |
| 2006 | 1,363,721 | 1,216,740 | 861,770 | 7,500,000 |
| 2007 | 1,700,000 | 1,055,000 | 925,530 | 16,200,000 |
| 2008 | 2,300,000 | 1,600,000 | 1,100,000 | 21,500,000 |
| 2009 | 982,668 | 2,700,000 | 769,936 | 12,800,000 |
| 2010 | 739,315 | 1,912,182 | 176,400 | 8,191,803 |

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

## USHIRIKA NA MASOKO

### Maendeleo ya Ushirika

247. Mwaka 2010, Serikali iliendelea na Programu ya mageuzi na maboresho ya Ushirika nchini ambapo vyama vikuu vya ushirika vipya vilianzishwa na vilivyokuwa vinasuasua viliunganishwa na vingine vilifutwa. Hadi kufikia mwaka 2010, idadi ya vyama vya ushirika ilikuwa 9,501, ikilinganishwa na vyama 9,510 mwaka 2009. Aidha, katika mwaka 2010, elimu na mafunzo juu ya masuala mbali mbali ya ushirika yalitolewa kwa vyama 103 na vikundi 30 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga, Kigoma, Kagera, Kilimanjaro, Lindi na Mtwara. Vilevile, katika kutekeleza Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, vyama vya ushirika katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, na Pwani vilikusanya Korosho za wakulima takribani kilo 85,000,000 na kuwezesha wakulima kupata bei nzuri ya kati ya shilingi 800/= na 1,000/= kwa kilo tofauti na bei ya awali ya kati ya shilingi 250/= na 300/= kwa kilo.

248. Vyama vya ushirika vya akiba na mikopo (SACCOS) viliongezeka na kuendelea kuimarishwa ili viweze kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi hususan, vijijini. Mwaka 2010, idadi ya SACCOS iliongezeka hadi kufikia 5,344 kutoka 5,332 mwaka 2009. Idadi ya wanachama iliongezeka na kufikia 911,873 kutoka 820,670 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Hisa za wanachama ziliongezeka kwa asilimia 9.9, hadi bilioni 36.8 kutoka shilingi bilioni 33.5 mwaka 2009. Akiba na amana za wanachama ziliongezeka hadi bilioni 174.5, kutoka shilingi bilioni 148.1 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 17.8. Aidha, mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kwa asilimia 20.8 hadi shilingi bilioni 463.4, kutoka shilingi bilioni 383.5 mwaka 2009.

Jedwali Na. 11.11: Maendeleo ya Ushirika

| Aina ya ushirika | Mwaka | | Badiliko % |
|---|---|---|---|
| | 2009 | 2010 | |
| SACCOS | 5,332 | 5,344 | 0.2 |
| AMCOS | 2,817 | 2798 | -0.7 |
| Ushirika wa Umwagiliaji | 113 | 113 | 0 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

**Mwenendo wa Bei za Mazao ya Biashara**

249. Mwaka 2010, wastani wa bei ya kahawa aina ya robusta ilishuka kwa asilimia 29, kutoka wastani wa Dola za Kimarekani 2.20 kwa kilo hadi wastani wa Dola 1.57. Kushuka huku kulichangiwa na kupungua kwa mahitaji ya kahawa ya robusta katika soko la dunia. Wastani wa bei ya Kahawa-Arabica ilipanda na kufikia Dola za Kimarekani 3.45 kwa kilo, kutoka Dola 2.98 kwa kilo mwaka 2009. Bei ya Chai ilipanda hadi dola za Kimarekani 2.91 kwa kilo, kutoka Dola 2.40 mwaka 2009. Mwaka 2010, hakukuwa na mabadiliko katika bei ya Pamba ambapo ilibaki Dola za Kimarekani 1.99 kwa kilo. Bei ya Mkonge ilishuka hadi kufikia Dola za Kimarekani 856 kwa kilo, kutoka Dola 1,209.88 mwaka 2009. Wastani wa bei ya Karafuu ilipanda na kufikia dola za Kimarekani 4,335.88 kwa kilo, kutoka Dola 4,021.46 kwa kilo.

Jedwali Na. 11.12 Mwenendo wa Wastani wa Bei za Mazao ya Biashara katika Soko la Dunia (USD/Kg)

| Zao | 2008 | 2009 | 2010 | Machi, 2010 | April, 2010 | Mei, 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa-robusta | 2.20 | 2.20 | 1.57 | 1.48 | 1.58 | 1.56 |
| Kahawa-Arabica | 2.98 | 2.98 | 3.45 | 3.63 | 3.73 | 3.82 |
| Chai | 2.26 | 2.40 | 2.91 | 2.62 | 2.77 | 2.83 |
| Pamba | 1.92 | 1.99 | 1.99 | 1.66 | 1.46 | 1.71 |
| Mkonge (M/T) | 1053.56 | 1209.88 | 908.00 | 856.00 | 856.00 | 856.00 |
| Karafuu (M/T) | 3967.33 | 4021.46 | 4335.88 | 4500 | 4710 | 4700 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

## UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

Jedwali Na. 35

| Msimu[1] | Miwa | | | | Sukari | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakulima | | | | | Iliyotumika[3] | |
| | Umma (000 Tani) | Binafsi (000 Tani) | Jumla (000 Tani) | Bei[2] (Sh./Tan) | Iliyozalishwa Tani | Jumla Tani | Kilo kwa kila mtu[4] |
| 1977/78 | 1008 | 116 | 1124 | 96.20 | 132979 | 111546 | 6.69 |
| 1978/79 | 1169 | 197 | 1366 | 96.20 | 114267 | 127712 | 7.42 |
| 1979/80 | 1180 | 210 | 1390 | 101.20 | 122530 | 112282 | 6.34 |
| 1980/81 | 854 | 193 | 1047 | 106.20 | 114667 | 115961 | 6.37 |
| 1981/82 | 1135 | 203 | 1338 | 137.30 | 124326 | 120629 | 6.44 |
| 1982/83 | 1090 | 113 | 1203 | 170.00 | 101996 | 93179 | 4.84 |
| 1983/84 | 1372 | 160 | 1532 | 238.00 | 131525 | 108369 | 54.8 |
| 1984/85 | 1148 | 105 | 1253 | 323.70 | 108102 | 111433 | 54.8 |
| 1985/86 | 1003 | 104 | 1107 | 352.30 | 100287 | 95379 | 4.56 |
| 1986/87 | 991 | 72 | 1063 | 463.00 | 94815 | 109462 | 5.09 |
| 1987/88 | 997 | 102 | 1099 | 600.00 | 101266 | 96271 | 4.35 |
| 1988/89 | 787 | 91 | 878 | 750.00 | 96227 | 126771 | 5.29 |
| 1989/90 | 963 | 98 | 1061 | 1748.45 | 111236 | 190750 | 5.47 |
| 1990/91 | 1068 | 116 | 1184 | 2525.90 | 118560 | 212585 | 5.93 |
| 1991/92 | 967 | 114 | 1081 | 3476.85 | 108480 | 202478 | 6.07 |
| 1992/93 | 1098 | 273 | 1371 | 5267.67 | 121414 | 204126 | 6.11 |
| 1993/94 | 1105 | 362 | 1467 | 6200.00 | 123949 | 139829 | 5.38 |
| 1994/95 | 914 | 370 | 1284 | 8600.00 | 104624 | 238424 | 5.38 |
| 1995/96 | 997 | 372 | 1369 | 8900.00 | 116810 | 268910 | .. |
| 1996/97 | 951 | 347 | 1298 | 9500.00 | 116100 | 275700 | 5.54 |
| 1997/98 | 808 | 176 | 984 | 10500.00 | 116100 | 271790 | 5.70 |
| 1998/99 | 948 | 320 | 1268 | 12500.00 | 113622 | 101272 | 5.87 |
| 1999/00 | 907 | 341 | 1248 | 12500.00 | 116927 | 100127 | 6.70 |
| 2000/01 | 1050 | 284 | 1334 | 14000.00 | 135534 | 122534 | 10.00 |
| 2001/02 | 1134 | 389 | 1523 | 14700.00 | 164498 | 142398 | 10.10 |
| 2002/03 | 1402 | 411 | 1813 | 15000.00 | 190120 | 167300 | 10.42 |
| 2003/04 | 1672 | 670 | 2342 | 16800.00 | 223839 | 290711 | 10.90 |
| 2004/05 | 1594 | 752 | 2346 | 20568.00 | 229617 | 328005 | 10.90 |
| 2005/06 | 1545 | 956 | 2501 | 22383.00 | 263317 | 343292 | 12.00 |
| 2006/07 | 1430 | 611 | 2041 | 29000.00 | 192095 | 366708 | 12.00 |
| 2007/08 | 1967 | 799 | 2766 | 32767.00 | 265434 | 382518 | 13.00 |
| 2008/09 | 2056 | 693 | 2749 | 32770.51 | 279850 | 396113 | 13.10 |
| 2009/10 | 1972 | 597 | 2569 | 42046.00 | 263461 | 398070 | 13.68 |
| Badiliko (%) 08/09-09/10 | 0.04 | 0.16 | 0.07 | -0.22 | 0.06 | 0.00 | 0.02 |
| Ongezeko (%) 77/78-09/10 | 0.96 | 4.15 | 1.29 | 436.07 | 0.98 | 2.57 | 1.01 |

Chanzo: Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni
2 Bei ya Miwa ni ile iliyo na asilimia 10.5 za Sucrose
3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar
4 Ni kwa Tanzania bara
* Sukari ya iliyozalishwa na wakulima/mashirika binafsi

## PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jadwali Na. 36

| Msimu [1] | Pamba yenye mbegu | | | | | Pamba iliyokobolewa mbegu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji Kiasi (tani) | | | Bei ya wastani (Shs/Kilo) | | Kiasi (tani) | | | Mauzo nchini | | |
| | | | | | | | | | Kiasi (tani) | Bei ya wastani (Shs/tani) | |
| | AR | BR | Jumla | AR | BR | AR | BR | Jumla | Jumla [2] | AR | BR |
| 1976/77 | 176694 | 17800 | 194694 | 2.00 | 1.00 | 61549 | 6074 | 67623 | 8146 | 9487 | 7230 |
| 1977/78 | 153292 | 14790 | 168082 | 2.30 | 1.15 | 46555 | 5821 | 52376 | 14422 | 12186 | 9370 |
| 1978/79 | 152267 | 14248 | 166515 | 2.40 | 1.20 | 51072 | 4696 | 55768 | 14263 | 12340 | 8810 |
| 1979/80 | 162087 | 18367 | 180454 | 3.00 | 1.30 | 52546 | 3931 | 56477 | 17284 | 13750 | 11040 |
| 1980/81 | 166233 | 8344 | 174577 | 3.20 | 1.50 | 54189 | 2962 | 57151 | 15634 | 13750 | 11040 |
| 1981/82 | 126799 | 6127 | 132926 | 3.70 | 1.70 | 42439 | 2153 | 44592 | 14070 | 15480 | 11730 |
| 1982/83 | 124559 | 3351 | 127910 | 4.70 | 2.50 | 40521 | 2381 | 42902 | 12660 | 15420 | 11730 |
| 1983/84 | 136151 | 4647 | 140798 | 6.00 | 3.70 | 41779 | 2175 | 43954 | 11771 | 15867 | 12038 |
| 1984/85 | 152355 | 4490 | 156845 | 8.40 | 4.50 | 50858 | 1154 | 52012 | 16236 | 26000 | 17400 |
| 1985/86 | 97384 | 8515 | 105899 | 13.00 | 7.00 | 29715 | 17775 | 47490 | 13247 | 52250 | 37350 |
| 1986/87 | 210454 | 4115 | 214569 | 16.90 | 9.10 | 55108 | 2338 | 57446 | 11389 | 52250 | 37350 |
| 1987/88 | 252177 | 2738 | 254915 | 19.45 | 9.10 | 67057 | 659 | 67716 | 13247 | 81350 | 67250 |
| 1988/89 | 184524 | 4720 | 189244 | 22.35 | 10.00 | 61552 | 1880 | 63432 | 11084 | 175000 | 140000 |
| 1989/90 | 112333 | 572 | 112905 | 28.00 | 11.00 | 37652 | 192 | 37844 | 13184 | 225000 | 190000 |
| 1990/91 | 148124 | 1017 | 149141 | 41.00 | 14.00 | 46880 | 341 | 49221 | 300000 | 300000 | 240000 |
| 1991/92 | 26641 | 32 | 26873 | 70.00 | 28.00 | 90706 | 11 | 90717 | 14301 | 325000 | 255000 |
| 1992/93 | 281984 | 22000 | 303984 | 60.00 | 28.00 | 85784 | .. | 85784 | 4405 | 542916 | .. |
| 1993/94 | 125434 | .. | 125434 | 120.00 | .. | 42895 | .. | 42895 | .. | .. | .. |
| 1994/95 | 125434 | .. | 125434 | 120.00 | .. | 42645 | .. | 42695 | .. | .. | .. |
| 1995/96 | 221148 | .. | 221146 | 207.00 | .. | 64782 | .. | 64782 | .. | .. | .. |
| 1996/97 | 251751 | 74 | 251751 | 170.00 | .. | 85162 | 25 | 85187 | .. | .. | .. |
| 1997/98 | 202217 | .. | 202217 | 180.00 | .. | 67780 | .. | 67780 | .. | .. | .. |
| 1998/99 | 105853 | .. | 105853 | 185.00 | .. | 35460 | .. | 35480 | .. | .. | .. |
| 1999/00 | 100500 | .. | 100500 | 123.00 | .. | 33686 | .. | 33686 | .. | .. | .. |
| 2000/01 | 123556 | .. | 123558 | 160.00 | .. | 41415 | .. | 41415 | .. | .. | .. |
| 2001/02 | 148180 | .. | 148180 | 165.00 | .. | 49668 | .. | 49415 | .. | .. | .. |
| 2002/03 | 187908 | 781 | 188669 | 160.00 | 50 | 62963 | 262 | 63245 | .. | .. | .. |
| 2003/04 | 139756 | 213 | 139969 | 280.00 | 100 | 46643 | 72 | 46915 | .. | .. | .. |
| 2004/05 | 341589 | .. | 341589 | 260.00 | 0 | 114496 | .. | 114496 | .. | .. | .. |
| 2005/06 | 376591 | .. | 376591 | 220.00 | 0 | 126228 | .. | 126228 | .. | .. | .. |
| 2006/07 | 130585 | .. | 130585 | 350.00 | 0 | 43770 | .. | 43770 | .. | .. | .. |
| 2007/08 | 200662 | - | 200662 | 450 | | 70773 | - | 70773 | 37488 | - | - |
| 2008/09 | 368697 | 0 | 368697 | 480 | 0 | 123582 | 0 | 123582 | 66554 | .. | .. |
| 2009/10 | 267644 | 0 | 267644 | 480 | 0 | 54851 | 0 | 54851 | 0 | 0 | 0 |
| Badiliko (%) 2008/09-2009/10 | -0.27 | | -0.27 | 0.00 | | -0.56 | | -0.56 | -100 | | |
| Ongezeko (%) 77/78-09/10 | 0.51 | | 0.37 | 239.00 | | -0.11 | | -0.19 | | | |

Chanzo: Bodi ya Mazao ya Pamba

1 Msimu ni kati ya Juni na Mei

2 Ni jumla ya AR na BR

.. Takwimu hazikupatikana

## ENEO LILILOPANDWA MICHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 37

| Msimu [1] | Eneo lililopandwa (hekta): mashamba | | | Majani Mabichi yaliyopatikana (tani) | | | | | | Bei kwa mkulima (Shs/Kilo) | Mauzo[2] Nchini (tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kumi Kati: mashamba | | | Kikanda: mashamba | | | | |
| | Makubwa | Madogo | Jumla | Makubwa | Madogo | Jumla | Kaskazini | Kusini | Jumla | | |
| 1976/77 | 9023 | 9217 | 18240 | 59300 | 13679 | 72979 | 27841 | 45138 | 72979 | 0.90 | 2994 |
| 1977/78 | 9214 | 9334 | 18548 | 65933 | 22598 | 88531 | 32784 | 55747 | 88531 | 1.50 | 4168 |
| 1978/79 | 9268 | 9280 | 18548 | 60062 | 24230 | 84292 | 27177 | 57115 | 842292 | 1.50 | 3735 |
| 1979/80 | 9268 | 9289 | 18557 | 61294 | 21780 | 83074 | 27249 | 55825 | 83074 | 1.50 | 4376 |
| 1980/81 | 9268 | 9289 | 18557 | 59603 | 18800 | 78403 | 25287 | 53136 | 78403 | 1.50 | 5487 |
| 1981/82 | 9268 | 9289 | 18557 | 59603 | 18800 | 784 03 | 25267 | 53136 | 78403 | 1.50 | 5487 |
| 1982/83 | 9288 | 9365 | 18633 | 56023 | 18540 | 74563 | 22622 | 51941 | 74563 | 1.50 | 6735 |
| 1983/84 | 9699 | 9177 | 18876 | 65309 | 18931 | 84240 | 22869 | 61371 | 84240 | 2.80 | 3763 |
| 1984/85 | 9699 | 9177 | 18876 | 51443 | 21493 | 72936 | 18346 | 54590 | 72936 | 2.80 | 4286 |
| 1985/86 | 9699 | 9177 | 18876 | 55680 | 21550 | 77230 | 22369 | 54861 | 77230 | 4.10 | 4714 |
| 1986/87 | 9699 | 9177 | 18876 | 52271 | 19201 | 71472 | 17564 | 53908 | 71472 | 4.90 | 6346 |
| 1987/88 | 9699 | 9177 | 18876 | 46752 | 17942 | 64694 | 12333 | 52361 | 64694 | 7.60 | 4556 |
| 1988/89 | 9699 | 9177 | 18876 | 45771 | 17851 | 63822 | 12749 | 50883 | 63832 | 9.90 | 4280 |
| 1989/90 | 9699 | 9177 | 18876 | 52194 | 18874 | 71068 | 18099 | 52969 | 71088 | 134.0 | 3559 |
| 1990/91 | 9699 | 9177 | 18876 | 70442 | 22434 | 92876 | 23531 | 69345 | 92876 | 17.00 | 3491 |
| 1991/92 | 9699 | 9177 | 18876 | 62994 | 20229 | 83223 | 19298 | 63927 | 83223 | 28.00 | 2750 |
| 1992/93 | 9699 | 9197 | 18896 | 80896 | 19934 | 100830 | 32218 | 68412 | 100630 | 45.00 | 3278 |
| 1993/94 | 10029 | 9197 | 19226 | 81159 | 21231 | 102390 | 32148 | 70242 | 102390 | 45.00 | 11124 |
| 1994/95 | 10149 | 9197 | 19346 | 93608 | 22641 | 116249 | 36825 | 79424 | 116249 | 50.00 | .. |
| 1995/96 | 10652 | 9332 | 19984 | 79968 | 13803 | 93771 | 25935 | 67836 | 93771 | 55.00 | 2350 |
| 1996/97 | 11113 | 9451 | 20564 | 83126 | 7803 | 90929 | 21992 | 68937 | 93771 | 55.00 | .. |
| 1997/98 | 11416 | 9451 | 20867 | 113448 | 7100 | 120548 | 30137 | 90411 | 120548 | 55.00 | .. |
| 1998/99 | 11416 | 9451 | 20867 | 98800 | 7000 | 105800 | 26450 | 79350 | 150800 | 55.00 | .. |
| 1999/2000 | .. | .. | .. | 99848 | 6092 | 105940 | 24439 | 81502 | 105941 | 55.00 | .. |
| 2000/2001 | 10811 | 10364 | 21175 | 109007 | 9728 | 118735 | 29419 | 89318 | 118735 | 65.00 | 2386 |
| 2001/2002 | 10811 | 10364 | 21175 | 97297 | 13999 | 111296 | 22794 | 88502 | 111296 | 80.00 | 2683 |
| 2002/2003 | 11097 | 9762 | 20899 | 100677 | 31718 | 132395 | 28679 | 103716 | 132395 | 85.00 | 3158 |
| 2003/2004 | 11485 | 10801 | 22286 | 95986 | 31993 | 127979 | 26384 | 101595 | 127979 | 88.00 | 3225 |
| 2004/2005 | 11271 | 11442 | 22713 | 94172 | 39246 | 133418 | 20849 | 112769 | 133418 | 86.00 | 4004 |
| 2005/2006 | 11310 | 10977 | 22287 | 91337 | 31881 | 123218 | 29046 | 94172 | 123218 | 93.00 | 3881 |
| 2006/2007 | 11271 | 11956 | 23227 | 109632 | 49024 | 158656 | 39673 | 118983 | 158656 | 100.00 | 4737 |
| 2007/08 | 11272 | 11449 | 22722 | 97310 | 51160 | 148470 | 33458 | 115015 | 148471 | 111.00 | 4263 |
| 2008/09 | 11271 | 11449 | 22721.55 | 100644 | 41167 | 141811 | 31677 | 110134 | 141811 | 118 | 4464 |
| 2009/10 | 11272.1 | 11449.45 | 22721.55 | 106021 | 44716 | 150737 | 33309 | 117428 | 150737 | 124 | 5084 |
| Badiliko (%) 2008/09-2009/10 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.05 | 0.09 | 0.06 | 0.05 | 0.07 | 0.08 | 0.05 | 0.14 |
| Ongezeko (%) 76/77-2009/10 | 0.25 | 0.24 | 0.25 | 0.79 | 2.27 | 1.07 | 0.20 | 1.60 | 1.07 | 138.78 | 0.70 |

Chanzo: Bodi ya Chai Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

.. Takwimu hazikupatikana

## KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 38

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (Tani) | | | | Bei (Sh./kilo) | | | Mauzo nchini+ | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ARABICA | | ROBUSTA | JUMLA | ARABICA | | ROBUSTA | KIASI | THAMANI |
| | Laini | Ngumu | | | Laini | Ngumu | Maganda | (Tani) | (shs'000) |
| 1976/77 | 35263 | 2424 | 10995 | 48682 | 15.00 | 11.00 | 8.90 | 1625 | 95 |
| 1977/78 | 38222 | 2851 | 12023 | 53096 | 10.89 | 17.50 | 5.27 | 758 | 63 |
| 1978/79 | 33853 | 2551 | 12946 | 49350 | 9.07 | 14.16 | 4.64 | 587 | 82 |
| 1979/80 | 30850 | 2968 | 14216 | 48034 | 11.42 | 13.32 | 5.55 | 336 | 56 |
| 1980/81 | 52301 | 3223 | 11237 | 66761 | 12.36 | 10.50 | 4.50 | 687 | 70 |
| 1981/82 | 36090 | 3753 | 10947 | 50790 | 14.90 | 10.50 | 5.93 | 997 | 130 |
| 1982/83 | 38852 | 2216 | 12728 | 53796 | 15.17 | 10.55 | 10.55 | 1020 | 20 |
| 1983/84 | 36436 | 1729 | 11509 | 49674 | 22.87 | 16.35 | 16.35 | 1730 | 25 |
| 1984/85 | 36270 | 1974 | 10836 | 49080 | 29.68 | 15.07 | 15.07 | 895 | 36 |
| 1985/86 | 41042 | 2820 | 11285 | 55147 | 45.80 | 20.90 | 20.90 | 1408 | 94 |
| 1986/87 | 39060 | 2702 | 16975 | 58737 | 50.75 | 29.00 | 29.00 | 1146 | 966 |
| 1987/88 | 32804 | 2514 | 10389 | 45707 | 66.00 | 37.70 | 37.00 | 1122 | 1206 |
| 1988/89 | 41230 | 2280 | 11620 | 55130 | 90.00 | 51.00 | 51.00 | 1220 | 2293 |
| 1989/90 | 34945 | 1702 | 16427 | 53074 | 165.00 | 66.50 | 55.00 | 783 | 1449 |
| 1990/91 | 31304 | 1416 | 11403 | 44123 | 165.00 | 66.50 | 60.50 | 783 | 1510 |
| 1991/92 | 37065 | 1926 | 8996 | 47987 | 230.00 | 100.00 | 70.00 | 1140 | 2558 |
| 1992/93 | 36901 | 2128 | 12217 | 51246 | 316.00 | 123.00 | 100.00 | 765 | 1282 |
| 1993/94 | 26361 | 2448 | 7577 | 36386 | 923.00 | 904.00 | 700.30 | .. | |
| 1994/95 | 27137 | 1542 | 7157 | 35836 | 1965.00 | 1481.10 | 1453.60 | .. | |
| 1995/96 | 35142 | 2096 | 9710 | 46948 | 1229.30 | 1301.60 | 1169.00 | .. | |
| 1996/97 | 32933 | 1279 | 9279 | 43491 | .. | .. | .. | .. | |
| 1997/98 | 19789 | 1894 | 9165 | 30848 | .. | .. | .. | .. | |
| 1998/99 | 23605 | 2590 | 13523 | 39718 | 1936.00 | 1064.00 | 1040.00 | .. | |
| 1999/00 | 18171 | 3593 | 1078 | 32842 | 1486.60 | 1894.80 | 476.47 | .. | |
| 2000/01 | 37176 | 3805 | 17007 | 57988 | .. | .. | .. | .. | |
| 2001/02 | 38000 | 3500 | 12000 | 53500 | .. | .. | .. | .. | |
| 2002/03 | 37294 | 4766 | 34368 | 76428 | .. | .. | .. | .. | |
| 2003/04 | 20716 | 1850 | 16138 | 38704 | 1800.00 | 1200.00 | 600.00 | 38704 | 465 |
| 2004/05 | 23870 | 888 | 9133 | 33891 | 2593.50 | 1976.00 | 1235.00 | 33891 | 625 |
| 2005/06 | 24116 | 1362 | 8856 | 34334 | 1200.00 | 420.00 | 270.00 | 33300 | 793042 |
| 2006/07 | 33345 | 2417 | 19076 | 54838 | 2840.00 | 1796.00 | 1616.00 | 548 | 12986 |
| 2007/08 | 26330 | 1588 | 15606 | 43524 | 2995.00 | 1875.00 | 1734.00 | 43523 | 89 |
| 2008/09 | 37207 | 1727 | 29643 | 68577 | 2887 | 2172 | 1836 | 68577 | 1656155 |
| 2009/10 | 22217 | 915 | 11457 | 34599 | 3988 | 2475 | 1563 | 34599 | 1087410 |
| Badiliko (%) 2008/09-09/10 | -0.40 | -0.47 | 0.61 | 0.-5 | 0.38 | 0.14 | -0.15 | -0.50 | -0 |
| Ongezeko (%) 1976/77-09/10 | -0.4 | -0.6 | 0.0 | -0.3 | 264.9 | 224.0 | 174.6 | 20.3 | 1142 |

Chanzo: Bodi ya Kahawa Tanzania

\+ Kahawa iliyosafishwa

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Ni ya muda

.. Takwimu hazikupatikana

ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

Jedwali Na. 39

| Msimu[1] | Eneo (Hekta) | | | Katani Iliyopatikana | | Mauzo nchini* | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uliokomaa | Usiokomaa | Jumla | Kiasi (tani) | Bei kwa Mkulima (shs/tani) | Kiasi (tani) | Thamani (Sh. milioni) |
| 1977/78 | 11626 | 38626 | 150252 | 91873 | 2474 | 25104 | 57.7 |
| 1978/79 | 107371 | 32589 | 139960 | 81384 | 2549 | 32023 | 95.8 |
| 1979/80 | 106866 | 26024 | 132890 | 85978 | 3135 | 35730 | 125.4 |
| 1980/81 | 99771 | 21642 | 121413 | 73753 | 3749 | 19687 | 68.0 |
| 1981/82 | 82257 | 17998 | 100255 | 60635 | 3784 | 30851 | 117.4 |
| 1982/83 | 85314 | 15720 | 101034 | 46187 | 4797 | 22384 | 94.9 |
| 1983/84 | 69799 | 13121 | 82920 | 38255 | 6410 | 12573 | 70.0 |
| 1984/85 | 62307 | 11796 | 74103 | 32247 | 7213 | 13075 | 88.3 |
| 1985/86 | 67606 | 13606 | 81212 | 30151 | 16099 | 19842 | 200.0 |
| 1986/87 | 67606 | 13606 | 81212 | 33170 | 19472 | 16477 | 407.0 |
| 1987/88 | 32932 | 20866 | 53798 | 33268 | 38750 | 20635 | 862.0 |
| 1988/89 | 47651 | 30584 | 78235 | 32265 | 64604 | 22661 | 1464.0 |
| 1989/90 | 48826 | 33780 | 82606 | 33743 | 94003 | 25563 | 2403.0 |
| 1990/91 | 49374 | 36240 | 85614 | 36001 | 89633 | 10398 | 932.0 |
| 1991/92 | 49374 | 36240 | 85614 | 24309 | 89203 | 17644 | 1582.2 |
| 1992/93 | 49374 | 36240 | 85614 | 21221 | 107079 | 18067 | 1517.8 |
| 1993/94 | 54485 | 24608 | 79093 | 29002 | 163540 | 17694 | 4031.0 |
| 1994/95 | 52953 | 25757 | 78710 | 24716 | 216028 | 18206 | 2829.0 |
| 1995/96 | 52018 | 27153 | 79171 | 28902 | 370807 | 18719 | 2549.0 |
| 1996/97 | 50459 | 28507 | 78967 | 25022 | .. | 18606 | 3374.0 |
| 1997/98 | 48745 | 29997 | 78742 | 22180 | .. | 18819 | .. |
| 1998/99 | 151669 | 33997 | 185666 | 23229 | .. | 6712 | 2146.0 |
| 1999/00 | 34645 | 7942 | 42587 | 41084 | .. | 16033 | 5617.8 |
| 2000/01 | 34645 | 11473 | 46118 | 23542 | 368077 | 7569 | 2786.0 |
| 2001/02 | 34645 | 11473 | 46118 | 23641 | 337732 | 4947 | 1671.0 |
| 2002/03 | 39462 | 10611 | 50073 | 23280 | 450000 | 6300 | 2835.0 |
| 2003/04 | 29493 | 12204 | 41697 | 26768 | 540000 | 6370 | 4027.0 |
| 2004/05 | 45079 | 14500 | 59579 | 27794 | 617342 | 8218 | 5070.0 |
| 2005/06 | 26384 | 13264 | 39649 | 30934 | 810000 | 10787 | 8813.0 |
| 2006/07 | 28273 | 13608 | 41882 | 33327 | 975000 | 11010 | 10152.0 |
| 2007/08 | 28577 | 15622 | 44199 | 34057 | 1000000 | 16997 | 15800.0 |
| 2008/09 | 35751 | 18023 | 53774 | 25996 | 1000000 | 11496 | 10100 |
| 2009/10 | 30556 | 11849 | 42405 | 24092 | 1200000 | 12761 | 10375 |
| Badiliko (%) | | | | | | | |
| 2008/09-09/10 | -14.5% | 34.3% | -21.1% | -7.3% | 20.0% | 11.0% | 2.7% |
| Ongezeko (%) | | | | | | | |
| 1977/78-09/10 | 162.82% | 69.32% | -71.78% | -73.78% | 48404.45% | 49.17% | 17880.94% |

Chanzo: Bodi ya Katani

* Katani aina ya Line fibre. Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

.. Takwimu hazikupatikana

## TUMBAKU ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 40

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (tani) | | | | Bei (shs/kg) | | | Mauzo Nchini+ | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mvuke | Moshi | Hewa | Jumla | Mvuke | Moshi | Hewa | Kiasi (tani) | | Thamani (shs mil.) | |
| | | | | | | | | Mvuke | Moshi | Mvuke | Moshi |
| 1977/78 | 14451 | 2653 | 33 | 17137 | 7.40 | 5.20 | 4.80 | 3694 | 433 | 56.10 | 6.1 |
| 1978/79 | 14403 | 2654 | 30 | 17087 | 7.40 | 5.20 | 4.80 | 3254 | 1212 | 54.90 | 13.4 |
| 1979/80 | 13005 | 4195 | 34 | 17234 | 8.80 | 6.25 | 6.50 | 2829 | 1197 | 51.80 | 19.3 |
| 1980/81 | 12972 | 3670 | 33 | 16675 | 10.50 | 6.25 | 6.50 | 2981 | 958 | 57.70 | 4.3 |
| 1981/82 | 12164 | 4060 | 40 | 16264 | 12.60 | 7.70 | 6.80 | 3515 | 685 | 61.60 | 10.8 |
| 1982/83 | 9576 | 3987 | 52 | 13615 | 18.00 | 11.50 | 10.00 | 4048 | 462 | 99.00 | 31.1 |
| 1983/84 | 9009 | 1963 | 40 | 11012 | 18.00 | 11.50 | 10.00 | 3571 | 583 | 114.50 | 19.3 |
| 1984/85 | 10554 | 2726 | 36 | 13316 | 25.20 | 16.10 | 14.00 | 4417 | 333 | 179.80 | 13.2 |
| 1985/86 | 12113 | 415 | 21 | 12549 | 37.90 | 23.30 | 20.30 | 2302 | 281 | 126.30 | 13.3 |
| 1986/87 | 15009 | 1422 | 14 | 16445 | 49.25 | 30.30 | 26.40 | 4040 | 256 | 452.40 | 32.5 |
| 1987/88 | 11111 | 1807 | 8 | 12921 | 63.00 | 39.00 | 34.00 | 4089 | 259 | 651.90 | 45.1 |
| 1988/89 | 10187 | 1355 | 12 | 11554 | 75.60 | 48.75 | 37.32 | 4383 | 537 | 1074.10 | 88.2 |
| 1989/90 | 8461 | 3347 | 5 | 11808 | 93.04 | 76.49 | 40.25 | 8027 | 1057 | 2554.50 | 392.0 |
| 1990/91 | 10718 | 5733 | 8 | 16459 | 117.00 | 91.00 | 61.00 | 3645 | 531 | 4319.40 | 301.3 |
| 1991/92 | 18754 | 4566 | 2 | 23322 | 264.61 | 157.86 | 106.54 | 5364 | 172 | 7457.90 | 114.4 |
| 1992/93 | 18756 | 4566 | 2 | 23324 | 313.95 | 221.28 | 234.20 | 5372 | 209 | 7463.40 | 255.6 |
| 1993/94 | 21838 | 3953 | 6 | 25797 | 343.97 | 253.00 | 286.00 | 3164 | 285 | 4540.60 | 1120.0 |
| 1994/95 | 18269 | 4362 | 19 | 22650 | 364.58 | 353.30 | 373.22 | 18260 | 4360 | 10309.00 | 1984.0 |
| 1995/96 | 23415 | 5163 | - | 28598 | 561.00 | 455.00 | - | 1319 | 183 | 1785.00 | 1331.0 |
| 1996/97 | 27101 | 8279 | - | 35380 | 632.00 | 551.00 | - | 2914 | 86 | 1236.00 | 1332 |
| 1997/98 | 42041 | 9054 | - | 51095 | 714.00 | 477.00 | - | 2647 | 117 | 1890.00 | 1320 |
| 1998/99 | 32041 | 5482 | - | 37957 | 530.00 | 454.00 | - | 979 | 68 | 2077.00 | 2439 |
| 1999/00 | 18232 | 6202 | - | 24434 | 603.00 | 566.00 | - | - | - | - | - |
| 2000/01 | 18231 | 6578 | - | 24809 | 543.00 | 556.00 | - | 2176 | 3392 | 5649.00 | - |
| 2001/02 | 25905 | 1799 | - | 27704 | 519.00 | 428.00 | - | 1595 | 348 | 4996.00 | - |
| 2002/03 | 23074 | 4798 | - | 27872 | 563.00 | 547.00 | - | 2325 | 45 | 5940.00 | - |
| 2003/04 | 30124 | 3423 | - | 43547 | 725.00 | 680.00 | - | 2245 | 138 | 6862.00 | - |
| 2004/05 | 41394 | 5983 | 74 | 47451 | 918.11 | 781.83 | 729.23 | 3144 | 252 | 6881.00 | 427 |
| 2005/06 | 50494 | 5228 | 741 | 56464 | 983.00 | 735.00 | 635.00 | 3486 | 168 | 9335.00 | 392 |
| 2006/07 | 49576 | 1038 | 170 | 50784 | 1264.00 | 881.00 | 980.00 | 3685 | 0 | 14302.00 | 0 |
| 2007/08 | 52597 | 2474 | 286 | 55357 | 1144.000 | 849.000 | 957.000 | 4067 | 231 | 15392 | 1 |
| 2008/09 | 56,663 | 3641 | 437 | 60,741 | 2,741 | 1,659 | 1,698 | 5,544 | 0 | 26,167 | 0 |
| 2009/10 | 88,808 | 4901 | 497 | 94,202 | 2,946 | 1,691 | 1,773 | 2,210 | 148 | 9,699 | 593 |
| Badiliko (%) 08/09 - 09/10 | 0.57 | 0.35 | 0.14 | 0.56 | 0.07 | 0.02 | 0.04 | -0.60 | - | -0.63 | - |
| Ongezeko (%) 77/78-09/10 | 5.15 | 0.85 | 14.06 | 4.50 | 397.11 | 324.19 | 368.38 | -0.40 | -0.66 | 171.89 | 95.7 |

Chanzo: Bodi ya Tumbaku Tanzania

\+ Mauzo ya Tumbaku Moshi ni pamoja na Tumbaku Hewa

1 Msimu ni kati ya Aprili na Machi

\- Takwimu hazikupatikana

## MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI

Jedwali Na. 41

| Msimu[1] | Maua yaliyonunuliwa (tani) | | | | Mauzo Nchini: Kiasi (tani) | | | Mauzo Nchini: Thamani (Sh.'000) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kaskazini | Kusini | Jumla | Bei[2] (Sh./kg) | Ulomvu (Crude Extract) | Poda | Dawa (Dry Mack) | Ulomvu (Crude Extract) | Poda | Dawa (Dry Mack) |
| 1977/78 | 173 | 2379 | 2552 | 4.00 | 1.4 | 89.0 | 1609.0 | 332.00 | 880.00 | 555.00 |
| 1978/79 | 50 | 1550 | 1600 | 4.00 | 1.1 | 95.0 | 270.0 | 338.00 | 1298.00 | 224.00 |
| 1979/80 | 25 | 1596 | 1624 | 6.00 | 0.7 | 156.0 | 216.0 | 322.00 | 2829.00 | 550.00 |
| 1980/81 | 59 | 1943 | 2002 | 7.50 | 1.7 | 224.0 | 303.0 | 184.00 | 4870.00 | 846.00 |
| 1981/82 | 70 | 1817 | 1887 | 10.00 | 2.1 | 180.0 | 254.0 | 1280.00 | 4596.00 | 988.00 |
| 1982/83 | 32 | 1569 | 1601 | 10.00 | 0.7 | 175.0 | 241.0 | 500.00 | 4700.00 | 1330.00 |
| 1983/84 | 19 | 1419 | 1438 | 14.00 | 1.0 | 223.0 | 175.0 | 764.00 | 5936.00 | 1329.00 |
| 1984/85 | 8 | 1534 | 1542 | 19.50 | 2.1 | 151.0 | 373.0 | 3563.00 | 7100.00 | 1585.00 |
| 1985/86 | 12 | 1340 | 1352 | 21.10 | 0.5 | 215.0 | 207.0 | 978.00 | 12900.00 | 1419.00 |
| 1986/87 | 12 | 1219 | 1231 | 29.50 | 0.3 | 183.0 | 358.0 | 1092 | 17535.00 | 3663.00 |
| 1987/88 | 6 | 1406 | 1412 | 35.40 | 1.0 | 140.0 | 321.0 | 3900.00 | 16600.00 | 4100.00 |
| 1988/89 | 8 | 1305 | 1313 | 47.80 | 0.6 | 106.0 | 239.0 | 3021.00 | 15389.00 | 5436.00 |
| 1989/90 | 8 | 1582 | 1590 | 60.00 | 0.8 | 139.0 | 253.0 | 6681.00 | 22907.00 | 1636.00 |
| 1990/91 | 16 | 1656 | 1672 | 120.00 | 0.8 | 59.0 | 253.0 | 11654.00 | 26120.00 | 2315.00 |
| 1991/92 | 43 | 2425 | 2468 | 230.00 | 0.3 | 38.0 | 59.0 | 18390.00 | 19040.00 | 672.00 |
| 1992/93 | 60 | 2034 | 2004 | 230.00 | 1.0 | 70.0 | - | 26500.000 | 39900.00 | - |
| 1993/94 | 10 | 450 | 460 | 250.00 | 0.0 | 40.0 | - | 17500.00 | 22800.00 | - |
| 1994/95 | 10 | 450 | 480 | 260.00 | 0.0 | 284.0 | - | 2112.00 | 16180.00 | - |
| 1995/96 | 6 | 430 | 438 | 300.00 | 0.0 | - | - | - | - | - |
| 1996/97 | 6 | 262 | 262 | 300.00 | 0.0 | - | - | - | - | - |
| 1997/98 | 6 | 430 | 430 | 300.00 | 5.0 | - | - | - | - | - |
| 1998/99 | - | 500 | 500 | 320.00 | 5.0 | - | - | - | - | - |
| 1999/00 | | 571 | 571 | 320.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2000/01 | 3 | 1463 | 1466 | 400.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2001/02 | 36 | 1899 | 1735 | 420.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2002/03* | 111 | 979 | 1090 | 380.00 | 2 | 90 | - | 106920.00 | 99891.00 | - |
| 2003/04 | 85 | 751 | 842 | 360.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2004/05 | 90 | 910 | 1000 | 360.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2005/06 | - | 2800 | 2800 | 360.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2006/07 | - | 1600 | 1600 | 700.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2007/08 | - | 1470 | 1470 | 1050.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2008/09 | 0 | 1600 | 1600 | 1500.00 | 36.4 | 105 | 624 | 0 | 0 | 0 |
| 2009/10 | 0 | 1,780 | 1,780 | 1500.00 | 57.0 | 69.0 | 1035.0 | 37361.0 | 1473.0 | 248.0 |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | | |
| 2008/09-2009/10 | | 0.1 | 0.1 | 0.0 | 0.6 | -0.3 | 0.7 | | | |
| Ongezeko (%) | | | | | | | | | | |
| 77/78-2009/10 | | -0.3 | -0.3 | 374.0 | 39.7 | -0.2 | -0.4 | 111.5 | 0.7 | -0.6 |

Chanzo: Bodi ya Pareto Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Bei ni kwa maua ya daraja la tano

\- Takwimu hazikupatikana

* Takwimu hizi hadi December 30 2002, Msimu bado unaendelea

## KOROSHO ZILIZONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 42

| Msimu[1] | Zilizonunuliwa (Tani) | | | Bei (shs/kilo) | | Mauzo Nchini | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Gredi ya Juu | Gredi ya Chini | Jumla | Gredi ya Juu | Gredi ya Chini | Kiasi (Kg) | Thamani (sh '000) |
| 1977/78 | 54238 | 14245 | 68483 | 1.15 | 0.95 | 20083 | 38760 |
| 1978/79 | 44190 | 12878 | 57068 | 1.70 | 1.40 | 24620 | 69798 |
| 1979/80 | 38102 | 3314 | 41416 | 1.80 | 1.50 | 22044 | 62495 |
| 1980/81 | 47792 | 8766 | 56558 | 3.00 | 2.00 | 36205 | 159121 |
| 1981/82 | 41221 | 3110 | 44331 | 5.00 | 3.50 | - | - |
| 1982/83 | 30721 | 2245 | 32966 | 5.00 | 3.50 | - | - |
| 1983/84 | 48177 | 2129 | 48306 | 7.00 | 4.90 | - | - |
| 1984/85 | 31842 | 690 | 32532 | 9.80 | 6.90 | - | - |
| 1985/86 | 16066 | 2835 | 18901 | 11.75 | 8.30 | - | - |
| 1986/87 | 15324 | 1224 | 16548 | 18.20 | 12.85 | - | - |
| 1987/88 | 23274 | 1013 | 24287 | 30.00 | 20.00 | 134082 | 142080 |
| 1988/89 | 18602 | 873 | 19275 | 40.00 | 27.00 | 275016 | 224440 |
| 1989/90 | 16829 | 230 | 17059 | 84.00 | 56.00 | 152752 | 497970 |
| 1990/91 | 27426 | 1444 | 28870 | 110.00 | 73.00 | 161703 | 887750 |
| 1991/92 | 41238 | 6037 | 41238 | 137.00 | 89.00 | 151804 | 654517 |
| 1992/93 | 39323 | 6887 | 39323 | 160.00 | 100.00 | - | - |
| 1993/94 | 46603 | 4789 | 46603 | 200.00 | 185.00 | - | - |
| 1994/95 | 63403 | - | 63403 | 330.00 | - | - | - |
| 1995/96 | 81729 | - | 81729 | 380.00 | - | - | - |
| 1996/97 | 63033 | - | 63033 | 300.00 | - | - | - |
| 1997/98 | 99915 | - | 99915 | 330.00 | - | - | - |
| 1998/99 | 106442 | - | 106442 | 460.00 | - | - | - |
| 1999/00 | 121207 | - | 121207 | 600.00 | - | 5071 | 3043 |
| 2000/01 | 122283 | - | 122283 | 250.00 | - | 934 | 233 |
| 2001/02 | 64886 | 14394 | 79280 | 300.00 | 180 | 2928 | 878 |
| 2002/03 | 79300 | 15700 | 95000 | 360.00 | 290 | 5630 | 2122 |
| 2003/04 | 65000 | 15000 | 80000 | 462.00 | 370 | 6061000 | 2521376 |
| 2004/05 | 59425 | 11575 | 71000 | 750.00 | 600 | 7013017 | 4733786 |
| 2005/06 | 81976 | 15470 | 77446 | 600.00 | 480 | 10738 | 6354240 |
| 2006/07 | 82154 | 8587 | 90741 | 600.00 | 480 | 22299 | 13001000 |
| 2007/08 | 89,639 | 8,633 | 98,273 | 610.00 | 488 | 98273 | 59335652 |
| 2008/09 | 48,633 | - | 48,633 | 700.00 | 560 | 48633410 | 34043387 |
| 2009/10 | 118,825 | 355 | 119,180 | 1700.00 | 1200 | 119179718 | 202.6 |
| Badiliko (%) | | | | | | | |
| 2008/09-2009/10 | 1.44 | | 1.45 | 1.43 | 1.14 | 1.45 | -1.00 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | |
| 77/78-09/10 | 1.19 | -0.98 | 0.74 | 1477.26 | 1262.16 | 5933.38 | -0.99 |

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Korosho

1 Msimu ni kati ya Oktoba mpaka Septemba

\- Takwimu hazikupatikana

## MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA

Jedwali Na. 43 (Tani)

| Mazao | 2002/03 | 2003/04 | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | Badiliko % 08/09 - 09/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kalani | 23,280 | 26,758 | 27,794 | 30,934 | 33,327 | 34,057 | 25,480 | 24,092 | -5.4% |
| Kahawa | 76,428 | 38,704 | 33,891 | 34,334 | 54,838 | 43,524 | 68,577 | 34,599 | 49.5% |
| Pamba[1] | 188,689 | 139,969 | 341,589 | 376,591 | 130,585 | 200,662 | 123,582 | 54,851 | 55.6% |
| Tumbaku | 27,872 | 43,547 | 47,451 | 56,464 | 50,784 | 55,357 | 60,741 | 94,202 | 55.1% |
| Pareto | 709 | 842 | 1,000 | 2,800 | 1,600 | 1,470 | 1,600 | 1,780 | 11.3% |
| Chai[2] | 132,395 | 127,979 | 133,418 | 123,218 | 158,656 | 148,471 | 141,811 | 150,737 | 6.3% |
| Korosho | 95,000 | 80,000 | 71,000 | 77,446 | 90,741 | 98,273 | 48,633 | 119,180 | 145.1% |
| Miwa | 1,813 | 2,342 | 2,346 | 2,501 | 2,041 | 2,766 | 2,749 | 2,569 | 6.5% |

Chanzo: : Bodi zinazohusika

1 Yenye mbegu

2 Majani mabichi

## SURA YA 12

## MALIASILI NA UTALII

**Kiwaugo cha ukuaji**

250. Mwaka 2010, kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za kiuchumi za misitu na uwindaji kilikuwa asilimia 4.1, ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2009. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.4, ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2009.

**Misitu na Nyuki**

251. Mwaka 2010, sekta ndogo ya misitu na nyuki ilikusanya shilingi 46.6 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 25.2 bilioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 85.1. Ongezeko hili lilitokana na mauzo makubwa yaliyofanyika katika shamba la miti la Sao Hill, kupungua kwa uagizaji wa mbao toka nchi jirani, mauzo ya magogo ya Mitiki kwa mnada katika mashamba ya miti ya Mtibwa, kuimarika kwa doria kwenye maeneo ya uvunaji, usafirishaji na masoko, kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya misitu hapa nchini pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wafanyabiashara wa mazao ya misitu kuhusu taratibu na kanuni za kufanya biashara hiyo.

252. Aidha, mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi yalipungua kutoka dola za kimarekani 61,399.86 mwaka 2009, hadi dola za kimarekani 10,752.62 mwaka 2010. Kushuka kwa mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi kulitokana na makampuni mengi kuacha au kupunguza kuuza mbao nje ya nchi kwa kuwa mahitaji ya wateja wa nje ni mbao za kuanzia inchi 6 wakati Sheria ya Misitu inazuia uuzaji wa mbao nje ya nchi zinazozidi unene wa inchi 4. Vilevile, kusisitizwa kwa uchakataji wa magogo ndani ya nchi pia kulichangia kuzuia uuzaji wa mazao ya misitu nje ya nchi.

253. Mwaka 2010, Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki iliendelea kutoa mafunzo ya misitu na ufugaji nyuki katika vyuo vyake vitatu vya Ohnotonyi-Arusha, Chuo cha Viwanda vya Misitu–Moshi na Chuo cha Ufugaji Nyuki-Tabora. Mafunzo haya ni jitihada za Serikali za kuhakikisha wataalamu wa kutosha wa

uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na ufugaji nyuki wanapatikana katika soko la ajira.

254. Mwaka 2010, Serikali iliendelea na mpango wa kuhifadhi misitu ya mikoko nchini ambapo jumla ya hekta 238 zilipandwa mikoko katika Delta ya Mto Rufiji. Kati ya hizo, hekta 76 zilipandwa kupitia mpango wa kuchunguza athari za mabadiliko ya tabianchi chini ya mradi wa WWF na hekta 162 zimepandwa kwa fedha kutoka mradi wa MACEMP. Aidha, Wilaya 63 ziliwezeshwa kutekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwenye vijiji 2,445 vyenye hekta 4,328,700 ikilinganishwa na vijiji 2,328 vyenye ukubwa wa hekta 4,122,500 mwaka 2009. Kati ya hivyo, vijiji 1,575 vinasimamia misitu ya jamii yenye jumla ya hekta 2,550,000 na vijiji 870 vinasimamia misitu kwa pamoja yenye jumla ya hekta 1,778,700.

255. Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi, Serikali iliendelea kuhamasisha shughuli za upandaji miti zinazofanyika nchini kupitia Siku ya Taifa ya Upandaji Miti. Aidha, jumla ya miche ya miti 619,363,136 ilipandwa kitaifa katika kipindi cha mwaka 2005/06 na 2009/10, ikiwa ni sawa na hekta 563,057.3 kwa kipindi cha miaka minne au wastani wa hekta 140,764.3 kwa mwaka. Kiwango cha upandaji miti nchini kinaongezeka kutokana na mwamko unaozidi kukua miongoni mwa jamii kwa kuzingatia juhudi za uhamasishaji zinazofanyika.

256. Mwaka 2010, jumla ya miche 10,278,681 ya aina mbalimbali ilikuzwa na kupandwa kwenye jumla ya hekta 7,008.12 za maeneo ya wazi na yale yaliyovunwa, ikilinganishwa na miche 7,806,652 iliyokuzwa na kupandwa katika hekta 6,805.8 za maeneo ya wazi mwaka 2009. Vilevile, katika kipindi hicho, jumla ya hekta 15,639.68 za miti zilipogolewa matawi na kupaliliwa, ikilinganishwa na hekta 7,829.8 mwaka 2009. Aidha, barabara za kuingilia mashambani zenye urefu wa kilometa 6,147.72 pamoja na mipaka na barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilometa 1,741.7 zilitengenezwa, ikilinganishwa na kilometa 2,275.5 za mipaka na barabara za kuzuia moto zilizotengenezwa mwaka 2009. Tathmini iliyofanyika mwaka 2010 katika

mashamba 15 ilionesha kuwa mashamba hayo yana miti yenye mita za ujazo 1,362.365.38.

257. Mwaka 2010, wastani wa tani 9,380 za asali zenye thamani ya shilingi. bilioni 35.17 na wastani wa tani 625 za nta zenye thamani ya shilingi bilioni 4.5 zilizalishwa. Uzalishaji huu ni sawa na asilimia 7 tu ya uwezo wa uzalishaji nchini. Mauzo ya asali nje ya nchi yalipungua kwa asilimia 11.7 toka tani 485.8 mwaka 2009 hadi kufikia tani 428.8 mwaka 2010. Hata hivyo, mapato yatokanayo na uuzaji wa asali nje yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 1.09 mwaka 2009, hadi shilingi bilioni 1.27 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 16.5.

258. Mwaka 2010, wastani wa bei ya asali katika masoko ya nje ya nchi ilikuwa kati ya Dola za Kimarekani 1,800 hadi 2,500 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa kati ya Dola 1600 hadi 1800 kwa tani mwaka 2009. Aidha, wastani wa bei ya nta mwaka 2010 uliendelea kuwa kama ilivyokuwa mwaka 2009. Wastani wa bei ya nta ulikuwa kati ya Dola za Kimarekani 4,500 na 5,200 kwa tani katika masoko ya nje. Katika soko la ndani, mkulima aliuza asali kati ya shillingi 1,500 na shillingi 2,000 kwa kilo moja na nusu. Aidha, katika soko la ndani mkulima aliuza nta kwa bei ya kati ya sh 3,800 na sh 4,000 kwa kilo moja.

259. Mwaka 2010, mauzo ya asali nje ya nchi yalipungua kwa asilimia 11.7, kufikia tani 428.8 kutoka tani 485.8 mwaka 2009. Aidha, mapato yatokanayo na mauzo ya asali nje ya nchi yalifikia shilingi 1,271.1 milioni, ikilinganishwa na shilingi 1.097.2 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 15.8. Vilevile, mauzo ya nta nje ya nchi mwaka 2010 yaliongezeka kwa asilimia 2.2 na kufikia tani 568.3, kutoka tani 556.0 mwaka 2009. Aidha, mapato yatokanayo na mauzo ya nta nje ya nchi yalifikia shilingi 3,731.9 milioni, ikilinganishwa na shilingi 3,525.2. milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia .5.9.

Jedwali Na.122: Mauzo ya Mazao ya Nyuki ( Asali na Nta) nje ya Nchi, 2006-2010

| ASALI | | | NTA | |
|---|---|---|---|---|
| MWAKA | UZITO (KG) | THAMANI (TSH) | UZITO (KGS) | THAMANI (TSH) |
| 2006 | 325,729 | 538,102,710 | 364,532 | 2,036,643,691 |
| 2007 | 156,012 | 218,348,125 | 320,660 | 1,909,188,517 |
| 2008 | 612,960 | 1,199,283,500 | 580,154 | 3,653,036,682 |
| 2009 | 485,842 | 1,097,642,183 | 556,000 | 3,525,245,806 |
| 2010 | 428,825 | 1,271,121,001 | 568,260 | 3,731,939,869 |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Misitu na Nyuki

260. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kukiwezesha kikosi cha doria za rasilimali za misitu ili kulinda rasilimali hizo dhidi ya uvunaji usio endelevu. Jumla ya shillingi 432,485,346 zilikusanywa kutokana na faini na mauzo ya mazao ya misitu yaliyokamatwa na kutaifishwa kutokana na ukiukwaji wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002. Vifaa vilivyokamatwa ni pamoja na mkaa gunia 4,899, mbao vipande 26,399, magogo vipande 1,052, nguzo 5,140, baiskeli 51 na misumeno 95 .

## Wanyamapori

261. Mwaka 2010, sekta ndogo ya wanyamapori ilikusanya jumla ya shilingi 313.99 milioni ikilinganishwa na shilingi 535.7 milioni mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 41.4. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanyamapori kwenye baadhi ya vitalu kutokana na maeneo hayo kutumika kwa shughuli za ulishaji wa mifugo, kilimo, upasuaji mbao na uchomaji mkaa. Vilevile, upungufu huo ulichangiwa na: kupungua kwa uwindaji wa kitalii, utalii wa picha na malipo ya leseni za biashara ya nyara; na ubovu wa miundombinu. Kwa upande mwingine, mapato yaliongezeka katika vyanzo vya vibali vya kusafirisha nyara nje ya nchi, vibali vya kukamata wanyamapori, hati za kumiliki nyara na ada nyinginezo. Hii ilitokana na kuongezeka kwa viwango vya ada za vyanzo hivyo na usafirishaji wa nyara katika mwaka 2010.

**Jedwali Na 12.3: Mwenendo wa Ukusanyaji Maduhuli katika Sekta ndogo ya Wanyamapori kwa Kipindi cha Mwaka 2006 hadi 2010**

| | | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uwindaji wa kitalii | USD | 12,030,510 | 14.704,370 | 19,760,812 | 18.444,881 | 14,443,417 | -21.7% |
| Utalii wa picha | USD | 790,009 | 1,332.385 | 2,387,728 | 2,706.603 | 2,576.677 | -4.8% |
| | TZS | 37,614.400 | 89,729.250 | 114,758.392 | 261,639,400 | 128,704,850 | -50.8% |
| Leseni ya Biashara ya nyara | TZS | 145,105.000 | 189.888.495 | 153,084,905 | 172,046,203 | 16,122,000 | -90.6% |
| Vibali vya kusafirisha nyara nje ya nchi | TZS | 8,295,000 | 10,457,500 | 10,206,000 | 5,651,750 | 14,705,750 | 160.2% |
| Vibali vya kukamata wanyamapori | TZS | 235,969.377 | 74,478.766 | 408.476,566 | 87,559,229 | 137,055,190 | 56.5% |
| Hati za Kumiliki nyara | TZS | 2,185,900 | 2,885,400 | 2,353,400 | 1,462,000 | 2,231,840 | 52.7% |
| Ada nyinginezo | TZS | 16,148.526 | 84,703.267 | 111,453,174 | 7,361,669 | 15.174,066 | 106.1% |
| **Jumla** | USD | 12,820,519 | 16,036,755 | 22,148,540 | 21,151,484 | 17.020,094 | -19.5% |
| | TZS | 445,318,203 | 452,142,678 | 800,332.437 | 535,720.251 | 313,993,696 | -41.4% |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Wanyamapori.

262. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kulinda rasilimali za wanyamapori dhidi ya ujangili na uvunaji usio endelevu. Katika mwaka 2010, jumla ya siku za doria 77,446 zilifanyika katika mapori ya akiba na maeneo ya wazi ikilinganishwa na siku za doria 42,544 mwaka 2009. Jumla ya kesi 766 zenye watuhumiwa 1,672 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali, ikilinganishwa na kesi 714 zenye watuhumiwa 3,052 mwaka 2009. Jumla ya kesi 286 zilimalizika kwa washtakiwa kulipa faini ya jumla ya shilingi 491.8 milioni na wengine walifungwa jela miezi 392, ikilinganishwa na kesi 426 ambazo zililipiwa faini ya shilingi 131.1 milioni mwaka 2009.

263. Katika kulinda maisha na mali za wananchi dhidi ya wanyama wakali na waharibifu, sekta ndogo ilifanya siku za doria 2,111 katika wilaya 17 mwaka

2010 ikilinganishwa na siku za doria 2,100 katika wilaya 23 ambazo ziliathirika zaidi na matukio ya uvamizi wa wanyamapori mwaka 2009. Wilaya hizo ni Manyoni, Rombo, Hai, Siha, Nanyumbu, Singida Vijijini, Bunda, Monduli, Serengeti, Biharamulo, Karagwe, Mkuranga, Iringa, Babati, Moshi Vijijini, Muleba na Kondoa. Aidha, ili kuhakikisha kunakuwepo na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, sensa ya wanyamapori ilifanyika katika maeneo ya Mkomazi, Saadani, Wami – Mbiki, Selous – Niassa Corridor, Serengeti, Natron na Longido.

264. Mwaka 2010, jumla ya kilometa 100 za barabara zilikarabatiwa katika mapori ya akiba ya Selous, Mkungunero na Kijereshi ikilinganishwa na kilometa 110 katika pori la Selous mwaka 2009, ili kuwezesha mapori ya akiba kupitika kwa ajili ya doria, uwindaji wa kitalii na utalii wa picha. Aidha, mwaka 2010, kilometa 50 za mipaka zilifyekwa katika mapori ya akiba ya Mpanga-Kipengele na Liparamba, ikilinganishwa na kilometa 101.5 zilizofyekwa katika mapori ya akiba ya Ikongoro/Gurumeti na Lukwika.

**UVUVI**

265. Mwaka 2010, shughuli za kiuchumi za uvuvi zilikua kwa asilimia 1.5, ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2009. Kiwango hiki kidogo cha ukuaji kilitokana na utumiaji wa vifaa duni vya uvuvi, uharibifu wa mazalia ya samaki na kupungua kwa mahitaji ya samaki katika soko la nje. Aidha shughuli za kiuchumi za uvuvi zilichangia asilimia 1.4 ya Pato la Taifa mwaka 2010, sawa ilivyokuwa mwaka 2009.

266. Katika mwaka 2010, jumla ya tani 347,157 za samaki zenye thamani ya wastani wa shilingi 774.5 milioni zilivunwa, ikilinganishwa na tani 335,675 zenye thamani ya shilingi 408 milioni mwaka 2009. Kati ya hizo, tani 294,474, sawa na asilimia 84.8 zilitokana na uvuvi katika maji baridi na tani 52,683, sawa na asilimia 15.2 zilitokana na uvuvi katika maji chumvi.

267. Mwaka 2010, wavuvi wadogo 163,601 walijishughulisha na uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi 50,001 ikilinganishwa na wavuvi 174,540 na vyombo 56,164 mwaka 2009. Mwaka 2010, mauzo ya mazao ya uvuvi nje yalikuwa kilo 39.2 milioni na samaki wa mapambo 37,924 ambazo zilikuwa na thamani ya shilingi 263.3 bilioni ikilinganishwa na kilo 41.1 milioni za mazao ya uvuvi na samaki wa mapambo 53,188 wenye thamani ya shilingi 207.4 bilioni mwaka 2009. Mapato yatokanayo na ushuru wa mauzo hayo yaliongezeka kutoka shilingi 6,047.5 milioni mwaka 2009, hadi shilingi 6,490.2 milioni mwaka 2010.

268. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kuimarisha vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi. Katika kipindi hicho, boti 12 zilinunuliwa na kugawanywa katika vituo vya doria vya Kipili, Kanyigo, Kasumulo, Sota, Mafia, na Kilwa ambavyo vilipatiwa boti moja kwa kila kituo na Dar es Salaam, Tanga, na Mtwara vilipatiwa boti mbili kwa kila kituo. Vilevile, injini mbili zilinunuliwa kwa ajili ya vituo vya Kigoma na Bukoba na boti nyepesi (rubber dinghies) nne zilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya Dar es Salaam, Mafia, Mtwara na Tanga.

269. Mwaka 2010, jumla ya siku-kazi za doria 2,882 zilifanyika katika maeneo ya masoko; viwanda vya samaki; bandarini; viwanja vya ndege; maduka ya nyavu; maghala ya samaki; vituo vya mabasi; vituo vya treni; na mizani Kibaha ili kudhibiti uvuvi haramu, ikilinganishwa na doria 9,617 zilizofanyika mwaka 2009. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa zana haramu na vifaa mbalimbali vinavyotumika kinyume cha sheria za nchi. Vifaa vilivyokamatwa ni pamoja na makokoro 22, kamba za kokoro mita 44,542, nyavu ndogo za makila 692, nyavu za utali 362, nyavu za dagaa 74, vyadarua 18, bunduki 2, nyavu za kimia 5, mikuki 6, mitungi ya gesi 29, baruti 3, detonator vipande 300, mbolea kilo 100, vioo jozi 3, mitumbwi 57, maboti 10, injini za boti 12, gari 13, baiskeli 3 na pikipiki. Vilevile, Sangara wachanga kilo 12,108, sato wachanga kilo 4,248, samaki wa kokoro kilo 5,275, dagaa kilo 4,831, majongoo bahari kilo 159, samaki wa baruti kilo 752 na Samaki wakubwa kilo 2,198 waliovuliwa kinyume cha sheria walikamatwa. Aidha, mwaka 2010 idadi ya watuhumiwa 98 walikamatwa na kesi 14 zilifunguliwa

mahakamani, ikilinganishwa na watuhumiwa 987 waliokamatwa mwaka 2009. Jumla ya shilingi 9,170,000 zilikusanywa kutokana na faini mbalimbali. Vilevile, vikundi 512 vya usimamizi wa rasilimali ya uvuvi (BMUs) vimeimarishwa, ambapo vikundi 438 viko katika Ziwa Victoria, 29 bwawa la Mtera, 20 bwawa la Nyumba ya Mungu, 11 Mto Ruhuhu, 6 Mafia na 8 Rufiji.

270. Mwaka 2010, kaguzi 2,222 zilifanyika katika viwanda 32 vinavyosindika minofu ya samaki na maghala 11 yanayohifadhi mazao ya uvuvi. Aidha, sampuli 623 za samaki, maji na udongo zilichunguzwa kwenye maabara ya taifa ya uthibiti ubora wa samaki (Nyegezi – Mwanza), Shirika la Viwango Tanzania (Dar es Salaam), Shirika la Viwango (Afrika ya Kusini) na Chemiphar (Uganda) ili kutambua uwepo wa vimelea haribifu, mabaki ya viwatilifu na madini tembo, ikilinganishwa na sampuli 975 mwaka 2009. Mwaka 2010, kilo 40,498,495 za samaki na mazao yake, na samaki wa mapambo 18,590 zilikaguliwa kabla ya kuuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na kilo 31,263,286 za samaki na mazao yake na samaki wa mapambo 51,663 mwaka 2009.

Jedwali Na. 11.9: Hali ya Uvunaji wa Samaki kwa Mwaka 2010

| Ukanda wa Wavuvi | Idadi ya wavuvi | Idadi ya vyombo | Uzito (tani) | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Ziwa Victoria | 95,303 | 26.983 | 243.564.4 | 608,910,975.0 |
| Ziwa Tanganyika | 12,574 | 7,129 | 32,003.14 | 48,004,702.50 |
| Ziwa Nyassa | 6.557 | 2.013 | 11,460.34 | 17,190,510.00 |
| Ziwa Rukwa | 1,676 | 1.032 | 4,254.09 | 6,381,135.00 |
| Bwawa la Mtera | 1.572 | 1,284 | 754 | 1,131,000.00 |
| Bwawa la Nyumba ya Mungu | 3,466 | 1,167 | 1,006.58 | 2,013,157.68 |
| Ziwa kitangiri | 457 | 224 | 76.02 | 152,040.00 |
| Ziwa Babati | 222 | 91 | 126.00 | 189,000.00 |
| Ziwa Jipe | 78 | 50 | 14.00 | 21,000.00 |
| Other Minor water | 5,375 | 2,364 | 1,215.00 | 850,500.00 |
| Marine Artisanal | 36,321 | 7,664 | 52,683.38 | 89,639,934.00 |
| **Jumla** | 163,601 | 50,001 | 347,156.9 | 774,483,954.2 |

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

## Jedwali Na. 11. 10 Uvunaji Wa Rasilimali ya Uvuvi Mwaka 2005 – 2010

| Mwaka | Maji baridi | | | Maji chumvi | | | Jumla (Maji chumvi na Baridi) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavuvi | Vyombo | Uzito (tani) | Wavuvi | Vyombo | Uzito (tani) | Wavuvi | Vyombo | Uzito (tani) |
| 2005 | 103,443 | 32,248 | 320,566.0 | 29,754 | 7,190 | 54,968.6 | 133,197 | 39,438 | 375,535 |
| 2006 | 126,790 | 44,362 | 292,518.7 | 29,754 | 7,190 | 48,590.5 | 156,544 | 51,552 | 341,109 |
| 2007 | 126,790 | 44,362 | 284,346.9 | 36,247 | 7,489 | 43498.5 | 163,037 | 51,851 | 327,845 |
| 2008 | 133,791 | 44,838 | 281,690.9 | 36,247 | 7,489 | 43,130.2 | 170,038 | 52,327 | 324,821 |
| 2009 | 135,769 | 45,234 | 288,059 | 36,321 | 7,664 | 47,616 | 172,090 | 52,898 | 335,675 |
| 2010 | 127,280 | 42,337 | 294,474 | 36,321 | 7.664 | 52,683 | 163,601 | 50,001 | 347,157 |

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

## Utalii

271. Katika mwaka 2010, idadi ya watalii kutoka nje ya nchi waliotembelea vivutio mbalimbali iliongezeka kwa asilimia 9.6, hadi watalii 782,699, kutoka watalii 714,367 mwaka 2009. Aidha, mapato yaliyotokana na utalii, yalikuwa Dola za Kimarekani 1.25 bilioni, ikilinganishwa na dola za Kimarekani 1.16 bilioni zilizopatikana mwaka 2009. Ongezeko hili lilichangiwa na juhudi za kutangaza na kuhamasisha utalii pamoja na uboreshaji wa sekta ya huduma za kitalii hususan, hoteli na miundombinu.

**Jedwali Na 12.4: Watalii waliotembelea Hifadhi za Taifa 2008 - 2010**

| Na. | Jina la hifadhi | Aina ya Wageni | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wageni kutoka Nje | Watanzania | Wageni kutoka Nje | Watanzania | Wageni kutoka Nje | Watanzania |
| | | 2008 | | 2009 | | 2010 | |
| 1 | ARUSHA | 39,778 | 43,484 | 40,268 | 9,235 | 34,308 | 30,162 |
| 2 | GOMBE | 1096 | 325 | 1,202 | 432 | 1,166 | 1,001 |
| 3 | KATAVI | 3,161 | 2250 | 1882 | 292 | 1,484 | 1,330 |
| 4 | KILIMANJARO | 155,275 | 6,954 | 41,879 | 1,183 | 50,193 | 3,545 |
| 5 | KITULO | 117 | 413 | 366 | 187 | 151 | 158 |
| 6 | LAKE MANYARA | 112,687 | 46,477 | 118,565 | 16,361 | 112,982 | 48,288 |
| 7 | MAHALE | 2,888 | 191 | 810 | 58 | 865 | 44 |
| 8 | MIKUMI | 21,038 | 17,629 | 25,282 | 10,616 | 18,936 | 22,872 |
| 9 | MKOMAZI | 433 | 552 | 647 | 263 | 566 | 572 |
| 10 | RUAHA | 21832 | 12355 | 14,125 | 3,118 | 12,623 | 8,797 |
| 11 | RUBONDO | 721 | 490 | 472 | 153 | 501 | 381 |
| 12 | SAADANI | 2,482 | 2,293 | 2,755 | 1,335 | 2,127 | 4,442 |
| 13 | SERENGETI | 225,606 | 218,375 | 202,537 | 58841 | 228,644 | 69,369 |
| 14 | TARANGIRE | 95,760 | 43,883 | 77,739 | 10,018 | 85,778 | 34,752 |
| 15 | UDZUNGWA | 2,837 | 1,731 | 3163 | 1395 | 2,945 | 2,707 |
| Jumla | | 685,711 | 397,402 | 531,692 | 113,487 | 553,269 | 228,420 |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Hifadhi za Taifa (TANAPA)

272. Mwaka 2010, Jumla ya watalii 523,646 walitembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kati yao watalii 281,513 walitoka nje ya nchi na watalii 242,133 walikuwa ni wa ndani, ikilinganishwa na jumla ya watalii 438,179 mwaka 2009 ambapo waliotoka nje walikuwa 234,767 na wa ndani 203,412.

**Jedwali Na. 12.5: Watalii waliotembelea Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro mwaka 2010**

| Mwezi | Wageni kutoka Nje | Watanzania | Jumla ya Wageni |
|---|---|---|---|
| Januari | 22,296 | 20,123 | 42,419 |
| Februari | 26,933 | 18,971 | 45,904 |
| Machi | 16,165 | 15,277 | 31,442 |
| Aprili | 9,619 | 12,669 | 22,288 |
| Mei | 11,995 | 13,952 | 25,947 |
| Juni | 19,865 | 19,301 | 39,166 |
| Julai | 38,563 | 26,469 | 65,032 |
| Agosti | 40,007 | 27,954 | 67,961 |
| Septemba | 25,804 | 23,450 | 49,254 |
| Oktoba | 26,286 | 22,217 | 48,503 |
| Novemba | 17,949 | 18,241 | 36,190 |
| Desemba | 26,031 | 23,509 | 49,540 |
| **Jumla kuu** | **281,513** | **242,133** | **523,646** |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

273. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kupitia Bodi ya Utalii Tanzania. Katika kipindi hicho, majarida mbalimbali kama vile 'Tanzania Tourism Directory', 'Accommodation Directory', gazeti la 'Tantravel', pamoja na DVD na CD', zilitolewa na Bodi

ya Utalii Tanzania kwa lengo la kutangaza vivutio. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Utalii Tanzania ilihudhuria maonesho 15 ya utalii katika nchi mbalimbali duniani. Vilevile, Serikali iliendelea kutumia fursa za maonesho mbalimbali ya ndani yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Nanenane, 'Karibu Fair', Siku ya Utalii na mashindano ya urembo katika kukuza utalii wa ndani na kupunguza utegemezi wa soko la nje.

| Arusha, Manyara | 3292 | 3325 | 15296 | 15449 | 15603 | 3230 | 3230 | 3295 | 3327 | 15195 |
| Kilimanjaro | 6902 | 6971 | 11548 | 11664 | 11780 | 6828 | 6828 | 6964 | 7033 | 11699 |
| Tanga | 8365 | 8149 | 10054 | 10151 | 10256 | 8320 | 8320 | 8487 | 8571 | 10185 |
| Morogoro | 11062 | 11193 | 8123 | 8204 | 8286 | 11062 | 11061 | 11283 | 11395 | 8229 |
| Pwani | - | | 24155 | 24396 | 24640 | - | - | - | - | 24025 |
| Dar es Salaam, Pwani*** | 27604 | 27880 | 61 | 61 | 62 | 27143 | 27414 | 27686 | 27960 | 61 |
| Lindi | 29 | 30 | 115 | 117 | 118 | 25 | 26 | 26 | 26 | 117 |
| Mtwara | 65 | 66 | 977 | 987 | 997 | 61 | 61 | 62 | 62 | 990 |
| Ruvuma | 1977 | 1996 | 9099 | 9190 | 9282 | 1962 | 1982 | 2002 | 2022 | 9218 |
| Iringa | 15073 | 15224 | 2884 | 2913 | 2942 | 15062 | 15213 | 15363 | 15516 | 2922 |
| Mbeya | 2810 | 2838 | 238 | 241 | 243 | 2787 | 2814 | 2812 | 2871 | 241 |
| Singida | 20 | 20 | 807 | 815 | 823 | 20 | 20 | 21 | 21 | 818 |
| Tabora | 227 | 230 | 128 | 129 | 130 | 219 | 221 | 224 | 226 | 130 |
| Rukwa | 87 | 88 | 678 | 685 | 692 | 81 | 82 | 82 | 83 | 687 |
| Kigoma | - | | 2195 | 2217 | 2239 | - | - | - | - | 2223 |
| Shinyanga | 226 | 229 | 9511 | 9606 | 9702 | 217 | 219 | 221 | 224 | 9634 |
| Kagera | 1818 | 1836 | 7181 | 7253 | 7326 | 1758 | 1776 | 1794 | 1811 | 7275 |
| Mwanza | 6894 | 6963 | 3145 | 3480 | 3515 | 6842 | 6910 | 6979 | 7048 | 3490 |
| Mara | 3739 | 3776 | 659 | 686 | 673 | 3726 | 3763 | 3800 | 3830 | 668 |
| Jumla | 90468 | 91374 | 107386 | 108460 | 109545 | 89343 | 89941 | 91130 | 92034 | 108340 |

| Jina la mkoa | Mishahara (T. Shs. Milioni) 2006 | 2007 | 2008 | 2009* | 2010** | Thamani iliyoongezeka (Tshs. Milioni) 2006 | 2007 | 2008 | 2009* | 2010** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | - | - | | - | 584 | - | - | - | - | 8562 |
| Arusha, Manyara | 6976 | 7006 | 7076 | 7146 | 22329 | 72512 | 73237 | 72286 | 73017 | 356830 |
| Kilimanjaro | 10261 | 10005 | 10108 | 10511 | 12308 | 31958 | 32278 | 31858 | 32181 | 137290 |
| Tanga | 10296 | 10340 | 10443 | 10517 | 12225 | 20250 | 20453 | 20187 | 20391 | 237041 |
| Morogoro | 22369 | 22464 | 22689 | 22913 | 21453 | 49885 | 50384 | 49729 | 50233 | 288858 |
| Pwani | - | - | - | - | 133234 | - | - | - | - | 624421 |
| Dar es Salaam, Pwani*** | 79789 | 80130 | 80932 | 81733 | 79 | 411352 | 415465 | 410062 | 414217 | 435 |
| Lindi | 21 | 21 | 21 | 22 | 1512 | 34 | 34 | 31 | 34 | 4139 |
| Mtwara | 734 | 738 | 745 | 752 | 534 | 11 | 11 | 11 | 11 | 7505 |
| Ruvuma | 721 | 724 | 731 | 739 | 16578 | 1183 | 1195 | 1179 | 1191 | 32645 |
| Iringa | 14511 | 14603 | 14749 | 14895 | 6322 | 15076 | 15226 | 15028 | 15181 | 22191 |
| Mbeya | 3753 | 3769 | 3807 | 3845 | 533 | 25053 | 25304 | 24975 | 25228 | 2312 |
| Singida | 3 | 3 | 3 | 3 | 1330 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4447 |
| Tabora | 18878 | 18859 | 19148 | 19338 | 1037 | 32688 | 33015 | 32586 | 32916 | 1360 |
| Rukwa | 20 | 20 | 20 | 20 | 1575 | 123 | 125 | 123 | 124 | 5324 |
| Kigoma | - | - | - | - | 10089 | - | - | - | - | 19140 |
| Shinyanga | 2630 | 2641 | 2668 | 2694 | 9757 | 30365 | 30659 | 30270 | 30577 | 32941 |
| Kagera | 3577 | 3590 | 3628 | 3664 | 13729 | 42293 | 42716 | 42160 | 42588 | 102068 |
| Mwanza | 9170 | 9209 | 9302 | 9394 | 10053 | 30902 | 31211 | 30805 | 31137 | 82384 |
| Mara | 7429 | 7461 | 7535 | 7610 | 5696 | 15643 | 15799 | 15591 | 15752 | 13703 |
| Jumla | 191170 | 191987 | 193907 | 195826 | 280951 | 779329 | 787121 | 776864 | 781756 | 1901615 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimerekebishwa

** Takwimu za awali

*** Kuanzia mwaka 2003 takwimu za mkoa wa Pwani zimejumuishwa na mkoa wa DSM

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

VIGEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWANDA

Jedwali Na. 65

| Mwaka | Mchango katika Pato la Taifa % (Bei za 2001) | Ukuaji wa Sekta (Bei za 2001) | Mchango katika Mauzo nje % | Mchango katika Mauzo nje yasiyo Asilia (%) | Ongezeko la mauzo nje ya bidhaa za viwanda (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1998 | 8.37 | 5.50 | 8.10 | 15.40 | - |
| 1999 | 8.47 | 6.04 | 5.50 | 12.40 | -15.7% |
| 2000 | 8.46 | 4.80 | 6.50 | 11.71 | 44.2% |
| 2001 | 8.38 | 4.98 | 7.23 | 9.05 | 29.4% |
| 2002 | 8.40 | 7.45 | 7.40 | 8.52 | 17.3% |
| 2003 | 8.57 | 9.01 | 6.79 | 8.42 | 27.2% |
| 2004 | 8.69 | 9.41 | 8.28 | 9.37 | 31.4% |
| 2005 | 8.87 | 9.82 | 9.31 | 11.81 | 41.8% |
| 2006 | 9.02 | 8.50 | 11.24 | 13.81 | 25.4% |
| 2007 | 9.15 | 8.73 | 15.28 | 16.04 | 57.9% |
| 2008 | 9.36 | 9.90 | 23.84 | 32.25 | 139.9% |
| 2009 | 9.54 | 8.00 | 17.74 | 15.00 | -31.7% |
| 2010 | 9.61 | 7.90 | 26.14 | 25.87 | 90.3% |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Uchumi

# SURA YA 15

# UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

## UJENZI

### Kiwango cha Ukuaji

295. Mwaka 2010, kiwango cha ukuaji wa shughuli za ujenzi kilikuwa asilimia 10.2, ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2009. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi na ukarabati wa: barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; viwanja vya ndege; na miundombinu ya maji. Aidha, mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.0 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2009.

### Mtandao wa Barabara

296. Mwaka 2010, Tanzania ilikuwa na mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 91,049 ikilinganishwa na kilomita 85,000 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Kati ya hizo, kilomita 12,786.18 ni za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, kilomita 20,225.82 ni barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu nchini na kilomita 58,037 ni barabara za wilaya zinazounganisha wilaya na vijiji pamoja na barabara viunganishi.

297. Mwaka 2010, kilomita 8,364.73 za barabara kuu zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilomita 7,119.96 mwaka 2009, sawa na uboreshaji wa asilimia 5. Kilomita 3,578.53 za barabara kuu zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilomita 2,332.22 mwaka 2009. Aidha, kilomita 842.93 za barabara kuu zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilomita 1,161.11 mwaka 2009. Hii inaonesha kuwa sehemu kubwa ya barabara zilikarabatiwa na kupandishwa hadhi.

298. Mwaka 2010, jumla ya kilomita 10,749.38 za barabara za Mikoa zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilomita 8,462.41 mwaka 2009. Hii ina maana kuwa ubora wa barabara za mikoa uliongezeka kwa asilimia 27.0 mwaka 2010. Kilomita 6,931.62 zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na

kilomita 7,131.77 mwaka 2009. Aidha, kilomita 2,545.12 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilomita 3,363.21 mwaka 2009. Mchanganuo wa hali ya barabara hadi kufikia Desemba 2010 umeoneshwa katika Jedwali Na.15.1.

**Jedwali Na. 15.1 Hali ya Mtandao wa Barabara Hadi Kufikia Desemba 2010**

| Aina ya Barabara | Hali Nzuri | | Hali ya Wastani | | Hali Mbaya | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | km | % | km | % | km | % | |
| Barabara Kuu | | | | | | | |
| Lami | 3,847.88 | 75% | 1128.71 | 22% | 153.92 | 3% | 5,130.50 |
| Zisizo na Lami | 4,516.85 | 59% | 2,449.82 | 32% | 689.01 | 9% | 7,655.68 |
| **Jumla ndogo** | **8,364.73** | **65%** | **3,578.53** | **28%** | **842.93** | **7%** | **12,786.19** |
| **Barabara za Mikoa** | | | | | | | |
| Lami | 597 | 85% | 98.28 | 14% | 7.02 | 1% | 702 |
| Zisizo na Lami | 10,152.38 | 52% | 6,833.34 | 35% | 2,538.10 | 13% | 19,523.82 |
| **Jumla ndogo** | **10,749.38** | **53%** | **6,931.62** | **34%** | **2,545.12** | **13%** | **20,225.82** |
| **Jumlakuu** | **19,114.11** | **58%** | **10,510.15** | **32%** | **3,388.05** | **10%** | **33,012.00** |

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

**Matengenezo ya Barabara na Madaraja**

299. Mwaka 2010, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) ilizifanyia matengenezo na ukarabati barabara kuu za mikoa zenye urefu wa kilomita 28,647, ikilinganishwa na kilomita 27,878 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Aidha, katika mwaka 2010, Serilikali kupitia TANROADS ilifanya matengenezo ya madaraja 2,480, ikilinganishwa na madaraja 2,232 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 11.1.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

300. Mwaka 2010, makusanyo ya mapato ya Mfuko wa Barabara yaliongezeka hadi kufikia shilingi 278.231 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 263.399 bilioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 5.64. Mwaka 2010,

Serikali iliendelea na ufuatiliaji wa matumizi ya Mfuko kwa kufanya Ukaguzi wa Kiutaalamu na wa Kifedha kwenye miradi ya barabara. Katika ufuatiliaji huo, mapungufu kadhaa yalibainishwa na hatua ziliendelea kuchukuliwa katika kurekebisha mapungufu hayo. Aidha, mwongozo wa matumizi ya Fedha za Mfuko kwa Mawakala wa barabara uliandaliwa ili kuruhusu hatua kali kuchukuliwa endapo kutakuwa na matumizi mabaya ya mfuko.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

301. Mwaka 2010, Bodi ya Usajili wa Makandarasi iliendelea kusajili wakandarasi kwa viwango vilivyokidhi mahitaji na kuzingatia usalama wa umma. Mwaka 2010, Bodi ilisajili Makandarasi wapya 860, ikilinganishwa na makandarasi 930 mwaka 2009. Aidha, Bodi ilifanya ukaguzi katika miradi 2,112 ya ujenzi, ambapo miradi 1,307 ilikuwa haina kasoro, sawa na asilimia 61.9 ya miradi iliyokaguliwa na miradi 805 ilikuwa na kasoro ikiwemo kutokuzingatia afya na usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi zinazozidi daraja la usajili. Makandarasi katika miradi yenye upungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria

302. Aidha, Bodi ilianza kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano (2010 – 2014) unaolenga kuongeza ufanisi katika maeneo makuu manne ambayo ni: Maadili katika Sekta ya Ujenzi, hususan, katika Biashara ya Ukandarasi; Uwezo na Umahiri wa Wakandarasi; Usalama kwa Watendaji Kazi katika Sehemu za Kazi na Umma kwa Ujumla; na Ufanisi wa Bodi.

303. Mwaka 2010, Bodi iliendesha kozi tano za mafunzo ya Makandarasi katika mikoa ya Shinyanga, Rukwa, Dar es Salaam na Mtwara kama ilivyofanya mwaka 2009 ambapo kozi kama hizi ziliendeshwa katika mikoa ya Kagera, Dar es salaam, Ruvuma, Kilimanjaro, Morogoro na Tabora. Jumla ya washiriki 285 walihudhuria kozi hizo mwaka 2010, ikilinganishwa na washiriki 373 waliohudhuria mwaka 2009. Aidha, mwaka 2010, maonesho ya teknolojia, vifaa na huduma za ujenzi yalifanyika katika mkoa wa Dar es Salaam ambapo washiriki 1,231 walihuhudhuria.

**Bodi ya Usajili ya Wahandisi**

304. Mwaka 2010, Bodi ya Usajili ya Wahandisi ilisajili wahandisi 596 ikilinganishwa na wahandisi 862 mwaka 2009. Aidha, Bodi ilisajili Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 9, ikilinganishwa na kampuni 17 mwaka 2009. Kati ya makampuni hayo, 8 yalikuwa ya kigeni na 6 ya kizalendo. Kushuka kwa usajili kulitokana na Bodi kuchelewa kuteuliwa na hivyo kufanya vikao vya usajili kupungua kutoka vikao sita hadi vikao vinne; na ufinyu wa bajeti ambao uliathiri idadi na maendeleo ya wahandisi wahitimu waliokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo.

**Jedwali Na.15.2: Usajili wa Wahandisi kwa Mwaka 2009 - 2010**

| Aina za usajili | Usajili 2009 | Usajili 2010 |
|---|---|---|
| Wahandisi | 25 | 23 |
| Wahandisi Washiriki | 13 | 5 |
| Wahandisi Wahitimu | 525 | 411 |
| Wahandisi Wataalamu | 165 | 67 |
| Wahandisi Wataalamu wa Muda | 91 | 65 |
| Wahandisi Washauri | 17 | 9 |
| Wahandisi Washauri wa Muda | 9 | 2 |
| Kampuni za Wahandisi Washauri za Kizalendo | 9 | 6 |
| Kampuni za Wahandisi Washauri za Nje | 8 | 8 |
| **JUMLA** | **862** | **596** |

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

305. Mwaka 2010, Bodi ilisimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu 622. Takwimu za Wahandisi Wahitimu waliojiunga na Mpango wa Mafunzo kwa vitendo tangu kuanza kwa Mpango zimeoneshwa katika jedwali Na. 15.3.

Jedwali Na. 15.3: Wahandisi Wahitimu Mpango wa Mafunzo kwa vitendo 2002/2003 – 2009/2010

| Mwaka | Idadi ya waliojiunga | Wanaoghar imiwa na Serikali | Wanaoghari miwa na waajiri wao | Waliomali za Mafunzo | Walioajiri wa kabla ya kumaliza | Walioah irisha |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2002/03 | 120 | 110 | 10 | - | 60 | 8 |
| 2003/04 | 169 | 162 | 7 | 20 | 95 | 9 |
| 2004/05 | 212 | 195 | 17 | 10 | 120 | 15 |
| 2005/06 | 167 | 137 | 30 | 121 | 81 | 12 |
| 2006/07 | 218 | 113 | 105 | 78 | 85 | 20 |
| 2007/08 | 159 | 128 | 31 | 136 | 34 | 12 |
| 2008/09 | 265 | 156 | 109 | 140 | 79 | 41 |
| 2009/10 | 263 | 104 | 159 | 176 | 60 | 12 |
| **Jumla** | **1,573** | **1,105** | **468** | **681** | **614** | **129** |

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

**Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

306. Mwaka 2010, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili jumla ya wabunifu majengo 20 na wakadiriaji majenzi 13, ikilinganishwa na wabunifu majengo 94 na wakadiriaji majenzi 54 mwaka 2009 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Bodi kufikia 487. Usajili huu ni ongezeko la asilimia 7.3, ikilinganishwa na jumla ya wataalamu 454 waliosajiliwa mwaka 2009. Aidha, makampuni 13 ya wabunifu majengo na makampuni 8 ya ukadiriaji majenzi yalisajiliwa mwaka 2010, ikilinganishwa na makampuni 55 ya wabunifu majengo na makampuni 30 ya ukadiriaji majenzi yaliosajiliwa mwaka 2009. Hii inafanya jumla ya makampuni yaliyosajiliwa mwaka 2010 kufikia 242 ikilinganishwa na jumla ya makampuni 221 yaliosajiliwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Vilevile, Bodi ilisajili wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi wenye sifa za kati nane mwaka 2010 na kufanya jumla ya wataalamu wa sifa za kati kufikia 66, kutoka wataalam 58 mwaka 2009. Ongezeko la wataalam waliosajiliwa lilitokana na juhudi za Serikali kugharamia mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu katika taaluma hizi na hatua za makusudi zilizochukuliwa za kuwahamasisha wahitimu wenye sifa zilizoainishwa kwenye sheria Na. 4 ya mwaka 2010 kusajiliwa na Bodi.

307. Mwaka 2010, usajili wa mbunifu majengo mmoja, mkadiriaji majenzi mmoja na kampuni moja ya ubunifu majengo wote wakiwa wa nje, ulifikia ukomo kutokana na kukamilika kwa miradi waliosajiliwa nayo na hivyo Bodi kufuta usajili wao kwa mujibu wa sheria. Aidha, ukaguzi wa majenzi ulifanyika katika mikoa 21 ya Tanzania Bara ambapo miradi 1,259 ya majenzi ilikaguliwa, ikilinganishwa na miradi 999 iliyokaguliwa mwaka 2009.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

308. Mwaka 2010, Baraza la Ujenzi la Taifa liliendesha mafunzo kwa wadau 243 wa sekta kuhusu shughuli za zabuni; menejimenti ya mikataba na madai ya gharama za ujenzi wa barabara; shughuli za matengenezo na ukarabati wa majengo; na usuluhishi wa migogoro. Aidha, ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi ulifanyika katika miradi 29 ya ujenzi yenye jumla ya thamani ya shilingi 1,528 bilioni. Hii inajumuisha miradi ya barabara (21), majengo (17) na maji (1).

**Wakala wa Majengo Tanzania**

309. Mwaka 2010, Wakala wa Majengo Tanzania ulifanya matengenezo ya nyumba za viongozi katika Jiji la Dar es Salaam na nyumba za Wakuu wa Wilaya za Lushoto, Tanga, Moshi, Mbeya na Ukerewe. Aidha, Wakala ulinunua maeneo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika mikoa ya Dar es Salaam (Kiluvya), Mbeya, Mwanza na Arusha. Hata hivyo, kulikuwa na kasi ndogo ya ujenzi wa nyumba kwa ajili ya watumishi wa Serikali kutokana na sababu kadhaa zikiwemo: gharama kubwa za viwanja; kukosekana kwa miundombinu katika viwanja hivyo; na kupanda kwa gharama za ujenzi.

## MAENDELEO YA ARDHI

310. Mwaka 2010, hati za kumiliki ardhi 26,839 zilisajiliwa na kutolewa kwa wananchi ikilinganishwa na hati 26,231 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa kasi ya utoaji wa hati miliki baada ya kuanzishwa kwa ofisi za ardhi katika kanda sita na kuzipatia watumishi na vitendea kazi.

Jedwali Na. 15.4 UPIMAJI WA VIJIJI NCHINI KATI YA MWAKA 2008 – 2010

| Wialya | Idadi ya Vijiji vilivyopimwa Mwaka 2008 | Wilaya | Idadi ya Vijiji vilivyo pimwa Mwaka 2009 | Wilaya | Idadi ya Vijiji vilivyo pimwa Mwaka 2010 |
|---|---|---|---|---|---|
| Shinyanga Vijijini | 107 | Tandahimba | 126 | Singida Vijijini | 35 |
| Karagwe | 60 | Newala | 123 | Bahi/Chamwino | 54 |
| Mtwara Vijijini | 120 | Masasi | 107 | Tarime | 39 |
| Mvomero | 98 | Nanyumbu | 72 | Rorya | 63 |
| Morogoro | 132 | Tunduru | 50 | Sengerema | 23 |
| Kondoa | 173 | Magu | 10 | Muleba | 98 |
| - | - | Iramba | 118 | Misenyi | 73 |
| - | - | Musoma | 85 | Karagwe | 45 |
| - | - | Singida Vijijini | 153 | Ngara | 68 |
| - | - | Hai | 56 | Kigoma Vijijini | 21 |
| - | - | Siha | 37 | Kahama | 221 |
| - | - | Bunda | 106 | Bariadi | 22 |
| - | - | Serengeti | 58 | Tabora Vijijini | 127 |
| - | - | - | - | Babati | 5 |
| - | - | - | - | Kilosa/Mahenge | 87 |
| - | - | - | - | Shinyanga Vijijini/Kishapu | 226 |
| Jumla | 690 | | 1,101 | | 1,207 |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

311. Mwaka 2010, jumla ya vijiji 1,207 vilipimwa mipaka yake, ikilinganishwa na vijiji 1,101 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Vilevile, vijiji 3,265 viliandaliwa na kupatiwa vyeti vya ardhi ya vijiji, ikilinganishwa na vyeti vya ya vijiji 2,624 mwaka 2009. Upimaji huu wa mipaka ya vijiji unawezesha kuandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kupima mashamba ya wanavijiji na kutoa Hatimiliki za Kimila.

**Jedwali Na. 15.5: Utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hatimiliki za Kimila**

| (a) Cheti cha Ardhi ya Kijiji | | | | | | (b) Hatimiliki za Kimila | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka 2008 | | Mwaka 2009 | | Mwaka 2010 | | Mwaka 2008 | | Mwaka 2009 | | Mwaka 2010 | |
| Mkoa | Idadi (Vijiji) | Mkoa | Idadi (Vijiji) | Mkoa | Idadi (Vijiji) | Mkoa | Idadi (Hatimiliki za Kimila) | Mkoa | Idadi (Hatimiliki za Kimila) | Mkoa | Idadi (Hatimiliki za Kimila) |
| Mbeya | 207 | Mtwara | 581 | Pwani | 16 | Mbeya | 2,236 | Manyara – Babati | 14,137 | Pwani | 2927 |
| Iringa | 86 | Iringa | 286 | Dodoma | 144 | Iringa | 493 | Shinyanga – Bariadi | 17,456 | Mara | 449 |
| Ruvuma | 30 | Mwanza | 389 | Iringa | 406 | | - | Ruvuma - Namtumbo | 4,850 | Morogoro | 549 |
| Arusha | 80 | Singida | 175 | Manyara | 7 | | - | Singida – Manyoni | 3,850 | Dodoma | 632 |
| Shinyanga | 50 | Kilimanjaro | 43 | Ruvuma | 46 | | - | | - | Iringa | 800 |
| Mwanza | 12 | Kagera | 155 | Shinyanga | 493 | | - | | - | Babati | 30,556 |
| Manyara | 42 | Shinyanga | 504 | Singida | 273 | | - | | - | Ruvuma | 8,714 |
| Pwani | 14 | Rukwa | 117 | Mtwara | 548 | | - | | - | Shinyanga | 38,334 |
| Kagera | 10 | Mbeya | 220 | Mwanza | 374 | | - | | - | Singida | 6,428 |
| Jumla | 531 | | 2470 | | 2307 | | 2729 | | 40293 | | 89389 |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

312. Mwaka 2010, jumla ya hatimiliki za kimila 89389 zilitolewa kwa wananchi, ikilinganishwa na hatimiliki za kimila 40,293 mwaka 2009. Ongezekeo hilo lilitokana na kuhamasika kwa wananchi juu ya umuhimu na faida za kupima na kupata hatimiliki za kimila ambazo ni pamoja na kuitumia hatimiliki hiyo kama rehani wakati wa kuomba mikopo kutoka kwenye vyombo vya fedha na katika mfuko wa pembejeo. Maeneo ambayo hatimiliki hizo zilitolewa ni pamoja na wilaya za Babati, Bariadi, Namtumbo, Manyoni, Rufiji, Bagamoyo, Nachingwea, Mbozi, Handeni, Mvomero, Mpwapwa na Iringa. Aidha, viwanja 28,859 vilipimwa na kumilikishwa kwa wananchi mwaka 2010, ikilinganishwa na viwanja 38,710 mwaka 2009. Vilevile, jumla ya mashamba 666 yalipimwa nchini, ikilinganishwa na upimaji wa mashamba 623 mwaka 2009.

Jedwali Na. 15.6 Idadi ya Viwanja na Mashamba Yaliyopimwa Nchini

| Na. | MKOA | VIWANJA | | MASHAMBA | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwaka 2009 | Mwaka 2010 | Mwaka 2009 | Mwaka 2010 |
| 1. | Arusha | 1547 | 930 | 22 | 165 |
| 2. | Pwani | 1141 | 1966 | 174 | 140 |
| 3. | D'Salaam | 7971 | 4175 | 3 | 4 |
| 4. | Dodoma | 97 | 885 | 0 | 1 |
| 5. | Iringa | 708 | 2947 | 9 | 14 |
| 6. | Kagera | 454 | 738 | 36 | 92 |
| 7. | Kigoma | 1414 | 448 | 0 | 1 |
| 8. | Kilimanjaro | 1372 | 1133 | 52 | 85 |
| 9. | Lindi | 594 | 425 | 3 | 13 |
| 10. | Manyara | 2204 | 569 | 16 | 11 |
| 11. | Mara | 859 | 458 | 17 | 21 |
| 12. | Mbeya | 1024 | 691 | 25 | 41 |
| 13. | Morogoro | 1563 | 2262 | 87 | 20 |
| 14. | Mtwara | 1461 | 1242 | 14 | 3 |
| 15. | Mwanza | 9175 | 6514 | 2 | 38 |
| 16. | Rukwa | 976 | 308 | 2 | 4 |
| 17. | Ruvuma | 797 | 131 | 12 | 5 |
| 18. | Shinyanga | 1659 | 765 | 10 | 2 |
| 19. | Singida | 657 | 222 | 0 | 0 |
| 20. | Tabora | 1310 | 671 | 14 | 0 |
| 21. | Tanga | 1727 | 1379 | 125 | 6 |
| JUMLA | | 38,710 | 28,859 | 623 | 666 |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

313. Mwaka 2010, jumla ya mashauri (kesi) 9,320 yalipokelewa kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Kati ya hayo, mashauri 7,174 ambayo ni sawa na asilimia 77.0 ya mashauri yaliyopokelewa yaliamuliwa, ikilinganishwa na mashauri 7,123 mwaka 2009. Hii ni katika utekelezaji wa Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002, inayohimiza mashauri ya ardhi yaamuliwe kwa wakati ili kuepusha migogoro na kuwawezesha wananchi kuishi kwa amani na utulivu nchini.

Jedwali Na. 15.1 Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Nyumba 2009 – 2010

| Baraza | Mashauri Yaliyokuwepo mwaka 2009 | Mashauri Yaliyoamuliwa mwaka 2009 | Mashauri YaliyokuwePo mwaka 2010 | Mashauri Yaliyoamuliwa mwaka 2010 |
|---|---|---|---|---|
| Arusha | 927 | 390 | 388 | 257 |
| Babati | 817 | 399 | 283 | 269 |
| Bukoba | 1,472 | 476 | 664 | 679 |
| Chato | 198 | 99 | 81 | 49 |
| Dodoma | 426 | 191 | 222 | 205 |
| Geita | 171 | 24 | 121 | 112 |
| Ifakara | 412 | 167 | 299 | 204 |
| Ilala | 1,858 | 373 | 403 | 209 |
| Iramba | - | - | - | - |
| Iringa | 391 | 182 | 161 | 137 |
| Karatu | 236 | 135 | 91 | 54 |
| Kigoma | 415 | 120 | 143 | 121 |
| Kinondoni | 1,800 | 704 | 450 | 378 |
| Kondoa | - | - | 126 | 160 |
| Korogwe | - | - | 233 | 70 |
| Lindi | 95 | 57 | 52 | 47 |
| Maswa | - | - | 123 | 67 |
| Mbeya | 564 | 165 | 292 | 200 |
| Mbinga | 155 | 114 | 152 | 121 |
| Mkuranga | - | - | 64 | 62 |
| Morogoro | 726 | 161 | 418 | 245 |
| Moshi | 678 | 275 | 303 | 297 |
| Mtwara | 237 | 106 | 66 | 74 |
| Musoma | 566 | 246 | 383 | 333 |
| Mwanza | 1,594 | 478 | 414 | 269 |
| Njombe | 182 | 89 | 70 | 42 |
| Pwani | 538 | 249 | 231 | 202 |
| Rukwa | 252 | 148 | 154 | 147 |
| Rungwe | 158 | 70 | 231 | 173 |
| Same | 22 | 7 | 47 | 44 |
| Shinyanga | 546 | 165 | 196 | 71 |
| Simanjiro | 99 | 46 | 89 | 71 |
| Singida | 502 | 227 | 206 | 196 |
| Songea | 291 | 134 | 150 | 112 |
| Tabora | 238 | 103 | 149 | 126 |
| Tanga | 370 | 144 | 165 | 220 |
| Tarime | 867 | 354 | 358 | 263 |
| Temeke | 1,158 | 525 | 1303 | 859 |
| Ukerewe | - | - | 39 | 29 |
| **Jumla** | **18,961** | **7,123** | **9,320** | **7,174** |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

MAENDELEO YA MAKAZI NA VIJIJI

314. Mwaka 2010, mipango ya matumizi ya ardhi iliandaliwa kwa vijiji 113 katika Wilaya 21, ikilinganishwa na vijiji 146 katika Wilaya 29 mwaka 2009. Katika vijiji hivyo, maeneo ya huduma za jamii pamoja na hifadhi za vyanzo vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori na maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na mashamba makubwa yalitengwa kwa kushirikisha wananchi. Lengo la mipango hiyo ni kuwawezesha watumiaji wa ardhi kuwa na mipango endelevu inayozingatia mahitaji ya sasa na baadaye.

### Jedwali Na.15.8: Idadi ya Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, 2009 – 2010

| Wilaya | Idadi ya Vijiji (Mwaka 2009) | Wilaya | Idadi ya Vijiji (Mwaka 2010) |
|---|---|---|---|
| Babati | 9 | Babati | 13 |
| Bagamoyo | 8 | Bagamoyo | 2 |
| Bariadi | 9 | Bariadi | 23 |
| Bunda | 2 | Handeni | 4 |
| Ileje | 0 | Ileje | 2 |
| Kibaha | 0 | Kibaha | 3 |
| Kigoma vijijini | 0 | Kigoma vijijini | 11 |
| Kilombero | 12 | Kilombero | 2 |
| Kilosa | 4 | Kisarawe | 12 |
| Kiteto | 2 | Kondoa | 5 |
| Kongwa | 2 | Kongwa | 2 |
| Lindi | 2 | Longido | 2 |
| Ludewa | 2 | Mbozi | 2 |
| Manyoni | 9 | Misenyi | 2 |
| Mbinga | 4 | Namtumbo | 2 |
| Mkinga | 9 | Monduli | 2 |
| Mkuranga | 1 | Mkuranga | 7 |
| Morogoro | 4 | Nanyumbu | 6 |
| Morogoro Vijijini | 22 | Singida | 2 |
| Mpanda | 2 | Tanga | 1 |
| Musoma | 3 | Ulanga | 8 |
| Namtumbo | 15 | - | - |
| Njombe | 1 | - | - |
| Nkasi | 2 | - | - |
| Serengeti | 5 | - | - |
| Tandahimba | 2 | - | - |
| Tunduru | 4 | - | - |
| Ulanga | 9 | - | - |
| Uyui | 2 | - | - |
| **Jumla** | **146** | | **113** |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

315. Serikali kupitia Programu ya kurasimisha makazi yaliyojengwa kiholela nchini, ilipima jumla ya viwanja 6,938 mwaka 2010 katika Jiji la Mwanza, ikilinganishwa na viwanja 3,322 vilivyopimwa mwaka 2009. Kati ya viwanja vilivyopimwa, wamiliki 402 walipatiwa hati za kumiliki ardhi. Hati zilizosainiwa zinaendelea kutayarishwa, kusajiliwa na kutolewa kwa wananchi. Vilevile, kupitia programu hiyo, jumla ya leseni za makazi 2,778 zilitolewa Jijini Dar es Salaam. Mradi huu unatekelezwa kwa kuwashirikisha wananchi kuchangia gharama za upimaji wa ardhi na umilikishaji.

## MAENDELEO YA NYUMBA

316. Mwaka 2010, Shirika la Nyumba la Taifa liliendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Miradi hii ni pamoja na ukamilishaji wa nyumba katika mikoa ya Dar es Salaam - Mtaa wa Chwaku (2) na Dodoma - eneo la Medeli (20). Aidha, Shirika liliendelea na ujenzi mkoani Arusha - eneo la Kibla (48) na eneo la LDA (4) na Jijini Dar es Salaam - Mbweni JKT (34) na Kinondoni – Chwaka (2). Vilevile, miradi ya ubia 75 inayotekelezwa na Shirika kwa kushirikiana na sekta binafsi ilikuwa katika hatua mbali mbali za utekelezaji.

317. Mwaka 2010, Shirika liliendelea na matayarisho ya ujenzi wa miradi mikubwa ambayo ni pamoja na michoro, upembuzi yakinifu na utafutaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi. Mayatarisho hayo ni ya ujenzi wa nyumba 290 eneo la Medeli – Dodoma na nyumba 260 za makazi ya mpito Jijini Dar es Salaam. Nyumba za mpito zitawapatia makazi ya muda wapangaji wanaoishi kwenye nyumba zilizoko kwenye viwanja vitakavyoendelezwa upya kwa kujenga majengo makubwa.

318. Mwaka 2010, Serikali ilipata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 40 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuinua sekta ya nyumba nchini. Fedha hizo zitawezesha kuwepo kwa uraratibu wa mikopo ya nyumba nchini; kufanyika kwa utafiti wa kuwepo kwa mikopo midogo ya ujenzi wa nyumba; kufanyika utafiti wa soko la nyumba nchini; na kulijengea uwezo Shirika la Nyumba kuwa mwendelezaji mkuu wa ardhi.

## SURA YA 16

# MAWASILIANO NA UCHUKUZI

**Utangulizi**

319. Mwaka 2010, shughuli za kiuchumi za uchukuzi na mawasiliano zilikua kwa asilimia 7.0 na asilimia 22.1, ikilinganishwa na asilimia 6.0 na asilimia 21.9 mwaka 2009, kwa mtiririko huo. Ukuaji katika shughuli za kiuchumi za mawasiliano ulitokana na kuongezeka kwa uwezekezaji katika sekta ya mawasiliano na kuongezeka kwa wateja wa simu za viganjani na makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano. Aidha, ukuaji katika shughuli za kiuchumi za uchukuzi ulitokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria waliosafiri kwa njia ya barabara, anga na majini pamoja na kuongezeka kwa shehena katika bandari hususan bandari ya Dar es Salaam. Mchango wa shughuli za uchukuzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 5.1, ukilinganisha na asilimia 5.0 mwaka 2009, ambapo mchango wa shughuli za mawasiliano uliendelea kuwa asilimia 2.1, kama ilivyokuwa mwaka 2009.

## UCHUKUZI

**Usafiri Wa Barabara**

320. Mwaka 2010, jumla ya leseni za usafirishaji kwa mabasi ya abiria 31,523 zilitolewa, ikilinganishwa na leseni 25,114 zilizotolewa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 26. Aidha, jumla ya leseni 43,312 zilitolewa kwa magari ya mizigo ikilinganishwa na leseni 36,853 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 17.5. Kuongezeka kwa leseni zilizotolewa kulitokana na kuboreshwa kwa utaratibu wa uwasilishaji wa maombi ya leseni kwa kutumia tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) (www.sumatra.org.tz) na utoaji wa elimu kwa umma. Vilevile, kufunguliwa kwa ofisi za SUMATRA katika mikoa ya Morogoro, Tabora, Kigoma, Mara, Kagera na Arusha kulisogeza huduma za Mamlaka karibu na wananchi.

### Usafiri wa Abiria mijini

321. Mwaka 2010, idadi ya mabasi mijini iliongezeka kufikia mabasi 14,714, ikilinganishwa na mabasi 12,534 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 17.4. Miji ya mikoa iliyokuwa na mabasi mengi ni pamoja na Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Mwanza. Idadi ya mabasi madogo katika jiji la Dar es Salaam iliendelea kupungua, kutoka mabasi 2,086 mwezi Desemba, 2009, hadi mabasi 1,672 mwezi Desemba, 2010, sawa na upungufu wa asilimia 20. Hata hivyo, mabasi makubwa yaliongezeka kutoka mabasi 3,488 mwezi Desemba 2009, hadi mabasi 4,385 mwezi Desemba, 2010, sawa na ongezeko la asilimia 26. Kupungua kwa mabasi madogo katika jiji la Dar es Salaam kulitokana na hatua zilizochukuliwa na SUMATRA za kutotoa leseni mpya kwa mabasi madogo. Hatua hiyo imechochea uingizaji wa mabasi makubwa katika usafiri wa umma na hivyo kupunguza msongamano jijini na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za usafiri.

**Jedwali Na. 16.1: Idadi ya Mabasi ya Abiria katika Miji na Mikoa**

| Mkoa | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 150 | 170 | 220 | 154 | 167 | 126 | 142 | 405 | 185.2% |
| Arusha | 1,118 | 1,045 | 837 | 892 | 1,367 | 1,255 | 1,607 | 1,620 | 0.8% |
| Moshi | 220 | 720 | 143 | 170 | 178 | 310 | 625 | 650 | 40% |
| Lindi | 3 | 11 | 18 | 15 | 57 | 46 | 52 | 54 | 3.8% |
| Tanga | 120 | 169 | 136 | 105 | 162 | 93 | 184 | 313 | 70.1% |
| Morogoro | 312 | 300 | 300 | 400 | 236 | 267 | 289 | 350 | 21.1% |
| Pwani | - | 130 | 143 | 145 | - | - | - | - | |
| Dar es salaam | 5,801 | 6,600 | 7,000 | 8,972 | 6,144 | 5,716 | 6,043 | 7,573 | 25.3% |
| Mtwara | 35 | 29 | 14 | 28 | 49 | 30 | 62 | 54 | -12.9% |
| Ruvuma | 52 | 76 | 78 | 171 | 202 | 93 | 84 | 95 | 13.1% |
| Iringa | 97 | 113 | 154 | 160 | 174 | 210 | 611 | 587 | -3.9% |
| Shinyanga | - | - | - | - | - | - | - | - | |
| Mbeya | 355 | 475 | 544 | | 375 | 1,180 | 1,115 | 1,433 | 28.5% |
| Singida | - | 9 | 17 | 14 | 88 | 34 | 56 | 83 | 48.2% |
| Tabora | 15 | 37 | 44 | 16 | 22 | 17 | 11 | 18 | 63.6% |
| Kigoma | 66 | 472 | 507 | 538 | 507 | 219 | 174 | 182 | 4.6% |
| Bukoba | 19 | 21 | 10 | 16 | 19 | 14 | 26 | 21 | -19.2% |
| Musoma | 49 | 47 | 48 | 48 | 28 | 16 | 26 | 57 | 119.2% |
| Mwanza | 660 | 776 | 886 | 892 | 1,190 | 1,290 | 1,370 | 1,152 | -15.9% |
| Manyara | - | 47 | 59 | 61 | 49 | 37 | 10 | 15 | 50.0% |
| Rukwa | 13 | 32 | 43 | 20 | 49 | 53 | 47 | 52 | 10.6% |
| Jumla | 9,085 | 11,279 | 11,201 | 12,817 | 11,063 | 11,016 | 12,534 | 14,714 | 17.4% |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA)

322. Mwaka 2010, idadi ya mabasi ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam ilikuwa 22 (ukijumuisha mabasi 5 ya Mradi wa Kubeba Wanafunzi ya CRDB Benki), ukilinganisha na mabasi 17 mwaka 2009. Kwa wastani jumla ya mabasi 12 yalikuwa barabarani kwa siku mwaka 2010 ikilinganishwa na wastani wa mabasi 10 mwaka 2009. Mwaka 2010, Shirika lilifanya jumla ya safari 15,366, ikilingainshwa na safari 26,067 mwaka 2009. Aidha, abiria 1,191,634 walisafiri kwa mabasi ya Shirika ikilinganishwa na abiria 1,491,755 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 20.1.

323. Mapato ya Shirika yaliyotokana na usafirishaji kwa mwaka 2010 yalikuwa shilingi milioni 462.1, ikilinganishwa na shilingi milioni 627.4 mwaka 2009. Aidha, mwaka 2010 mapato yasiyotokana na shughuli za usafirishaji kama vile kodi ya upangishaji wa majengo ya Shirika, uuzaji wa mali chakavu yalikuwa shilingi milioni 264.5, ikilinganishwa na shilingi milioni 302.3 zilizokusanywa mwaka 2009. Kupungua kwa mapato, kulitokana na kupungua kwa abiria na kiwango kidogo cha ukodishwaji binafsi wa mabasi. Matumizi yalifikia shilingi milioni 1,053.7 mwaka 2010, ikilinganishwa na shilingi milioni 1,200.9 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 12.3. Kupungua kwa matumizi kulitokana na juhudi zilizofanywa na uongozi katika kubana matumizi yasiyo ya lazima.

## USAFIRI KWA NJIA YA RELI

324. Mwaka 2010, utendaji katika njia ya reli ulishuka kutokana na uchakavu wa miundombinu pamoja na uflnyu wa bajeti. Utendaji huu ulipunguza uchukuzi kwa njia ya reli ambapo asilimia 3.6 ya shehena iliyotoka Bandari ya Dar es Salaam ilisafirishwa kwa njia ya reli, ikilinganishwa na asilimia 9.4 mwaka 2009.

### Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

325. Mwaka 2010, Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), ilisafirisha tani 256,190, za mizigo, ikilinganishwa na tani 453,000 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 43.4. Aidha, jumla ya abiria 290,046 walisafiri mwaka

2010 ikilinganishwa na abiria 543,000 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 46.6. Hali hii ilisababishwa na kupungua kwa huduma za treni za abiria na mizigo kutokana na kupungua kwa idadi ya injini zinazofanya kazi kufuatia kusimamishwa kwa injini 25 za kukodi za aina ya 73 class, zilizokuwa zimekodishwa kutoka Kampuni ya RITES ya India.

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

326. Mwaka 2010, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ilisafirisha jumla ya tani 552,505 za mizigo, ikilinganishwa na tani 253,263 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 20.4. Idadi ya abiria waliosafiri mwaka 2010 walikuwa 757,987, ikilinganishwa na abiria 794,983 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 4.7. Hali hii ilitokana na kuchakaa na kupungua kwa idadi ya injini imara za treni kutokana na ufinyu wa bajeti pamoja na migomo ya wafanyakazi.

## USAFIRI WA ANGA

**Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA)**

327. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) iliendelea kuhudumia viwanja vya ndege kwa kuzingatia sera ya kuwezesha viwanja vya ndege kujiendesha kibiashara, kujitosheleza kwa mapato na kujitegemea. Idadi ya safari za ndege viwanjani iliongezeka kwa asilimia 7.6, kutoka jumla ya safari 115,620 mwaka 2009, hadi safari 124,356 mwaka 2010. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri kupitia katika viwanja vinavyoendeshwa na Mamlaka iliongezeka kwa asilimia 8.5 kutoka abiria 1,970,656 mwaka 2009 hadi kufikia 2,137,253 mwaka 2010.

328. Mizigo iliyopitishwa katika viwanja husika ilipungua kwa takriban asilimia 1.0, kutoka tani 22,587.7 mwaka 2009, hadi tani 22,364.5 mwaka 2010. Kushuka kwa kiasi cha mizigo kunatokana na kupungua kwa bidhaa zilizoingizwa nchini kulikotokana na msukosuko wa uchumi duniani. Vilevile, vifurushi na barua vilipungua kwa asilimia 26.9 kutoka tani 1,490.5 mwaka 2009 hadi tani 1,089.4 mwaka 2010.

Jedwali 16.2: Idadi ya Safari za Ndege, Abiria, Mizigo na Vifurushi

| Aina | 2008 | 2009 | 2010 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|
| Idadi ya safari za ndege | 123,494 | 115,620 | 124,356 | 7.6 |
| Idadi ya abiria | 2,118,694 | 1,970,656 | 2,137,253 | 8.5 |
| Tani za mizigo | 30,107.90 | 22,587.70 | 22,364.50 | -1.0 |
| Tani za vifurushi | 1,487.00 | 1,490.50 | 1,089.40 | -26.9 |

Chanzo: Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania

329. Mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 24.6 mwaka 2009 hadi kufikia shilingi bilioni 31.4 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 27.6. Ongezeko hilo lilitokana na kupanuka na kukua kwa shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege. Kwa upande mwingine, gharama za uendeshaji ziliongezeka kutoka sh. bilioni 20.0 mwaka 2009, hadi kufikia sh. bilioni 22.5 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.6.

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA

330. Mwaka 2010, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ilikamilisha ujenzi wa kituo cha hali ya hewa kilichopo Mpanda, na hivyo kuongeza idadi ya vituo kufikia 28 nchini. Pia, katika kipindi hicho kituo cha hali ya hewa na kilimo cha Mbimba, Mbozi kilianza kufanya kazi rasmi na hivyo kuboresha huduma za hali ya hewa kwa sekta ya Kilimo. Aidha, mamlaka ilikamilisha ujenzi wa Kituo cha rada katika vilima vya Bangulo-Pugu Mkoani Dar es Salaam. Kwa ujumla Mamlaka ilitoa huduma kwa Sekta nane za kiuchumi na kijamii ambazo ni: kilimo, utafiti, ujenzi, utalii, afya, nishati, madini na bima.

331. Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Hali ya Hewa Ulimwenguni (WMO) iliingia katika mradi wa utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa utoaji huduma bora katika sekta ya usafiri wa anga zinazotambuliwa na Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO) na mwaka 2010, Mamlaka ilipata hati inayotambulika Kimataifa kuhusiana na utoaji huduma hizo.

## USAFIRI WA MAJINI

332. Mwaka 2010, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ilitoa vyeti 6,049 ikilinganishwa na vyeti 5,581 vilivyotolewa mwaka 2009 kwa wafanyakazi wa vyombo vya majini waliokidhi viwango vya mafunzo kwa mujibu wa makubaliano ya Kimataifa. Aidha, mwaka 2010, ajali za majini zilikuwa 13, sawa na ilivyokuwa mwaka 2009. Jumla ya watu 54 walipotea kwenye matukio ya ajali za majini mwaka 2010, ikilinganisha na watu 40 waliopotea mwaka 2009. Ajali nyingi kati ya hizo zilitokea katika miezi ya Machi, Aprili, Mei na Juni kutokana na upepo mkali katika bahari na maziwa. Vilevile, Kituo cha Uokoaji na Utafutaji (MRCC) kilichopo Dar es Salaam kiliendelea kuimarishwa ili kurahisisha upatikana wa habari za matukio ya ajali majini.

**Jedwali Na. 3 Mwenendo wa Ajali katika Usafiri wa Majini**

| Mwaka | Jan | Feb | Mar | Apr | Mei | Jun | Jul | Ago | Sep | Oct | Nov | Dec | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2009 | 0 | 2 | 4 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |
| 2010 | 1 | 0 | 1 | 3 | 2 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 |

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini.

### Uchukuzi Baharini

333. Mwaka 2010, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia shehena za uzito wa tani 10,045,462 ambazo ni ongezeko la asilimia 12.4, ikilinganishwa na tani 8,937,232 zilizohudumiwa mwaka 2009. Ongezeko la shehena limetokana na, kukua kwa shughuli za kiuchumi za nchi zinazotumia bandari za Mamlaka. Aidha, Bandari ya Dar es Salaam ilihudmnia asilimia 88.5 ya shehena yote iliyopitia katika bandari za Mamlaka. Meli zilizohudumiwa na Bandari ya Dar es salaam mwaka 2010 zilikuwa 4,371, sawa na ongezeko la asilimia 0.5, ikilinganishwa na meli 4,349 zilizohudumiwa mwaka 2009. Ongezeko la shehena lilitokana na kukua kwa shehena ya magari, shehena za majimaji hasa mafuta na shehena ya kichele hasa mbolea na ngano kwa ajili ya Tanzania na nchi jirani.

Jedwali Na.16.4: Shehena Iliyohudumiwa kwa Kila Bandari (Tani)

| | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|
| Dar es salaam | 7,642,825 | 7,432,220 | 7,476,618 | 7,796,044 | 8,895,023 |
| Tanga | 460,626 | 512,372 | 490,119 | 495,659 | 598,538 |
| Mtwara | 149,769 | 143,072 | 130,763 | 155,848 | 85,214 |
| KLM | 17,402 | 27,845 | 36,565 | 21,245 | 32,924 |
| Mwanza | 546,482 | 480,568 | 393,832 | 327,204 | 346,294 |
| Kigoma | 125,547 | 107,990 | 98,448 | 132,404 | 79,620 |
| Kyela | 12,989 | 18,098 | 7,960 | 8,828 | 7,849 |
| **Jumla** | **8,955,640** | **8,722,165** | **8,634,305** | **8,937,232** | **10,045,462** |

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

334. Mwaka 2010, abiria waliosafiri kupitia Bandari ya Dar es Salaam waliongezeka kutoka abiria 744,753 mwaka 2009, hadi abiria 892,125, sawa na ongezeko la asilimia 19.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya soko la usafiri wa abiria kati ya Dar es Salaam na Zanzibar.

335. Shehena iliyohudumiwa katika bandari za Mtwara na Kigoma ilipungua mwaka 2010 kutokana na kupungua kwa mazao yanayosafirishwa nje. Sababu nyingine za kupungua kwa shehena zilizohudumiwa katika bandari nyingine ni: kukosekana kwa meli za mwambao kati ya Mtwara na Dar es Salaam; uchache wa meli za kubeba mabehewa katika ziwa Victoria; miundombinu hafifu (reli na barabara) ya kuunganisha bandari na vyanzo vya shehena; pamoja na hali mbaya ya miundombinu ya bandari.

336. Wastani wa siku za kusubiri nje ya bandari kabla ya kuhudumiwa kwa meli za kontena katika Bandari ya Dar es Salaam ulipungua kutoka siku 5 mwaka 2009, hadi siku 3.6 mwaka 2010, sawa na ongezeko la ufanisi wa asilimia 28. Vilevile, katika mwaka 2010, wastani wa muda wa meli kugeuza na kuanza safari nyingine katika kitengo cha makontena ulipungua kufikia siku 6.3, ikilinganishwa na siku 8.2 mwaka 2009, sawa na ongezeko la ufanisi la

asilimia 30.2. Kupungua kwa wastani wa muda wa meli kugeuza na kuanza safari nyingine na siku za meli kusubiri nje ya bandari kabla ya kuhudumiwa kulitokana na kuboreshwa kwa taratibu za uondoshaji wa mizigo bandarini. Aidha, uanzishwaji wa vituo vya nchi kavu kwa ajili ya kuhifadhia makasha kulipunguza msongamano wa makasha katika bandari na hivyo kuongeza tija ya nyenzo za upakiaji na upakuaji.

337. Mwaka 2010, Kitengo cha Kontena (TICTS) kilichopo bandari ya Dar es Salaam kilihudumia jumla ya kontena (TEUs) 369,903, ikilinganishwa na kontena (TEUs) 326,978 zilizohudumiwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Sababu za kukua kwa shehena ya kontena ni pamoja na ukuaji wa uchumi na ongezeko la mizigo inayosafirishwa katika kontena kama magari, shehena ya shaba na mazao ya kilimo.

**Jedwali Na. 16.5: Uhudumiaji wa Meli katika Kitengo cha Makontena Bandari ya Dar es Salaam**

| Mwezi | Muda wa kusubiri | | Upakuaji | | Muda wa meli kufika hadi kuondoka | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2009 | 2010 | 2009 | 2010 | 2009 | 2010 |
| Januari | 12.7 | 3.6 | 6.2 | 3.6 | 18.9 | 7.1 |
| Februari | 14.7 | 4.2 | 4.1 | 4.2 | 18.8 | 8.4 |
| Machi | 8.0 | 4.1 | 3.5 | 3.5 | 11.5 | 7.7 |
| Aprili | 2.5 | 3.2 | 2.9 | 2.8 | 5.4 | 6.0 |
| Mei | 3.4 | 2.6 | 2.3 | 2.7 | 5.7 | 5.3 |
| Juni | 2.7 | 1.7 | 2.5 | 2.4 | 5.2 | 4.1 |
| Julai | 2.6 | 5.3 | 3.7 | 2.7 | 6.3 | 8.0 |
| August | 1.7 | 2.5 | 2.2 | 2.1 | 3.9 | 4.6 |
| Septemba | 2.9 | 2.7 | 2.6 | 2.3 | 5.5 | 5.0 |
| Oktoba | 3.4 | 3.7 | 2.7 | 2.2 | 6.1 | 5.9 |
| Novemba | 2.9 | 5.0 | 3.3 | 2.3 | 6.2 | 7.3 |
| Desemba | 3.3 | 4.8 | 3.0 | 2.8 | 6.3 | 7.6 |
| **Wastani** | **5.0** | 3.6 | 3.2 | **2.7** | **8.2** | 6.3 |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

## UCHUKUZI KWENYE MAZIWA

### Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

338. Katika mwaka 2010, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ilisafirisha jumla ya tani 77,776 za mizigo na abiria 325,595, ikilinganishwa na tani 123,279 za mizigo na abiria 474,272 zilizosafirishwa mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 31.3 kwa abiria, na asilimia 36.9 kwa mizigo. Sababu ya kupungua kwa mizigo na abiria ni utendaji usioridhisha wa reli, ushindani wa meli na mabasi, kuharibika kwa meli za MV. Butiama na MV. Mwongozo, na kuchakaa kwa meli.

### Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP)

339. Mwaka 2010, kampuni ya SINOTASHIP ilisafirisha mizigo kwa kuendesha meli moja kubwa (1), Mv Changshun II yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa wakati mmoja ikilinganishwa na mwaka 2009 ambapo kampuni ilisafirisha mizigo kwa kutumia meli mbili ndogo zenye uwezo wa kubeba tani 30,000 kwa pamoja. Mwaka 2010, utendaji wa kampuni uliimarika ambapo kampuni ilisafirisha shehena na mizigo yenye jumla ya tani 456,000, ikilinganishwa na tani 132,000 mwaka 2009. Aidha, kampuni ilipata wastani wa mapato ya Dola za kimarekani 6,026,689.49, ikilinganishwa na mapato ya dola za kimarekani 9,681,718 kwa mwaka 2009. Katika mwaka 2010 wastani wa gharama za uendeshaji zilikuwa Dola za kimarekani 5,852,539.93 ikilinganishwa na Dola za kimarekani 8,957,718 mwaka 2009. Hivyo, faida iliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2010 ni Dola za kimarekani 1,561,667.09, ikilinganishwa na faida ya dola za kimarekani 724,000 mwaka 2009, sawa na ongezeko la faida kwa asilimia 115.7.

## HUDUMA ZA MAWASILIANO

### Shirika la Posta Tanzania

340. Mwaka 2010, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 17,221,000 ndani ya nchi, ikilinganishwa na barua 15,183,230 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 13.4. Aidha, barua 7,902,000 zilitumwa nje ya nchi mwaka 2010 kupitia Shirika ikilinganishwa na barua 7,753,960 mwaka 2009,

sawa na ongezeko la silimia 1.9. Kuongezeka kwa barua zilizotumwa ndani na nje ya nchi kulitokana na utumaji wa barua za kibiashara.

341. Mwaka 2010, jumla ya vifurushi 18,417 vilisafirishwa ndani ya nchi, ikilinganishwa na vifurushi 18,988 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 3.0. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa ushindani wa Makampuni binafsi na ukosefu wa nyenzo kama magari ya kukusanyia vifurushi. Vifurushi 13,332 vilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2010, ikilinganishwa na vifurushi 6,999 vilivyosafirishwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 90. Ongezeko hili lilitokana na kuimarika kwa matumizi ya "Track and Trace" katika huduma ya vifurushi vya nje na kukua kwa biashara ya kupeleka sampuli nje ya nchi.

342. Rejesta zilizotumwa nchini mwaka 2010, zilikuwa 396,249, ikilinganishwa na rejesta 386,408 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 3.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa usambazaji wa matokeo ya mitihani na vyeti mbalimbali vya wanafunzi wa shule za sekondari. Aidha, rejesta zilizotumwa nje ya nchi mwaka 2010 zilikuwa 27,899, ikilinganishwa na rejesta 42,688 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 35. Upungufu huo ulitokana na wateja kupendelea kutumia huduma za "courier" kupeleka nyaraka zao badala ya rejesta.

343. Mwaka 2010, utumaji wa fedha ndani ya nchi kwa njia ya haraka ulipungua hadi kufikia watumiaji 41,956 kutoka watumiaji 62,019 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 32. Huduma hii ilishuka kutokana na kuongezeka kwa ushindani kutoka kwenye makampuni ya simu. Aidha, utumaji wa fedha nje ya nchi kwa njia ya haraka ulikuwa 2,010 mwaka 2010, ikilinganishwa na watumaji 1,736 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 16. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa vyuo na wanafunzi mbalimbali katika nchi za Afrika hususan (Kenya, Uganda, Rwanda na Comoro).

344. Mwaka 2010, utumaji wa barua kwa njia ya haraka ndani ya nchi uliongezeka na kufikia barua 437,084, kutoka barua 285,070 mwaka 2009,

sawa na ongezeko la asilimia 53. Hali kadhalika, idadi ya barua za haraka zilizotumwa nje ya nchi ilikuwa 26,896 mwaka 2010, ikilinganishwa na barua 18,208 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 48. Ongezeko hili lilitokana na kuboreshwa kwa huduma ya elektroniki ya "Track & Trace".

345. Katika mwaka 2010, huduma ya Utumaji wa Barua na Nyaraka ndani ya Miji "Intracity City Urgent Mail" (CUM) ilianza rasmi (Juni 2010) katika mikoa ya Dar es salaam, Arusha na Tanga. Barua na nyaraka zilizotumwa kwa njia hii katika mwaka 2010 zilikuwa 12,982.

346. Mwaka 2010, utumaji wa fedha kwa njia ya nukushi ndani ya nchi ulikuwa 44,964, ikilinganishwa na nukushi 150,173 zilizotumwa mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 70. Upungufu huo ulitokana na biashara hii ya utumaji wa fedha kutumia zaidi njia ya elektroniki "mobile" akaunti.

347. Mwaka 2010, idadi ya watu waliotuma fedha kwa njia ya mtandao wa Computer (Electronic Money Transfer) ilikuwa 75,282. Huduma hii imeanza mwaka 2010 katika makao makuu ya mikoa 14 na inaendelea kuenezwa katika makao makuu ya Mikoa na Wilaya zenye umeme na mawasiliano ya uhakika.

348. Mwaka 2010, huduma ya utumaji wa ujumbe wa haraka ndani ya nchi ulipungua kufikia watumiaji 25,127, kutoka watumiaji 28,095 mwaka 2009, ikiwa ni upungufu wa asilimia 11. Upungufu huu ulitokana na ushindani mkubwa wa matumizi ya simu za viganjani na "internet". Vilevile, huduma ya utumaji wa ujumbe wa haraka nje ya nchi ilipungua kutoka watumiaji 157 mwaka 2009 kufikia watumiaji 153 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 3.

349. Mwaka 2010, Utumaji wa fedha kwa Hawala za Posta ndani ya nchi iliongezeka na kufikia watumiaji 10,966, kutoka watumiaji 10,626 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Matumizi ya huduma hii yaliongezeka kutokana na Shirika la Posta kupewa fursa ya kutuma malipo ya Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu.

350. Mwaka 2010, utoaji wa huduma ya fedha kwa njia ya Giro ndani ya nchi uliongezeka nakufikia watumiaji 118,637, kutoka watumiaji 100,876 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 18. Ongezeko hili lilitokana na huduma hii kutumika kulipa mishahara, kulipa wanahisa wa makampuni mbalimbali na kulipa pensheni za wastaafu. Aidha, ongezeko hili limetokana na makampuni husika kupata faida na hivyo kutoa gawio.

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

351. Mwaka 2010, idadi ya makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano kwa njia ya sauti ilikuwa 7 kama ilivyokuwa mwaka 2009. Makampuni hayo ni TTCL, Vodacom, Airtel (Zain), Tigo, Zantel na Benson Online na Dovetel (Sasatel). Idadi ya watumiaji wa simu za viganjani iliongezeka kutoka 17,469,486 mwaka 2009, hadi kufikia watumiaji 20,983,853 Desemba 2010, sawa na ongezeko la asilimia 20.1. Vilevile, watumiaji wa simu za mezani walikuwa 174,511 mwaka 2010 ikilinganishwa na watumiaji 172,922, mwaka 2009, sawa na na ongezeko la asilimia 0.9. Aidha, idadi ya makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano kwa njia ya takwimu (data) iliongezeka kutoka makampuni 61 mwaka 2009, hadi kufikia makampuni 80 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 29. Idadi ya watumiaji wa huduma za tovuti (internet) iliongezeka kutoka watumiaji 4,378,392 mwaka 2009 hadi kufikia watumiaji 4,956,000 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 13.2, kama inavyoonekana katikajedwali Na. 16.6.

352. Mwaka 2010, zoezi la usajili wa namba za simu za mkononi liliendelea. Hadi Desemba 2010, jumla ya namba za simu za mkononi 19,000,000 zilikuwa zimesajiliwa, ikilinganishwa na namba za simu za mkononi 9,138,749 zilizosajiliwa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 107.9.

**Jedwali Na. 16.6: Idadi ya Wanaotumia Simu za Mikononi na Mezani**

| Na. | Idadi ya Kampuni za Simu | Idadi ya Wateja | | Badiliko % |
|---|---|---|---|---|
| | | 2009 | 2010 | |
| 1 | VODACOM | 6,883,661 | 8,670,536 | 26 |
| 2 | TIGO | 4,178,089 | 4,477,510 | 7 |
| 3 | ZAIN | 4,910,359 | 6,021,091 | 23 |
| 4 | ZANTEL MOBILE | 1,378,595 | 1,700,528 | 23 |
| 5. | SASATEL | 14,825 | 24,827 | 67 |
| 6. | ZANTEL FIXED | 15,601 | 15,457 | -1 |
| 7. | TTCL MOBILE | 115,681 | 86,965 | -25 |
| 8. | TTCL Fixed | 157,321 | 159,054 | 1 |
| 9. | BENSON | 3,101 | 2,396 | -23 |
| | **JUMLA** | **17,657,233** | **21,158,364** | **20** |
| | **Watumiaji wa simu za mikononi** | **17,484,311** | **20,983,853** | **20** |
| | **Watumiaji wa simu mezani** | **172,922** | **174,511** | **1** |

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Jedwali Na. 16.7: Idadi ya Wanaotumia Tovuti (Internet)**

| Na. | | 2009 | 2010 | Badiliko % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kituo cha huduma za tovuti | 215,640 | 260,280 | 21 |
| 2. | Taasisi/Mashirika | 2,588,000 | 2,663,200 | 3 |
| 3. | Watumiaji Binafsi | 1,574,752 | 1,932,816 | 23 |
| | JUMLA | 4,378,392 | 4,956,000 | 13 |

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

## TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

### Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

353. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano imekamilika na huduma za Mkongo huu zinatolewa na Kitengo Maalum kilichoundwa ndani ya Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL). Tayari Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa umeifikia mikoa 16, nchini ambayo ni Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara na Kagera. Aidha, vituo 63 vya kutolea huduma vimejengwa katika maeneo mengi yakiwemo yale ya mipakani: Rusumo (Rwanda); Kabanga (Burundi); Namanga (Kenya); Kasumulo (Malawi); na Tunduma (Zambia).

354. Awamu ya pili ya mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ilianza kutekelezwa tangu tarehe 1 Agosti, 2010. Awamu hii itatekelezwa kwa kipindi cha miezi 18 hadi mwezi Machi 2012 na inahusisha ujenzi wa takriban kilometa 2,700 ambao utapita katika njia za: Dar es Salaam-Lindi-Mtwara-Songea-Makambako; Tunduma-Sumbawanga-Tabora-Kigoma-Biharamulo; Musoma-Sirari; Tanga-Horohoro; Unguja na Pemba.

### Vituo vya Mawasiliano (Telecenters)

355. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kuanzisha na kuimarisha vituo vya mawasiliano (Telecentres). Idadi ya vituo vya mawasiliano iliongezeka hadi kufikia 15 mwaka 2010, ikilinganishwa na vituo 9 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 66.7. Aidha, Taasisi nyingine za Kiserikali na Sekta binafsi kama COSTECH, DIT na Vodacom zimeonesha nia ya kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuanzisha na kuendeleza vituo ambapo COSTECH waliweza kuanzisha vituo 47 katika maeneo mbalimbali nchini.

**Uanzishaji wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta.**

356. Mwaka 2010, zoezi la uanzishaji wa mfumo wa anuani mpya za kitaifa lilifanyika katika Manispaa ya Dodoma Kata za: Kiwanja cha ndege, Uhuru, Makole, Viwandani, Uhindini, Tambukareli na Kilimani. Vilevile, utekelezaji unatarajiwa kuendelea katika maeneo ya Ilala, Temeke, Zanzibar na Moshi kulingana na upatikanaji wa fedha. Kukamilika kwa mradi wa Anuani za Makazi na simbo za Posta kutasaidia: Kurahisisha ukusanyaji wa kodi mbalimbali za Serikali; Utambuaji wananchi kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA); Uandikishaji wapiga kura; Utoaji wa Vitambulisho vya Kitaifa; Usalama wa wananchi na mali zao; Ufikishaji wa huduma za jamii kama maji, umeme, mawasiliano, ugawaji misaada na bima; Huduma za dharura na uokoaji kama zima moto, magari ya wagonjwa, mafuriko; na Biashara na uchumi (huduma za benki, mahoteli, maduka makubwa).

## SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

**Uendelezaji wa utafiti wa kisayansi nchini**

357. Mwaka 2010, idadi ya taasisi na vituo vya utafiti vya umma vilivyoshirikishwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ilikuwa 87. Aidha, taasisi na vituo hivyo zilihusisha sekta zifuatazo: kilimo (18), mifugo na uvuvi (10), viwanda na nishati (8), maliasili (10), afya (8), vyuo vikuu (33). Mwaka 2010, jumla ya taasisi 11 za sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali hapa nchini yaliingia kwenye shughuli za utafiti. Pia Serikali iliwezesha kufanyika kwa tafiti tisa katika maeneo ya Afya na Lishe, Mazingira na Maliasili, Teknolojia mpya na zinazoibukia, Kilimo, Mifugo, na Nishati.

**Masijala ya Utafiti Tanzania**

358. Mwaka 2010, watafiti 250 kutoka nje ya nchi walisajiliwa na kupatiwa hati za kufanya tafiti nchini katika maeneo ya wanyama pori, afya, jiografia, historia, siasa, uchumi, teknohama, sanaa, lugha, kilimo, watu wa kale, na ualimu. Watafiti hao walitoka Marekani, Uingereza, Japani na nchi nyingine za Ulaya. Aidha, tafiti hizo zilifanyika zaidi katika sekta ya wanyama pori, afya, sayansi ya jamii na sanaa.

**Uendelezaji wa Rasilimali Watu**

359. Mwaka 2010, Taasisi za Ufundi na Teknolojia za Dar es saalam na Mbeya kwa ujumla ziliongeza udahili wa Wanafunzi kutoka 3,414 mwaka 2009, hadi kufikia wanafunzi 4,515, sawa na ongezeko la asilimia 32. Aidha, ujenzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela- Arusha unaendelea kwa kukamilisha ukarabati wa majengo ya iliyokuwa CARMATEC huko Tengeru Arusha.

**Udhibiti wa Mionzi**

360. Mwaka 2010, Tume ya Nguvu za Atomiki ilikagua vituo 106 vya X-Ray, kati ya vituo 150 vinavyotoa huduma ya mionzi ayonisha ikilinganishwa na vituo 96, kati ya vituo 150 vya X-Ray vilivyokaguliwa mwaka 2009, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.4. Aidha, mwaka 2010, wafanyakazi 1,180 katika vituo hivyo walipimwa viwango vya mionzi (Personnel Dosimetry Service), ikilinganishwa na wafanyakazi 668 waliopimwa mwaka 2009 sawa na ongezeko la asilimia 76.6. Viwango vya Mionzi kwa wafanyakazi wote vilionyesha kuwa kuna usalama wa sehemu za kazi kwa ujumla.

361. Mwaka 2010, upimaji wa vyanzo vya mionzi katika sampuli 4,564 za vyakula na mbolea ulifanyika na kuzitolea vibali (leseni) ikilinganishwa na sampuli 689 za vyakula na mbolea vilivyopimwa mwaka 2009. Pia, mwaka 2010 upimaji wa vyanzo vya mionzi katika vituo 26 vilipimwa, kama ilivyokuwa mwaka 2009. Aidha, mwaka 2010, minara 70 ya simu za viganjani ilifanyiwa ukaguzi wa kiwango cha mionzi isiyoayonisha (non-ionizing radiation), ikilinganishwa na minara 90 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 22.2.

Jedwali Na. 67

## SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| Maelezo | Kipimo | 2000 | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli | kms. | 2721 | 2721.5 | 2721.5 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 |
| Magari ya Moshi: | Namba | 81 | 81 | 77 | 103 | 103 | 99 | 99 | 84 | 45 | 43 | 25 |
| Mvuke | Namba | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| Dizell | Namba | 80 | 80 | 76 | 102 | 102 | 98 | 98 | 83 | 45 | 0 | 0 |
| Mainlain | | - | - | - | 77 | 77 | 73 | 73 | 62 | 5 | 5 | 21 |
| Shunting | | - | - | - | 25 | 25 | 25 | 25 | 21 | 40 | 38 | 4 |
| Jumla ya mabehewa: | Namba | 1472 | 1478 | 1479 | 1779 | 1592 | 1951 | 1828 | 1912 | 1648 | 1357 | 1071 |
| Abiria | Namba | 91 | 97 | 98 | 82 | 83 | 82 | 54 | 102 | 45 | 68 | 50 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 1148 | 1104 | 1104 | 1104 | 1104 | 1464 | 1369 | 1369 | 1190 | 1093 | 648 |
| Mafuta | Namba | 164 | 164 | 164 | 164 | 164 | 164 | 164 | 208 | 244 | 178 | 179 |
| Mifugo | Namba | 51 | 51 | 51 | 69 | 69 | 69 | 69 | 76 | 18 | 39 | 88 |
| Mengineyo | Namba | 18 | 62 | 62 | 360 | 172 | 172 | 172 | 157 | 151 | 105 | 106 |
| Uchukuzi | Namba | | | | | | | | | | | |
| Abiria | 000 | - | 728 | 685 | 666 | 464 | 514 | 594 | 524 | 392 | 285 | 284 |
| Mizigo | Tani'000 | - | 1351 | 1446 | 1443 | 1002 | 1169 | 775 | 714 | 429 | 237 | 265 |

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

## RELI YA UHURU - TAZARA

Jedwali Na. 68

| Maelezo | Kipimo | 2000 | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli Kuu | Km | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 |
| Magari ya Moshi | Namba | 89 | 89 | 21 | 22 | 58 | 58 | 21 | 19 | 10 | 16 | 15 |
| Reli Kuu | Namba | 44 | 75 | 14 | 15 | 42 | 42 | 15 | 14 | 8 | 11 | 10 |
| Ya kuongeza | Namba | 14 | 14 | 7 | 7 | 16 | 16 | 6 | 5 | 2 | 5 | 5 |
| Mabehewa ya abiria | Namba | 128 | 128 | 67 | 60 | 75 | 75 | 66 | 71 | 62 | 53 | 36 |
| Abiria | Namba | 102 | 102 | 106 | 102 | 61 | 61 | 52 | 59 | 53 | 44 | 31 |
| Chakula | Namba | 14 | 14 | 6 | 5 | 5 | 5 | 6 | 8 | 4 | 3 | 2 |
| Vifurushi | Namba | 13 | 12 | 9 | 8 | 9 | 9 | 8 | 4 | 5 | 6 | 3 |
| Mabehewa ya mizigo | Namba | 2225 | 2220 | 2110 | 1401 | 1556 | 1518 | 1455 | 1458 | 1371 | 1412 | 1620 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 1446 | 1948 | 2019 | 1088 | 1354 | 1364 | 1297 | 1295 | 1217 | 1174 | 1381 |
| Mifugo | Namba | 28 | 24 | 5 | 2 | 2 | 16 | 20 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Mafula | Namba | 209 | 114 | 82 | 103 | 83 | 81 | 72 | 81 | 114 | 196 | 197 |
| Barafu | Namba | 20 | 20 | 4 | 4 | 3 | 8 | 3 | 10 | 4 | 7 | 7 |
| Mengineyo | Namba | 93 | 2 | - | 148 | 22 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |
| Breki | Namba | 73 | 64 | 64 | 15 | 64 | 26 | 44 | 46 | 17 | 16 | 16 |
| Balast | Namba | 56 | 48 | 28 | 45 | 28 | 21 | 17 | 18 | 17 | 17 | 17 |
| Uchukuzi mizigo (Tani) | 000 | 638 | 558 | 677 | 147 | 298 | 470 | 555 | 569 | 525 | 333 | 540 |
| Abiria | 000 | 1609 | 1262 | 1212 | 261 | 390 | 611 | 1063 | 1000 | 1177 | 923 | 758 |

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru - TAZARA

+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini Tanzania

## USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 69

| Maelezo | Kipimo | 2000 | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 5232 | 3676 | 3120 | 2350 | 2898 | 3895 | 4154 | 3038 | 697 | 1842 | 1274 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 3425 | 1013 | 4011 | 4285 | 5848 | 11506 | 18257 | 16588 | 7260 | 17472 | 18721 |
| Jumla ya abiria | 000 | 551 | 479 | 516 | 648 | 525 | 1072 | 664 | 714 | 310 | 141 | 228 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000wt | 2860 | 4193 | 4514 | 5346 | 4179 | 4307 | 6320 | 5703 | 2316 | 4946 | 4954 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000wt | 2864 | 3422 | 3627 | 4416 | 3390 | 3599 | 5292 | 4932 | 2136 | 4382 | 4559 |
| Za kawaida | 000wt | 1230 | 1562 | 2022 | 2650 | 1928 | 2107 | 3164 | 2762 | 1053 | 2430 | 2159 |
| Saruji | 000wt | 380 | 286 | - | - | - | 0 | 0 | 0 | 0 | 1852 | 0 |
| Mafuta | 000wt | 1126 | 1445 | 1402 | 1696 | 1382 | 1311 | 1909 | 2054 | 1013 | 100 | 2400 |
| Mengineyo1 | 000wt | 128 | 129 | 203 | 70 | 80 | 181 | 219 | 116 | 70 | 565 | 0 |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000wl | 576 | 664 | 717 | 930 | 623 | 708 | 1027 | 761 | 181 | 466 | 466.1 |
| Za kawaida | 000wl | 538 | 624 | 664 | 848 | 581 | 654 | 971 | 713 | 153 | 24 | 419 |
| Mafuta | 000wt | 38 | 40 | 53 | 82 | 32 | 35 | 34 | 48 | 28 | 7 | 47 |
| Mengineyo1 | 000wt | - | - | - | - | 10 | 19 | 22 | 0 | 0 | 68 | 0 |
| Mabadilishano | 000wl | 27 | 20 | 168 | 253 | 251 | 308 | 371 | 126 | - |  | 0.1 |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, mollasses, tallow fats n.k

\- Takwimu hazikupatikana

## USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

| Maelezo | Kipimo | 2000 | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 111 | 118 | 186 | 234 | 185 | 215 | 281 | 242 | 95 | 144 | 215 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 953 | 430 | 264 | 258 | 440 | 628 | 964 | 551 | 133 | 671 | 1059 |
| Jumla ya abiria | 000 | 7 | 0.7 | 0.5 | 2.7 | 4 | 6.4 | 6.6 | 7.1 | 8.3 | 0 | 0 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000wt | 168 | 194 | 201 | 259 | 162 | 289 | 519 | 542 | 178 | 359 | 529 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000wt | 80 | 108 | 104 | 118 | 127 | 165 | 307 | 330 | 836 | 213 | 357 |
| Zakawaida | 000wt | 68 | 79 | 81 | 93 | 113 | 111 | 195 | 242 | 817 | 147 | 313 |
| Mafuta | 000wt | 12 | 29 | 22 | 25 | 14 | 54 | 112 | 88 | 19 | 66 | 44 |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000wt | 88 | 84 | 97 | 141 | 104 | 134 | 212 | 212 | 66 | 145 | 171 |
| Zakawaida | 000wt | 88 | 84 | 97 | 141 | 104 | 134 | 212 | 212 | 66 | 145 | 171 |
| Mafuta | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | | 0 |
| Mabadilishano | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

## USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

| Maelezo | Kipimo | 2000 | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 203 | 136 | 194 | 138 | 85 | 215 | 281 | 99 | 36 | 32 | 58 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 465 | 264 | 392 | 263 | 106 | 628 | 964 | 251 | 131 | 31 | 455 |
| Jumla ya abiria | 000 | 63 | 36 | 62 | 33 | 10 | 6.4 | 6.6 | 10 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000 | 176 | 175 | 177 | 141 | 169 | 289 | 519 | 112 | 82 | 95 | 107 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000wt | 81 | 61 | 78 | 70 | 44 | 165 | 307 | 53 | 26 | 23 | 39 |
| Za kawaida | 000wt | 57 | 40 | 57 | 59 | 30 | 111 | 195 | 47 | 22 | 23 | 36 |
| Mafuta | 000wt | 17 | 21 | 20 | 11 | 14 | 54 | 112 | 6 | 4 | 0 | 3 |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000wt | 96 | 109 | 99 | 71 | 75 | 134 | 212 | 59 | 56 | 72 | 68 |
| Za kawaida | 000wt | 96 | 109 | 99 | 71 | 75 | 134 | 212 | 59 | 56 | 72 | 68 |
| Mafuta | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mabadilishano | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

## HUDUMA ZA POSTA

EDWALI Na. 70

| Maelezo | Kipimo | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi ndogo Posta | Namba | 190 | 149 | 139 | 136 | 162 | 162 | 167 | 202 | 171 |
| Franchised Post Offices | Namba | 83 | 83 | 91 | 92 | 91 | 86 | 113 | 81 | 81 |
| Ofisi kamili | Namba | 151 | 154 | 157 | 157 | 129 | 113 | 172 | 170 | 170 |
| Jumla | Namba | 424 | 386 | 387 | 385 | 382 | 361 | 452 | 453 | 422 |
| Masanduku binafsi | 000 | 305.076 | 168881 | 171 7 | 171.8 | 172 | 173 | 173 5 | 117 | |
| Masanduku yaliyokodishwa | 000 | 137 467 | 143691 | 1480 | 147.5 | 146 | 150 | 130 2 | 87 2 | 120 3 |
| Masambi yasiyotimizwa | 000 | 0 129 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 4 1 | 0 |
| Mifuko pe kee iliyokodishwa | Namba | 222 | 215 | 222 | 214 | 203 | 217 | 182 | 62 | 183 |
| Barua zilizotumwa bila vifurushi | Mill | 2504 | 213 | 25 2 | 0 | 28 1 | 23.7 | 15 | 14 | 29 2 |
| Nchini | Mill | | | 20 1 | | 19 9 | 16 9 | 9 8 | 14 | 18 7 |
| Nje ya nchi | Mill | | | 5.1 | | 8 2 | 6.8 | 5 2 | | 10.5 |
| Regista na barua za amana | 000 | 356 561 | 450066 | 562.8 | 488.7 | 1003 | 530 | 306.9 | 377 | 480.4 |
| Nchini | 000 | | | | | 915 | 452 | 146.5 | 0 | 305 |
| Nje ya nchi | 000 | | | | | 40 | 37 | 136 2 | 0 | 154 |
| Vifurushi nchini | 000 | 31 976 | 29442 | 43 3 | 484 | 36 | 29 | 18 | 8.6 | 14 6 |
| Vifurushi vya nje | 000 | 5 76 | 6699 | 7 9 | 6.6 | 12 | 12 | 6 2 | 2 | 6.8 |
| Leseni za kuuza stamp | Namba | 10767 | 11100 | 10113 | 10099 | 12824 | 6324 | 6242 | 6256 | 25145 |
| Huduma za haraka, barua na vifuru | " | | | | | | | | | |
| Ndani ya nchi | " | 260486 | 309736 | 247268 | 297061 | 312110 | 262381 | 216762 | 493709 | 283711 |
| Nje ya nchi | " | 19675 | 29409 | 30693 | 37331 | 36930 | 12289 | 14650 | 4012 | 18766 |
| EMS Money Fax | " | 188790 | 216710 | 259449 | 300357 | 533821 | 379084 | 366 382 | 23165 | 82002 |
| EMS Fax (Fax message received) | " | 4440 | 16112 | 22394 | 22968 | 23328 | 14659 | 121901 | 103558 | 31594 |
| Overnight Mail Services | " | | | | | | | | | |
| Mifuko ya barua iliyosafirishwa | " | 53572 | 70170 | 71199 | 70066 | 101486 | 75900 | 85595 | 65912 | 76983 |
| vifurushi vya magazeti vilivyosafirs | " | 81477.9 | 21992 | 20204 | 21692 | 28753 | 20314 | 12754 | 13934 | 2752 |
| Huduma za gari ndogo | | | | | | | | | | |
| Jumla ya barua zilizosafirishwa | " | 8555 | 6567 | 5337 | 5993 | 3690 | 6542 | 4328 | 268 | 0 |
| Amana za haraka zilizotolewa | " | 284495 | 251685 | 218937 | 207997 | 210440 | 214558 | 0 | 20057 | 8169 |
| Amana za haraka zilizolipwa | | 216961 | 271924 | 224630 | 147020 | 233325 | 132080 | 93508 | 23069 | 11881 |
| Amana za haraka za nje ya nchi: | | | | | | | | | | |
| Zilizotumwa | " | 2210 | 1393 | 1602 | 1586 | 1788 | 1519 | 1354 | 1030 | 1027 |
| Zilizopokelewa | " | 1605 | 1061 | 1202 | 1001 | 1105 | 686 | 671 | 150 | 150 |
| Amana za posta zilizotolewa | " | 28683 | 16445 | 12714 | 8277 | 8029 | 9152 | 8062 | 8831 | 1924 |
| Amana za posta zilizolipwa | " | 25643 | 15113 | 12653 | 7565 | 7639 | 4615 | 5709 | 5480 | 3262 |
| Savings Bank Transactions | | | | | | | | | | |
| Uwekaji amana (Deposit) | " | 173304 | 144156 | 102288 | 66885 | 42255 | 25382 | 24574 | 9535 | 18863 |
| Uchukuaji amana (Withdrawal) | " | 157532 | 132538 | 89517 | 55392 | 32294 | 19534 | 21122 | 11663 | 23025 |

Chanzo: Shirika la Posta

## KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA (ATCL)*

Jedwali Na.73

| Maelezo | Kipimo | 2000 | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tani-Kilometa: | | | | | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 000 | 53207 | 47631 | 40524 | 28023 | 91769 | 33198 | 42627 | 32533 | - | 5313 | 9482 |
| Zilizotumika | 000 | 21289 | 19843 | 17258 | 11351 | 58579 | 18121 | 22085 | 18480 | - | 1508 | 2888 |
| Matumizi | % | 40.0 | 41.7 | 42.6 | 41.0 | 47.25 | 54.6 | 51.8 | 56.7 | - | 28.4 | 30.5 |
| Vitikilometa: | | | | | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 000 | 419419 | 393098 | 317522 | 238618 | 343250 | 334427 | 365265 | 306461 | 469426 | 41396 | 59724 |
| Vilivyotumika | 000 | 197749 | 182101 | 163597 | 123433 | 164563 | 185085 | 221307 | 190006 | 129000 | 16469 | 30527 |
| Matumizi | % | 47.1 | 46.3 | 51.5 | 51.7 | 47.9 | 55.3 | 60.6 | 62.0 | 27.5 | 39.8 | 51.1 |
| Abiria ++ | 000 | 195 | 177 | 137 | 157 | 271 | 197 | 224 | 190 | 188 | 27 | 41 |
| Mizigo ya ziada | Tani | NA | NA | NA | NA | NA | NA | NA | 103 | 30 | 9 | 8 |
| Mizigo mingine | Tani | 3100.6 | 13864 | 2232.6 | 1379 | 1506 | 1200 | 1502 | 1323 | 1044 | 54 | 145 |
| Shehena za Posta | Tani | 252.2 | 2843 | 161.93 | 82 | 235 | 214 | 299 | 241 | 162 | 11 | 30 |

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

\+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria [illegible]

NA Takwimu [illegible]

SURA YA 17

NISHATI

**wango cha Ukuaji**

2. Mwaka 2010, shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilikua kwa ilimia 10.2, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.4 mwaka 2009. Ukuaji u ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya gesi asili katika kuzalisha ieme na shughuli zingine. Mchango wa shughuli za kiuchumi za umeme na si katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.8 mwaka 2010, ikilinganishwa na ilimia 1.7 mwaka 2009.

**ieme**

3. Umeme ullozalishwa katika Grid ya Taifa mwaka 2010 ulikuwa saa za gawati 3,625.36, ikilinganishwa na saa za Gigawati 3,279.95 zilizozalishwa vaka 2009. Kati ya hizo, umeme wa maji ulikuwa saa za Gigawati 2,701.07; umeme wa dizeli kwenye gridi ulikuwa saa za Gigawati 924.29. Umeme wa eli uliozalishwa nje ya Gridi ya Taifa katika mwaka 2010 ulikuwa saa za gawati 78.85, ikilinganishwa na saa za Gigawati 68.86 mwaka 2009. Aidha, ieme ulionunuliwa kutoka nchi jirani mwaka 2010 ulikuwa saa za Gigawati 16 ikilinganishwa na saa za Gigawati 64.88 mwaka 2009. Vilevile, umeme gesi asili uliozalishwa ulikuwa saa za Gigawati 1,688.81 na umeme ozalishwa na wazalishaji binafsi ulikuwa saa za Gigawati 1,563.96.

4. Mwaka 2010, upotevu wa umeme ulikuwa saa za Gigawati 1,686 kama yokuwa mwaka 2009. Aidha, wastani wa bei za umeme kwa saa za kilowati a mwaka 2010 ulikuwa shilingi 85.5, ikilinganishwa na shilingi 114.8 aka 2009. Aidha, mwaka 2010, mauzo ya umeme yalikuwa saa za Gigawati .57 zenye thamani ya shilingi bilioni 470.584, ikilinganishwa na saa za awati 4,687 zenye thamani ya shilingi bilioni 413.501 mwaka 2009, sawa ongezeko la asilimia 13.8.

Jedwali Na. 74

| Kituo | 2007 | | 2008 | | 2009 | | 2010* | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uwezo MW | Uzalishaji GWh | Uwezo MW | Uzalishaji GWh | Uwezo MW | Uzalishaji GWh | Uwezo MW | Uzalishaji GWh |
| GRIDI YA TAIFA | | | | | | | | |
| Kidatu (Mtengeni) | 204.00 | 1026.65 | 204.0 | 1044.00 | 204.0 | 1005.63 | 204.0 | 1110.55 |
| Mtera | 80.00 | 371.97 | 80.0 | 341.02 | 80.0 | 450.65 | 80.0 | 433.31 |
| Hale Tanga | 21.00 | 60.25 | 21.00 | 67.18 | 21.0 | 47.05 | 21.0 | 48.00 |
| New Pangani | 68.00 | 302.46 | 68.0 | 301.95 | 68.0 | 105.61 | 68.0 | 202.99 |
| Nyumba ya Mungu (Hydro) | 8.00 | 17.07 | 8.0 | 25.66 | 8.0 | 35.55 | 8.0 | 39.17 |
| Kihansi | 180.00 | 855.00 | 180.0 | 543.15 | 180.0 | 945.62 | 180.0 | 867.52 |
| Uwemba Mini Hydro | | | | 2.87 | 0.8 | 3.00 | 0.8 | 3.00 |
| Jumla Hydro | 561.00 | 2512.39 | 561.0 | 2045.87 | 561.8 | 2616.50 | 561.8 | 2703.36 |
| | | | | | | | | |
| Umeme Diesel | 36.37 | 0.03 | 36.37 | 0.00 | 34.77 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Umeme GTS | | | | | | | | |
| Umeme wa Wartsila | | | | 266.07 | 104.30 | 670.11 | 100.00 | 1668.3 |
| Tegeta Wartsila | | | | | 45.00 | 12.51 | 45.05 | 243.31 |
| Dodoma (Zuzu) | 7.44 | 0.02 | 7.44 | 2.18 | 7.44 | 2.12 | 7.44 | 1.07 |
| Mbeya (Iyunga) | 13.00 | 0.01 | 13.00 | 6.00 | 13.00 | 0.00 | 13.00 | 0.00 |
| Musoma | 2.56 | | 2.56 | | 2.56 | 0.00 | 2.56 | 0.00 |
| Mwanza (Nyakato) | 12.50 | - | 12.50 | - | 12.50 | 0.00 | 12.50 | 0.00 |
| Tabora | 10.20 | 0.05 | 10.20 | 0.01 | 10.20 | 0.00 | 10.20 | 0.00 |
| Jumla Thermal | 80.97 | 11.44 | 80.97 | 886.06 | 229.38 | 650.35 | 190.25 | 914.07 |
| | | | | | | | | |
| JUMLA GRIDI | 641.97 | 2552.85 | 641.97 | 2917.03 | 791.18 | 3300.35 | 752.05 | 3615.01 |
| | | | | | | | | |
| MITAMBO MINGINE - ISOLATED STATIONS | | | | | | | | |
| Bukoba | 2.56 | 0.10 | 2.56 | 0.00 | 2.56 | 0.12 | 2.56 | 0.15 |
| Kigoma | 6.11 | 14.70 | 6.11 | 17.82 | 6.25 | 15.10 | 6.22 | 20.22 |
| Kilwa Masoko | 1.24 | 2.16 | 1.24 | 2.24 | 1.30 | 2.49 | 1.50 | 1.10 |
| Lindi | 2.28 | 5.41 | 2.28 | 11.04 | 0.00 | 0.00 | 0.00 00 | 0.00 |
| Mafia | 0.55 | 2.87 | 0.85 | 2.15 | 0.85 | 2.01 | 0.55 | 2.70 |
| Masasi | 3.50 | 0.58 | 3.80 | 0.00 | 1.14 | 0.00 | 1.11 | 0.10 |
| Njombe | 1.25 | 1.24 | 1.28 | | 1.28 | 0.00 | 1.25 | 0.00 |
| Songea | 5.02 | 15.08 | 5.02 | 17.15 | 6.43 | 16.35 | 6.01 | 15.16 |
| Sumbawanga | 3.14 | | 3.14 | | 1.50 | 0.00 | 1.50 | 0.00 |
| Mtwara | 3.02 | 4.91 | 1.92 | 3.95 | 1.60 | 1.32 | 1.66 | 0.90 |
| Ikwiriri | 0.65 | 1.67 | 0.85 | 1.77 | 0.85 | 2.10 | 0.55 | 2.52 |
| Tunduru | 0.70 | 2.57 | 0.70 | 1.81 | 2.00 | 2.35 | 2.01 | 3.75 |
| Mpanda | 1.30 | 10.50 | 3.30 | 13.74 | 3.30 | 13.31 | 3.50 | 10.12 |
| Liwale | 0.75 | 1.00 | 0.75 | 1.31 | 0.10 | 1.32 | 0.61 | 0.57 |
| Ngara | 0.05 | 1.05 | 1.05 | 2.17 | 0.05 | 2.58 | 3.05 | 2.25 |
| Biharamulo | 0.08 | 2.28 | 0.65 | 2.02 | 0.00 | 3.42 | 0.45 | 3.16 |
| Mbinga | | | | 1.14 | 2.30 | 2.14 | 2.26 | 3.10 |
| Ludewa | | | | 0.16 | 1.28 | 0.05 | 1.18 | 0.82 |
| JUMLA MITAMBO MINGINE | 35.45 | 72.61 | 38.45 | 68.22 | 31.63 | 68.81 | 36.61 | 78.81 |
| | | | | | | | | |
| JUMLA KUU - TANESCO | 681.42 | 2563.53 | 681.42 | 2956.25 | 827.81 | 3359.03 | 788.66 | 3694.72 |
| | | | | | | | | |
| KUTOKA VYANZO VINGINE (Umenunuliwa) | | 1689.17 | | 1440.12 | | 1440.04 | | 1843.50 |
| | | | | | | | | |
| JUMLA YA UMEME ULIOTENGENEZWA | | 4284.40 | | 4445.37 | | 4801.07 | | 5535.74 |

[illegible]
[illegible]
[illegible]
* Zanzibar (Projection)

## MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI

Jedwali Na. 75

(Mill. KWH)

| Mwaka | Tanzania Bara | | | Zanzibar | Jumla | Umeme Uliopotea | Jumla ya Umeme Uliotengenezwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Taa za Mitaani | Matumizi ya Nyumbani | Biashara na Viwanda | | | | |
| 2001 | 0.55 | 980 | 965 | 127 | 2073 | 675 | 2748 |
| 2002 | 0.10 | 1108 | 1085 | 133 | 2326 | 464 | 2790 |
| 2003 | 0.04 | 1029 | 1257 | 145 | 2431 | 232 | 2663 |
| 2004 | 0.05 | 1131 | 1419 | 161 | 2711 | 40 | 2751 |
| 2005 | 0.03 | 900 | 1519 | 185 | 2604 | 544 | 3148 |
| 2006 | 0.09 | 871 | 1593 | 204 | 2668 | 924 | 3592 |
| 2007 | 0.01 | 1420 | 1459 | 231 | 3288 | 917 | 4205 |
| 2008 | 0.01 | 1647 | 1722 | 229 | 3598 | 827 | 4425 |
| 2009 | 0.01 | 1432 | 1498 | 186 | 3116 | 1686 | 4802 |
| 2010 | 0.01 | 1671 | 2247 | 174 | 4092 | 1046 | 5138 |

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)
MW Megawatt
GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH
* Za Awali (Provisional)

## MAUZO YA UMEME KWA MIKOA

Jedwali Na. 76

(GWH)

| Mkoa | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 46 | 48 | 49 | 59 | 68 | 79 | 83 |
| Arusha | 194 | 202 | 193 | 223 | 296 | 236 | 269 |
| Manyara | | | | | 14 | 17 | 19 |
| Kilimanjaro | 101 | 102 | 96 | 110 | 109 | 88 | 124 |
| Tanga | 143 | 156 | 154 | 165 | 169 | 166 | 209 |
| Morogoro | 86 | 113 | 107 | 119 | 136 | 121 | 179 |
| Coast & | | | | | 104 | 94 | 106 |
| Dar-es-Salaam | 1263 | 1110 | 1136 | 1574 | 1641 | 1200 | 1789 |
| Lindi | 10 | 10 | 12 | 12 | 11 | 11 | 13 |
| Mtwara | 19 | 20 | 20 | 29 | 23 | 29 | 27 |
| Ruvuma | 13 | 13 | 13 | 14 | 15 | 15 | 21 |
| Iringa | 59 | 60 | 61 | 79 | 79 | 85 | 101 |
| Mbeya | 105 | 95 | 99 | 109 | 115 | 125 | 139 |
| Singida | 15 | 18 | 46 | 28 | 18 | 26 | 26 |
| Tabora | 111 | 67 | 71 | 37 | 98 | 84 | 97 |
| Rukwa | 9 | 9 | 11 | 12 | 11 | 12 | 17 |
| Kigoma | 13 | 9 | 12 | 10 | 12 | 12 | 16 |
| Shinyanga | 174 | 176 | 177 | 195 | 196 | 253 | 313 |
| Kagera | 20 | 28 | 35 | 36 | 37 | 33 | 44 |
| Mwanza | 127 | 136 | 132 | 151 | 173 | 192 | 215 |
| Mara | 42 | 47 | 40 | 95 | 44 | 52 | 110 |
| Jumla Tanzania B | 2550 | 2419 | 2464 | 3057 | 3369 | 2930 | 3917 |
| | | | | | | | |
| Zanzibar | 161 | 185 | 204 | 231 | 229 | 186 | 174 |
| | | | | | | | |
| JUMLA | 2711 | 2604 | 2668 | 3288 | 3598 | 3116 | 4091 |

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)
MW Megawatt
GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH
* Za Awali (Provisional)

### Utafutaji Mafuta na Gesi

365. Mwaka 2010, mikataba hai ya utafutaji mafuta ilikuwa 22. Aidha, uchukuaji wa takwimu za mitetemo (seismic surveys) pamoja na uchimbaji wa visima vya utafutaji ulifanyika katika maeneo ya Mkuranga, Mtwara na Songo Songo. Katika utafutaji huo, jumla ya visima 17 vilichimbwa katika maeneo yafuatayo: Mtwara/Mnazi Bay- visima vinne; Songo Songo- visima vitatu; Mkuranga- visima vitatu; baharini kwenye kina kirefu- visima vitatu; Lindi (Mandawa) - visima viwili; Rufiji - kisima kimoja; na Mafia - kisima kimoja . Kufuatia uchimbaji huo, maeneo yafuatayo yamegundulika kuwa na gesi: Mkuranga, Nyuni (Songo Songo) na baharini kwenye kina kirefu mashariki mwa kisiwa cha Mafia na mashariki ya mji wa Mtwara .

### Bei za Mafuta

366. Jumla ya mahitaji ya mafuta kwa mwaka 2010 ilikuwa mi tani 1.7 millioni. Bei za mafuta ghafi (crude oil) katika soko la Dunia kwa mwaka 2010 ilikuwa wastani wa Dola za Kimarekani 86 kwa pipa ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 60 kwa pipa mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 43.3. Aidha, bei ya mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia ilikuwa ni wastani wa Dola za Kimarekani 770 kwa pipa kwa mafuta ya petrol, 695 kwa dizeli na Dola 733 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 541.3, 458.2 na 496.1 mwaka 2009, kwa mtiririko huo. Bei za mafuta hapa nchini kwa mwaka 2010 zilikuwa wastani wa shilingi 1,550 kwa lita moja kwa mafuta aina ya dizeli, shilingi 1,600 kwa petroli na shilingi 1,150 kwa mafuta ya Taa.

## NISHATI MBADALA

### Maporomoko Madogo ya Maji

367. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kuratibu shughuli za uhamasishaji na uendelezaji wa vyanzo vya umeme wa maporomoko ya maji. Vyanzo vya uzalishaji wa umeme wa maporomoko madogo ya maji vilibainishwa katika mikoa ya Iringa, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Kagera, na Tanga. Utafiti wa awali

unaonesha kuwa vyanzo hivyo vinaweza kuzalisha kiasi cha jumla ya MW 390 za umeme.

**Umeme wa jua**

368. Mwaka 2010, mifumo ya umeme nuru ya maonesho ilifungwa katika shule za Sekondari kumi na mbili (12) na vituo vya afya 77 katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, jumla ya mafundi 200 na wafanyabiashara wa umeme nuru 120 walipata mafunzo ya ufundi na biashara na wanatoa huduma za umeme nuru katika mikoa iliyotajwa. Matumizi ya umeme nuru yameweza kupunguza uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na hewa ya ukaa inayotokana na matumizi ya petroli, dizeli na mafuta ya taa.

**Jotoardhi na Biofueli**

369. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kuandaa mazingira ya uendelezaji endelevu wa biofueli ili kutumia fursa zilizopo na kuhakikisha kwamba uendelezaji wa biofueli unafanyika bila kuleta athari hasi kwa wananchi, mazingira, bioanuai, misitu, na upatikanaji wa chakula. Aidha, makampuni mawili yalijitokeza kuwekeza kwenye biofueliambayo ni AgroEcoenergy Tanzania Ltd ya Uswidi kwa ajili ya ulimaji wa miwa; na Envirovest ya Mauritius kwa ajili ya kilimo cha michikichi. Vile vile, kwa upande wa biodizeli, makampuni kama Diligent Tanzania Ltd (Arusha); Prokon Renewable Energy (Rukwa); Kakute (Arusha); Sunbiofuel (Pwani); na Jatropha Tanzania Ltd (Arusha) yaliendeleza teknolojia hii kwa kutumia mbegu za mibono kaburi.

# SURA YA 18

## MAJI

### Utangulizi

370. Usimamizi wa rasilimali za maji, utafiti na ufuatiliaji wa vyanzo vya maji uliendelea nchini kote mwaka 2010. Utafiti wa kutambua vyanzo vya maji katika mabonde saba uliendelea ambapo vyanzo vitano vya maji na visima vya maji 1,216 vilitambuliwa kwa lengo la kuratibu matumizi sahihi ya maji. Maeneo 155 katika mabonde yote saba yalitambuliwa kwa ajili ya kuchimba visima vya maji. Aidha, jumla ya hati 63 za haki ya kutumia maji zilitolewa kwa wakulima na vikundi vya watumia maji.

371. Mwaka 2010, sampuli 1,648 kutoka vyanzo mbalimbali vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani vilikusanywa na kufanyiwa utafiti wa kimaabara ikilinganishwa na sampuli 3,569 mwaka 2009. Kati ya hizo, sampuli 1,461, sawa na asilimia 88.7 zilikuwa na viwango vinavyokubalika kwa matumizi ya binadamu. Aidha, sampuli 213 za majitaka toka viwandani na mitambo ya kusafishia maji zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara katika miji ya Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Morogoro, Musoma, Mwanza na Tanga. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa, sampuli 195, sawa na asilimia 91.5 yalikidhi viwango vya kutupwa kwenye mazingira.

372. Mwaka 2010, uhakiki wa ubora wa maji kutoka vyanzo mbalimbali kwenye mabonde ya maji ulifanyika ambapo sampuli 825 za maji zilikusanywa. Kati ya hizo, 605 zilikusanywa kutoka katika mito, 200 kutoka kwenye maziwa, na 20 zilichukuliwa kwenye mabwawa. Matokeo yalionesha uchafuzi wa vyanzo vya maji ulitokana na vijidudu, mtibuko wa matope na masimbi yenye athari kwa viumbe hai na miundombinu. Hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kukabiliana na uchafuzi huo kwa kutumia sheria za maji na sheria ndogo za halmashauri.

### Huduma ya Maji Vijijini

373. Mwaka 2010, miradi 333 ya kusambaza maji vijijini ilikamilika, kati ya hiyo 221 ilijengwa na miradi 112 ilikarabatiwa. Miradi hiyo iliwezesha kuwepo

kwa vituo 1,169 vya kuchotea maji ambavyo viliwawezesha wanavijiji 416,250 kupata huduma ya maji safi na salama. Katika utekelezaji wa programu ya maji vijijini na usanifu mazingira, jumla ya wanavijiji 931,408 walielimishwa na kuhamasishwa kuhusu usafi wa mazingira. Vilevile, vyoo bora vya shimo 763 vilijengwa na kukamilika ikilinganishwa na vyoo 599 mwaka 2009.

374. Idadi ya wananchi wa vijijini waliopata huduma ya maji iliongezeka kutoka wanavijiji 19,685,659 mwaka 2009, hadi kufikia 20,545,945 mwaka 2010. Wananchi waliopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini mwaka 2010 ilikuwa asilimia 57.8, ikilinganishwa na asilimia 58.7 mwaka 2009. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa utekelezaji wa miradi midogo ya maji kutokana na maandalizi ya utekelezaji wa miradi mikubwa katika wilaya ambazo ziko chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

**Huduma za Maji Mijini**

375. Mwaka 2010, uzalishaji wa maji mijini uliongezeka hadi mita za ujazo milioni 116.5, kutoka mita za ujazo milioni 109.7 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Katika kipindi cha mwaka 2010, Mamlaka za Maji 19 za miji mikuu ya mikoa ziliweza kutoa huduma ya maji kwa watu 3,523,335 kati ya watu 3,962,650, ikilinganishwa na watu 3,167,054 kati ya watu 3,649,600 mwaka 2009, wanaoishi kwenye mamlaka hizo.

376. Hadi kufikia Desemba 2010, idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika miji mikuu ya mikoa ilikuwa asilimia 86.1, miji mikuu ya wilaya asilimia 53.0 na jiji la Dar es Salaam asilimia 55.0. Kiwango kidogo cha utoaji huduma ya maji katika jiji la Dar es Salaam kilitokana na ongezeko kubwa la wakazi lililopelekea mahitaji zaidi ya maji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na uchakavu wa miundombinu.

377. Mamlaka za maji katika miji mikuu ya mikoa zilikusanya shilingi bilioni 40.3 mwaka 2010, ikilinganishwa na shilingi bilioni 35.8 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Ongezeko hilo lilitokana na wateja wapya 261,770

waliounganishwa katika mfumo wa maji, ikilinganishwa na wateja wapya 244,422 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 7.1

**JUMLA YA VISIMA VILIVYOCHIMBWA MWAKA 2010**

Jedwali 78

| MKOA | IDADI YA VISIMA |
|---|---|
| Arusha | 57 |
| Kilimanjaro | 24 |
| Tanga | 8 |
| Manyara | 34 |
| Dodoma | 15 |
| Shinyanga | 135 |
| Singida | 74 |
| Tabora | 28 |
| Mtwara | 22 |
| Rukwa | 21 |
| Mbeya | 4 |
| Iringa | 5 |
| Morogoro | 32 |
| Dar es Salaam | 57 |
| Pwani | 10 |
| Kigoma | 11 |

Chanzo: Wizara ya kilimo, chakula na Ushirika

USAMBAZAJI WA MAJI KATIKA MIJI MIKUU YA MIKOA - 2010

Jedwali Na. 79

| Mamlaka | Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo) | Mapato (Tshs) |
|---|---|---|
| Arusha | 14,721,190 | 4,228,767,804 |
| Babati | 1,150,694 | 412,582,337 |
| Bukoba | 2,290,311 | 781,849,481 |
| Dodoma | 9,667,795 | 4,080,208,091 |
| Iringa | 4,229,160 | 2,129,065,911 |
| Kigoma | 3,117,511 | 502,410,725 |
| Lindi | 328,902 | 203,796,544 |
| Mbeya | 11,236,254 | 3,339,539,484 |
| Morogoro | 8,900,610 | 3,801,407,363 |
| Moshi | 9,102,782 | 3,102,872,040 |
| Mtwara | 1,659,664 | 972,731,617 |
| Musoma | 3,848,175 | 1,247,335,118 |
| Mwanza | 23,492,486 | 7,304,948,210 |
| Shinyanga | 3,491,099 | 1,506,671,775 |
| Singida | 1,527,053 | 500,960,728 |
| Songea | 2,361,703 | 734,974,362 |
| Sumbawanga | 1,763,680 | 402,940,915 |
| Tabora | 4,149,561 | 1,340,824,081 |
| Tanga | 9,513,697 | 3,696,449,819 |
| | **116,552,326.97** | **40,290,336,405.25** |

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

# SURA YA 19

## ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

**Elimu ya Awali**

378. Mwaka 2010, idadi ya wanafunzi katika elimu ya awali iliongezeka hadi 925,465, kutoka wanafunzi 896,146 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Kati ya hao, wavulana walikuwa 461,628 na wasichana 463,837. Idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ilikuwa 883,667, ambapo wavulana walikuwa 440,202 na wasichana 443,465. Idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 41,798, ambapo wavulana walikuwa 21,426 na wasichana 20,372. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za awali ulikuwa 1:71 mwaka 2010, ikilinganishwa na 1:52 mwaka 2009. Uwiano huu unaonesha kuwa ongezeko la idadi ya wanafunzi haliwiani na idadi ya walimu mwaka 2010. Kuongezeka kwa idadi ya uandikishwaji wa wanafunzi wa awali kulitokana na Sera ya Elimu ya kuhimiza kila shule ya msingi ya Serikali kuwa na madarasa ya Elimu ya awali; na wazazi wengi kuhamasika kuandikisha watoto wao kwenye elimu ya awali ambayo inatolewa bure.

**Elimu ya Msingi**

379. Mwaka 2010, idadi ya wanafunzi katika Elimu ya Msingi ilipungua hadi 8,419,305, kutoka wanafunzi 8,441,553 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 0.3. Kati yao wanafunzi 4,203,269 walikuwa wavulana, sawa na asilimia 49.9, wakati wasichana walikuwa 4,216,036 sawa na asilimia 50.1. Idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza ilipungua kutoka wanafunzi 1,358,790 mwaka 2009, hadi wanafunzi 1,356,574 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 0.2. Kushuka kwa idadi ya wanafunzi katika shule za msingi kulitokana na utekelezaji wa MMEM I uliopelekea kupungua kwa mrundikano wa uandikishaji wa wanafunzi.

380. Mwaka 2010, idadi ya shule za msingi za Serikali na zisizo za Serikali iliongezeka hadi shule 15,816, kutoka 15,727 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 0.6. Idadi ya shule za Serikali ilipungua, kutoka 15,301 mwaka 2009, hadi 15,265 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 0.24. Hii ilitokana na baadhi ya shule kupandishwa hadhi na kuwa shule za sekondari.

381. Kiwango cha jumla cha uandikishaji wa wanafunzi kilipungua hadi asilimia 106.4 mwaka 2010, kutoka asilimia 110.5 mwaka 2009. Vilevile, kiwango halisi cha uandikishaji kilipungua hadi asilimia 95.4 mwaka 2010, ikilinganishwa na asilimia 95.9 mwaka 2009. Idadi ya walimu katika shule za Serikali iliongezeka kutoka walimu 157,185 mwaka 2009, hadi walimu 165,856 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Wastani wa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi uliimarika kutoka 1:54 mwaka 2009, hadi 1:51 mwaka 2010. Aidha, kiwango cha kukatisha masomo kilishuka hadi asilimia 2.6 mwaka 2010, kutoka asilimia 3.7 mwaka 2009.

**Elimu ya Sekondari**

382. Idadi ya shule za sekondari katika mwaka 2010 iliongezeka hadi 4,266, kutoka shule 4,102 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 4.0. Kati ya hizo, shule 3,397 zilikuwa za Serikali na 869 zisizo za Serikali. Idadi ya shule za sekondari za Serikali iliongezeka, kutoka shule 3,283 mwaka 2009 hadi shule 3,397 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 3.5.

383. Idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari wa kidato cha kwanza hadi cha sita iliongezeka kutoka wanafunzi 1,466,402 mwaka 2009, hadi 1,638,699 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 11.7. Kati ya hao, wasichana walikuwa 728,528, sawa na asilimia 44.5 na wavulana walikuwa 910,171, sawa na asilimia 55.5, ikilinganishwa na wasichana 653,457 (asilimia 44.6) na wavulana 812,945 (asilimia 55.4) mwaka 2009. Ongezeko la wanafunzi katika shule za sekondari kwa mwaka 2010 lilitokana na hatua za makusudi za Serikali za kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anayefaulu elimu ya msingi anajiunga na elimu ya sekondari.

**Elimu ya Ualimu**

384. Mwaka 2010, idadi ya vyuo vya ualimu ilikuwa 92, ikilinganishwa na vyuo 77 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Kati ya hivyo, vyuo vya Serikali vilikuwa 34 na vyuo visivyo vya serikali 58. Idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu vya Serikali ilikuwa 25,814 mwaka 2010, ikilinganishwa na wanachuo 21,723 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 18.8. Kati ya wanachuo hao, wasichana walikuwa 11,236 (asilimia 43.5) na wavulana walikuwa 14,578 (asilimia 56.5). Katika mwaka 2010, wanachuo walichukua mafunzo katika ngazi zifuatazo: Elimu Maalumu wanachuo 458; Cheti 9,022; Stashahada (tarajali) 13,679; na Stashahada (mafunzo kazini) 2,655. Idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu visivyo vya serikali ilipungua kutoka wanachuo 13,648 mwaka 2009, hadi 10,834 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 20.6.

| Jedwali 19.1 IDADI YA WANAFUNZI WALIOANDIKISHWA KATIKA MWAKA 2009-2010 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO | 2009 | | | 2010 | | |
| **SHULE ZA AWALI** | Wavulana | Wasichana | Jumla | Wavulana | Wasichana | Jumla |
| Shule za Awali za Serikali | 422,893 | 428,191 | 851,084 | 440,202 | 443,465 | 883,667 |
| Shule za Awali zisizo za Serikali | 22.974 | 22,088 | 45,062 | 21,426 | 20,372 | 41,798 |
| | **445,867** | **450,279** | **896,146** | **461,628** | **463,837** | **925,465** |
| **SHULE ZA MSINGI I-VII** | | | | | | |
| Shule za Msingi za Serikali | 4,182,915 | 4,130,165 | 8,313,080 | 4,127,500 | 4,139.526 | 8,267,026 |
| Shule za Msingi zisizo za Serikali | 65.849 | 62,624 | 128.473 | 75,769 | 76,510 | 152,279 |
| | **4248764** | **4192789** | **8441553** | **4203269** | **4216036** | **8419305** |
| **SHULE ZA SEKONDARI** | | | | | | |
| Shule za Sekondari za Serikali | 728.322 | 565.369 | 1293,691 | 792,974 | 608,356 | 1,401,330 |
| Shule za Sekondari zisizo za Serikali | 84,623 | 88,088 | 1,727,711 | 117,197 | 120,172 | 237,369 |
| | **812945** | **653457** | **3021402** | **910171** | **728528** | **1638699** |
| **VYUO VYA UALIMU** | | | | | | |
| Vyuo vya serikali | 12,409 | 9,300 | 21,723 | 14,578 | 11,236 | 25814 |
| Vyuo Visivyo vya Serikali | 5,809 | 7,839 | 13,648 | 5,473 | 5,361 | 10,834 |
| | **18,218** | **17,139** | **35,371** | **20,051** | **16,597** | **36,648** |
| **VYUO VIKUU NA VYUO VIKUU VISHIRIKI** | | | | | | |
| Vyuo Vikuu vya serikali | 21,275 | 49.510 | 70,785 | 27,997 | 56,884 | 83,828 |
| Vyuo Vikuu Visivyo vya Serikali | 9737 | 15043 | 24740 | 14242 | 20881 | 35123 |
| | **31,012** | **64,553** | **95,525** | **42,239** | **77,765** | **118,951** |
| Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | | | | | | |

**Elimu ya Watu Wazima**

385. Idadi ya wananchi walioshiriki katika Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) ilipungua kwa asilimia 3.4, kutoka washiriki 957,289 mwaka 2009, hadi washiriki 924,893 mwaka 2010. Kati ya hao, wanaume walikuwa 451,108, sawa na asilimia 48.8 na wanawake walikuwa 473,785, sawa na asilimia 51.2, ikilinganishwa na washiriki wanaume 449,103 (asilimia 46.9) na wanawake 508,106 (asilimia 53.1) mwaka 2009.

386. Idadi ya washiriki wa Mpango wa Elimu ya Masafa na Ana kwa Ana iliongezeka, kutoka 39,689 mwaka 2009 hadi washiriki 51,993 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 31.0. Kati ya washiriki hao, wanaume walikuwa 28,336, sawa na asilimia 54 na wanawake walikuwa 23,657, sawa na asilimia 46, ikilinganishwa na wanaume 18,336 (asilimia 46) na wanawake 21,353 (asilimia 54) mwaka 2009.

387. Idadi ya washiriki wa Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) ilipungua, kutoka wanafunzi 82,989 mwaka 2009, hadi 72,799 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 12.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa watoto na vijana walio nje ya shule kufaulu na kuingia katika mfumo wa kawaida wa elimu ya msingi.

**Ukaguzi wa shule na vyuo**

388. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za elimu ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora. Mwaka 2009/10, jumla ya shule/vyuo/taasisi/asasi 9,960 za elimu zilikaguliwa ikilinganishwa na shule/vyuo/taasisi/asasi 5,610 zilizokaguliwa mwaka 2008/09. Idadi hii, ni sawa na asilimia 49.6 ya lengo la kukagua shule/vyuo/taasisi/asasi 20,094 mwaka 2009/10.

Jedwali Na. 19.2: Taasisi/vyuo/asasi zilizokaguliwa 2009/10

| Aina ya Taasisi/Asasi | Idadi iliyolengwa kukaguliwa | Idadi halisi iliyokaguliwa | Kiwango cha utekelezaji (% ya idadi iliyolengwa kukaguliwa) |
|---|---|---|---|
| Madarasa ya Elimu ya Awali | 5,137 | 2570 | 50.0 |
| Shule za Msingi | 6,763 | 3,406 | 50.4 |
| Vituo vya Elimu ya Ufundi | 151 | 55 | 36.4 |
| Shule/madarasa ya Elimu Maalumu | 115 | 56 | 48.7 |
| Vituo vya Elimu ya Watu Wazima | 6,187 | 2,588 | 41.8 |
| Shule za Sekondari | 1,664 | 1,258 | 75.6 |
| Vyuo vya Ualimu | 77 | 27 | 35.1 |
| **Jumla** | **20,094** | **9,960** | **49.6** |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

## Elimu ya Ufundi na Mafunzo

389. Mwaka 2010, idadi ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo vilikuwa 224, ikilinganishwa na vyuo 221 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Kati ya hivyo, vyuo 133 vilikuwa ni vya Serikali na 91 visivyo vya Serikali ikilinganishwa na vyuo 128 vya Serikali na 93 visivyo vya Serikali mwaka 2009.

390. Mwaka 2010, idadi ya wanachuo waliojiunga katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ilikuwa 58,494, ikilinganishwa na wanachuo 49,185 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Kati ya hao, wanachuo 50,554 walikuwa katika vyuo vya Serikali na 7,940 walikuwa katika vyuo visivyo vya Serikali ikilinganishwa na wanachuo 41,214 waliokuwa katika vyuo vya Serikali na 7,967 waliokuwa katika vyuo visivyo vya Serikali mwaka 2009.

391. Mwaka 2010, idadi ya wasichana waliojiunga katika vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ilikuwa 25,018, ikilinganishwa na wasichana 21,244 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 17.8. Kati ya idadi hiyo, vyuo vya Serikali vilikuwa na wasichana 21,058 na vyuo visivyo vya Serikali vilikuwa

na wasichana 3,960, ikilinganishwa na wasichana 17,056 katika vyuo vya Serikali na 4,188 katika vyuo visivyo vya Serikali mwaka 2009.

### Elimu ya Ufundi Stadi

392. Mwaka 2010, idadi ya Vyuo vya Ufundi Stadi ilikuwa 900, ikilinganishwa na vyuo 889 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 1.2. Kati ya hivyo, vyuo 22 vilikuwa ni vya Serikali na 878 visivyo vya Serikali ikilinganishwa na vyuo 21 vya Serikali na vyuo 868 visivyo vya Serikali mwaka 2009.

393. Idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Ufundi Stadi iliongezeka hadi 116,613 mwaka 2010 kutoka 72,938 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 59.9. Idadi ya wanafunzi wa kike ilikuwa 54,605, sawa na asilimia 47 ya wanafunzi wakati idadi ya wanafunzi wa kiume ilikuwa 62,008, sawa na asilimia 53 ya wanafunzi wote waliosajiliwa mwaka 2010.

### Elimu ya Juu

394. Mwaka 2009/10, idadi ya vyuo vikuu ilikuwa 31. Kati ya hivyo, vyuo vikuu vya Serikali vilikuwa 11 na vya binafsi vilikuwa 20, sawa na ilivyokuwa mwaka 2008/09. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya Serikali iliongezeka kutoka 70,785 mwaka 2008/09 hadi 83,828 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la wanafunzi 23,043 au asilimia 18.4. Kati ya hao, wanawake walikuwa 27,997, sawa na asilimia 33 na wanaume walikuwa 55,831, sawa na asilimia 66.6, ikilinganishwa na wanawake 22,083, sawa na asilimia 31.2 na wanaume 48,702, sawa na asilimia 68.8 mwaka 2008/09.

395. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu visivyo vya Serikali iliongezeka kutoka 24,740 mwaka 2008/09, hadi 35,123 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 42.0. Kati ya hao, wanawake walikuwa 14,242, sawa na asilimia 40.5 na wanaume walikuwa 20,881, sawa na asilimia 59.5, ikilinganishwa na wanawake 9,737, sawa na asilimia 39.4 na wanaume 15,003, sawa na asilimia 60.6 mwaka 2008/09.

396. Mwaka 2009/10, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya serikali na visivyo vya serikali ilikuwa 118,951, ikilinganishwa na wanafunzi 95,525 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 24.5. Kati ya hao, idadi ya wanafunzi wa kike ilikuwa 42,016 sawa na asilimia 35.3 ya wanafunzi wote mwaka 2009/10.

397. Mwaka 2009/10, Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 197.3 bilioni kwa wanafunzi 74,498, ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi 140,295 bilioni kwa wanafunzi 58,841 mwaka 2008/09. Aidha, kasi ya urejeshwaji mikopo imekuwa ikiongezeka kwa kiasi kikubwa tangu Bodi ilipoanza shughuli za urejeshwaji mikopo. Katika mwaka 2010, Bodi ilikusanya jumla ya shilingi 3,082,392,983.32, ikilinganishwa na shilingi 1,615,040,895.35 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 90.9. Hadi kufikia Desemba 2010, Bodi ilikusanya jumla ya shillingi 6,089,567,254.

## SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 80 (Namba)

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1986 | 10789 | 9855 | 8401 | 8679 | 2363 | 2276 | 42363 |
| 1987 | 11626 | 10870 | 9528 | 9162 | 2313 | 2322 | 45821 |
| 1988 | 14258 | 11195 | 10373 | 9180 | 2313 | 2240 | 49559 |
| 1989 | 16034 | 14815 | 11275 | 10018 | 2980 | 2360 | 57482 |
| 1990 | 18654 | 16340 | 14199 | 11157 | 3777 | 2859 | 66986 |
| 1991 | 18892 | 18679 | 15459 | 13915 | 3646 | 3355 | 73946 |
| 1992 | 19299 | 19443 | 17044 | 14864 | 4136 | 3874 | 78660 |
| 1993 | 20267 | 20110 | 17597 | 16713 | 4261 | 4016 | 82964 |
| 1994 | 21589 | 19823 | 17513 | 16474 | 4179 | 3863 | 83441 |
| 1995 | 25200 | 22237 | 19118 | 17067 | 4541 | 3903 | 92[illegible]66 |
| 1996 | 28289 | 23874 | 20197 | 16468 | 4528 | 4035 | 97391 |
| 1997 | 32043 | 29748 | 23810 | 19697 | 6412 | 4846 | 116556 |
| 1998 | 37094 | 31218 | 24925 | 21182 | 5163 | 4748 | 124330 |
| 1999 | 39144 | 36682 | 28589 | 23996 | 6305 | 5248 | 139964 |
| 2000 | 43643 | 36734 | 31132 | 25456 | 6654 | 6143 | 149762 |
| 2001 | 47204 | 45078 | 30531 | 29188 | 7198 | 6601 | 165800 |
| 2002 | 56101 | 50371 | 36989 | 29045 | 7711 | 7126 | 187343 |
| 2003 | 52863 | 60643 | 36906 | 35653 | 7780 | 6885 | 200730 |
| 2004 | 98738 | 67294 | 46546 | 36385 | 8353 | 7572 | 264888 |
| 2005 | 134963 | 109398 | 46188 | 46489 | 9710 | 8444 | 355192 |
| 2006 | 196391 | 151448 | 72167 | 42584 | 18211 | 9691 | 490492 |
| 2007 | 401011 | 218[illegible]60 | 105770 | 70796 | 21789 | 11668 | 829094 |
| 2008 | 395930 | 332393 | 175353 | 95214 | 25240 | 11743 | 1035873 |
| 2009 | 480529 | 308131 | 159789 | 167355 | 31201 | 12695 | 1159700 |
| 2010 | 382207 | 398870 | 293519 | 279995 | 26065 | 20674 | 1401330 |
| Badiliko (%) 2009 - 2010 | -20.5 | 29.4 | 83.7 | 67.3 | -16.5 | 62.9 | 20.8 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

## IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali 80 A

| Aina ya Taasisi | 2008 | | | 2009 | | | 2010 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikali | Binafsi | Jumla |
| Shule za Msingi | 15257 | 416 | 15673 | 426 | 15301 | 15727 | 15265 | 551 | 15816 |
| Shule za Sekondari | 3039 | 759 | 3798 | 3283 | 819 | 4102 | 3397 | 869 | 4266 |
| Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari) | 33 | 34 | 67 | 34 | 43 | 77 | 34 | 58 | 92 |
| **Jumla** | 18329 | 1209 | 19538 | 3743 | 16163 | 19906 | 18696 | 1478 | 20174 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

## IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA

Jedwali 80B

| | 2008 | | | 2009 | | | 2010 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla |
| **I. Elimu ya msingi:** | | | | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII | 4261831 | 4148263 | 8410094 | 4248764 | 4192789 | 8141553 | 4203269 | 4216036 | 8419305 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za serikali Darasa la I-VII | 4203180 | 4093428 | 8296608 | 4182915 | 4130165 | 8313080 | 4127500 | 4139526 | 8267026 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII | 58651 | 54835 | 113486 | 65849 | [illegible] | 128473 | 75769 | 76510 | 152279 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi | 76638 | 78257 | 154895 | 80066 | 77119 | 157185 | 82170 | 83686 | 165856 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za serikali | 74479 | 74954 | 149433 | 76765 | 74711 | 151476 | 78331 | 80750 | 159081 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi | 2159 | 3303 | 5162 | 3301 | 2408 | 5709 | 3839 | 2936 | 6775 |
| **II. Elimu ya sekondari:** | | | | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI | 679124 | 543279 | 1222403 | 812945 | 653457 | 1466102 | 910171 | 728528 | 1638699 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za serikali, kidato I-VI | 58118 | 451755 | 509873 | 728322 | 565369 | 1293691 | 792974 | 608366 | 1401330 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI | 95006 | 91524 | 186530 | 81623 | 88088 | 172711 | 117197 | 120172 | 237369 |
| Idadi ya walimu katika shule za serikali | 23122 | 9713 | 32835 | 17240 | 9192 | 26432 | 19666 | 10586 | 30252 |
| Idadi ya walimu katika shule za binafsi | 16790 | 8181 | 24971 | 5732 | 1790 | 7522 | 8155 | 2110 | 10265 |
| Jumla ya Walimu wote | 39912 | 17894 | 57806 | 22972 | 10982 | 33954 | 27521 | 12696 | 40517 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

## MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU

Jedwali 80C

| | 2007 | | | 2008 | | | 2009 | | | 2010 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla |
| Shahada | - | - | - | 4209 | 1749 | 5958 | 5352 | 2636 | 7988 | - | - | - |
| Stashahada | 4215 | 1744 | 5959 | 16154 | 8411 | 24565 | 17593 | 10909 | 28502 | 8229 | 5450 | 13679 |
| Daraja A | 4074 | 5483 | 9557 | 66214 | 69665 | 135879 | 70567 | 72357 | 142924 | 4288 | 4734 | 9022 |
| Daraja B | - | - | - | 22223 | 16762 | 38985 | 17678 | 13388 | 31066 | - | - | - |
| Mafunzo Kazini | 1747 | 1491 | 3238 | 106800 | 96587 | 205387 | - | - | - | - | - | - |
| Jumla | 10036 | 8718 | 18754 | 217600 | 193174 | 410774 | 111190 | 99290 | 210480 | 12517 | 10184 | 22701 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

- Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WANAFUNZI KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU KWA JINSIA

Jedwali Na. 80 D

| Taasisi/Kozi | 2009/2010 | | |
|---|---|---|---|
| 1. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) | Waume | Wake | Jumla |
| B.A General | | | 0 |
| B.A Education | 478 | 422 | 900 |
| B. COM General | | | 0 |
| B. Education (PESC) | | | 0 |
| B.A with Education | 655 | 365 | 1020 |
| B.A (Archaelogy) | 16 | 9 | 25 |
| B.A (Archaelogy & Geography) | 0 | 0 | 0 |
| B.A (Culture & Heritage) | 5 | 29 | 34 |
| B.A (Language Studies) | 10 | 9 | 19 |
| B.A (Economics) | 57 | 37 | 94 |
| B. A (Economics & Commerce) | | | 0 |
| B. A (Economics & Statistics) | | | 0 |
| B.A (Economics & Geography) | 2 | 0 | 2 |
| B.A (Economics & Sociology) | 3 | 4 | 7 |
| B.A (Economics & Statistics) | 15 | 10 | 25 |
| B.A (Fine and Performing Arts) | 17 | 9 | 26 |
| B.A (Geography & Env. studies) | 73 | 30 | 103 |
| B.A (Geography & Statistics) | | | 0 |
| B.A (History & Archeology) | 22 | 9 | 31 |
| B.A (History & Polit. Science) | 17 | 12 | 29 |
| B.A (Polit. Science & public Admin) | 78 | 36 | 114 |
| B.A (Polit. Science & Economics) | 3 | 0 | 3 |
| B.A (Polit. Science & Language) | 14 | 9 | 23 |
| B.A (Polit. Science & Sociology) | 20 | 33 | 53 |
| B.A (Sociology) | 87 | 161 | 248 |
| B. A (Statistics) | 29 | 9 | 38 |
| BA (History) | 0 | 0 | 0 |
| B.A Journalism | 4 | 9 | 13 |
| B. A Mass communication | 8 | 17 | 25 |
| B.A Public Relations and advertersing | 16 | 20 | 36 |
| B.Commerce | 358 | 177 | 535 |
| BSc in computer science | 69 | 14 | 83 |
| BSc, With computer csience | 17 | 2 | 19 |
| BSc (Education) | | | 0 |
| BSc. With Education | 44 | 37 | 81 |
| BSc. General | 1 | 0 | 1 |
| BSc.with Geology | 15 | 2 | 17 |
| BSc Geology | | | 0 |
| BSc.(Engineering Geology) | | | 0 |
| BSc Engineering | | | 0 |
| B.B.A | 29 | 17 | 46 |
| B. Ed. Commerce | 19 | 6 | 25 |
| B. Ed. In Psychology | 0 | 0 | 0 |
| B. Ed. In Education Psychology | 31 | 33 | 64 |
| B. Ed. Science | 33 | 3 | 36 |
| B. Ed. Adult Education | 39 | 30 | 69 |
| B. Ed. Arts | 32 | 37 | 69 |
| Bachelor of law | 70 | 82 | 152 |
| BSc Comp. Eng & Info Tech. | 32 | 14 | 46 |
| BSc Electr. Engineering | 19 | 4 | 23 |
| BSc Electro power Eng. | 10 | 1 | 11 |

Jadwali Na. 80B Linaendelea

| | | | |
|---|---|---|---|
| BSc. Chem. & processing Eng | 24 | 16 | 40 |
| BSc. Electro Mech. Eng | 8 | 4 | 12 |
| BSc. Food and Biochemical | 8 | 9 | 17 |
| BSc. Mech. Eng | 18 | 0 | 18 |
| BSc. Mining Eng. | 25 | 3 | 28 |
| BSc. Mineral Proc. Eng. | 20 | 4 | 24 |
| BSc. Civil & Struct. Eng | 31 | 10 | 41 |
| BSc. Telecom Eng. | 36 | 12 | 48 |
| BSc. Transportation Eng. | | | 0 |
| BSc. Civil & Transportation Eng | 30 | 5 | 35 |
| BSc. Production Eng. | 4 | 3 | 7 |
| BSc. Civil & water Res. Eng. | 24 | 6 | 30 |
| BSc. Eng. Civil | | | 0 |
| BSc. Electronics | | | 0 |
| BSc. Electronics Sc. & Comm. | | | 0 |
| BSc. Mol. Bio & Biotech | 12 | 4 | 16 |
| BSc. Aquatic Sc. And Env. Sc. & Con | 12 | 2 | 14 |
| BSc. Wildlife csience and conservation | 33 | 11 | 44 |
| BSc. Fish & Aquatic Sc. & Con | | | 0 |
| BSc. Industrial Engineering and Management | 20 | 14 | 34 |
| BSc. ICS | | | 0 |
| Adv. Diploma in Journalism | | | 0 |
| Lp in Culturee mngt. & Tour | | | 0 |
| Diploma in Computer Sciences | | | 0 |
| Diploma in Fisheries | | | 0 |
| Certificate in law | | | 0 |
| Certificate in Journalism | | | 0 |
| Certificates in Computer Science | | | 0 |
| Occasional/Short Course: Term | | | 0 |
| **Jumla** | 2752 | 1801 | 4553 |
| Idadi ya Walimu | 110 | 54 | 164 |
| **2. Chuo Kikuu Kishiriki Muhimbili (MUHAS)** | | | |
| MD (Doctor of Medicine) | | | |
| B.Sc. Pharmacy | 113 | 42 | 155 |
| BSc. Nursing | 22 | 10 | 32 |
| D.D.S (Doctor of Dental Surgery) | 4 | 8 | 12 |
| BSc. Env. Health | 17 | 4 | 21 |
| B. Sc. Nursing Mg. | 12 | 10 | 22 |
| B.Medical Labaratory Science | 2 | 0 | 2 |
| B. Sc. In Radiotherapy Treatment | 9 | 0 | 9 |
| B.Sc. in nursing Midwifery | 2 | 0 | 2 |
| IPH | 1 | 4 | 5 |
| ITM | | | 0 |
| Adv. Dip. Dermatovenereology | | | 0 |
| Adv. Dip. Nursing | 7 | 5 | 12 |
| Adv. Dip. Medical Laboratory Techn. | 4 | 9 | 13 |
| Dip. Diagnostic Radiography | 15 | 13 | 28 |
| Dip. Enviromental Health Science | 12 | 6 | 18 |
| Dip. Medical Labolatory Techn. | 34 | 13 | 47 |
| Dip. Orthopaedic Techn | 20 | 16 | 36 |
| Dipl. In Nursing | 5 | 3 | 8 |
| Dip. Pharmaceutical Sciences | 1 | 19 | 20 |
| **Jumla : Chuo Kikuu Muhimbili** | 280 | 162 | 442 |
| **Idadi ya Walimu** | 124 | 88 | 212 |

Jedwali Na. 80D Linaendelea

| 3. Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) | 2009/2010 | | |
|---|---|---|---|
| | Waume | Wake | Jumla |
| B. SC. AGRICULTURE GENERAL | 94 | 13 | 107 |
| B. SC. HORTICULTURE | 22 | 3 | 25 |
| B. SC. ANIMAL SCIENCE | 71 | 20 | 91 |
| B. SC. AQUACULTURE | 25 | 7 | 32 |
| B. SC. RANGE MANEGEMENT | 26 | 7 | 33 |
| B. SC. AGRONOMY | 54 | 7 | 61 |
| B. SC. AGRICULTUREAL ECONOMICS & AGRIBUSINESS | 155 | 46 | 201 |
| B. SC. AGRICULTURAL EDUCATION & EXTESION | 83 | 36 | 119 |
| B. SC. FOOD SCIENCE & TECHNOLOGY | 27 | 27 | 54 |
| B. SC. HOME ECONOMICS & HUMAN NUTRITION | 11 | 42 | 53 |
| B. SC. AGRICULTURAL ENGINEERING | 29 | 1 | 30 |
| B. SC. FORESTRY | 67 | 12 | 79 |
| B. SC. WILDLIFE | 69 | 24 | 93 |
| B. SC. BACHELOR OF TOURISM MANAGEMENT | 56 | 68 | 124 |
| B. SC. ENVIRONMENTAL SCIENCE & MANAGEMENT | 52 | 24 | 76 |
| B. SC. INFORMATICS | 41 | 3 | 44 |
| B. SC. EDUCATION (Chemistry & Biology) | 72 | 18 | 90 |
| B. SC. EDUCATION (Geography & Biology) | 37 | 25 | 62 |
| B. SC. EDUCATION (Chemistry & Mathematics) | 19 | 1 | 20 |
| B. SC. EDUCATION (Informatics & Mathematics) | 38 | 1 | 39 |
| B. SC. EDUCATION (Geography & Mathematics) | 14 | 4 | 18 |
| BACHELOR OF VETERINARY MEDICINE | 73 | 5 | 78 |
| B. SC. BIOTECHNOLOGY & LABORATORY SCIENCE | 70 | 18 | 88 |
| BA RURAL DEVELOPMENT | 140 | 77 | 217 |
| BACHELOR TOURISM AND MANAGEMENT | | | |
| BACHELOR OF RURAL DEVELOPMENT | | | |
| B. SC. APPLIED AGRICULTURAL EXTENSION | | | |
| B. SC. AGRICULTURAL EDUCATION | | | |
| B. SC. FAMILY AND CONSUMER STUDIES | | | |
| B. SC. HUMAN NUTRITION | | | |
| B. SC BIOPROCESSING & POST-HARVEST ENGINEERING | | | |
| B. SC. IRRIGATION & WATER RESOURCE ENGINEERING | | | |
| Jumla : SUA | 1345 | 489 | 1834 |
| Idadi ya Walimu | 374 | 82 | 456 |

Jedwali Na. 8OD L inaendelea...

| | 2009/2010 | | |
|---|---|---|---|
| 4. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) | Wanume | Wake | Jumla |
| BA (General) | 132 | 33 | 165 |
| B.A (Education) | 230 | 100 | 330 |
| B. ED (Special Education) | 3 | 3 | 6 |
| B A (Tourism) | 59 | 13 | 72 |
| B. Education | 255 | 103 | 408 |
| B Sc. (General) | 102 | 30 | 132 |
| B. Sc. (Education) | 53 | 16 | 69 |
| B. Commerce (General) | | | 0 |
| B. Commerce (Education) | | | 0 |
| BBA (General) | 286 | 62 | 348 |
| BBA (Education) | 48 | 17 | 65 |
| B A Social work | 29 | 37 | 66 |
| BA Sociology | 86 | 72 | 158 |
| B A. J | 18 | 1 | 19 |
| BA (Mass Communication) | 29 | 12 | 41 |
| B. Sc. (ES) | 38 | 6 | 44 |
| LLB | 322 | 68 | 390 |
| BSc. ICT | 29 | 4 | 33 |
| POSTGRADUATE DEGREE: | | | |
| MSc. (CED) | 0 | 0 | 0 |
| M.CED | 226 | 159 | 385 |
| MSc. | 1 | 1 | 2 |
| M A | 106 | 52 | 158 |
| M. Dist. Education | 3 | 1 | 4 |
| M.Ed | 179 | 90 | 269 |
| PGOL | 40 | 7 | 47 |
| PGDE | 91 | 69 | 160 |
| LLM | 0 | 0 | 0 |
| LLMIT&T | 60 | 19 | 79 |
| MBA | 692 | 137 | 829 |
| Ph.D | 41 | 8 | 49 |
| NON DEGREE COURSE: | | | |
| Foundation Course | 0 | 0 | 0 |
| OD CYP Diploma | 27 | 8 | 35 |
| CCDE | 2 | 2 | 4 |
| ODDEOL | 38 | 16 | 54 |
| CPPH | 1 | 0 | 1 |
| OFC | 738 | 533 | 1271 |
| PTE- Certificate | 0 | 0 | 0 |
| ODPTE | 277 | 220 | 497 |
| ODPPH | 5 | 4 | 9 |
| Jumla : OUT | 4037 | 1974 | 6011 |
| Idadi ya Walimu | 183 | 83 | 266 |
| 5. Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) | | | |
| B.Architecture (ARCH) | | | |
| Architecture in Interior Design (AID) | | | |
| Architecture in Land Scape (ALA) | 240 | 43 | 283 |
| B.Sc Land Economics) | 18 | 7 | 25 |
| B Sc. (Urb.Planning) | 3 | 1 | 4 |
| B Sc. (Building Surveying (BS)) | 174 | 71 | 245 |
| B Sc. (Land Mgt. and Valuation) | 0 | 0 | 0 |
| B Sc. (Env. Engineering) | 28 | 15 | 43 |
| B Sc Geomatics | 174 | 53 | 227 |
| Real Estate Finance and Management (REFM) | | | 0 |
| Property and Facilities Management (PPM) | 85 | 16 | 101 |
| Finance and Accounts (BAF) | 69 | 19 | 88 |
| Environmental Science and Management | 43 | 14 | 57 |
| Municipal and Industrial Service (MISE) | 0 | 0 | 0 |
| Environmental Laboratory Technology (ELST) | 69 | 64 | 133 |
| Housing and Infrastructure Planning (HIP) | 35 | 6 | 41 |
| Arts in Economics | 18 | 24 | 42 |
| Regional Development Planning (RDP) | 48 | 8 | 56 |
| Geoinformatics (GI) | 7 | 0 | 7 |
| Geodetic Science (GS) | 27 | 11 | 30 |
| Information System Management (ISM) | 37 | 10 | 53 |
| Construction Management (CM) | 15 | 0 | 15 |
| Civil Engineering | 24 | 31 | 55 |
| Diploma in (GFM4) | 53 | 17 | 70 |
| Graduate Diploma | 0 | 0 | 0 |
| Jumla : ARU | 1184 | 419 | 1603 |
| Idadi ya Walimu | | | 251 |

Jadwali Na. 60D Linaendelea

| 6. Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) | 2009/10 | | |
|---|---|---|---|
| | Waume | Waka | Jumla |
| B.A KISWAHILI | 106 | 126 | 204 |
| B.A KISWAHILI LINGUISTIC | 44 | 39 | 83 |
| B.A KISWAHILI LITERATURE | 24 | 29 | 53 |
| B.A FINE ART DESIGN | 7 | 0 | 7 |
| B.A FRENCH | 13 | 7 | 20 |
| B.A ENGLISH | 38 | 22 | 60 |
| B.A KOREA | 1 | 0 | 1 |
| B.A FIRM THEATRE | 3 | 0 | 3 |
| B.A LITERATURE | 14 | 15 | 29 |
| B.A TOURISM & CULTURAL HERITAGE | 239 | 97 | 336 |
| B.A HISTORY | 109 | 35 | 144 |
| B.A ENVIROMENTAL DISASTER MANAGEMENT | 91 | 27 | 76 |
| B.COM | 53 | 10 | 63 |
| B COM (ACCOUNTING) | 483 | 184 | 667 |
| B COM (HRM) | 79 | 42 | 121 |
| B COM (FINANCE) | 216 | 78 | 284 |
| B COM (MARKETING) | 85 | 30 | 125 |
| B.COM (INTERNATIONAL BUSINESS) | 16 | 5 | 21 |
| B COM (SMALL BUSINESS INTERPRENEURSHIP) | 14 | 6 | 20 |
| B COM (TOURISM HOSPITALITY MANAGEMENT) | 5 | 1 | 6 |
| B.A DEVELOPMENT STUDIES | 69 | 60 | 129 |
| B.A ECONOMICS & STATISTICS | 62 | 12 | 74 |
| B.A GEOGRAPHY & ENVIROMENTAL STUDIES | 193 | 69 | 262 |
| B.A POLITICAL SCIENCE & PUBLIC ADMINSTRATION | 359 | 215 | 574 |
| B.A SOCIALOGY | 204 | 327 | 531 |
| B.A STATISTICS | 22 | 3 | 25 |
| B.A PUBLIC ADMINISTRATION | 312 | 333 | 645 |
| BACHELOR OF LAW | 65 | 33 | 98 |
| B.A ECONOMICS AND SOCIALOGY | 65 | 35 | 100 |
| B.A ENVIROMENTAL ECONOMICS & POLICY | 20 | 13 | 41 |
| B.A INTERNATIONAL RELATION | 302 | 219 | 521 |
| B.A ECONOMICS | 118 | 31 | 149 |
| BBA | 397 | 180 | 577 |
| BBA EVIRNING | 19 | 10 | 29 |
| B.A PROJECT PLANNING MANAGEMENT & COMMUNITY DEVELOPMENT | 459 | 221 | 680 |
| B.A EDUCATION | 2282 | 813 | 3095 |
| BED ART | 570 | 317 | 887 |
| BED MANAGEMENT AND ADMINISTRATION | 291 | 153 | 444 |
| BED COMMERCE | 214 | 64 | 278 |
| BED POLICY PLANNING & MANAGEMENT | 191 | 72 | 263 |
| BED SPECIAL NEEDS | 97 | 43 | 140 |
| BSC ECONOMICS | 84 | 23 | 107 |
| BED SCIENCE | 98 | 30 | 128 |
| BED EARLY CHILD HOOD EDUCATION | 119 | 07 | 176 |
| BED PYSIOLOGY | 153 | 49 | 202 |
| BED ADULT EDUCATION & COMMUNITY DEVELOPMENT | 148 | 77 | 225 |
| BED SC (ICT) | 7 | 1 | 8 |
| BED GUIDENCE & COUNSELING | 53 | 53 | 106 |
| BSC STATISTICS | 148 | 22 | 170 |
| BSC CHEMISTRY | 25 | 5 | 30 |
| BSC BIOLOGY | 16 | 7 | 23 |
| BSC PHYSICS | 6 | 1 | 7 |
| BSC MATHEMATICS | 58 | 3 | 61 |
| MEDICAL DOCTOR | 75 | 14 | 89 |
| BSC. NURSING | 26 | 25 | 51 |
| BSC BUSINESS INFORMATION SYSTEM | 18 | 1 | 19 |
| BSC COMPUTER ENGINEER | 46 | 3 | 49 |
| BSC. INFORMATION SYSTEM | 266 | 47 | 313 |
| BSC COMPUTER SCIENCE | 206 | 23 | 229 |
| BSC SOFT WARE ENGINEERING | 30 | 0 | 30 |
| BSC. TELECOMMUNICATION ENGINEERING | 69 | 8 | 77 |

Jedwali Na. 80D Linaendelea

| | Waume | Wake | Jumla |
|---|---|---|---|
| BSC APPLIED GEOLOGY | 30 | 2 | 32 |
| BSC MINERAL PROCESSING ENGINEERING | 8 | 0 | 8 |
| BSC MINING ENGINEERING | 6 | 2 | 8 |
| BSC NURSING MIDWIFERY | 0 | 0 | 0 |
| BSC VITUAL EDUCATION | 0 | 0 | 0 |
| BSC IN HEALTH INFORMATION SYSTEM | 0 | 0 | 0 |
| BA IN ARABIC | 0 | 0 | 0 |
| B.COM IN MANAGEMENT SCIENCE | 0 | 0 | 0 |
| B.COM PROCUREMENT MANAGEMENT | 0 | 0 | 0 |
| B.COM IN INFORMATION MANAGEMENT | 0 | 0 | 0 |
| BA IN PHILOSOPHY | 0 | 0 | 0 |
| BCS IN COMPUTER AND INFORMATION SERCURITY | 0 | 0 | 0 |
| BSC IN VITUAL EDUCATION | 0 | 0 | 0 |
| BSC IN PETROLEUM ENGINEERING | 0 | 0 | 0 |
| PHD | 28 | 12 | 40 |
| DIPLOMA IN COMPUTER SCIENCE | 32 | 9 | 41 |
| CERTIFICATE IN COMPUTER SCIENCE | 7 | 0 | 7 |
| POSTGRADUATE DIPLOMA IN EDUCATION | 12 | 2 | 14 |
| MASTER OF ART IN EDUCATION | 47 | 20 | 67 |
| MASTER OF BUSNESS ADMINSTRATION | 44 | 11 | 55 |
| MASTER OF BUSINESS ADMINSTRATION(EVERNING) | 18 | 12 | 30 |
| EXCUTIVE MASTER OF BUSINESS ADMINSTRATION | 8 | 3 | 11 |
| MASTER OF PUBLIC ADMINSTRATION | 23 | 15 | 38 |
| EVERNING MASTER OF PUBLIC ADMINSTRATION | 10 | 10 | 20 |
| MASTER OF INTERNATIONAL RELATION | 20 | 8 | 28 |
| MASTER OF DEVELOPMENT STUDIES | 40 | 19 | 59 |
| EVERNING MADS | 12 | 8 | 20 |
| MASTER OF ART IN SOCIALOGY | 10 | 6 | 16 |
| MASTER OF ART IN NATURAL SCIENCE | 29 | 12 | 41 |
| MASTER OF ART IN DEMOGRAPHY | 20 | 1 | 21 |
| MASTER OF ART IN KISWAHILI BY DESERTATION | 0 | 1 | 1 |
| MASTER OF ART IN ENGLISH BY DESERTATION | 1 | 0 | 1 |
| FULL TIME MASTER OF ART IN LINGUISTIC | 11 | 8 | 19 |
| FULL TIME MASTER OF ART IN KISWAHILI LITERATURE | 17 | 22 | 39 |
| FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN COMPUTER SCIENCE | 20 | 4 | 24 |
| FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN DRY LAND BIODIVERSITY CONSERVATION | 3 | 4 | 7 |
| FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN TELECOMMUNICATION ENGINEERING | 0 | 0 | 0 |
| EVERNING MASTER OF SCIENCE IN TELECOMMUNICATION ENGINERING | 0 | 0 | 0 |
| FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN NURSING - MENTAL HEALTH | 0 | 0 | 0 |
| JUMLA: (UDOM) | 10097 | 4627 | 14724 |
| Idadi ya Walimu | 396 | 140 | 536 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Jedwall Na.81

SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Namba JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1987 | 15709 | 15526 | 13188 | 12245 | 801 | 756 | 58225 |
| 1988 | 18007 | 18897 | 15326 | 14358 | 966 | 702 | 68256 |
| 1989 | 20789 | 19279 | 18415 | 14759 | 1045 | 716 | 75003 |
| 1990 | 23585 | 21870 | 17599 | 17685 | 1481 | 1094 | 83314 |
| 1991 | 27554 | 25143 | 19237 | 17371 | 1922 | 1639 | 92866 |
| 1992 | 29027 | 27044 | 19378 | 17891 | 2018 | 1758 | 97116 |
| 1993 | 25703 | 27651 | 21894 | 18367 | 2223 | 2097 | 97935 |
| 1994 | 28657 | 26971 | 22784 | 19809 | 2573 | 2011 | 102805 |
| 1995 | 28498 | 26242 | 24098 | 21199 | 2334 | 1938 | 104309 |
| 1996 | 28002 | 25807 | 22494 | 20318 | 3168 | 2243 | 102032 |
| 1997 | 29768 | 27461 | 22406 | 20627 | 3408 | 3381 | 107051 |
| 1998 | 27125 | 24756 | 22029 | 20409 | 4826 | 3428 | 102573 |
| 1999 | 28333 | 25747 | 23120 | 20255 | 5667 | 4493 | 107615 |
| 2000 | 30789 | 26601 | 23469 | 20430 | 5894 | 5011 | 112194 |
| 2001 | 36305 | 30820 | 25004 | 20762 | 5892 | 5116 | 123899 |
| 2002 | 41593 | 34209 | 27540 | 20681 | 6418 | 5534 | 135975 |
| 2003 | 46891 | 38506 | 26385 | 21650 | 6430 | 4859 | 144721 |
| 2004 | 48752 | 46167 | 33240 | 24476 | 8847 | 6229 | 167711 |
| 2005 | 45276 | 46321 | 32063 | 29248 | 9183 | 7046 | 169137 |
| 2006 | 46968 | 48013 | 42878 | 29796 | 9569 | 7956 | 185180 |
| 2007 | 47437 | 46927 | 41340 | 35746 | 11299 | 8667 | 191416 |
| 2008 | 42971 | 43232 | 43177 | 35980 | 12576 | 8594 | 186530 |
| 2009 | 44255 | 36384 | 37064 | 34061 | 11851 | 9096 | 172711 |
| 2010 | 56620 | 57876 | 50778 | 46820 | 12269 | 13006 | 237369 |
| Badiliko (%) | 27.9 | 59.1 | 37.0 | 37.5 | 3.5 | 43.0 | 37.4 |

# SURA YA 20

## AFYA

### Utangulizi

398. Katika mwaka 2010, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kuboresha huduma za afya na kuhakikisha zinatolewa kwa viwango stahiki. Mpango Maalum wa Afya ya Msingi (MMAM) uliendelea kutekelezwa kulingana na mpango kazi. Mitaala ya kufundishia wataalam wa kada za afya ilipitiwa na kuboreshwa ili iendane na mahitaji ya sasa. Huduma za afya ya uzazi na mtoto ziliendelea kupewa kipaumbele ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Vilevile, huduma za ushauri nasaha na kupima virusi vya UKIMWI ziliendelea kutolewa pamoja na kuhakikisha dawa za kurefusha maisha kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI zinapatikana na kutolewa kwa wakati. Aidha, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa mifumo ya kukusanya na kuchambua takwimu za sekta ya afya inaimarishwa ili kuwezesha upatikanaji na utoaji wa takwimu sahihi za sekta ya afya.

### Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya

399. Serikali, kupitia MMAM na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma ya afya nchini. Mwaka 2010, vituo vya kutolea huduma za afya viliongezeka hadi kufikia 6,321, ikilinganishwa na vituo 6,221 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 1.6. Mgawanyo wa vituo hivyo kwa mwaka 2010 ni kama ifuatavyo: Serikali ilikuwa na hospitali 97, vituo vya afya 449 na zahanati 3,773; mashirika ya umma hospitali 11, vituo vya afya 5 na zahanati 70; na sekta binafsi na mashirika ya kujitolea yalikuwa na hospitali 128, vituo vya afya 230 na zahanati 1,289.

400. Mwaka 2010, idadi ya vitanda katika vituo vyote vya afya nchini ilikuwa 45,241, ikilinganishwa na vitanda 39,842 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Kati ya hivyo, vitanda 23,523 vilikuwa katika vituo vya Serikali, na vitanda 2,161 vilikuwa katika vituo vya watu binafsi.

**Jedwali Na.20.1: Idadi ya Vitanda kwa Aina ya Vituo vya Kutolea Tiba na Umiliki kwa Mwaka 2010**

| Umiliki | Aina ya Kituo | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Hospitali | Kituo cha Afya | |
| Serikali | 15,828 | 7,695 | **23,523** |
| Mashirika ya kidini | 14,638 | 3,151 | **17,789** |
| Mashirika ya Umma | 1,647 | 121 | **1,768** |
| Binafsi | 1,167 | 994 | **2,161** |
| **Jumla** | **33,280** | **11,961** | **45,241** |

401. Mwaka 2010, jumla ya mahudhurio katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma nchini kwa wagonjwa wa nje (out-patient) yalikuwa 35,776,667, ikilinganishwa na 40,067,864 mwaka 2009, sawa na upungufu wa asilimia 10.7. Kati ya hao, asilimia 47 walikuwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, na asilimia 53 walikuwa umri wa miaka mitano na zaidi. Idadi ya wagonjwa waliolazwa kwa mwaka 2010 ilifikia 795,703, ambapo asilimia 77.2 walikuwa ni watoto chini ya umri wa miaka mitano.

**Ukaguzi** wa vituo **vya Afya.**

402. Mwaka 2010, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilifanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Ukaguzi huo ulifanyika kwa awamu mbili katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya na Morogoro. Katika awamu ya kwanza, jumla ya vituo 273 vilikaguliwa. Kati ya hivyo, vituo 94 vilifungwa kutokana na kutokidhi viwango vya utoaji wa huduma za afya na vituo 179 vilipewa ilani ya kuboresha. Katika awamu ya pili, jumla ya vituo 82 vilikaguliwa na timu ya wataalam wa Afya. Kati ya hivyo, vituo 20 vilifungwa na vituo 62 vilipewa ilani ya kuboresha.

**Elimu ya Afya kwa Wananchi**

403. Katika mwaka 2010, huduma za afya ya mazingira ziliendelea kutolewa kwa njia ya kuelimisha wananchi kuboresha afya zao kupitia vipindi vya redio, kusambaza vipeperushi na kwa njia ya kuweka mabango yanayotoa elimu ya kujikinga na maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria, magonjwa ya milipuko, majanga na magonjwa yasio ya kuambukiza.

**Afya ya Uzazi na Mtoto**

404. Mwaka 2010, huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto ziliendelea kutolewa kwa kuzingatia ubora wa viwango vya kimataifa. Aidha, Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa Afya ya Uzazi na Mtoto 2005-2010 na Mpango Mkakati wa kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya watoto na vinavyotokana na uzazi 2008-2015, ili kufikia malengo namba 4 na 5 ya Maendeleo ya Milenia. Huduma za chanjo ziliendelea kupanuka kwa kuongeza vituo vya kutolea huduma hiyo, Chanjo zilizotolewa, zinakinga watoto dhidi ya magonjwa ya kifua kikuu, polio, kifaduro, pepopunda, donda koo, homa ya ini na surua.

405. Serikali iliendelea kutoa chanjo mpya ijulikanayo kama Haemophilus Influenza type B (Hib). Chanjo hiyo inakinga watoto chini ya mwaka mmoja dhidi ya Kichomi na Homa ya uti wa mgongo. Chanjo hiyo mpya ya Hib imeunganishwa na chanjo nyingine nne ambazo zilikuwa zinatolewa awali. Mchanganyiko huo wenye chanjo tano za DPT-HB-Hib unaitwa pentavalent. Chanjo hiyo inakinga watoto dhidi ya Kifaduro, Pepopunda, Donda koo. Homa ya ini na Kichomi pamoja na Homa ya uti wa mgongo.

**Muda wa kuishi**

406. Muda wa kuishi kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, inaonesha kuwa wastani wa muda wa kuishi kwa mwaka 2010 uliendelea kubaki kuwa miaka 55. Kwa upande wa wanaume, wastani wa muda wa kuishi uliendelea kuwa miaka 53 na wanawake miaka 56 kama ilivyokuwa mwaka 2009.

## Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria

407. Mwaka 2010, Serikali ilinunua na kusambaza dawa ya mseto kwenye vituo vya tiba vya umma 5000 ikiwa ni jitihada za kupambana na ugonjwa wa malaria. Aidha, Serikali ilitoa mafunzo ya matumizi ya kipimo cha haraka cha kubaini vimelea vya malaria (Rapid Diagnostic Test) kwa wataalam wa maabara na waganga kwa mikoa 11. Sambamba na hilo, Serikali ilisambaza vyandarua vyenye viuatilifu kupitia mpango wa hati punguzo kwa mama wajawazito na watoto wachanga. Aidha, ugawaji wa vyandarua bila malipo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano umefanyika nchi nzima. Ugawaji wa vyandarua katika kaya bila malipo umefanyika katika mikoa 12, na inakadiriwa vyandarua 14,700,000 vitagawiwa katika kampeni hii.

408. Aidha, Serikali ilifanya uhamasishaji kupitia Mkakati wa Mawasiliano kwa Jamii kwa Kukabiliana na Malaria (Communication Strategy for Malaria Interventions). Uhamasishaji huo ulifanyika kwa njia ya Radio, Televisheni na machapisho mbalimbali. Katika ngazi ya vijiji, uhamasishaji ulifanyika kupitia Watumishi wa Kujitolea Vijijini (Community Change Agents). Vilevile, mtandao wa wanahabari wanaoandika habari za ugonjwa wa malaria na udhibiti wake (JAMANET) ulifanyiwa mafunzo ya uhamasishaji.

## Chakula na Lishe

409. Kulingana na ripoti ya Utaliti wa Afya na Demografia (Tanzania Demographic and Health Survey – (TDHS) ya mwaka 2010, kiwango cha udumavu wa watoto walio chini ya miaka mitano kilipungua kutoka asilimia 38 mwaka 2004/05, hadi asilimia 35 mwaka 2010; upungufu wa uzito kwa watoto walio chini ya miaka mitano ulipungua kutoka asilimia 22 mwaka 2004/05 hadi asilimia 21 mwaka 2010; na hali ya ukondefu iliongezeka kutoka asilimia 3 mwaka 2004/05, hadi asilimia 4 mwaka 2010. Aidha, watoto walio chini ya umri wa miaka mitano wenye uzito uliozidi au kiribatumbo walikuwa asilimia 5.

410. Mwaka 2010, asilimia 61 ya watoto walio na umri wa miezi 6 hadi 59 walipatiwa matone ya vitamini A. Aidha, asilimia moja ya watoto wa umri huo walipatiwa vidonge vya madini ya chuma. Utafiti wa Afya na Demografia wa

mwaka 2010 ulionesha kuwa wanawake wajawazito wanaomeza vidonge vyenye madini ya chmna kwa siku 90 au zaidi ilikuwa asilimia 4. Wengi wa wanawake wajawazito humeza vidonge hivyo kwa chini ya siku 60. Hali ya ulishaji kwa mujibu wa utafiti huo inaonesha kuwa asilimia 50 ya wanawake hunyonyesha watoto maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo. Aidha, hospitali 69 kati ya 143, sawa na asilimia 58. 8 zilizofanyiwa tathmini katika mikoa ya Tanzania Bara, zimefikia vigezo vya kuwa hospitali rafiki wa mtoto kwa kutekeleza vidokezo kumi muhimu vya kufanikisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama.

411. Huduma nyingine zinazohusu malezi ya watoto ziliendelea kuimarishwa. Mwaka 2010, watoa huduma ya afya 465 walipata mafunzo ya ulishaji watoto wachanga na wadogo wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Maeneo yaliyonufaika na mafunzo hayo kwa Tanzania Bara ni pamoja na wilaya za Makete, Bagamoyo, Temeke, Magu, Kigoma, Hai, Mafinga, Masasi, Mtwara Vijijini, Iringa Vijijini, Mufindi, Njombe, Ludewa, Kilolo, Songea Vijijini, Mbinga, Namtumbo, Tunduru, Iramba, Urambo, Nzega, Maswa na Kahama. Wilaya nyingine ni Tabora Vijijini, Uyui, Singida Vijijini, Sikonge, Igunga, Bariadi, Bukombe, Mbozi, Mbarali, Sumbawanga Vijijini, Nkasi, Mpanda, Chunya na Rungwe. Pia maeneo mengine yaliyonufaika na mafunzo hayo ni Manispaa za Iringa, Tabora, Songea, Singida, Shinyanga, Sumbawanga, Jiji la Mbeya na Unguja kwa upande wa Tanzania Visiwani.

412. Kutokana na ripoti ya Utafiti wa Afya na Demografia ya mwaka 2010, asilimia 82 ya kaya za watanzania wanatumia chumvi iliyowekewa madini joto. Hili ni ongezeko la asilimia 8 ukilinganisha na asilimia 74 iliyoripotiwa mwaka 2004/05.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

413. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kutoa na kuratibu huduma za ustawi wa jamii kwa watu wenye ulemavu, wazee, watoto walio katika mkinzano na sheria na watoto walio katika mazingira hatarishi. Hudmna hizi zinalenga

kulinda haki za makundi haya na kuimarisha utoaji wa huduma katika taasisi husika. Katika kuhakikisha watoto walio katika mkinzano na sheria wanapata haki zao, Serikali ilijenga bweni la wasichana katika shule ya maadili, Irambo na kujenga mahabusu mbili za watoto katika mikoa ya Mbeya na Mtwara. Aidha, katika mwaka 2010, moduli za uwezeshaji haki jamii zilipitiwa na kufanyiwa marekebisho ili ziendane na sheria mpya ya mtoto ya mwaka 2009.

414. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Jumla ya leseni 16 zilitolewa mwaka 2010 kwa ajili ya usajili wa vituo hivyo. Leseni hizo zilipelekea kuongezeka kwa idadi ya vituo kufikia 93, vyenye jumla ya watoto 3,767 wakiwemo wasichana 1,573 na wavulana 2,194.

## VYOMBO VYA AFYA NCHINI

Jedwali Na. 84

| Aina ya Vyombo | Serikali | | | Mashirika ya Umma | | | Mashirika ya Dini na ya Kujitolea | | | Sekta Binafsi | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2008 | 2009 | 2010 | 2008 | 2009 | 2010 | 2008 | 2009 | 2010 | 2008 | 2009 | 2010 | 2008 | 2009 | 2010 |
| Hospitali Maalum | 6 | 6 | | 0 | 0 | | 0 | 0 | | 0 | 0 | | 6 | 6 | 0 |
| Hospitali za Mkoa | 18 | 18 | | 0 | 0 | | 0 | 0 | | 0 | 0 | | 18 | 18 | 0 |
| Hospitali za Wilaya | 90 | 90 | 97 | 0 | 0 | 11 | 0 | 0 | 97 | 0 | 0 | 31 | 90 | 90 | 236 |
| Hospitali nyingine | 3 | 0 | | 6 | 15 | | 96 | 116 | | 24 | 47 | | 129 | 178 | 0 |
| Vituo vya Afya | 395 | 431 | 449 | 4 | 151 | 5 | 124 | 41 | 155 | 72 | 114 | 75 | 595 | 737 | 684 |
| Zahanati | 3649 | 3526 | 3773 | 112 | 189 | 70 | 689 | 635 | 717 | 613 | 842 | 572 | 5063 | 5192 | 5132 |
| Nyinginezo* | 0 | 0 | 269 | 0 | 0 | | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 269 |
| JUMLA | 4161 | 4071 | 4588 | 122 | 355 | 86 | 909 | 792 | 969 | 709 | 1003 | 678 | 5901 | 6221 | 6321 |

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

* Ni pamoja na kliniki maalum, nursing homes, huduma za maabara na x-ray binafsi

## HUDUMA ZA AFYA: WALIOFAULU MAFUNZO KWA MWAKA 2010

Jedwali 85

| Aina ya mafunzo | 2010 |
|---|---|
| Assistant Medical Officer | 211 |
| Assistant Dental Officer | 12 |
| Health Officers | 146 |
| Health Records Technician | 20 |
| Clinical Officers | 430 |
| Clinical Assistants | 360 |
| Dental Therapist | 41 |
| Laboratory Assistant | 240 |
| Laboratory Technicians | 160 |
| Physiotherapist | 17 |
| Radiologist | 37 |
| Public Health | 16 |
| Orthopaedic Technician | 14 |
| Pharmaceutical Assistants | 26 |
| Optometry Technician | 12 |
| | 3 |
| Dental Laboratory Technologist | |
| Pharm. Technologist | 58 |
| Med. Lab. | 30 |
| Nursing | 3790 |
| Opthalmic Nurse | 22 |
| Theatre Mngmt | 21 |
| **Jumla** | **5666** |

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

## IDADI YA WATAALAM WA AFYA

Jedwali Na. 87

| Kada | 2010 |
|---|---|
| Madaktari wote (wageni na wazalendo) | 578 |
| Madaktari wazalendo (MO)+ | - |
| Madaktari wasaidizi (AMO) | 1,527 |
| Wafamasia (PH) | 200 |
| Wafamasia wasaidizi (APhO) | 129 |
| Matabibu (MA) | - |
| Clinical officers | 5,781 |
| Waganga wasaidizi vijijini (RMA) | - |
| Mabwana Afya (HO) | 1,242 |
| Wauguzi | 9,286 |
| Dental | 65 |
| Assistant Dental | 422 |
| Wauguzi wakunga (MCHA) | 855 |
| Wengine | 909 |

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

## IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI - 2010

Jedwali Na. 87A

| Aina ya Huduma | Anayemiliki | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Shirika la Umma | Shirika la kujitolea/ Dini | Binafsi | Jumla |
| Hospitali za Rufaa/ Maalum | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Hospitali za Mkoa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Hospitali za Wilaya | 15,828 | 1,647 | 14,638 | 1,167 | 33,280 |
| Hospitali nyingine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Vituo vya Afya | 7,695 | 121 | 3,151 | 994 | 11,961 |
| Zahanati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 23,523 | 1,768 | 17,789 | 2,161 | 45,241 |

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

# SURA YA 21

# MAENDELEO YA JAMII

## Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

415. Mwaka 2010, Serikali iliendesha mafunzo katika vyuo 53 vya Maendeleo ya Wananchi. Mafunzo hayo yalihusu stadi za uashi, useremala, ushonaji, mapishi, ufundi magari, kilimo cha mboga, ufugaji na kujikinga na janga la UKIMWI. Idadi ya wananchi walionufaika na mafunzo hayo ilikuwa 31,039, ikilinganishwa na wananchi 29,557 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa fani na uboreshaji wa majengo katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Mafunzo ya muda mrefu yalitolewa kwa wananchi 4,913; kozi fupi wananchi 1,989; kozi nje ya chuo wananchi 9,176; na mafunzo yaliyotolewa kwa ushirikiano na asasi nyingine ndani na nje ya vyuo yaliyohusisha wananchi wapatao 13,347, ikilinganishwa na wananchi 4,708 kozi ndefu, wananchi 6,411 kozi fupi, wananchi 4,443 kozi nje ya chuo na wananchi 13,995 mafunzo ndani na nje ya chuo kwa ushirikiano na asasi nyingine.

416. Mwaka 2010, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilipandishwa hadhi na kuwa katika orodha ya vyuo vya Elimu ya juu. Kwa mwaka wa masomo 2010/2011, chuo kilikuwa na jumla ya wanachuo 259. Mafunzo ya ngazi ya Stashahada katika Taaluma ya Maendeleo ya Jamii yalitolewa katika vyuo vya Rungemba, Buhare, Monduli na Missungwi, ambapo katika mwaka wa masomo 2010/2011, vyuo hivyo vilikuwa na jumla ya wanachuo 947. Aidha, mafunzo ya ngazi ya Cheti katika Taaluma ya Maendeleo ya Jamii yalitolewa katika vyuo vya Ruaha, Uyole, Mlale, Mabughai, Missungwi na Buhare, ambapo katika mwaka wa masomo 2010/2011 kulikuwa na jumla ya wanachuo 2,676.

## Jinsia na Mendeleo ya Wanawake

417. Mwaka 2010, Benki ya Wanawake Tanzania iliendelea kutoa huduma kwa watu binafsi, makampuni na vikundi mbalimbali katika jamii. Mwaka 2010, akaunti zilizofunguliwa ziliongezeka hadi kufikia akaunti 21,281, kutoka

akaunti 4,220 mwaka 2009. Kati ya hizo, wanawake walikuwa asilimia 80.0, wanaume asilimia 18.3 na makundi mengine asilimia 2.1. Kulikuwa na ongezeko la asilimia 8.7 kwa akaunti zilizofunguliwa na wanawake, wakati idadi ya wanaume waliofungua akaunti ilipungua kwa asilima 10.7. Hii ilitokana na uhamasishaji mdogo kuhusu Benki hiyo ambayo hudhaniwa kuwa ni ya wanawake tu. Aidha, mwaka 2010, Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 10.1. Mikopo hiyo ilitolewa kwa wateja 4,081 kupitia vikundi na wateja 431 kwa watu binafsi na makampuni, sawa na asilimia 90 na asilimia 10, kwa mtiririko huo. Vile vile, mafunzo ya biashara yalitolewa kwa wanawake wajasiriamali 450 na waliwezeshwa kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya mwaka 2010.

418. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kutoa mafunzo kuhusu utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na albino kwa wakuu wa vituo vya polisi 40 na viongozi wa vijiji 43. Mafunzo hayo yalitolewa kutoka mikoa ya Kigoma, Arusha, Dodoma, Tabora na Manyara na kwa wasimamizi wa sheria 106 katika wilaya za Rorya, Tarime, Bukombe na Kahama.

419. Aidha, katika mwaka 2010, Serikali Kuu ilitoa jumla ya shilingi milioni 80 kwa Halmashauri 10 zilizomaliza marejesho katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake.

**Maendeleo ya Watoto**

420. Mwaka 2010, Serikali ilifanya utafiti wenye lengo la kutathimini ukubwa wa tatizo la watoto wanaoishi mitaani katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya, Iringa, Dodoma, Arusha, Singida na Mwanza. Utafiti huo ulihusisha watoto 2,295 ambapo 538 walikuwa wasichana na 1,757 walikuwa wavulana. Utafiti huo ulibaini kwamba asilima 50 ya watoto walikimbilia mitaani kwa sababu ya ukatili majumbani, mitaani na shuleni. Aidha, asilimia 35 ya watoto hao walikimbilia mitaani kwa sababu ya umaskini, asilimia 11 kutokana na ukosefu wa upendo na usimamizi hafifu wa watoto na asilimia 4 ilitokana na kufarakana kwa wana ndoa katika familia.

421. Utafiti ulibaini pia kuwa, watoto wa mitaani wanakumbana na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kunyanyaswa na kufanyiwa ukatili (asilimia 29); kukosa elimu, chakula, mavazi, malazi na huduma za afya (asilimia 15); kuzurura mitaani (asilimia 24); kutumikishwa katika kazi zenye madhara kwa afya zao (asilimia 13); kubakwa na kulawitiwa (asilimia 10); na kupata matatizo ya njaa (asilimia 9).

422. Aidha, mwaka 2010, Serikali ilifanya utafiti katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu ukatili dhidi ya watoto. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa asilimia 30 ya wasichana na asilimia 15 ya wavulana wamekumbana na ukatili wa kimapenzi. Matokeo ya tafiti hizo ni pamoja na kuandaliwa kwa Mpango Mkakati wa Jamii wa Kudhibiti Tatizo la Watoto Wanaoishi Mitaani na Mkakati wa Taifa wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto.

**Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs)**

423. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kusajili Mashirika hayo chini ya Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002. Katika mwaka 2010, mashirika 554 yalisajiliwa, kati ya hayo 526 yalipatiwa Cheti cha Usajili na 28 yalipatiwa Cheti cha Ukubalifu.

424. Mwaka 2010, Serikali kupitia Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ilitembelea NGOs 25 katika mikoa ya Iringa na Tanga na kutoa ushauri wa kitaalam wa namna ya kuboresha huduma kwa wananchi. Aidha, Bodi hiyo ilikutana na wadau wa Sekta ya NGOs 286 katika mikoa hiyo na kubadilishana uzoefu, kwa kubainisha mafanikio na namna bora ya kukabiliana na changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya NGOs ya mwaka 2001.

425. Mwaka 2010, Serikali iliwezesha ubadilishanaji wa taarifa za NGOs kwa wadau mbalimbali, ambapo jumla ya wadau 4,045 walipatiwa taarifa

mbalimbali za NGOs kupitia Ofisi ya Msajili, Tovuti ya Taifa ya Uratibu wa NGOs, Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Maonesho ya Nane-Nane. Walionufaika na taarifa hizo ni pamoja na Taasisi za Fedha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Kiserikali, Taasisi za Elimu ya Juu na Watu Binafsi.

## MWENENDO WA VIASHIRIA VYA MADENI




## UKUAJI HALISI NA MCHANGO WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KATIKA UKUAJI WA PATO LA TAIFA



## MWENENDO WA UKUAJI WA PATO LA TAIFA




## MWENENDO WA MFUMUKO WA BEI, JANUARI - DESEMBA 2010

